NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Pili – Tarehe 4 Aprili, 2018

*(Saa Tatu Asubuhi Kikao Kilianza )*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae, Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 pamoja na Maoni ya

Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Jitu Soni kwa niaba ya Mwenyekiti.

**MHE. JITU V. SONI – MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Maoni ya Kamati hiyo juu ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka 2017/2018 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2018/2019.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI. Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya Uratibu na Udhibiti wa UKIMWI) kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU OFISI YA WAZIRI MKUU):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

Na.10

### Asilimia 10 Inayotengwa na Halmashauri Nchini

**MHE. GODFREY W. MGIMWA (K. n. y. MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA)** aliuliza:-

Tangu kutangazwa sheria ya kuzitaka Halmashauri zote nchini kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya wanawake na vijana.

Je, ni nini kinaifanya Serikali kutokuwa na taarifa ya mfuko huo kujua una kiasi gani cha fedha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suzana Chogisasi Mgonokulima, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la maelekezo yanayozitaka Halmashauri zote nchini kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo ya wanawake asilimia tano na mikopo ya vijana asilimia tano ni Azimio la Bunge la Agosti 1993, chini ya kifungu cha 17(1) cha Sheria ya *Exchequer and Audit Ordinance* ya mwaka 1961; likiazimia kuanzishwa kwa Mifuko Maalum ya Mikopo kwa Vijana na Wanawake kwa kuchangiwa asilimia 10 ya mapato ya ndani ya kila halmashauri kila mwaka. Baada ya azimio hilo Serikali ilitoa maelekezo mahsusi kwa Halmashauri zote nchini kutenga fedha hizo kuanzia mwaka wa fedha 1993/1994.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto kadhaa za kiutekelezaji ambazo zimekuwa zikisababisha utekelezaji wa azimio hilo usifikie asilimia 100. Miongoni mwa changamoto hizo ni kutofikia viwango vya makusanyo ya ndani vilivyopangwa kwa mwaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano katika mwaka wa fedha 2016/2017 jumla ya shilingi 665,414,828,000 za mapato ya ndani zilipangwa kukusanywa na Halmashauri zote nchini; lakini mapato halisi yaliyokusanywa ilipofika mwisho wa mwaka yalikuwa ni shilingi 544,897,803,696 tu. Kutokana na ukusanyaji kutotabirika na hivyo kutofikia viwango tarajiwa, badala ya kiasi cha shilingi bilioni 56.8 kukopeshwa wanawake na vijana kama ilivyokuwa imetengwa, ni shilingi 17.5 tu sawa na asilimia 31, ndizo zilizotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwakumbusha wakurugenzi wa halmashauri zote 185 Tanzania Bara kwamba kutotoa asilimia 10 ya mapato ya ndani ni tabia ambayo husababisha waandikiwe deni kwenye taarifa za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kupitia Bunge lako Tukufu, naagiza kuanzia sasa ni lazima kila Halmashauri itoe asilimia 10 ya mapato halisi ya ndani kama ilivyoelekezwa na Serikali ili kutokusababisha madeni ya aina hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgimwa swali la nyongeza.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nitakuwa na swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri nyingi zimekuwa hazitengi fedha hizi kwa ajili ya vijana na akina mama; lakini vile vile tuna tatizo sasa hivi ambalo tungekuwa makini zaidi kuliangalia suala la ndugu zetu walemavu, kwamba kuweze kuwa na uwezekano sasa wa kuzitenga fedha kutoka katika hizi asilimia 10 kwa ajili ya walemavu, vijana na akina mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu majibu ya msingi yameshatolewa ningependa kufahamu kwa hizi

Halmashauri ambazo kwa ujumla zimeshindwa kutenga fedha hizi kwa ajili ya vijana kama mimi akina mama; na kama tulivyoongea kuhusu walemavu ningependa kufahamu sasa.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba inazibana halmashauri hizi ili ziweze kupata mapato ya ndani kwa uhakika na kuhakikisha kwamba inatenga fedha hizi kwa ajili ya makundi haya? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali la nyongeza ambalo linawagusa akina mama na vijana nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kupitia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ameshatoa waraka tangu mwaka jana mwezi wa saba kuelekeza Halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba wanatenga asilimia 10 kwa ajili ya mikopo ya vijana na wanawake na hilo ndiyo maana nimesema hapa kupitia Bunge lako Tukufu kwamba ni lazima watenge na wasipotenga sasa Serikali itaanza kuchukua hatua za kiutumishi dhidi ya Wakurugenzi ambao hawatengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwa sababu kinachotakiwa kufanyika ni kutenga kile ambacho kimekusanywa, kama kimekusanywa bilioni 10 basi asilimia 10 ya bilioni 10 lazima itengwe kwa ajili ya wanawake na vijana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri hilo la kuchukuliwa hatua hilo, naona inabidi lichukuliwe sawa sawa. Naona watakuwa wamekusikia kwamba watachukuliwa hatua za kinidhamu wasipotenga hizo asilimia 10. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Janet Mbene swali la nyongeza.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Na mimi naomba kuuliza swali la nyongeza kuwa hili suala la kutenga asilimia 10 wa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu linaonekana kama halijakaa kisheria sana na ndiyo maana wakati mwingine wanatumia hiyo *loopholes* za kuepuka kutenga hilo fungu.

Je, Serikali ina mkakati wowote wa kuhakikisha kuwa sheria au kanuni zinarekebishwa ili kuhakikisha kuwa hili jambo linakuwa kisheria zaidi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba tumeshapokea maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu pendekezo la kupitia upya sheria ambayo ndiyo tunaiangalia ambayo ilikuwa ndio misingi wa kuanzishwa hii mifuko ili tuweze kuona kwamba tunaweza kurekebisha sehemu gani ili kuweze kuzibana zaidi Halmashauri kuhusu kutenga asilimia 10.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Sima swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa fedha hizi zimeleta mgogoro sana zinapowekwa kwenye akaunti ya pamoja, je, Serikali haioni haja sasa kuzielekeza Halmashauri kuanzisha akaunti maalum kwa ajili ya hii asilimia 10 peke yake? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba tumechukua maoni ya Mheshimiwa Sima ambayo naamini ni maoni ya Waheshimiwa Wabunge wote na tutalifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa vipo vikundi vya akina mama ambavyo vimeanzishwa na kuunda *SACCOS,* lakini halmashauri hawatoi pesa hiyo asilimia 10 kuvipatia vikundi hivyo na wakati vikundi hivyo havijaweza kukopeshwa na mabenki au taasisi mbalimbali za kifedha.Je, ni kwa nini sasa Serikali isiagize Halmashauri ili vikundi hivyo navyo vilivyoundwa kama *SACCOS* viweze kukopeshwa pesa hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Genzambuke kwa kuzidi kuvijali vikundi vya *SACCOS* ambavyo vimeanzishwa kwenye Halmashauri nyingi hapa nchini ikiwemo Halmashauri ya Kasulu pale anakotoka.

Hili suala ni wazo zuri na mimi naomba sana sana badala ya kulijibu hapa haraka haraka tulichukue tukalifanyie kazi zaidi kwa sababu malengo Mfuko wa Vijana na Wanawake ni kukopesha wale vijana ambao wanajishughulisha na kazi za uzalishaji mali moja kwa moja. Sasa hili suala la kusema kwamba tuwakopeshe halafu na wao wakopeshane ni wazo jipya ambalo linahitaji kujadiliwa zaidi kitaalam ili tuweze kutoa maelekezo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba tu niliarifu tu Bunge lako Tukufu kwamba pamoja na kuendelea kulifanyia kazi jambo hili naomba kuendelea kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuwa katika kutoa mikopo kwa vijana kupitia Mfuko wa Vijana wa asilimia tano, zile zinazotengeneza asilimia 10 kwenye Halmashauri tayari Serikali ilishagiza vijana kupitia halmashauri zao waunde *SACCOS* za vijana ili waweze kunufaika na mikopo hiyo na kupitia kwenye hizo *SACCOS* waweze kujikopesha na mikopo hiyo iwe *revolving. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo pamoja na vijana ni lazima pia kuwaangalia na akina mama. Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na hasa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limeanza kuweka mkakati maalum wa kuhakikisha linafikia vikundi vya *VICOBA* na *SACCOS* za wanawake na vijana katika nchi nzima ya Tanzania. Nimuombe sana Mheshimiwa Genzabuke, kwa kuwa kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi tuna mifuko takribani 17 ya kuwawezesha wananchi Mheshimiwa Genzabuke awasiliane na mimi tuwaelekeze akina mama hawa wa Kigoma wanaweza wakasaidiwaje. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea, Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 11

### Upungufu wa Matundu ya Vyoo Mashuleni

**MHE. ESTER A. MAHAWE** aliuliza:-

Takwimu zinaonesha upungufu mkubwa wa matundu ya vyoo zaidi ya 200,000 katika shule mbalimbali za sekondari na msingi.

(a) Je, nini mkakati wa Serikali wa kumaliza tatizo hilo?

(b) Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kuja na mkakati mbadala kama ilivyofanya wakati wa kumaliza tatizo la madawati na maabara nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuna upungufu wa matundu ya vyoo 276,198 kwa shule za msingi na 20,534 kwa shule za sekondari. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya matundu ya vyoo 6,708 kwa shule za msingi na 2,071 kwa shule za sekondari yamejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya tathmini ya kina tumebaini kuwa zinahitajika jumla ya shilingi bilioni 646.822 kumaliza tatizo hilo. Wizara yangu imetoa maelekezo kwa halmashauri zote kwamba katika Bajeti ya mwaka 2018/2019, fedha za ruzuku ya maendeleo ambazo ni jumla ya shilingi bilioni 55.2 endapo zitapitishwa na Bunge, sehemu kubwa ya fedha hizo ielekezwe kwenye kipaumbele cha miundombinu ya elimu ikiwemo vyoo kwenye shule zote ambazo tayari wananchi watakuwa wamechangia nguvu zao.

Uamuzi huo utatoa nyongeza kubwa sana kwenye Bajeti ya shilingi bilioni 19.97 ambayo imetengwa chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia mahsusi kwa ajili ya matundu ya vyoo katika shule za msingi na shule za sekondari. Mkakati wa Serikali ni kutumia fedha hizo kumalizia kazi za ujenzi ambazo zitakuwa zimeanzishwa na wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Mahawe, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa ruzuku hii iliyotajwa hapa kila Halmashauri imejipangia namna gani itatumia hizo ruzuku na hakuna *uniformity* katika matumizi hayo, na kama ambavyo tulimaliza suala la upungufu wa madawati na maabara nchini, je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kutoa maagizo makali kidogo ili kumaliza suala hili la upungufu wa vyoo mashuleni?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wanaoteseka sana katika suala zima la upungufu wa vyoo nchini ni hasa mabinti walioko kwenye shule za sekondari. Kila mtu anafahamu wanapokuwa kwenye mzunguko ule kidogo wanapata taabu kulingana na ukosefu wa vyoo tena vyenye maji safi.

Je, ni lini sasa hususani katika Mkoa wetu wa Manyara Serikali itachukua hatua ya kumaliza tatizo hili hasa katika shule ya Komoto na Bagara Sekondari pale Babati Mjini? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Ester Mahawe kwa swali la msingi pamoja na maswali yake ya nyongeza. Ni changamoto kubwa sana ambayo tunakabiliana nayo na yeye mwenyewe ni shahidi manake ni mdau katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyozungumza tumekuwa na mikakati mbalimbali kuhusu miundombinu mbalimbali hususani maabara na madarasa. Lakini kwa wakati huu ambao bado tunahangaika kumalizia ujenzi wa maabara hususani kumalizia maboma ya maabara

na kuzipatia vifaa, na bado wananchi wanaendelea kuchangia; mimi nilikuwa namuomba Mheshimiwa Mahawe aungane na sisi kwamba tutoe kwanza kipaumbele kwenye hizi fedha ambazo zimetengwa ili kusudi tuone zitafikia hatua gani wakati huo huo tunamalizia suala la maabara ili baadaye tuweze kuchukua hatua zaidi kama anavyopendekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuhusu miundombinu ya maji katika shule zetu. Tumeshatoa maelekezo kwamba kila shule inapopanga ujenzi wa madarasa ni muhimu sana wakazingatia kuweka miundombinu ya kuvuna maji ya mvua. Hiyo ni miundombinu ambayo ni ya gharama nafuu badala ya kuwa na miradi ya maji ya kutumia vyanzo vingine ambavyo vinatumia fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hilo ni agizo lilishatolewa na maelekezo yalishatolewa. Inatakiwa sasa Wakurugenzi wa halmashauri zote pale ambapo shule inajengwa lazima kuwe na miundombinu ya maji ya mvua, ikiwa ni pamoja na shule ambazo amezitaja, baada tu ya kikao cha leo nitafuatilia kule Halmashauri ya Babati ili kusudi tuweze kujua hizo shule Mkurugenzi ana mpango gani kuzipatia huduma za maji. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa miundombinu hiyo katika vyoo kwenye shule zetu za msingi na sekondari bado haizingatii mahitaji ya watoto wenye ulemavu; na baadhi ya watoto wenye ulemavu wanalazimika kutambaa katika vyoo hivyo ambavyo wakati mwingine ni vichafu na vinahatarisha afya kwa watoto wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nashukuru kwa majibu yake, lakini

sijasikia hata yeye mwenyewe kuona kwa jicho la pili uhitaji wa watoto hawa wenye mahitaji maalum katika vyoo hivi. Ni nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha kwamba wanazingatia mahitaji ya watoto wenye ulemavu ili na wao waweze kusoma vizuri? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Amina Mollel kwa kufuatilia hasa hasa masuala yanayowahusu wanafunzi wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba michoro ya zamani ilikuwa na upungufu wa kutozingatia mahitaji ya watoto au wanafunzi wenye ulemavu. Hata hivyo michoro ambayo ilipitishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia mwaka jana yote imezingatia kwamba darasa, choo na bweni na miundombinu mingine ya shule ambayo inatumiwa na wanafunzi lazima izingatie mahitaji ya watoto wenye ulemavu, na ushahidi ni mabweni mapya na madarasa mapya na vyoo vipya ambavyo vimejengwa tangu mwaka jana mwezi wa saba vyote vimezingatia mahitaji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Amina Mollel kwenda kufanya ukaguzi kwenye maeneo yote ambayo hatimaye tutaelekeza wafanye marekebisho, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama Mbunge wa Madaba sasa aulize swali lake.

Na. 12

**Kuwajengea Uwezo Wakulima na Wafugaji**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA** aliuliza:-

Idadi ya watu nchini inazidi kuongezeka, ongezeko hili linaenda sambamba na ongezeko la mahitaji ikiwemo ardhi kwa ajili ya kilimo na ufugaji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea uwezo wakulima na wafugaji ili waendeshe shughuli zao katika maeneo madogo lakini kwa tija kubwa na kuwaondolea adha wanazozipata?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali huwajengea uwezo wakulima na wafugaji nchini kupitia elimu na ushauri wa kitaalam ambao hutolewa na Maafisa Ugani walioko kwenye Kata na Vijiji vya Halmashauri zote nchini. Hadi Desemba, 2017 tunao Maafisa Ugani 13,532. Kati ya hao Maafisa Ugani 8,232 ni wa kilimo cha mazao, 4,283 ni wa mifugo, 493 ni wa uvuvi na 524 ni wa ushirika.

Elimu ya kilimo na ufugaji bora hutolewa kupitia mashamba darasa 11,213 nchi nzima kwa wakulima na wafugaji wakubwa na wadogo, vikundi vya ushirika vya miradi ya umwagiliaji kwa njia ya mitaro na njia ya matone *(drip irrigation)* na vikundi vya ushirika vya ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia awamu ya pili ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo itakayoanza kutekelezwa mwaka ujao 2018/2019 Serikali inaandaa mradi wa kilimo cha kutumia vitalu nyumba *(green house)* utakaotekelezwa kwa kila halmashauri kujenga vitalu nyumba visivyopungua viwili ili kusambaza teknolojia mpya

ya kilimo yenye uwezo mkubwa wa kuzalisha shehena ya mazao mengi katika eneo dogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mingine ni pamoja na kufanya sensa mahsusi ya kuwatambua wakulima wadogo na wakubwa, kuwasajili, kujua uwezo wao na kujua mahitaji yao ya mbegu, mbolea na madawa. Zoezi hilo limeanza na mazao ya kahawa, tumbaku, korosho, chai na pamba kwa mazao ya biashara; pamoja na mazao ya mahindi, mpunga, ngano na muhogo kwa upande wa mazao ya chakula. Takwimu hizo zitasaidia utekelezaji wa mikakati ya kuongeza uzalishaji kwa kuhakikisha pembejeo za kilimo zinawafikia wakulima mapema ili zitumike kwa wakati stahiki wa kilimo kwa lengo la kuongeza tija.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mhagama, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niipongeze sana Serikali kwa mkakati huu mzuri ambao umeiuweka na kwa sehemu imetekeleza lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile moja kati ya migogoro ambayo inatokana na tatizo hili ambalo limeelezwa ni migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Na kwa vile migogoro hii kwa sehemu kubwa inachangiwa na ukosefu wa mipango bora ya matumizi ya ardhi kwa baadhi ya maeneo, na kwa vile pamoja na jitihada nzuri za Serikali migogoro hii imechangiwa na Halmashauri za wilaya hasa watumishi ambao hawapo tayari kwenda kufanya kazi hii bila kulipwa posho, sasa je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba vijiji vyote ambavyo havina mpango bora wa ardhi vipatiwe mpango huo? Na pili ina mpango gani kuhakikisha kwamba watumishi ambao hawapo tayari kwenda kufanya kazi hizi bila kupata posho wanachukuliwa hatua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama kwa kuijali sana hii sekta ambayo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu, hata viwanda vinategemea sana sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vijiji ambavyo hadi sasa havina mipango ya matumizi bora ya ardhi tunayo changamoto kubwa sana, moja, ili kijiji kipime, kiwe na mpango wa matumizi bora ya ardhi yake bajeti ambayo inahitajika angalau kuweza kuwezesha upimaji huo inaanzia kati ya shilingi milioni tano hadi milioni nane na baadhi ya vijiji ambavyo ni vikubwa hadi milioni kumi. Sasa kwa sababu Halmashauri nyingi bado hazijawa na uwezo wa kuwa na fedha hizo utekelezaji umekuwa ni wa pole pole sana, ikiwemo Halmashauri yake ya Madaba hadi sasa ni vijiji nane tu ndio vina mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa wito kwa vijiji ambavyo vina fedha, vipo vijiji ambavyo vina fedha, vigharamie mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa manufaa ya kiuchumi ya wananchi wa vijiji hivyo. Wakurugenzi wa halmashauri zote nchini wafanye mapitio ya vijiji vyote na kuvishauri vile ambavyo vina uwezo wa kugharamia zoezi hilo viweze kugharamia, na vile ambavyo havina kabisa uwezo halmashauri ijipange kugharamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tunawachukulia hatua gani watumishi ambao hawataki kwenda kufanya kazi vijijini hadi walipwe posho. Nataka nitoe angalizo kwao, kwamba walipoajiriwa walipewa maeneo ya kufanya kazi. Kama mtu amepewa eneo la kijiji halafu ndani ya kijiji hataki kufanya kazi mpaka alipwe posho huyu mtu tunatakiwa tupate taarifa zake mapema iwezekanavyo ili tuweze kumchukulia hatua na Wakurugenzi wa Halmashauri waanze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatoa maagizo wale watumishi ambao wana mazoea ya kukaa Makao Makuu ya Halmashauri bila kwenda kutembelea vijiji waanze kupangiwa kazi na Wakurugenzi wa Halmashauri bila kujali kama kuna posho au hakuna, ili mradi tu aweze kuwezeshwa vyombo vya usafiri vya kuweza kuwafikisha kwenye vijiji wanavyotakiwa kwenda kufanya kazi, basi. Kwa hiyo, hiyo ndio ushauri wangu na maelekezo yangu kupitia Bunge lako Tukufu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru sana Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa majibu yake mazuri kulingana na swali lililoulizwa juu ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi. Wizara imejipanga vizuri katika mwaka wa fedha unaokuja kwa ajili ya kupima maeneo ambayo yana migogoro mingi, hasa yale maeneo yanayozunguka kwenye mbuga za wanyama. Tayari ile Tume ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi imeshaingia makubaliano pia na wenzetu wa *TANAPA,* kwa hiyo kuna vijiji vingi ambavyo vitapimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo tukumbuke tu kwamba mpango wa kupanga matumizi bora ya ardhi au masuala ya mpango miji ni jukumu la Halmashauri zenyewe husika. Kama alivyosema Naibu Waziri bado pia vijiji na maeneo ambayo yanakuwa na pesa wanayo fursa hiyo. Kama Wizara tuna-*facilitate* uwezekano wa kuweza kuwapa elimu na namna bora ya kupima, lakini Wizara tumejipanga vizuri na tutakwenda kupunguza sana kero hii. Kwa hiyo, tunachowaomba sana wananchi tuwe tayari katika suala hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba niongezee na niliarifu Bunge lako tukufu kwamba

Wizara ya Kilimo tumeandaa mpango mkakati wa kilimo *ASDP II* ambao utahusisha zaidi ya Wizara sita. Hata hivyo kutokana na swali la msingi ni kwamba katika hizi *green house* tumepanga kila halmashauri iweze kuwa na *green house* ili wananchi waweze kujifunza, kwa sababu hizo *green house* ambazo tunazizungumzia zinachukua eneo dogo lakini uzalishaji wake unakuwa ni mkubwa zaidi na vile vile ni katika kuendeleza hii tasnia yetu ya *horticulture*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni kwamba Wizara tunatoa mafunzo na maelekezo ambayo yanafanyika kwa kutumia udongo na teknolojia mbalimbali za kuhifadhi udongo huo ili kuzuia mmomonyoko na vile vile kuweza kuongeza tija kwa ajili ya kupunguza tatizo hili nililolisema, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa tutaendelea; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 13

### *X-Ray* ya kisasa Hospitali ya Mkoa wa Morogoro

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA** aliuliza:-

Hospitali ya Mkoa wa Morogoro pamoja na changamoto zinazoikabili za kuwa na wagonjwa wengi, kukosekana kwa Hospitali za Wilaya, kupokea majeruhi wa ajali mbalimbali lakini hadi sasa hospitali hiyo inatumia *X-ray* za zamani ambazo ni chakavu hivyo kusababisha usumbufu mkubwa kwa wagonjwa.

Je, ni lini Serikali itapeleka *x-ray* ya kisasa *(Digital X-ray)* ili kuondokana na adha kubwa wanayopata wagonjwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali namba 13 lililoulizwa na Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inatambua umuhimu wa huduma ya uchunguzi kwa kutumia mionzi ya rediolojia. Aidha, Wizara inatambua changamoto ya uchakavu wa mitambo ya radiolojia na gharama kubwa za matengenezo inayoathiri upatikanaji wa huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imepanga kuleta mashine mpya 34 za kisasa za *digital* ambazo zinatengenezwa na Kampuni ya Philips, na hii inatokana na mkataba wa matengenezo wa mwaka 2012 na 2016 ambao mbali ya matengenezo waliyotakiwa kufanya walitakiwa vilevile kubadilisha mashine chakavu na kuweka mashine mpya. Mashine hizi zitafungwa katika hospitali za rufaa zote za mikoa Tanzania Bara ikiwepo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro. Awamu ya kwanza ya kuletwa mashine hizi inatarajiwa kuwa ni Juni, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na gharama kubwa ya kununua na kufanya matengenezo ya vifaa vya uchunguzi Wizara imeanza kufanya uchambuzi ikiwa ni pamoja na kuangalia uzoefu wa nchi nyingine ambazo zilishaanza kuweka utaratibu wa kukodisha vifaa na kulipia huduma. Wizara inatarajia kutumia uzoefu huo kuandaa miongozo itakayowezesha kutekelezwa kwa utaratibu huo kwa ufanisi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Jasmine Bunga, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu haya, maana kwa siku nyingi sana tulikuwa tumeahidiwa na majibu

yalikuwa hivi hivi, lakini haya mpaka tumepewa *date* kwamba Juni tutapata hiyo *x-ray digital* tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuuliza maswali ya nyongeza kwamba; kwa kweli pamoja na kupata hiyo *digital x-ray* lakini bado kuna huduma nyingine ya mashine za kisasa ambazo zitasaidia hawa majeruhi kuweza kuchunguzwa zaidi. Kwa mfano tumeshuhudia hivi majuzi Waheshimiwa wenzetu Wabunge walivyopata ajali ilibidi wakimbizwe haraka sana kwenda Muhimbili kule kwa ajili ya uchunguzi zaidi, lakini kama tungekuwa na mashine hizi tungesaidia hata wagonjwa kuokoa usumbufu na maisha yao na gharama; mashine hizo ni *MRI* na *CT-Scan.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaomba kuuliza, je, Wizara ni lini sasa mtatuletea pia katika Hospitali hii ya Mkoa wa Morogoro mashine za *MRI* na *CT-SCAN* ili kupunguza hata rufaa kule Muhimbili na kupunguza msongamano lakini pia kuokoa maisha ya wagonjwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia pale Morogoro kama tunavyoona ile hospitali inapokea wagonjwa wengi sana wa ndani ya mkoa lakini pia na mikoa mingine. Sasa bado kuna huu usumbufu ambao unapata wagonjwa kwamba *operating theatre* ya mifupa haipo wanatumia *theatre* moja, je, ni lini sasa pia Serikali itatenga fedha za kujenga *theatre* hii ili kuokoa maisha ya wagonjwa na kuondoa usumbufu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tisekwa ambaye leo anaadhimisha siku yake ya kuzaliwa, nimpongeze kwa hilo, lakini nimpongeze vilevile kwa maswali yake mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tunaendelea kujipanga; tunatambua kwamba Mkoa wa Morogoro, mikoa ya Iringa, Mkoa wa Pwani pamoja na Dar es Salam ziko katika *highway* na kumekuwa na ajali nyingi ikiwa ni pamoja na ambayo imetokea kwa Waheshimiwa Wabunge wiki iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto tuna mradi ambao tunashirikiana na wenzetu wa Benki ya Dunia kuweka huduma za dharura na ajali na tumejaribu sana kulenga katika mikoa ya Iringa, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam ambapo huduma mbalimbali za dharura zitawekwa ikiwa ni pamoja na *ambulance* na kuangalia sasa uwezekano wa kuweka hizo huduma za *CT-Scan* na *MRI* katika hospitali hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo Serikali imetukabidhi Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto hospitali zote za rufaa za mikoa. Tumezifanyia tathmini za kina na katika bajeti ya 2018/2019 katika moja ya maeneo ambayo tutaenda kuboresha ni pamoja na kuongeza vyumba vya upasuaji. Kwa hiyo naomba sana Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono bajeti yetu ya Wizara ya Afya itakapofika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa tatizo la wingi wa wagonjwa katika Hospitali ya Morogoro inafanana na wingi wa wagonjwa katika Hospitali ya Mkoa wa Songea ambao unasababishwa na kukosekana kwa Hospitali ya Wilaya ya Songea. Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya Songea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama

nilivyosema katika jibu langu la msingi, Serikali imetukabidhi hospitali za rufaa za mikoa na tunaendelea na maboresho; lakini kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuna fedha ambazo wamezitenga kwa lengo la kuhakikisha kwamba baadhi ya Wilaya ambazo hazina Hospitali za Wilaya ziweze kujenga. Lengo ni kuhakikisha kwamba ule mtiririko wa huduma kutoka katika zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, hospitali za mkoa, hospitali za kanda mpaka hospitali maalum za kitaifa unazingatiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, naomba kuongezea kidogo katika majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kutambua umuhimu wa kuwepo na hospitali za wilaya za kutosha, katika bajeti ya mwaka 2018/2019 tunaenda kujenga Hospitali za Wilaya 67. Sina uhakika na naomba Mungu iwe katika hizo Wilaya 67 na Songea ikawepo, ni vizuri tukatizama katika orodha ili tukaona nao kama wapo, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Wilaya ya Lushoto inatumia *x-ray* ya zamani na pia ni ndogo haina uwezo. Je, ni lini Serikali itapeleka *x-ray* ya kisasa *(digital x-ray)* ili kuondoa adha wanayoipata wagonjwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma za *x-ray.* Kama alivyokuwa amesema katika swali lake la msingi, ni kweli tulikuwa na *x-ray* pale lakini katika mkataba huu ambao tunao na Philips lengo letu sasa ni kuziondoa zile *x-ray* za zamani na kuweka *x-ray* mpya; na tutalizingatia hilo kwamba mgao huu mpya utakapokuja basi na Hospitali ya Lushoto nayo iweze kuwa katika sehemu zile ambazo zitapata.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba utusaidie, hawa Phillips ni wale waliokuwa wanasumbua Mafia ama si hawa? Maana Mbunge wa Mafia leo hajazungumza lakini ni hawa Philips au si hawa, waliofanya Mafia wasiwe na mashine kwa mwaka mzima? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa swali lako la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ina mkataba wa utoaji wa huduma za *x-ray* nchi nzima kwa kupitia kampuni hii ya Philips.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani utatufafanulia hapo baadae, kama ni hawa wameshatusumbua Mafia, Mbunge wa Mafia ameshaongea humu ndani sijui mara ngapi kuhusu hao Philips. Kama ni hao Wizara itusaidie kuangalia jambo hili. Kama si hao ni sawa lakini kama ni hao tafadhali kwa sababu wametusumbua Mafia kila siku tunasikiliza swali hilo hilo kutoka Mafia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 14

**Kupiga Marufuku Uingizaji wa Nyama Kutoka Nje ya Nchi**

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA** aliuliza:-

Tanzania ni nchi ya pili kwa kuwa na mifugo mingi Barani Afrika.

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka wa kupiga marufuku uingizwaji wa nyama kutoka nchi za nje ili kuruhusu ukuaji wa viwanda vya nyama nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Tanzania ni nchi ya pili kwa kuwa na mifugo mingi Barani Afrika baada ya Ethiopia. Aidha kumekuwepo na uingizaji wa nyama ya ng'ombe, nguruwe na kondoo kwa wastani wa tani 2,000 kwa mwaka kuanzia mwaka 2013 hadi 2015. Hata hivyo kiasi hicho kimepungua kuanzia mwaka 2016 tani 1,182.79 na mwaka 2017/2018 tani 1,225 kutokana na kuwepo kwa machinjio na viwanda 23 vyenye uwezo wa kuzalisha tani 44,820.6 za nyama na bidhaa zake kwa mwaka zenye ubora linganifu na nyama inayotoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2016/2017 jumla ya nyama tani 2,608.93 yenye thamani ya dola za kimarekani bilioni 5,679,217.28 iliuzwa katika nchi za Oman, China, Hong Kong, Dubai na Vietnam. Vilevile idadi ya machinjio nchini kwa sasa ni 1,632 na yana uwezo wa kuchinja nyama kiasi cha tani 625,992 kwa mwaka.

Pia masoko ya nyama inayozalishwa ndani ya nchi yameongezeka ambapo inauzwa katika hoteli za kitalii, maduka maalum *(super markets)* na migodi yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inafanya tathmini ya kina kuhusu biashara ya mifugo na mazao yake ili kujua kwa uhakika kiasi cha nyama kinachoingizwa nchini, masoko na uwezo wa viwanda vya ndani katika kuzalisha nyama na mazao yenye ubora na viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kuzalisha, kuchakata na kusindika nyama na bidhaa zake zenye viwango na ubora unaokubalika. Pia, imeweka mapendekezo ya kuongeza tozo ya uingizaji wa nyama na bidhaa zake ili kuleta ushindani wa haki katika soko la ndani utakaowezesha kukua kwa viwanda vya ndani, kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa uingizaji wa nyama kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba wizara inaupokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya kuufanyia kazi na kwa kuzingatia matokeo ya tathmini tunayoendelea hivi sasa.

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri kabla hujatoka hapo mbele, dola za kimarekani bilioni tano, ni bilioni tano au milioni tano ili kumbukumbu za kwenye Taarifa za Bunge zikae sawasawa. Ni bilioni tano au milioni tano?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunikumbusha, naomba isomeke dola za kimarekani 5,679,217.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Zainab Katimba swali la nyongeza.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali lakini pia nashukuru kwa kuchukua ushauri wangu. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mkakati wa kufikia uchumi wa viwanda unalenga pamoja na mambo mengine kutatua changamoto ya ajira hususan kwa vijana, na kwa kuwa viwanda vya ngozi nchini vinakabiliwa na changamoto ya kodi kubwa katika malighafi ya kuchakata ngozi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa *tax incentives* kwa viwanda vinavyozalisha mazao yanayotokana na mifugo ili kufikia malengo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, je, Serikali haioni haja ya kuwa na *breeding program* ili kuongeza kiwango na ubora wa mazao yanayotokana na mifugo Tanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba na naomba nimpongeze sana kwa maswali yake mazuri yanayolenga katika kuhakikisha kwamba Tanzania ya viwanda inapatikana lakini pia tunazalisha ajira kupitia sekta yetu muhimu ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza linaeleza juu ya suala la kufanya mkakati au Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuvipendelea viwanda vyetu vya ndani katika tasnia ya ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yetu tayari imeshapeleka mapendekezo Wizara ya Fedha ya kuhakikisha kwamba kodi zote zinazotozwa katika *accessories* za uchakataji wa ngozi ziweze kupunguzwa ama kuondolewa kabisa ili kusudi kuweza kuhamasisha uwekezaji zaidi kwenye tasnia hii ya ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tumehakikisha tunapendekeza Wizara ya Fedha iweze kuongeza viwango kwa bidhaa za ngozi zinazotoka nje ya nchi kuingia nchini hasa za mitumba ili kusudi kuweza ku-*discourage* uagizaji wa bidhaa hizo na uwekezaji zaidi ufanyike ndani ya nchi yetu, na huu ndio mtazamo wetu kama Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili linahusu mpango mkakati wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wa kuweza kupata mifugo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mpango wa kuhamasisha, tunaita *artificial insemination* au uhimilishaji wa mifugo yetu na hii tumefanya kwa kuanzisha vituo maeneo mbalimbali takriban vituo sita katika nchi, na tunacho kituo kikubwa sana pale Arusha cha *NAIC* pale *Usa River* ambacho kinazalisha mbegu bora. Vilevile zile mbegu zinatawanywa katika hivyo vituo vingine vilivyopo kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na mkakati huo tumekuwa tukinunua mbegu bora hata kutoka nje ilikuweza kuja kuongeza ubora wa mifugo yetu tuliyonayo hapa nchini. Vilevile tunakwenda katika kuhakikisha kwamba tunaboresha sheria yetu ya mbali za mifugo ili kusudi kuweza kwenda sambamba na mabadiliko hayo tunayoyataka ya kuboresha mifugo yetu hapa nchini ili tuweze kupata nyama bora na tuweze kupata maziwa bora na kwa wingi, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Nassir swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri wa Fedha

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nilipenda tu niongezee, kwanza nilitaka nithibitishe kwamba mapendekezo yaliyotoka Wizara ya Mifugo ni kweli yamefika Wizara ya Fedha na hapa mkononi mwangu nina bangokitita lina kurasa 53 ya mapendekezo ya maboresho ya kodi mbalimbali zikiwemo hizi za tasnia ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Zainab avute subira kidogo Serikali itaji-*pronounce* kupitia hotuba kuu ya Serikali. Nimuhakikishie kwamba kabisa ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba viwanda vyetu vya ndani vinapewa ahueni ya kodi mbalimbali kadri itakavyowezekana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Nassir swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tumekuwa tukiona wawekezaji wetu wa ndani wakijitahidi kuzalisha bidhaa mbalimbali zenye ubora wa hali ya juu.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kibiashara wa kuzipa kipaumbele bidhaa zetu zinazozalishwa nchini ili kuweza kuendana na ushindani wa soko hili ambalo lipo huru na lenye ushindani mkubwa ili sasa kuweza kufanana na nchi nyingine zinavyofanya? Ahsante nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kimsingi kupitia itifaki mbalimbali ambazo tunakuwa tumezisaini tunajitahidi kuwa na ushindani wa haki. Hata hivyo kwa bidhaa ambazo zinazalishwa ndani zinapewa kipaumbele na tunahamasisha wadau kupenda kununua zaidi bidhaa zetu za ndani kuliko hata hizo za nje. Vilevile wakati mwingine pia kuna tozo ambayo inatolewa katika baadhi ya bidhaa zinazotoka nje ili kufanya bidhaa za ndani ziweze kuwa na nafasi nzuri zaidi katika ushindani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa tutaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo sasa aulize swali lake.

Na. 15

**Kampuni Zinazotoa Huduma ya Usafirishaji Bandarini**

**MHE. MATTAR ALI SALUM** aliuliza:-

Usafiri wa kutumia bandari ni usafiri muhimu sana na ni wa lazima kwa watu wanaotoka Tanzania Bara kwenda Unguja na Pemba; na zipo kampuni zinazotoa huduma ya usafirishaji lakini hazitoshelezi katika kutoa huduma hiyo muhimu.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kununua meli ili kukidhi mahitaji ya usafirishaji wa watu wetu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba usafiri wa kutumia bandari ni usafiri muhimu sana na hutumiwa na watu wengi wanaoishi maeneo ya mwambao wa Bahari ya Hindi hususan wanaotoka Tanzania Bara kwenda Unguja na Pemba. Ni kweli pia kampuni zinazotoa huduma ya usafirishaji katika maeneo hayo hazitoshelezi katika kutoa huduma hiyo muhimu kulingana na uhitaji wa abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa mahitaji ya huduma za usafiri wa majini katika maeneo hayo kwetu ni fursa kwa sekta binafsi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kulitambua hilo Serikali imekuwa ikijenga mazingira wezeshi na kuihamasisha sekta binafsi kutoa huduma za usafiri kwa kutumia meli za kisasa kati ya wasafiri wanaotoka Tanzania Bara au kwingineko kwenda visiwa vya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla juhudi za Serikali zimekuwa zikilenga katika kuhakikisha kuwa wakazi wa maeneo ya mwambao na visiwa vya Unguja na Pemba wanapata huduma za usafiri kwa njia ya maji zilizo salama na hivyo kuwaepusha kutumia vyombo vya usafiri huo visivyokidhi matakwa katika kubeba abiria na mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uhamasishaji huo, kwa sasa kampuni ya meli ya Azam ilianza kutoa huduma ya usafiri baina ya Tanga, Unguja na Pemba kuanzia tarehe 29 Januari, 2017 kwa kutumia meli ya kisasa iitwayo *Azam Sealink 2.* Meli hii inatoa huduma kutokea Tanga kuelekea visiwa vya Unguja na Pemba mara moja kwa wiki. Aidha, kampuni hiyo iko tayari kuongeza safari baina ya Tanga, Unguja na Pemba kwa wiki mara itakapobainika kuwa abiria wanaosafiri katika maeneo hayo wameogezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaipongeza Kampuni ya Meli ya Azam kwa kuitikia wito wa kuanzisha huduma ya usafiri kwa njia ya maji baina ya Tanga, Unguja na Pemba na kuwataka wananchi kuepuka kutumia vyombo vya usafiri wa maji visivyokidhi matakwa katika kubeba abiria na mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kutumia nafasi hii kuendelea kutoa wito kwa wawekezaji wengine kama ilivyo kwa Kampuni ya Meli ya Azam kuwekeza katika vyombo vya kisasa vya usafiri kwa njia ya maji ili kutoa huduma ya usafiri katika maeneo ya mwambao ya Tanzania ikiwamo na Visiwa vya Unguja na Pemba. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mattar Salum swali la nyongeza.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi hii kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa baadhi ya majibu yake yamekuwa mazuri, lakini

katika majibu yake anasema kutokana na usafiri huu hautoshelezi, bado wananchi wetu wanapata taabu sana kupatikana usafiri huu wa kwenda Pemba. Wananchi wetu wanafika kulala bandarini kusubiri meli ya kwenda Pemba. Sasa ni kwa nini Serikali isitenge bajeti mahususi kwa ajili ya kununua meli ili iweze kufanya kazi hizi kuwahudumia wasafiri wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, bado usafiri huu ni ghali sana kwenda Zanzibar na kwingineko, sasa ni kwa nini Serikali isiingize mkono wake kuzisaidia kampuni hizi kwa wakati huu ili bei ya tiketi zishuke zisiwe hapa zilipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Maswasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama nilivyokiri katika swali la msingi kwamba usafiri wa majini kuelekea visiwa vya Pemba na Unguja hautoshelezi. Na ndiyo maana nikatoa wito kwa wawekezaji wengine wanaoweza kutoa huduma hizo wajitokeze kwa wingi washirikiane na Serikali katika kutoa huduma hiyo. Naamini watakapofanya hivyo matatizo yatapungua kwa kuwa ni kweli kabisa tunakiri kwamba bado kuna changamoto ya usafiri wa majini kwa ajili ya kutoka Dar es Salaam au Tanga kwenda visiwa vya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu gharama; kwanza kabisa, Serikali inazo meli mbili; kuna MV Maendeleo halafu MV Mapinduzi, zote zilinunuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, lakini bahati mbaya sasa hivi zipo kwenye matengenezo na marekebisho mbalimbali. Ninaamini zitakapokuwa katika hali yake ya kawaida zitasaidia katika kutoa huduma kwa wananchi wa visiwa vya Pemba na Unguja na bei itapungua. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed, Mbunge wa Mbarali sasa aulize swali lake.

Na. 16

**Ujenzi wa Barabara ya Rujewa – Mafinga**

**MHE. HAROON M. PIRMOHAMED** aliuliza:-

Barabara ya Rujewa – Madibira ni tegemeo na ni kiungo muhimu kati ya Rujewa – Madibira na Madibira – Mafinga na Serikali imekuwa ikitoa ahadi kwa muda mrefu kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami.

Je, ni lini sasa barabara hiyo itaanza kujengwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga yenye urefu wa kilometa 152.1 ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara nchini *(TANROADS).* Kazi ya usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami ilikamilika Agosti, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa sasa inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 kiasi cha shilingi bilioni 2.57 kilitengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara hii. Aidha, kwa sasa Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali barabara hii ili ipitike kirahisi kwa wakati wote wakati

inatafuta fedha za kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed swali la nyongeza.

**MHE. HAROON M. PIRMOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu lake Mheshimiwa Waziri amesema kazi ya usanifu pamoja na utayarishaji wa *tender documents* umefanyika tangu mwezi Agosti, 2012 sasa ni zaidi ya miaka mitano. Sasa nimuombe kwamba airuhusu Wizara yake itenge fedha kwa mwaka 2018/2019 kwa ajili ya kukamilisha barabara ya Rujewa – Madibira ili ujenzi wa lami ukamilike? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia, anafuatilia sana barabara hii. Nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti inayokuja tumetenga fedha za kutosha na kwamba ujenzi wa barabara hii utaanza.

Pia nikufahamishe Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Mbarali, pamoja na barabara hii pia iko barabara hii ya Igawa – Mbarali ambayo umekuwa ukiifuatilia; sehemu ya Mbarali – Ubaruku kilometa 8.9 nayo iko kwenye mpango katika mwaka unaofuata tutaijenga barabara hii. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza naipongeza Serikali kwa hatua kubwa inayochukua ya kutekeleza miradi ya barabara nchini.

Swali langu dogo, katika utaratibu wa awali nilijibiwa hapa Bungeni kwamba barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom mpaka Shinyanga iko katika hatua ya mwisho a kupatiwa fedha za usanifu kina.

Je, Serikali kwa mwaka huu wa fedha imetenga kiasi gani kwa ajili ya kufanya usanifu wa Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom mpaka Shinyanga kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, anaifuatilia sana hii barabara na anajua umuhimu wake. Barabara hii itakuwa kwa kweli ni dawa kwa ajili ya kusaidia uzalishaji katika eneo hili. Nafahamu hatua ile ya awali ya usanifu imekuwa ikiendelea, lakini katika mwaka huu wa fedha unaokuja tutaendelea na kuhakikisha kwamba utaratibu wa kukamilisha michoro na ujenzi wa barabara hii unaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wanaotoka maeneo ya Simiyu, Shinyanga na maeneo ya Arusha na Singida kwamba ule ukamilishaji wa ujenzi wa lile daraja pale Sibiti unaendelea. Vile vyuma vilivyokuwa vinasubiriwa kwa muda mrefu vilishafika, kwa hiyo sasa kipande kile tutaweza kupita wakati tunakamilisha hii hatua ya michoro na kuanza huu ujenzi. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, ile kasi ya kukamilisha kazi hii inaendelea vizuri, na kwamba hii barabara sasa iko kwenye hatua nzuri ya kuanza ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Kuchauka.

Na. 17

**Mgogoro wa Ardhi Kati ya Wananchi na SOMJI**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA (K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE)** aliuliza:-

Kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu sana unaohusu eneo lenye ukubwa wa ekari 357.5 Boko Dovya – Kawe – Kinondoni baina ya wananchi na watu wanaojitambulisha kuwa wamiliki halali wa eneo hilo maarufu kama SOMJI; wananchi katika hatua mbalimbali wamepeleka malalamiko Serikalini kuanzia ngazi ya Wilaya, Wizara ya Ardhi na hata kwa Waziri Mkuu lakini mpaka sasa hakuna utatuzi uliofanyika.

Je, hatua gani zimeanza kuchukuliwa ili kero hiyo ya muda mrefu imalizike?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi naomba kujibu swali namba 17 la Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali shamba hili lililokuwa na ukubwa wa ekari 366 Mbweni maarufu kama *Somji Farm* lilipimwa na upimaji namba E7/37F na kupewa namba ya upimaji 10,917 ya tarehe 15 Agosti, 1959. Baada ya upimaji shamba lilimilikishwa kwa Ndugu Hussein Somji pamoja na Ndugu Munaver Somji mwaka 1961 na baadae kuandaliwa hati iliyosajiliwa kwa namba 14,573 ya kipindi cha miaka 99.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya shamba hilo, ekari 5.8 zilitwaliwa kwa matumizi mahususi ya Serikali mwaka 1975 na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 670 la tarehe 30 Mei, 1975. Aidha, sehemu iliyobaki yenye ekari 357.5 ilitwaliwa na Serikali tena mwaka 2002 na kutangazwa

kwenye Gazeti la Serikali Namba 617 la tarehe 27, Septemba, 2002 kwa ajili ya kutumika katika mradi wa viwanja 20,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo eneo hilo halikuingizwa kwenye mradi kutokana na sehemu kubwa kuwa imevamiwa na wananchi. Pamoja na uvamizi huo, wamiliki wa awali walifungua mashauri mahakamani dhidi ya Serikali kupinga eneo lao kutwaliwa; shauri la Kikatiba namba moja la 2003 na shauri la Kikatiba namba 40 la 2010. Uwepo wa mashauri haya ulikwamisha juhudi za Serikali kushughulikia mgogoro huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni mara kadhaa imekaa na wahusika kwa lengo la kuweka utaratibu utakaowezesha wamiliki wa awali kulipwa fidia stahiki kwa fedha iliyopatikana kutokana na wanachi ambao watatakiwa kurasimishiwa maeneo waliyojenga.

Hata hivyo changamoto iliyopo ni katika kumilikisha makubaliano haya kwa wananchi kupitia kamati yao waliyounda, kutokuwa tayari kuchangia gharama za kurasimisha eneo hilo. Jitihada zaidi za wadau wengine akiwemo Mbunge zinahitajika katika kuwaelimisha wananchi kupitia Kamati yao kuwa tayari kushiriki katika upatikanaji wa ufumbuzi wa suala hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nataka kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya kuridhisha.

Lakini kwa niaba ya wananchi wa Dar es Salaam na hasa wa hili eneo la Kawe, huu mgogoro ni wa muda mrefu sana. Kama ambavyo Naibu Waziri anasema anataka kushirikisha sasa jamii kuona namna ya kuwapa fidia wale wamiliki wa mwanzo mimi naomba kwamba ushughulikiaji wa suala hili Mheshimiwa Naibu Waziri bado ni mdogo sana.

Sasa nataka tu nipate majibu ya uhakika kwamba Mheshimiwa Naibu Wziri unawahakikishia nini watu wa Kawe juu ya upatikanaji wa ardhi ili waweze kuondokana na adha hii ya upatikanaji wa ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tatizo hili la migogoro ya ardhi Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii alishawahi kutuletea taarifa Wabunge hapa Bungeni kwamba tuorodheshe migogoro mingi kwenye majimbo yetu, lakini asilimia kubwa ya migogoro ile bado haijashughulikiwa, nini kauli ya Serikali juu ya kushughulikia migogoro ya ardhi nchini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ameuliza tunawahakikishia nini wananchi hawa ili kuwapa maeneo mengine waweze kuwa na makazi. Nadhani kwenye jibu la msingi nimeeleza wazi, kwa sababu eneo lile walilivamia na kulikuwa na mashauri mahakamani na bado wananchi wale wakaonekana ni wavamizi. Hata hivyo kwa busara ya Serikali, kwa sababu tulishaona eneo lile limevamiwa kwa kiasi kikubwa, Wizara ikaamua kuwarasimishia, kwa hiyo walitakiwa kurasimishiwa ili waendelee kuwepo pale na wamiliki maeneo yale, lakini wale wananchi hawako tayari kurasimishiwa. Na tukumbuke eneo lile kisheria si la kwao, ni wavamizi na mahakama ilishatamka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama wao hawatakuwa tayari kwa zoezi ambalo Serikali imetaka kuwasaidia ili warasimishwe pale basi utaratibu mwingine Serikali haitasita kuchukua kwa sababu mahakama ilishatoa maamuzi na Serikali imeona iwasaidie kwa kuwarasimishia na wao wakae pale kihalali. Kwa hiyo, hatutakuwa na mpango mwingine nje ya pale waliponapo, kwa hiyo kama ni maeneo mengine itabidi wagharamie wenyewe kwenda kununua na waweze ku-*settle* kama ambavyo tunatoa viwanja kwa watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili anaongelea habari ya migogoro; ni kweli tuliorodhesha migogoro mingi na iliundwa Kamati ya Wizara zaidi ya tano na migogoro ile imekuwa ikishughulikiwa katika kila Wizara na migogoro ambayo ilikuwa inaelekea kule, lakini tayari kuna ushauri ambapo kuna kamati iliundwa kwa ajili ya kutoa ushauri wa namna ya kuwa na ufumbuzi wa kudumu wa migogoro ile na tayari Kamati ile ilishamaliza kazi yake, italetwa mtaona namna ambavyo tunakwenda kushughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa migogoro mingine yote ambayo ilikuwa ndani ya uwezo wa Wizara husika, moja wapo ikiwa ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Kilimo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Maliasili na Utalii; wote tumeshiriki pamoja na wenzetu ambao walikuwa wameandaliwa kufanya kazi hiyo.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Wizara inafanyia kazi na muda si mrefu mtapata ufumbuzi wa kudumu ambao umepangwa kwa ajili ya kuondokana na migogoro hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa muda tulio nao tutaendelea. Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza Mbunge wa Bukoba Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 18

**Kampuni ya Chai Maruku**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Kampuni ya Chai Maruku ilibinafsishwa kwa wawekezaji ili kuendeleza uzalishaji. Tangu kampuni hiyo imebinafsishwa, wakulima hawalipwi fedha za mauzo ya chai kwa wakati na wafanyakazi hawalipwi mishahara na stahiki zao ipasavyo.

Je, katika hali hiyo, kwa nini Serikali isivunje mkataba na mwekezaji na kurejesha umiliki Serikalini au kwa mwekezaji mwingine atakayejali maslahi ya wakulima na wafanyakazi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 2016 Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imekuwa ikifuatilia kwa karibu mwenendo wa utendaji na uendeshaji wa Kampuni ya Chai Maruku.

Ofisi ya Msajili wa Hazina inafanya vikao kwa nyakati tofauti kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Bodi ya Chai na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai kwa lengo la kutatua mgogoro uliokuwepo baina ya mwekezaji, wakulima pamoja na wafanyakazi wa kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vikao hivyo haki ya kila upande ilizingatiwa ikiwemo suala muhimu la haki za wafanyakazi pamoja na madai ya wakulima. Katika vikao vya mwezi Oktoba na Desemba, 2017 mwekezaji alikubali kulipa madai ya wakulima ya kiasi cha shilingi milioni 12. Aidha, majadiliano yanaendelea ili kutatua mgogoro wa madai ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sehemu kubwa ya mgogoro inaelekea kutatuliwa, Serikali haioni sababu ya kuvunja mkataba na mwekezaji kwa sasa. Hata hivyo, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu suala hili ili kuhakikisha kuwa haki za wakulima na wafanyakazi hazipotei.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jasson Rweikiza swali la nyongeza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nashukuru kwa majibu ya Serikali ambayo yametolewa, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Bukoba wanalima chai pamoja na mazao mengine. Wanajituma, wanaweka bidii kubwa sana kwa lengo la kukuza uchumi wao, uchumi wa familia zao na uchumi wa Taifa. Huyu mwekezaji kama jibu lilivyosema anawadhulumu wakulima hawa, hawalipi fedha zao, hawalipi haki zao; wakulima pamoja na wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamoja na majadiliano hayo ya mwezi Oktoba na mwezi Desemba mwaka jana, jibu linamalizia kwamba Serikali haioni saabu ya kuvunja mkataba. Kweli pamoja na dhuluma hii anayowafanyia mwekezaji huyu Serikali haioni sababu ya kuvunja naye mkataba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli inahimiza uchumi wa viwanda, lengo ni hilo hilo kuboresha ustawi wa Tanzania, kuongeza ajira na uchumi wa Taifa. Huyu anafanya kinyume na azma ya Serikali ya Awamu ya Tano, bado wanasema hawaoni sababu ya kuvunja mkataba, kweli hii ni sawa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitakuwa mtu wa mwisho kuona Watanzania wanadhulumiwa na mimi na Waziri wangu tukiwa ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango na ndiyo

maana katika jibu langu la msingi nimesema ameshafanya malipo yote na kwa sasa yuko *current* kwenye malipo ya wafanyakazi lakini pia malipo ya wakulima, anawalipa kila wanapomaliza kuuza chai yao anaendelea kuwalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kilichotokea huko nyuma, Kampuni hii ya *Spearshield Africa Company Limited* ilinunua hisa za asilimia 75 kwenye kiwanda hiki. Asilimia 25 zilitakiwa zinunuliwe na wakulima wenyewe hadi leo hii wakulima wameshindwa kununua hizi hisa asilimia 25 na uzalishaji wao ukawa si wa tija ndiyo maana mwekezaji akawa anazalisha chini ya ufanisi, akawa anashindwa kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwekezaji huyu pamoja na kwamba makubaliano ya awali ilikuwa baada ya kuchukua asilimia 25 aweze kuweka uwekezaji wa milioni 99 za Kitanzania, lakini kwa sababu ana nia thabiti mwekezaji huyu mpaka Desemba, 2016, tayari alishawekeza zaidi ya bilioni 3.8 kwenye ununuzi wa mitambo, kwenye kilimo na kuwawezesha wakulima kwenye ukulima bora wa mazao yao, kwa hiyo ana nia thabiti ya kufanya jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina sasa imempa maelekezo kwamba awe anatoa taarifa kila baada ya miezi miwili ya utendaji kazi wake, mahusiano yake na wakulima, lakini mahusiano yake na wafanyakazi, na ameanza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, naomba tumpe nafasi mwekezaji huyu, ameonesha dhamira ya kutosha, amewekeza kutoka milioni 999 zilizopo kwenye mkataba mpaka bilioni 3.8 , tumpe nafasi, ana nia thabiti atawawezesha ndugu zangu, wakwe zangu, shemeji zangu na wifi zangu wa Bukoba, kwa kiwanda hiki naamini watarejesha uchumi wao kama ilivyokuwa miaka ya 1960 na 1970.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tutamalizia swali letu la mwisho la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, Mbunge wa Kojani, sasa aulize swali lake.

Na. 19

**Zanzibar Kuwa na Uwakilishi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa Mabadiliko ya Kumi (10) ya Katiba ya Zanzibar yanaitambua Zanzibar kuwa ni nchi.

Je, ni lini Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itairuhusu Zanzibar kuwa na uwakilishi rasmi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, Mbunge wa Kojani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 2(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na mabadiliko yake imebainisha kuwa eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar na ni pamoja na sehemu yake ya bahari ambayo Tanzania inapakana nayo. Aidha, Jedwali la Kwanza kwenye Katiba hiyo limebainisha kuwa masuala ya mambo ya nje ni masula ya Muungano.

Kwa muktadha huo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo mwanachama katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa maslahi yote ya Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki yanazingatiwa ipasavyo. Kabla ya kushiriki katika Mikutano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kumekuwa na vikao vya maandalizi ambavyo hushirikisha pande zote mbili za Muungano ili kuandaa msimamo wa pamoja wenye kuzingatia maslahi ya pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hushiriki katika ngazi zote za Mikutano ya Wakuu wa Nchi Wanachama, Baraza la Mawaziri la Jumuiya na Mabaraza ya Mawaziri ya Kisekta yafuatayo:-

(a) Baraza la Mawaziri la Kisekta la Uwekezaji, Fedha, Viwanda na Biashara;

(b) Baraza la Mawaziri la Kisekta la Afya;

(c) Baraza la Mawaziri wa Kisekta la Uchumi, Mawasiliano na Hali ya Hewa;

(d) Baraza la Mawaziri la Kisekta la Elimu, Sayansi na Teknolojia, Utamaduni na Michezo;

(e) Baraza la Mawaziri la Kisekta la Jinsia, Vijana, Watoto na Maendeleo ya Jamii;

(f) Baraza la Mawaziri la Kisekta la Nishati;

(g) Baraza la Mawaziri la Kisekta la Kilimo na Usalama wa Chakula; na

(h) Baraza la Mawaziri la Kisekta la Amani na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mikutano hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hushiriki katika ngazi za wataalam, Makatibu Wakuu na Mawaziri. Aidha, kati ya Wabunge tisa wa Bunge la Afrika Mashariki, Wabunge watatu wanatokea Zanzibar. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, swali la nyongeza.

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, pamoja na kuwa Zanzibar ni mshirika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kuna mambo ambayo si ya Muungano kwa mfano kilimo, utalii, elimu ya msingi na sekondari, mifugo na mengineyo.

Je, kwa nini basi Zanzibar kama Zanzibar isiachiwe kujiwakilisha yenyewe katika masuala kama haya katika Jumuiya ya Afrika Mashariki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika ulimwengu huu kuna nchi ambazo zimeungana lakini zinaridhia baadhi yao kutoa mamlaka kushiriki katika mambo mbalimbali katika Jumuiya za Kikanda na Kitaifa. Kwa mfano, Switzerland kupitia tamko la Khartoum inaridhia baadhi ya nchi kushiriki katika masuala mbalimbali. Pia New Zealand kuna kisiwa cha Niue Island kinashiriki katika baadhi ya mambo. Pamoja na hayo kuna Umoja wa Visiwa vya Bahari ya Hindi ambayo Tanzania si mwanachama, kwa nini basi Zanzibar isiachiwe kujiunga na Jumuiya kama hii ikashiriki katika kufanikisha masuala yake? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ni kweli Serikali ya Zanzibar ina mamlaka katika sekta fulani za maendeleo kama vile kilimo, uchukuzi na kadhalika. Kutokana na makubaliano hayo chini ya Muungano mazao yatokanayo na uzalishaji ndani ya Zanzibar yanapata nafasi ya kuuzwa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuuza

ndani ya Afrika Mashariki Zanzibar inahakikishiwa soko la nafuu. Kwa hiyo, kile kinachozalishwa kule Zanzibar kinapata nafasi kwenye Jumuiya ambayo Zanzibar ni sehemu ya Serikali ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kama ilivyo katika Muungano wetu kuna mambo ambayo yanaainishwa ambayo ni ya Muungano na kuna mambo ambayo yameainishwa na kukubalika ambayo yako chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika nchi ambazo umetoa mifano nao wanakuwa na taratibu za mgao wa madaraka katika sekta mbalimbali. Sisi katika Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania tumeainisha na kukubaliana kwamba masuala ambayo yatakuwa chini ya Muungano ni kama kwa mfano Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Mambo ya Ndani na Mawasiliano ya Kimataifa. Haya inategemea na jinsi nchi ambazo zimeungana zinavyokubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna maeneo ambayo Tanzania inatakiwa kushiriki na labda bado hatujashiriki hilo ni suala ambalo linaweza kuzungumzwa na kuainishwa ndani ya Bunge hili. Kwa sasa hivi hapo tulipo Muungano wetu unakidhi kabisa katika nafasi yake ndani ya Jumuiya ya Kimataifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Nitaleta matangazo kwenu yaliyoifikia meza. Tangazo la kwanza linahusu wageni waliopo Bungeni siku ya leo. Tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Mheshimiwa Spika.

Kundi la kwanza ni wageni 143 wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni viongozi kutoka Ofisi yake, yaani Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Makatibu Wakuu, Ndugu Maimuna Tarishi - Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu na Bunge; Profesa Faustine Kamuzora - Katibu Mkuu, Sera na Uratibu na Ndugu Eric Shitindi - Katibu Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu. *(Makofi)*

Wengine ni wakuu wa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu yaani Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu na tutaanza na Mheshimiwa Jaji Francis Mutungi Msajili wa Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Jaji Mutungi naona umeona makofi ya Bunge zima hapa, nadhani yanaashiria jambo, ahsante sana. *(Makofi)*

Mwingine ni Dkt. Leonard Maboko - Mwenyekiti Mtendaji wa *TACAIDS;* Ndugu Ramadhan Kailima - Mkurugenzi wa Uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Nadhani haya makofi yanaashiria jambo.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**NAIBU SPIKA:** Ndugu Edwin Kakolaki - Kaimu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya; Ndugu Beng'i Issa - Katibu Mtendaji, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Dkt. Samwel Nyantahe - Mwenyekiti wa *LESCO*; Ndugu Irene Isaka - Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii na Mifuko ya Jamii *(SSRA);* Profesa Godius Kahyarara - Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* na Ndugu Masha Mshomba - Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Wellington Chibebe - Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* Ofisi ya Afrika Mashariki; Ndugu Hilda Kabisa - Kamishna wa Kazi; Ndugu Shanes Nungu - Kaimu Mkurugenzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi; Ndugu Khadija Mwenda - Mtendaji Mkuu wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA);* Ndugu Novatus Massao - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Tija la Taifa *(NIP);* Ndugu Boniface Chandaruba - Kaimu Mtendaji Mkuu wa *TaESA*. *(Makofi)*

Pia wako viongozi wa vyama vya wafanyakazi na waajiri ambao ni Dkt. Aggrey Mlimuka - Mkurugenzi Mtendaji

wa Chama cha Waajiri Tanzania *(ATE);* Ndugu Tumaini Nyamhokya - Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA);* Ndugu Qambos Sulle - Makamu wa Rais *TUCTA;* Ndugu Yahya Msigwa - Katibu Mkuu *TUCTA* na Ndugu Johannes Majura - Naibu Katibu Mkuu - *TUCTA.* Pia wameambatana na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali za Ofisi ya Waziri Mkuu.

Wageni wengine ni Ndugu Fadhili Liwaka ambaye ni Msaidizi wa Waziri Mkuu na Ndugu Kasambe Hokororo ambaye ni Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM Wilaya ya Ruangwa. *(Makofi)*

Karibuni sana wageni wetu mliotoka Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Kundi la pili ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wanne wa Mheshimiwa Ester Mmasi ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya KCMC wakiongozwa na Ndugu Majaliwa John ambaye ni Rais wa Serikali ya Wanafunzi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 28 wa Mheshimiwa Oscar Mukasa, huyu ni Mbunge wa Biharamulo ambao ni Viongozi wa Vikundi vya Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) kutoka Wilayani Mbozi, Mkoani Mbeya. Wageni hawa wameambatana na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Mheshimiwa Erick Ambakisye - Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi na Mheshimiwa Allan Mgulla - Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi.

Kundi la mwisho ni wageni watano wa Mheshimiwa Zacharia Issaay ambayo ni walimu kutoka Mbulu, Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni watatu ambao ni wakazi wa *Area D,* Mkoani Dododma, wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake. Karibuni sana wageni kutoka *Area D* na tunawakaribisha wageni wote mliotutembelea siku ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mazoezi rasmi ya michezo mbalimbali yataanza kesho tarehe 5 Aprili, 2018. Makocha na *captains* wa michezo mbalimbali watasimamia mazoezi hayo ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya ushiriki wetu katika mashindano ya Mabunge ya Afrika Mashariki yatakayofanyika mwishoni mwa mwaka huu nchini Uganda. Aidha, kwenye Mkutano huu wa Bunge kutafanyika matukio makubwa ya michezo na burudani kama ifuatavyo hapa mjini Dodoma:-

(i) Mpambano pendwa wa Wabunge wanachama na wapenzi wa Simba na Yanga kwa timu za soka na *netball. (Makofi)*

(ii) Mechi za kujipima nguvu kati ya *Bunge Sports Club* na timu mbalimbali.

(iii) *Bunge Sports Club* kwa kushirikiana na uongozi wa Bunge itaratibu burudani ya muziki ili kuwaburudisha Waheshimiwa Wabunge kwenye Mkutano huu wa miezi mitatu.

(iv) Kutakuwa na mechi ya kirafiki kati ya *Bunge Sports Club* na *EALA*. *(Makofi)*

Kipekee *Bunge Sports Club* inawashukuru sana wadhamini wake waliotuchangia vifaa vya michezo kwenye mashindano ya Mabunge ya *EALA* yaliyofanyika mwezi Desemba, 2017. Wadhamini hao ni pamoja na Mheshimiwa Abood Aziz *(Abood Bus Service);* Mheshimiwa Salum, ameandikwa hapa kwa jina lake maarufu, Mheshimiwa Salum Salum, huyu anaitwa Mheshimiwa Salum Mbuzi wa *Jambo Products; ASAS* Iringa na wengine wengi. *(Makofi)*

Michezo ni furaha, michezo ni afya, tuendelee kushiriki kwa pamoja. Amesaini Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club*. *(Makofi)*

Mwenyekiti nilijua hili tangazo linahusisha zile zawadi za watu walioletea Bunge medali, sasa naona hapo zimekosekana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa ratiba yetu tuliyonayo leo na kwa sababu hizi nyaraka wote mnazo ni wazi mnajua tutasikia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa utaratibu wetu, Kamati zinazoisimamia Wizara hii zitapata fursa ya kutoa maoni yao.

Pia asubuhi mwakilishi wa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani aliweka mbele hati ya kuonyesha kwamba hotuba yao itakuwepo.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika tarehe 19 Aprili, 2017 alitoa maelekezo kulingana na Kanuni ya 99(5) inayozungumzia muda wa kuleta taarifa hapa Bungeni. Kwa sababu ya changamoto zilizowahi kutokea siku za nyuma za taarifa kusomwa hapa zikiwa hazijaifikia Meza lakini pia Waheshimiwa Wabunge wakiwa hawana, Mheshimiwa Spika alitoa Waraka huo kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ni Mnadhimu wa Serikali lakini pia kwa Mheshimiwa Tundu Lissu ambaye ni Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Kwa waraka ule alioutoa Mheshimiwa Spika, alitoa utaratibu ambao nitawasomea ili twende wote vizuri. Mheshimiwa Spika alitoa utaratibu ufuatao:-

(i) Nyaraka zote zitakazowekwa kwenye Orodha ya Shughuli kwa ajili ya kuwasilishwa Mezani zitatakiwa kuwa Mezani kabla mwasilishaji hajaitwa kwa ajili hiyo vinginevyo hati hiyo haitaweza kusomwa. *(Makofi)*

(ii) Ili kutimiza masharti ya Kanuni ya 99(5) na kuleta ufanisi katika maandalizi ya Orodha ya Shughuli za Vikao kuanzia wakati huo Mheshimiwa Spika alipotoa agizo hili yaani kuanzia tarehe 19 Aprili, 2017, nyaraka hizo ziwasilishwe kwa Katibu wa Bunge jioni, siku moja kabla ya siku ambayo hoja husika imepangwa kuwasilishwa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo hayo, nyaraka nilizonazo hapa mbele ni hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na hotuba tatu za Kamati zinazohusu Wizara hii. Kwa maana hiyo, hotuba ya Waziri Mkuu haitakuwa na hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kutokana na Waraka huu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu, Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI zilizochambua bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2017/2018 na mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2018/2019. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizopo chini yake pamoja na Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena kujadili taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2017/2018 na mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutokana na fikra na uongozi wao makini katika ujenzi wa Taifa letu. Ni dhahiri kuwa juhudi zao katika kuongoza na kusimamia utekelezaji wa mipango ya Serikali zitaleta manufaa makubwa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumewapata Waheshimiwa Wabunge wapya kutokana na chaguzi ndogo zilizofanyika. Nitumie fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Mbunge wa Jimbo la Siha na Mheshimiwa Maulid Mtulia, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni kwa kuchaguliwa na kisha kuapishwa na Bunge lako Tukufu ili waendelee kuwatumikia wananchi wa majimbo yao na Watanzania kwa ujumla. Ni matumaini yangu kuwa Bunge lako Tukufu litaendelea kuwapatia ushirikiano wa kutosha ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018, Bunge lako lilimpoteza aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini, Mheshimiwa Leonidas T. Gama. Vilevile baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na wananchi tunaowawakilisha walipata misiba ya ndugu, jamaa na marafiki. Aidha, kulitokea maafa na majanga ambayo yalisababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Pia kumekuwepo na ajali za barabarani ikiwemo ajali mbaya iliyotokea tarehe 24 Machi, 2018 Wilayani Mkuranga na kugharimu maisha ya Watanzania 26. Naomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema waliopata majeraha. Aidha, natoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki kwa misiba iliyotokea. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa salamu za pole kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliopata majeraha mbalimbali kufuatia ajali ya gari tarehe 29 Machi, 2018 walipokuwa wakitoka Dodoma kuelekea Dar es

Salaam. Wabunge hao ni Mheshimiwa Haji Ameir Haji, Mbunge wa Makunduchi; Mheshimiwa Khamis Ali Vuai, Mbunge wa Mkwajuni; Mheshimiwa Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mbunge wa Chwaka; Mheshimiwa Makame Mashaka Foum, Mbunge wa Kijini na Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu. Tuzidi kumuomba Mwenyezi Mungu awajalie afya wenzetu hawa ili waweze tena kuungana nasi kutekeleza majukumu yao katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi kubwa ya kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kipekee niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI inayoongozwa na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini. Kamati hizo zimetoa mchango mkubwa wakati wa maandalizi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge.

Aidha, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuaminika na kuchaguliwa kuongoza Kamati hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Idara, Mashirika, Wakala na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na Taasisi zake kwa kutekeleza majukumu yao na kukamilisha kuandaa bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu; Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Mbunge wa Dodoma Mjini na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu; Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, Mbunge Viti Maalum na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu; Makatibu Wakuu Bibi Maimuna K. Tarishi; Profesa Faustin R. Kamuzora na Bwana Eric F. Shitindi; Wakurugenzi wote, Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na wafanyakazi wote kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana pia kuwashukuru washirika wa maendeleo zikiwemo nchi marafiki, taasisi na mashirika ya kimataifa, madhehebu ya dini na mashirika yasiyo ya kiserikali, kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali katika kujenga uchumi wa viwanda na kuiletea nchi maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kuniunga mkono na niwapongeze kwa kutekeleza shughuli za maendeleo jimboni kwa ufanisi wakati mimi Mbunge wao nikitekeleza majukumu ya kusimamia utendaji wa Serikali. Kipekee namshukuru sana mwenza wangu mpendwa Mary Majaliwa na familia yangu kwa upendo wao, uvumilivu na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ya kitaifa. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2018/2019 ni kuboresha utendaji wa Serikali na kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2018/2019. Aidha, mpango na bajeti umezingatia azma ya Serikali ya kufikia malengo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano ambao umepangwa kuhitimishwa mwaka 2020 mpaka 2021 ukiwa na dhima kuu ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea ukuaji uchumi na maendeleo ya watu. Vilevile mpango huu umezingatia azma ya kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya

mwaka 2025 lakini pia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 na utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizozitoa wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2015 pamoja na utekelezaji wa hotuba yake wakati akizindua Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa tunaingia kwenye Bunge la tatu la bajeti kwa Serikali ya Awamu ya Tano, hatuwezi kumsahau Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kutimiza ndoto na matarajio ya Watanzania kwa kujenga nchi yenye uchumi imara. Katika kipindi hiki, tumeshuhudia mambo makubwa aliyoyafanya yakiwemo kujenga ari ya uzalendo kwa kuilinda na kuisemea nchi yetu bila woga; kudumisha amani, utulivu na mshikamano; kuimarisha ulinzi na usalama kwa kukomesha vitendo vya mauaji yaliyojitokeza Mwanza, Amboni (Tanga), Mkuranga, Kibiti na Rufiji mkoani Pwani pamoja na kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine alizofanya Mheshimiwa Rais ni kujenga nidhamu ndani ya utumishi wa umma na kukemea uzembe; kuendesha vita dhidi ya rushwa na ufisadi kwenye taasisi za umma; kuanzisha mahakama ya rushwa na ufisadi; kuimarisha ulinzi wa rasilimali za nchi zikiwemo za madini na maliasili. Aidha, amefufua Shirika la Ndege la Tanzania na ndege nyingine ya tatu imeingia juzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ameanzisha ujenzi wa reli ya kisasa ya kiwango cha kimataifa; ameendeleza na ujenzi wa barabara zikiwemo barabara za juu *(flyovers)* na amenunua meli na vivuko kwenye mito na bahari zetu. Kazi nyingine ni ujenzi wa vyanzo vipya vya umeme kama vile *Stiegler's Gorge,* usambazaji wa umeme hadi vijijini na ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima-Uganda hadi Tanga-Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine makubwa aliyoyafanya ni kuimarisha huduma za afya hususan upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaatiba katika vituo vya kutolea huduma za afya; ujenzi wa vituo vya afya kote nchini; kutoa elimu ya msingi bila malipo kwa watoto wa Kitanzania; ujenzi wa miradi ya maji na kuimarisha bei za mazao ya kibiashara. Aidha, Mheshimiwa Rais ametimiza ndoto ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya kuhamishia Makao Makuu ya Serikali mjini Dodoma. Haya ni baadhi tu ya mambo aliyoyafanya na yatatolewa ufafanuzi wa kutosha kabisa kupitia Wizara za kisekta zitakapowasilisha bajeti zake huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi tatu Barani Afrika ambazo uchumi wake unakua kwa kasi na viashiria vya kiuchumi vinaonesha kuwa katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba, 2017 uchumi ulikua kwa asilimia 6.8, kiwango ambacho kilikuwa juu zaidi ikilinganishwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo uchumi wa Kenya ulikua kwa asilimia 6.1; Rwanda asilimia 6; Uganda asilimia 5.5; Burundi asilimia 0.0 na Sudan Kusini asilimia hasi 6.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, takwimu za hivi karibuni kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu zinaonesha kwamba katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba, 2017 pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha asilimia 7.1 ikilinganishwa na asilimia 7 ya mwaka 2016. Shughuli zilizochangia ukuaji huo kwa viwango vikubwa ni pamoja na uchimbaji wa madini na mawe asilimia 17.5; huduma za usambazaji maji safi na majitaka kwa asilimia 16.7; uchukuzi na uhifadhi wa mizigo asilimia 16.6; habari na mawasiliano asilimia 14.7 na ujenzi asilimia 14.1. Aidha, sekta ya kilimo, misitu na uvuvi ilikua kwa asilimia 3.6, kiwango ambacho hakijawahi kufikiwa tangu mwaka 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia Desemba, 2017 Deni la Taifa lilikuwa Dola za Marekani milioni 25,419.6. Viashiria vyote vya deni vinaonesha kuwa deni linahimilika kwani thamani ya deni la nje kwa pato la Taifa ni asilimia 19.7;

kwenye kitabu ni asilimia 19 lakini naomba isomeke asilimia 19.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40. Thamani ya deni la nje kwa uuzaji wa bidhaa za nje ni asilimia 81.8 na hiyo kwenye vitabu vyenu isomeke asilimia 81.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 150 na thamani ya deni la nje kwa mapato ya ndani ni asilimia 117.1; kwa hiyo kwenye vitabu vyenu isomeke 117 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 200 na kwenye vitabu tuliandika 250, kwa hiyo, isomeke 200.

Kwa kuzingatia vigezo hivyo, bado tuna uwezo wa kuendelea kukopa kutoka ndani na nje ili kugharamia shughuli za maendeleo. Kwa ujumla viashiria vya kuimarika kwa uchumi vinatoa mwelekeo mzuri wa kufikiwa kwa malengo yetu ya kuwa nchi ya kipato cha kati inayoongozwa na uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka 26 sasa imepita tangu mfumo wa siasa wa vyama vingi uanzishwe nchini. Katika kipindi hicho tumeona ushiriki wa Watanzania katika siasa ukiendelea kuongezeka na uhuru wa kujiunga na vyama vya siasa kwa kuridhishwa na itikadi za vyama hivyo pia ukiongezeka. Ni vyema tukajenga utamaduni wa kuheshimu wananchi pale wanapoamua kujiunga na chama cha siasa watakachokipenda. Jukumu letu kama viongozi wa siasa ni kunadi sera zetu kwa wananchi na kuhamasisha ujenzi wa demokrasia inayolenga kuleta maendeleo kwa wananchi wote bila ubaguzi wa aina yoyote pamoja na kudumisha amani, utulivu, mshikamano na kujenga umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, kumefanyika chaguzi ndogo za Wabunge katika Majimbo matano na Madiwani katika Kata 59 kwa ajili ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi kutokana na sababu mbalimbali. Chaguzi hizi zilisimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa ufanisi mkubwa. Katika chaguzi ndogo za Ubunge zilizofanyika katika Majimbo ya Songea Mjini, Singida Kaskazini, Longido, Kinondoni na Siha, Chama cha Mapinduzi (CCM) kilishinda majimbo yote. Vilevile katika uchaguzi wa Madiwani, CCM ilishinda katika Kata 58 na CHADEMA ilishinda

katika kata moja. Nichukue nafasi hii kuvipongeza vyama vyote vya siasa vilivyoshiriki katika chaguzi hizo na kipekee nakipongeza Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kupata ushindi mkubwa na wa kishindo katika maeneo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Msajili imeendelea kuhakikisha kuwa demokrasia ya vyama vingi vya siasa inaimarika. Katika mwaka 2017/2018 Ofisi ya Msajili iliratibu kikao cha Baraza la Vyama vya Siasa ambacho pamoja na kufanya uchaguzi wa viongozi wa Kamati za Baraza hilo, kilijadili mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria mpya ya Vyama vya Siasa na marekebisho ya Kanuni za Usajili wa Vyama vya Siasa. Vilevile Ofisi ya Msajili inaendelea kukusanya maoni ya wadau kwa lengo la kuandaa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 pamoja na Kanuni zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 kumefanyika vikao mbalimbali vya kisekta vya ushirikiano kati ya Wizara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali za Muungano wetu. Baadhi ya changamoto hizo ni masuala ya fedha, biashara na ajira katika taasisi za Muungano. Katika kipindi hicho viongozi na wataalam wa pande mbili za Muungano walikutana kwa ajili ya kujadili hoja zinazohusu sekta za fedha, biashara, viwanda na uwekezaji, ujenzi na uchukuzi, maliasili na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza zoezi la kuhamishia shughuli za Serikali Kuu hapa Dodoma. Tangu utekelezaji wa zoezi hilo uanze Septemba, 2016 jumla ya watumishi wa umma 3,829 kutoka Wizara na taasisi mbalimbali wamehamia Dodoma katika awamu ya kwanza na ya pili na awamu ya tatu inaendelea. Katika kufanikisha azma hii, Serikali inaboresha miundombinu ya barabara, reli, uwanja wa ndege, umeme, mifumo ya maji safi na maji taka. Ofisi pia zinaendelezwa, makazi na kuimarisha huduma za elimu, afya, mawasiliano na michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga kuijenga Dodoma kuwa mji bora na wa kisasa unaoendana na mahitaji na mifumo ya miji bora duniani. Ili kufikia azma hiyo, Serikali inashirikiana na wadau ikiwemo sekta binafsi na Mashirika ya Kimataifa kuujenga Mji wa Dodoma. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye mara tu baada ya kuhamia Dodoma amezindua Kampeni ya Kijanisha Dodoma inayolenga kuifanya Dodoma kuwa ya kijani. Kampeni hiyo inahusisha kuendeleza, kutunza na kuhifadhi maeneo ya ukanda wa kijani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niupongeze pia Umoja wa Mataifa na Mashirika yake kwa kufungua Ofisi zake za muda Mjini Dodoma mwezi Desemba, 2017. Natoa wito kwa mashirika mengine ya kimataifa na mabalozi waige mfano huu wa kuhamishia Ofisi zao Dodoma. Serikali itaendelea kutoa ushirikiano wa karibu kwa Mashirika ya Kimataifa na wanadiplomasia katika kurahisisha maandalizi yao ya kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, natoa wito kwa wawekezaji wa ndani na nje kuendelea kuwekeza Dodoma kwani kuna fursa nyingi za uwekezaji ikizingatiwa nafasi yake kijiografia inayosaidia mikoa yote hapa nchini kufikika kwa urahisi na haraka zaidi.

Nichukue fursa hii kuipongeza Kamati inayoratibu zoezi la Serikali kuhamia Dodoma inayosimamiwa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama (Mbunge), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Bibi Maimuna K. Tarishi, Katibu Mkuu (Waziri Mkuu na Bunge). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mipango mbalimbali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuunga mkono jitihada zinazofanywa na wananchi kujiletea maendeleo. Moja ya jitihada zilizofanywa na Serikali ni kuanzisha mifuko ya uwezeshaji ambayo inatoa mikopo kupitia vikundi vya vijana, wanawake, wazee, watu wenye ulemavu na makundi mengine yenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ulidhamini mikopo yenye thamani ya takribani shilingi bilioni 13 kwa *SACCOS* 58, *VICOBA* 172 na kampuni mbili. Aidha, Mfuko wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi umetoa mikopo ya shilingi bilioni 62.8 kwa wajasiriamali 85,982; Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.4 kwa vikundi 5,169 katika Halmashauri 153; Mfuko wa Kilimo Kwanza ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 62.7 kwa miradi 189 katika Wilaya 76.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Vijana umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 783 ambapo vijana 840 kutoka Halmashauri mbalimbali walinufaika. Aidha, katika kipindi hicho, Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia asilimia tano ya mapato yao ya ndani zilitengwa shilingi bilioni 15 ikiwa ni mikopo ya masharti nafuu kwa vijana. Vilevile Halmashauri 48 zilitenga ekari 217,882 kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali kwa vijana kote nchini. Katika mwaka 2018/ 2019 Serikali itaendelea kuwawezesha vijana kiuchumi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali inaratibu jumla ya mifuko na programu 31 za uwezeshaji ambazo usimamizi wake upo katika taasisi mbalimbali za Serikali na za binafsi. Kila mfuko au programu imeanzishwa kwa sheria yake au taratibu maalum zinazosimamia utendaji wa mfuko husika. Serikali imeona kuna umuhimu wa kupunguza idadi ya mifuko kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji wake ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Hivyo tumeanza kufanya mapitio ya utendaji wa mifuko hiyo kwa nia ya kuunganisha baadhi ya mifuko yenye majukumu yanayofanana. Hatua hiyo itasaidia kuwa na mifuko michache yenye tija ambayo itaharakisha kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kukuza ujuzi wa nguvukazi tuliyonayo ni miongoni mwa ajenda muhimu ya kisera katika kuwezesha wananchi kujikwamua kiuchumi. Serikali inatoa msukumo wa kipekee kupitia Programu ya

Ukuzaji Ujuzi nchini kwa lengo la kuwapatia ujuzi na stadi za kazi wananchi hasa kundi la vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ili waweze kumudu ushindani katika soko la ajira na hivyo kuwawezesha kushiriki katika ujenzi wa uchumi jumuishi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti uliofanywa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi mwaka 2014 unaonesha kuwa asilimia 79.9 ya nguvukazi ni yenye kiwango cha chini cha ujuzi, asilimia 16.6 kiwango cha kati wakati ni asilimia 3.6 tu ndiyo yenye kiwango cha juu. Ili kufikia uchumi wa viwanda, Serikali imedhamiria kubadili mwenendo huo kwa kuhakikisha nguvukazi yenye kiwango cha juu cha ujuzi inafika asilimia 12 na kiwango cha kati asilimia 34. Kwa msingi huo, Serikali inaendelea kutekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi pamoja na programu nyingine ili kukidhi matakwa ya uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 jumla ya vijana 7,817 wamewezeshwa kupata ujuzi kupitia programu hiyo. Kati yao, vijana 220 walipata mafunzo kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na vijana 3,440 kupitia Taasisi ya Don Bosco. Mafunzo waliyopewa ni katika fani za ufundi stadi wa ushonaji nguo, useremala, uashi, TEHAMA, uchongaji wa vipuri, ufundi magari, umeme, bomba, vyuma, terazo, vigae na ujuzi wa kutengeneza bidhaa za ngozi. Aidha, kupitia VETA vijana 3,989 walipata mafunzo ya kurasimisha ujuzi uliopatikana kwa mfumo usio rasmi kwa fani za uashi, useremala, ufundi magari, upishi na uhudumu katika hoteli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya vitendo yalitolewa pia kwa wahitimu 168 kupitia viwanda na kampuni mbalimbali katika fani ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi. Vilevile Serikali imeandaa na kuzindua Mwongozo wa Kitaifa wa Uanagenzi na Mwongozo wa Kitaifa wa Mafunzo ya Vitendo kwa wahitimu kwa lengo la kuweka utaratibu wa utoaji wa mafunzo hayo kwa wadau wote ili waweze kuajirika. Katika mwaka 2018/2019 Serikali itatoa mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri na stadi za kazi kwa vijana 10,500

katika fani mbalimbali. Ninazishukuru kampuni binafsi ambazo zinaendelea kutoa nafasi za mafunzo ya vitendo kwa wahitimu wetu. Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika nyanja mbalimbali ili tuweze kukuza ujuzi wa rasilimali watu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 Serikali imeendelea kuratibu juhudi za kukuza ajira nchini. Hadi kufikia Februari 2018 jumla ya ajira 482,601 katika sekta rasmi zimezalishwa nchini kwetu. Kati ya ajira hizo, ajira 345,547 sawa na asilimia 72 zimezalishwa kutokana na shughuli za umma ikiwemo miradi ya maendeleo ya Serikali kama vile ujenzi wa reli ya kisasa, ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na miradi ya *TASAF* na ajira 137,054 sawa na asilimia 28 zimezalishwa katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaandaa mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba Watanzania wazawa wanashiriki na kunufaika na miradi mikubwa ya kitaifa. Vikao kati ya Serikali na wafanyabiashara vimefanyika ili kuwaandaa kuwa sehemu ya utekelezaji wa mkakati huo. Katika mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kuratibu masuala ya ukuzaji ajira nchini ikiwa ni pamoja na kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Ajira ili iendane na mahitaji ya sasa ya soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kwamba kunakuwepo tija, ufanisi na mahusiano mema mahali pa kazi, Serikali inasimamia Sheria Na. 6 ya Ajira na Mahusiano Kazini na Sheria Na.7 ya Taasisi za Kazi. Sheria hizo zinalenga kuhakikisha kunakuwa na haki na wajibu kwa wafanyakazi na mwajiri vilevile kwamba vyote vinapatikana. Ili kufikia azma hiyo, Serikali imehimiza kuanzishwa kwa mabaraza ya wafanyakazi, kufunga mikataba ya hali bora pamoja na kufanya kaguzi mbalimbali mahali pa kazi ili kujiridhisha kuwa viwango vya kazi vinazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018 jumla ya kaguzi 102,860 zimefanyika katika maeneo mbalimbali ya kazi nchi nzima. Sambamba na

kaguzi hizo, elimu kuhusu sheria za kazi, wajibu na majukumu ya wajumbe wa baraza kwa waajiri na wafanyakazi kupitia vyama vyao ilitolewa. Jumla ya waajiri 640 na wafanyakazi 3,624 walipatiwa elimu hiyo. Aidha, mabaraza 441 ya wafanyakazi yaliundwa na 46 yalihuishwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ilipokea na kusajili migogoro ya kikazi 6,113 ambapo migogoro 4,816 sawa na asilimia 79, ilitatuliwa kwa njia ya usuluhishi na uamuzi. Katika mwaka 2017/2018, utafiti kuhusu sekta na vyanzo vinavyoongoza kwa migogoro ya kikazi umefanyika. Sekta ya usafirishaji iliongoza kwa kuwa na migogoro 547; ulinzi binafsi 512; viwanda 434; elimu 420; huduma za hoteli 399 na taasisi za umma 321. Aidha, aina ya vyanzo vinavyoongoza kusababisha migogoro ya kazi ni kuachishwa kazi bila kufuata taratibu sahihi; madai mbalimbali na kuvunjwa kwa mikataba isivyokuwa halali. Utafiti huu utaisaidia Serikali kwa kushirikiana na waajiri na vyama vya wafanyakazi kuweka mipango ya pamoja na kuzuia migogoro sehemu za kazi kabla haijatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi na kuendeleza mijadala yenye tija ili kupunguza migogoro mahali pa kazi. Serikali pia itaendelea kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ikiwa ni pamoja na kufanya kaguzi, kusajili, kusuluhisha na kuamua migogoro katika maeneo ya kazi. Aidha, itashirikiana kwa karibu na vyama vya wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kufanya majadiliano ya mara kwa mara kwa lengo la kuongeza tija na kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua mchango wa sekta binafsi katika kukuza uchumi wa Taifa letu. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na kuanzisha na kuboresha miundombinu wezeshi kama vile reli, barabara, umeme na maji. Hatua nyingine ni kupunguza na kufuta baadhi ya kodi zinazoathiri ufanisi wa sekta binafsi; kuhuisha sera na sheria na kuimarisha

majadiliano yenye manufaa baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018, jumla ya miradi 175 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 4.4 ilisajiliwa kupitia Kituo cha Uwekezaji nchini *(TIC).* Miradi hiyo inatarajiwa kutoa fursa za ajira 20,178.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa nia ya kuondoa changamoto zinazokwamisha maendeleo ya sekta binafsi. Katika mwaka 2017/2018 Serikali imefanya mikutano minne na wawakilishi wa sekta binafsi. Miongoni mwa mikutano hiyo, ni ule uliofanyika tarehe 19 Machi, 2018 ambao uliongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo kwa Wizara na Taasisi za umma kukutana na wawakilishi wa sekta binafsi ili kutatua kwa haraka changamoto zilizobainishwa katika mkutano huo. Serikali inawahakikishia wafanyabiashara na sekta binafsi kwamba inawathamini na itaendelea kushirikiana nao kutatua changamoto zinazowakabili ili kujenga uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 Serikali imeendelea kuimarisha na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii ikiwemo kutungwa kwa sheria inayounganisha Mifuko ya Pensheni ya *PSPF, LAPF, PPF na GEPF* na kuunda mfuko mmoja kwa ajili ya watumishi wa umma unaojulikana kama Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma. Sheria hiyo pia, imefanya marekebisho kwenye Sheria ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii ili kuufanya Mfuko huo uhudumie wafanyakazi wa sekta binafsi pamoja na kutoa huduma ya hifadhi ya jamii katika sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutungwa kwa sheria hiyo kutasaidia kuondoa changamoto iliyotokana na wingi wa mifuko ya hifadhi ya jamii inayolipa mafao yanayotofautiana kwa watumishi wa umma wenye masharti ya kazi yanayofanana. Vilevile sheria hiyo itasaidia kupunguza changamoto ya baadhi ya mifuko kutokuwa endelevu

kutokana na idadi ndogo ya wanachama lakini pia ushindani usiokuwa na tija na gharama kubwa za uendeshaji. Sheria imeweka kipindi cha mpito cha miezi sita kitakachoanza tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hiyo. Lengo ni kuwezesha maandalizi ya utekelezaji wake kufanyika pasipo kuathiri shughuli na huduma muhimu kwa wanachama wa mifuko iliyounganishwa ikiwa ni pamoja na kupokea mafao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwataarifu Watanzania kupitia Bunge hili kwamba tayari Mheshimiwa Rais amesaini Muswada huo kuwa sheria ya nchi. Utekelezaji wa sheria hii utaboresha mafao ya wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2018/2019 Serikali itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003 na hivyo kuandaa Sera ya Taifa ya Kinga ya Jamii ambayo itakuwa jumuishi. Lengo la Serikali ni kuwezesha huduma za hifadhi ya jamii kuwafikia wananchi wengi zaidi hususan waliopo katika sekta isiyo rasmi na kurahisisha upatikanaji wa huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuimarisha uratibu na utekelezaji wa Sheria Na. 9 ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010, kwa kuhakikisha upatikanaji wa haki na fursa kwa watu wenye ulemavu. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imeunda Kamati za watu wenye ulemavu katika Mikoa 12 ya Geita, Kagera, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Njombe, Pwani, Singida, Rukwa, Shinyanga, Simiyu na Tabora. Ufuatiliaji unaendelea kufanyika ili kuhakikisha kuwa mikoa mingine nayo inaunda Kamati hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa vifaa saidizi kwa jamii ya watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kufanya shughuli zao bila utegemezi. Baadhi ya vifaa vilivyotolewa ni viti mwendo 240, bajaji sita, magongo ya kutembelea 350, kofia pana 128, fimbo nyeupe 175, miwani maalum kwa wenye uoni hafifu 70, shime sikio 20, vyerehani nane, vifaa vya kukuzia maandishi 65, mafuta maalum ya kukinga ngozi dhidi ya mionzi ya jua

35, viti maalum vya kuogea 50 na nyenzo nyingine za kujimudu. Vilevile, Serikali imeendelea kuviboresha vyuo vya watu wenye ulemavu vya Yombo, Dar es Salaam na Sabasaba, Mkoani Singida. Serikali pia inakamilisha uanzishwaji wa kanzidata ya wahitimu wenye ulemavu kutoka vyuo mbalimbali nchini ili iwe rahisi kuwaunganisha na fursa za ajira zinazopatikana kwenye sekta binafsi na umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto kwa kutoa elimu ya ulinzi na usalama kwa watoa huduma katika vituo vinavyolea watoto wenye ulemavu wa ngozi kwenye Mikoa ya Shinyanga, Mara, Tabora, Simiyu, Tanga, Mwanza, Kigoma na Singida. Lengo la utoaji elimu ni kuwajengea uelewa na kuwapa mbinu watoa huduma waendelee kuimarisha ulinzi kwa watoto pamoja na kuwahimiza wazazi, walezi na jamii waone umuhimu wa kulea watoto hao kwenye ngazi ya familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kukamilisha uanzishwaji wa Mfuko wa Taifa wa Maendeleo wa Watu Wenye Ulemavu. Serikali pia itaendelea na zoezi la kuanzisha madawati ya watu wenye ulemavu na kuhamasisha sekta binafsi na umma kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu. Aidha, Serikali inahimiza waajiri wote nchini kuajiri watu wenye ulemavu wenye sifa kwenye nafasi mbalimbali na pia kutoa matangazo ya ajira yanayohamasisha wenye ulemavu kuomba nafasi zinazotangazwa. Vilevile itahamasisha na kuelimisha jamii kuhusu mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu ikiwemo kuwaheshimu, kuwatambua, kuwathamini na kutowanyanyapaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya uzalishaji na naanza na sekta ya kilimo hasa hali ya upatikanaji wa chakula. Hali ya uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya chakula nchini imeendelea kuimarika. Katika msimu wa 2016/2017 na 2017/2018, uzalishaji ulifikia tani milioni 15.9

ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 13.3 ya chakula kwa kipindi hicho. Kutokana na uzalishaji huo, nchi ilikuwa na ziada ya tani milioni 2.6 za mazao yote ya chakula na hivyo kujitosheleza kwa asilimia 120 ya mahitaji ya chakula nchini. Aidha, hadi kufikia Januari, 2018 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ulikuwa umenunua jumla ya tani 26,038 za mahindi na akiba ya chakula iliyopo ghalani ni tani 92,074. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeamua kuweka mkazo maalum wa kuyaendeleza kwa kasi mazao matano ya biashara ambayo ni chai, kahawa, korosho, pamba na tumbaku. Lengo ni kuongeza mapato ya wakulima, kuwa chanzo cha kuaminika cha malighafi katika uchumi wa viwanda na kuendelea kuwa chanzo kikuu cha ajira na fedha za kigeni vilevile. Uamuzi wa kuongeza usimamizi katika uzalishaji wa mazao hayo makuu ya biashara unatokana na ukweli kwamba kwa kipindi kirefu uzalishaji ulishuka kutokana na changamoto kadhaa. Miongoni mwa changamoto hizo ni kupungua tija katika uzalishaji, baadhi ya wakulima kuacha kulima mazao hayo kutokana na kukata tamaa kwa sababu mbalimbali zikiwemo vyama vya ushirika kutotekeleza vyema wajibu wao kulikuwa na wizi, dhuluma na pia ushiriki mdogo wa maafisa kilimo katika kusimamia kilimo cha kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine za kushuka uzalishaji wa mazao hayo ni huduma zisizoridhisha za ugani na utafiti, ukosefu wa pembejeo bora, utitiri wa tozo na wingi wa vyama vya msingi na vyama vikuu vya ushirika. Kwa mfano, uzalishaji wa zao la pamba ulipungua kutoka tani 456,814 mwaka 2013/2014 hadi tani 282,809 mwaka 2015/2016. Kwa upande wa tumbaku, uzalishaji katika kipindi cha miaka minne ulishuka kutoka tani 126,624 mwaka 2010/2011 hadi kufikia tani 60,929 mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua za kuimarisha utawala bora kwenye vyama vya ushirika kwa kusimamia chaguzi za vyama 2,537, chaguzi za viongozi wa bodi na vyama vya ushirika 532 na kufanya kaguzi katika

vyama vya ushirika 2,896 vikiwemo vyama vikuu. Kazi za kusimamia vyama vya ushirika zinaendelea. Pamoja na hatua hiyo, Serikali inasimamia uendelezaji wa mazao hayo moja kwa moja kupitia maafisa kilimo na Bodi za Mazao. Hatua nyingine ni kufuta baadhi ya tozo zilizokuwa kero katika mazao makuu ya biashara pamoja na kuhakikisha kwamba mauzo yanafanyika kwa njia ya wazi na inayoleta ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hatua zinazochukuliwa na Serikali kusimamia mazao makuu ya biashara tayari tumeanza kuona matokeo chanya kwa kuongezeka uzalishaji wake. Kwa mfano, hadi mwezi Machi, 2018 uzalishaji wa mazao ya asili ya biashara ulifikia tani 804,025. Uzalishaji huu unaashiria ongezeko la mavuno ikilinganishwa na mwaka 2016/2017. Ongezeko hilo la uzalishaji wa mazao ya biashara linakwenda sambamba na kuimarika kwa mwenendo wa bei za mazao hayo hususani korosho na kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kuimarisha vyama vya msingi vya ushirika vya mazao ya kilimo na masoko vinavyozalisha mazao ya kimkakati ya biashara ya pamba, kahawa, korosho, chai na tumbaku. Serikali inalenga kuimarisha masoko ya mazao hayo kwa kuhamasisha mfumo wa stakabadhi ghalani ambapo mazao hayo yatazalishwa na kuuzwa kupitia vyama vya ushirika kwa njia ya minada. Pamoja na hatua hizo, soko la bidhaa ambalo limeshaanzishwa litasaidia sana kuimarisha masoko ya mazao kwani yatakuwa yanauzwa kwa njia ya ushindani mkubwa huku wakulima wanaozalisha kwa ubora wakinufaika kwa bei ya juu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imerahisisha upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima baada ya kuanza kuagiza mbolea kwa kutumia mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja. Hadi kufikia Machi, 2018 upatikanaji wa mbolea hapa nchini ulikuwa tani 310,674 sawa na asilimia 64 ya mahitaji yote ya tani 485,000 kwa mwaka. Kwa upande wa mbegu bora za kilimo, upatikanaji umefikia tani 51,700 sawa

na asilimia 86.2 ya mahitaji ya tani 60,000 kwa mwaka. Kwa mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kuboresha mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja ili uendelee kuleta fanisi na tija iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 Serikali imekamilisha maandalizi ya awamu ya pili ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Programu hiyo itatekelezwa kwa miaka 10 katika vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Katika mwaka 2018/2019 Serikali itaweka mkazo katika kutekeleza malengo makuu ya programu hiyo. Msukumo utawekwa kwenye kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo ya kipaumbele kwa kuimarisha upatikanaji na matumizi ya pembejeo na zana za kilimo; kuimarisha huduma za ugani; kuimarisha kilimo cha umwagiliaji; kuimarisha huduma za utafiti na mazao ya kilimo na kuhakikisha matokeo ya utafiti yanawafikia wakulima; kuweka na kusimamia mipango ya matumizi bora ya ardhi ya kilimo; kuimarisha usindikaji wa mazao ya kilimo na kuwezesha upatikanaji wa masoko ya mazao haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tumeamua kwa dhati kabisa kusimamia kwa karibu sekta ya kilimo ambayo ndiyo inaajiri Watanzania wengi. Tutahakikisha kuwa mkulima ananufaika na kilimo chake kwa kuwafikishia wakulima pembejeo ikiwemo mbolea na mbegu bora kwa wakati; kuimarisha miundombinu ya kilimo na kuimarisha usimamizi wa vyama vya ushirika. Pia Serikali itatoa kipaumbele katika kufungamanisha sekta ya kilimo na viwanda kwa lengo la kuongeza thamani na faida kwenye shughuli za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba mifugo bora na ya kisasa ni fursa kubwa ya kupunguza umaskini hapa nchini. Hata hivyo, ili mifugo hiyo iweze kuleta matokeo makubwa, hususan upatikanaji wa soko la uhakika ndani na nje ya nchi, hapana budi mifugo itambuliwe bayana. Kutokana na mahitaji hayo ya utambuzi, Serikali inatekeleza zoezi la utambuzi wa mifugo kwa njia ya chapa

ya moto ambapo hadi Februari 2018, ng'ombe 16,408,022 wamepigwa chapa. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 94.4 ya ng'ombe 17,390,090 waliotegemewa kupigwa chapa. Zoezi hili ni endelevu na ninawaomba wadau watoe ushirikiano wa kutosha kwa Serikali ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa sekta ya maliasili na utalii katika ukuaji wa Pato la Taifa na kuongeza ajira, Serikali inaongeza juhudi za kulinda rasilimali za Taifa ikiwemo misitu, wanyamapori, malikale, ufugaji nyuki, uvuvi, pamoja na kuhakikisha rasilimali hizo zinanufaisha vizazi vya sasa na vijavyo. Serikali pia imechukua hatua za kuimarisha mifumo ya kukusanya mapato katika sekta hizo, kupambana na ujangili, kuzuia upotevu wa mazao ya misitu na kutatua migogoro ya mipaka kati ya vijiji na hifadhi. Katika mwaka 2017/2018 Serikali imeanza mapitio ya Sera za Taifa za Utalii, Misitu na Ufugaji Nyuki ili ziendane na mazingira ya sasa na kuimarisha zaidi ulinzi wa rasilimali hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na juhudi zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha sekta ya utalii, idadi ya watalii walioingia nchini mwaka 2017 imeongezeka hadi kufikia watalii milioni 1.33 ikilinganishwa na watalii milioni 1.28 mwaka 2016. Pia mapato yameongezeka na kufikia Dola za Marekani bilioni 2.19 mwaka 2017 ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 2.13 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia sita. Takwimu hizo zinabainisha kwamba sekta ya utalii ina fursa kubwa ya kulipatia Taifa fedha za kigeni na kuzalisha ajira kwa wingi. Tutaendelea kuimarisha sekta hii kwa kuvutia wawekezaji zaidi na kuimarisha miundombinu ya maeneo ya utalii pamoja na kuhamasisha utalii wa ndani, utalii wa mambo ya kale na kihistoria katika miji ya zamani ikiwemo Bagamoyo, Kilwa na Mikindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunatambua kwamba kaulimbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kujenga uchumi wa Taifa unaotegemea viwanda. Hadi kufikia Februari, 2018 viwanda vipya 3,306 vimeanzishwa. Aidha, Serikali inahamasisha uwekezaji katika viwanda kwa kutoa vivutio vya kodi na visivyo vya kodi kwa wawekezaji mahiri;

kuendeleza na kuboresha miundombinu wezeshi kama vile barabara, reli, bandari, umeme na maji. Pia kuhuisha sera, sheria na kanuni pamoja na kufuatilia utendaji wa viwanda vilivyobinafsishwa na kuchukua hatua stahiki kwa wamiliki walioenda kinyume na mikataba ya mauzo. Vilevile Mikoa na Halmashauri zote nchini zimeelekezwa kutenga maeneo ya uwekezaji wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya hifadhi ya jamii inashiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi wa viwanda ambapo pamoja na miradi mingine *NSSF* na *PPF* kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza wanatekeleza mradi mkubwa wa uzalishaji wa sukari mkoani Morogoro. Lengo la mradi huo ni kuzalisha tani 250,000 za sukari na umeme megawati 40. Mradi huo unatekelezwa katika shamba la Mkulazi lililopo Ngerengere lenye ukubwa wa hekta 63,000 na shamba la gereza la Mbigiri lenye ukubwa wa ekari 12,000 lililopo Dakawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa ekari 2,000 za mashamba ya miwa zimetayarishwa katika eneo la Mkulazi na ekari 1,100 zimepandwa miwa pale Mbigiri. Lengo la Serikali ni kukamilisha awamu ya kwanza ya ufungaji wa mitambo ya kiwanda cha Mbigiri ifikapo mwezi Desemba, 2018 ili uzalishaji uanze mwaka 2019. Taratibu zote zimefikiwa na kwa sasa tunasubiri mzabuni kufunga mitambo. Miradi hii itakapokamilika itazalisha zaidi ya ajira 100,000.

Aidha, tangu kuanza kwa utekelezaji wa mradi huu mwezi Juni, 2017 ajira za moja kwa moja 780 na ajira zisizo za moja kwa moja 24,000 ikijumuisha wakulima wadogo wa mbegu na kilimo cha nje zimezalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2018/2019 Serikali itatoa kipaumbele katika kutekeleza miradi ya kielelezo, uanzishwaji wa kanda maalum za kiuchumi pamoja na kuboresha mazingira ya biashara na kuvutia uwekezaji katika sekta ya viwanda. Vilevile Serikali itaweka msisitizo katika kubuni mikakati ya uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vidogo na vya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeimarisha usimamizi katika sekta ya madini ili kuiwezesha sekta hiyo kuchangia kikamilifu katika uchumi wa nchi lakini pia kuongeza mapato ya Serikali na kuzalisha ajira. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kukusanya taarifa za uzalishaji wa madini, kuimarisha ukaguzi wa uzalishaji na mauzo kwenye migodi mikubwa na midogo na kufuatilia ukusanyaji wa maduhuli. Zoezi la ukaguzi limewezesha kukamatwa kwa madini yaliyokuwa yakitoroshwa yenye thamani ya Dola za Marekani takribani 898,523 na shilingi milioni 557.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018 maduhuli ya Serikali yaliyokusanywa kutoka sekta ya madini yalifikia shilingi bilioni 180.4. Pamoja na mambo mengine mafanikio hayo yametokana na usimamizi makini katika sekta ya madini na uamuzi wa Serikali kufungua soko la Tanzanite nchini. Aidha, Serikali imeimarisha soko la madini nchini kwa kuhakikisha kuwa madini yanauzwa kwa ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba tarehe 20 Septemba 2017 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alielekeza ujengwe ukuta katika eneo linalozunguka mgodi wa Tanzanite uliopo Mererani ili kuimarisha ulinzi na kudhibiti utoroshaji wa madini hayo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa ukuta huo wenye mzunguko wa kilometa 24.5 umekamilika. Nitumie fursa hii, kuwapongeza viongozi na watendaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kukamilisha kazi hiyo kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kujenga uwezo wa wazawa ili washiriki kikamilifu katika sekta ya madini. Uwezeshaji huo utakwenda pamoja na utoaji mafunzo kwa wachimbaji wadogo kuhusu teknolojia mbadala ya uchenjuaji dhahabu kwa lengo la kupunguza athari za mazingira na maafa katika maeneo ya migodi. Aidha, Serikali itakamilisha taratibu za kumpata mwekezaji atakayejenga mitambo ya kuchenjua madini nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa rasilimali ya ardhi kama kitovu cha uzalishaji mali, Serikali inachuka hatua madhubuti za kuiendeleza. Hatua hizo ni pamoja na kutekeleza Mpango Kabambe wa Majiji, Manispaa na Miji; udhibiti wa migogoro baina ya watumiaji wa ardhi na uimarishaji wa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi nchini. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Mipango Kabambe ya Manispaa za Iringa, Singida na Mji wa Kibaha imekamilika na mipango mingine 20 ipo katika hatua mbalimbali za uandaaji. Hadi sasa, michoro 1,110 ya mipango miji iliidhinishwa kati ya 1,148 iliyopokelewa kutoka Halmashauri za Miji mbalimbali. Natoa wito kwa wananchi wote nchini wanapofanya shughuli za maendeleo kuzingatia mipango kabambe inayoandaliwa na Mamlaka za Upangaji Miji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua kadhaa za kukabiliana na changamoto ya migogoro ya ardhi miongoni mwa watumiaji ikiwemo migogoro ya mipaka ya vijiji, wakulima na wafugaji, wanavijiji na hifadhi na mapori ya akiba. Moja ya hatua zilizochukuliwa ni kuunda timu ya kisekta ya kushughulikia migogoro ya ardhi ambayo imetembelea Mikoa ya Geita, Kagera, Katavi, Morogoro na Tabora na kufanya majadiliano na wadau 1,106. Hatua mbalimbali za utatuzi wa migogoro ya ardhi zinaendelea kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua thabiti kuhakikisha kunakuwepo na umeme wa kutosha na wa uhakika kwa ajili ya uchumi wa viwanda. Hatua zilizochukuliwa zinalenga kuongeza uzalishaji, kuboresha miundombinu ya usafirishaji wa umeme na kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme vijijini na mijini. Katika mwaka 2017/2018, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mikubwa ya Kinyerezi I (megawati 185), Kinyerezi II (megawati 240) na tayari umeshazinduliwa jana na Mradi wa Umeme wa Maji wa Mto Rufiji *(Stiegler's Gorge)* utakaozalisha megawati 2,100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imepanua na kuboresha miundombinu ya kusafirisha umeme kwa

kutekeleza miradi mbalimbali. Miradi hiyo ni pamoja na: Mradi wa Rufiji - Chalinze - Dodoma wenye msongo wa kilovoti 400; Mradi wa Singida – Arusha – Namanga wenye msongo wa kilovoti 400; na Mradi wa Makambako – Songea wenye msongo wa kilovoti 220. Kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara sasa inaunganishwa pia na mtambo wa gesi wa Somanga ili kupunguza tatizo la umeme kwenye Mikoa hiyo ya Kusini. Utekelezaji wa miradi hii umeongeza hali ya upatikanaji umeme nchini kufikia asilimia 67.5. Aidha, uunganishaji umeme kwa watumiaji umefikia asilimia 49.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza awamu ya tatu ya Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini *(REA)* ambao umepangwa kufikisha huduma ya umeme kwenye vijiji 7,873 ambavyo havijapata umeme nchini. Kati ya hivyo, vijiji 7,697 vimepangwa kupatiwa umeme wa Gridi ya Taifa na vijiji 176 pamoja na visiwa vitapatiwa umeme nje ya gridi kwani ndiyo njia muafaka ya kuvipatia umeme kwa sasa. Katika mwaka 2018/2019 Serikali itaongeza fedha za Mfuko wa *REA* ili kuhakikisha vijiji vilivyosalia pamoja na taasisi zinazotoa huduma za kijamii vijijini zinapata umeme. Umeme huu utawekwa katika nyumba zote bila kujali uimara wa nyumba yenyewe. Serikali pia, itaendeleza miradi ya kuunganisha Gridi ya Taifa na gridi za nchi jirani za Zambia, Kenya, Burundi na Rwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 5 Agosti, 2017 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Rais wa Jamhuri ya Uganda, Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni waliweka Jiwe la Msingi la Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi bandari ya Tanga. Uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa mradi huo kwa upande wa Uganda ulifanyika katika eneo la Hoima tarehe 11 Novemba, 2017. Bomba hilo la kusafirisha mafuta ghafi litakuwa na urefu wa kilometa 1,445 ambapo kilometa 1,115 zitajengwa Tanzania. Mradi huo utakuwa na manufaa kwa wananchi wa pande zote mbili ambapo ajira takribani 10,000 zitazalishwa wakati wa ujenzi na ajira zaidi ya 1,000 wakati wa uendeshaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuboresha mtandao wa barabara nchini. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018 ujenzi wa kilometa 776.45 za barabara kuu kwa kiwango cha lami umekamilika na kilometa 1,760 zinaendelea kujengwa. Aidha, barabara zenye urefu wa kilometa 17,054 zimekarabatiwa katika kipindi hicho. Vilevile ujenzi wa madaraja ya Kilombero na Kavuu umekamilika na ujenzi wa madaraja ya Sibiti, Mto Mara, Lukuledi, Ruhuhu, Momba na Mlalakuwa unaendelea. Madaraja mengine 996 katika maeneo mbalimbali nchini yamekarabatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Hadi kufikia Februari 2018, ujenzi wa barabara ya juu katika eneo la *TAZARA* ulifikia asilimia 70 na ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Ubungo *(Ubungo Interchange)* umeanza. Aidha, maandalizi ya Awamu ya Pili hadi ya Nne ya Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka yanaendelea. Katika mwaka 2018/2019 Serikali imepanga kujenga kilometa 597 za barabara kuu na za mikoa kwa kiwango cha lami na kilometa 72 za kiwango cha lami zitakarabatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(Tanzania Rural and Urban Roads Agency – TARURA)* kwa lengo la kurahisisha huduma za usafirishaji na kuongeza kasi ya wananchi kujiletea maendeleo. *TARURA* imepewa jukumu la kusimamia ujenzi na matengenezo ya mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometa 108,946.2 za vijijini na mijini.

Katika mwaka 2017/2018 *TARURA* imesimamia matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa 4,183.3, madaraja 35, makalavati makubwa 43 na madogo 364 na *drift* nne. Napenda kutumia nafasi hii kutoa wito kwa *TARURA* kuwaelimisha wananchi, viongozi na watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu majukumu na mfumo wa utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa *(Standard Gauge)* itakayokuwa na urefu wa kilometa 1,219. Hadi sasa ujenzi wa kipande cha kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro chenye kilometa 300 umeanza na unatarajiwa kukamilika Novemba, 2019.

Aidha, tarehe 14 Machi, 2018, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa kipande cha kutoka Morogoro hadi Makutupora chenye urefu wa kilometa 442. Ujenzi wa reli hii utasaidia kukuza sekta nyingine za kiuchumi kama vile kilimo, viwanda, madini, utalii pamoja na kutoa fursa nyingi za ajira. Utekelezaji wa mradi huu unakadiriwa kutoa ajira 30,000 za moja kwa moja na nyingine 600,000 zisizo za moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 Serikali imeendelea kuboresha Bandari ya Dar es Salaam ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafiri wa majini. Uboreshaji huo utaanza na Gati Na. 1 – 7; kuongeza kina na upana wa lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli; kuimarisha mtandao wa reli bandarini pamoja na kujenga gati maalum la kuhudumia meli za magari.

Vilevile Mamlaka ya Bandari Tanzania imefungua ofisi katika baadhi ya nchi jirani kwa lengo la kuongeza urahisi wa kutoa huduma. Katika mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea na uboreshaji wa Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara hata zile za maziwa na mito.

Aidha, Serikali itatekeleza Mradi wa Dirisha Moja la Forodha *(Tanzania Electronic Single Window System - eSWS)* ili kuwaweka pamoja wadau wote wa kuondosha shehena bandarini na mipakani. Kukamilika kwa mradi huo, kutarahisisha na kupunguza muda na gharama za utoaji na upitishaji wa shehena bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 Serikali imeendelea kutekeleza Awamu ya Tatu ya Mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa mtandao wa miundombinu ya itifaki *(Internet Protocol – Multiplier Label Switching)* pamoja na ujenzi wa kituo cha kuhifadhia *data* ambacho hadi sasa mifumo ya taasisi 27 imeunganishwa ukiwemo mfumo wa ukusanyaji mapato wa *TRA*. Kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho kutaongeza usalama, usiri wa *data*, kujikinga na majanga na kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali na miundombinu ya mifumo katika Kituo cha *Data* cha Taifa na vituo vingine vitakavyojengwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya kufikisha huduma ya mawasiliano vijijini ambapo vijiji 1,921 vimepatiwa huduma hiyo. Aidha, Serikali imeimarisha huduma za simu na intaneti katika taasisi za umma ikiwemo shule, vituo vya afya, vituo vya polisi na ofisi za posta. Katika mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kupanua matumizi yake hadi katika ngazi ya Wilaya. Vilevile, kuendelea kusimamia kampuni za simu nchini ili ziweze kutoa kumbukumbu sahihi kwa lengo la kukokotoa mapato yatokanayo na malipo ya huduma za simu za kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetekeleza kwa mafanikio mpango wa utoaji wa elimu ya awali na elimumsingi bila malipo. Tangu kuanza kwa mpango huo, Serikali imekuwa inapeleka kwa wakati na moja kwa moja shuleni fedha zote za ruzuku ya elimumsingi. Kiasi cha shilingi bilioni 20.8 kinapelekwa kila mwezi kwa shule zote za msingi na sekondari nchini, ikijumuisha fedha za posho maalum kwa Walimu Wakuu, Waratibu wa Elimu Kata na Wakuu wa Shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji mzuri wa mpango wa elimumsingi bila malipo umechangia kuimarika kwa mahudhurio ya wanafunzi darasani; kuongezeka kwa ubora wa elimu inayotolewa shuleni kutokana na kuboreshwa kwa mazingira ya kujifunzia na kufundishia na kuongezeka

kwa udahili wa wanafunzi. Kwa mfano, idadi ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza imeongezeka kutoka 1,568,378 mwaka 2015 hadi 2,120,667 mwaka 2016; sawa na ongezeko la asilimia 35.2. Kwa mwaka huu, idadi ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza ni 2,078,379. Vilevile wanafunzi waliofaulu mtihani wa kuhitimu darasa la saba na kujiunga na kidato cha kwanza imeongezeka kutoka wanafunzi 448,826 mwaka 2015 hadi wanafunzi 538,826 mwaka 2016 na mwaka 2017 wanafunzi 562,695 wamechaguliwa kuingia sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 Serikali imejenga na kukarabati miundombinu ya shule za msingi na sekondari ikiwemo ukarabati wa shule za sekondari kongwe 89 ili kuboresha mazingira ya shule na kuinua ubora wa elimu. Aidha, Serikali imenunua na kusambaza vifaa vya maabara vyenye thamani ya shilingi bilioni 16.9 kwa shule za sekondari 1,696 kwa ajili ya kuimarisha ujifunzaji wa masomo ya sayansi kwa nadharia na vitendo. Vilevile, walimu 3,347 wa masomo ya sayansi na hisabati na mafundi sanifu wa maabara 386 wameajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kutoa kipaumbele kwenye elimu, imeleta hamasa kubwa kwa wananchi kuchangia maendeleo ya elimu. Napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa wananchi na wadau mbalimbali kuendelea kuchangia kwa hiari maendeleo ya elimu kupitia Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Aidha, naziagiza Halmashauri zote nchini kuratibu na kusimamia ipasavyo michango ya hiari ya elimu inayotolewa na wananchi na matumizi yake hususan kwa kuanzisha Mfuko Maalum wa Elimu katika Halmashauri husika ambao utasimamiwa na Bodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka shilingi bilioni 365 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 483 mwaka 2017. Hatua hiyo imewezesha idadi ya wanaonufaika na mikopo hiyo nayo pia kuongezeka kutoka wanafunzi 98,300 mwaka 2015 hadi wanafunzi 119,435 mwaka 2017/2018. Serikali pia

inaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya vyuo vya elimu nchini ili kuboresha mazingira ya vyuo hivyo na kuviwezesha kuzalisha wataalam mahiri wanaoweza kujiajiri au kuajiriwa katika soko la ajira. Natoa wito kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na vyuo vya elimu ya juu na wadau wa elimu kufanya tathmini na kuboresha mfumo wa ufundishaji wa wanafunzi wa elimu ya juu nchini ili kuwapatia mbinu zitakazowawezesha kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu wa mwaka 2017 hadi 2021 pamoja na mpango kazi wake unaolenga kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Utekelezaji wa mpango huo wa sekta ya elimu utasaidia kuongeza idadi ya wataalam wenye ujuzi wa kati na wa juu ifikapo mwaka 2021. Katika mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kutekeleza awamu ya pili ya ukarabati wa shule kongwe, kujenga ofisi za udhibiti ubora katika Wilaya mbalimbali nchini, kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya shule za sekondari na kujenga vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa maji kwa wananchi waishio vijijini kwa kujenga, kupanua na kukarabati miradi ya maji. Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya miradi 71 imekamilishwa vijijini na mingine 366 inaendelea kutekelezwa na utekelezaji wa miradi hiyo umewezesha kuongezeka idadi ya wananchi wanaopata maji vijijini. Pia Serikali imepanga kubadilisha mitambo inayotumia nishati ya dizeli kusukuma maji na kufunga mitambo inayotumia nishati ya jua ili kuwapunguzia wananchi gharama za uendeshaji na matengenezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2018/2019 Serikali itakamilisha ujenzi wa miradi ya maji 387 kwenye Halmashauri mbalimbali nchini na kukuza miradi mipya ya maji vijijini; kutekeleza miradi ya maji vijijini katika maeneo

kame na yenye shida kubwa ya maji; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa mabwawa pamoja na upanuzi wa miundombinu ya maji kutoka kwenye mabwawa na visima vilivyochimbwa. Vilevile Serikali itaendelea na ujenzi wa miradi mikubwa ya maji katika maeneo ya Tabora, Kigoma na Same - Mwanga- Korogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Machi, 2018, Serikali imejenga, kupanua na kukarabati miradi ya maji katika maeneo mbalimbali mijini ili kufikia malengo yaliyowekwa. Juhudi hizo zimewezesha hali ya upatikanaji wa maji kwenye miji mikuu ya mikoa kufikia wastani wa asilimia 78. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam na maeneo yanayohudumiwa na *DAWASA*, upatikanaji wa maji umefikia asilimia 75. Aidha, upatikanaji wa maji katika miji mikuu ya wilaya, miji midogo na maeneo yanayohudumiwa na miradi ya kitaifa umefikia asilimia 60. Katika mwaka 2018/2019 sekta itaendelea kukamilisha miradi mingi ya maji iliyopo na kuweza kuleta huduma hii bora ya maji kwenye maeneo tajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasimamia shughuli za utoaji wa chanjo nchini ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyowekwa kitaifa na kimataifa yanafikiwa. Hadi sasa Tanzania imefikia kiwango cha juu cha asilimia 97 ya utoaji wa chanjo ya *pentavalent* kwa watoto inayokinga magonjwa ya kifaduro, dondakoo, pepopunda, homa ya ini na mafua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kufikia kiwango hicho mwezi Desemba, 2017 Serikali ya Tanzania ilipongezwa na Shirika la Afya Duniani kwa hatua hiyo kubwa. Lengo la Shirika la Afya Duniani ni kila nchi kufikia kiwango cha uchanjaji wa asilimia 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio hayo yamefikiwa kutokana na usimamizi madhubuti wa Serikali katika utoaji wa chanjo. Niwapongeze sana viongozi na watendaji wa Wizara ya Afya pamoja na mamlaka zote zinazohamasisha na kutoa huduma za chanjo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaatiba katika vituo vya kutolea huduma za afya. Bajeti kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa dawa, chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi imeongezwa kutoka shilingi bilioni 252 mwaka 2016/2017 na kufikia shilingi bilioni 269 mwaka 2017/2018. Kutokana na ongezeko hilo upatikanaji wa aina 135 ya dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini umeimarika na kufikia asilimia 89.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeboresha na kuimarisha upatikanaji wa huduma za matibabu ya kibingwa nchini. Huduma zilizoimarishwa ni pamoja na upandikizaji wa figo na vifaa vya kuongeza usikivu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, upasuaji kwa kutumia tundu dogo na kufungua kifua katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete. Vilevile Serikali imeimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* ambapo dawa zinapatikana na muda wa kupata huduma ya mionzi ya saratani umepungua. Kutokana na maboresho hayo, idadi ya wagonjwa waliopewa rufaa ya matibabu nje ya nchi imepungua kutoka wagonjwa 304 mwaka 2016/2017 na kufikia 103 mwaka 2017/2018; hatua hiyo imesaidia kupunguza gharama kubwa ambazo Serikali ingetumia kuwapeleka wagonjwa hao nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya mipaka ya nchi yetu ni salama. Katika mwaka 2017/2018 Serikali imeendelea kuimarisha Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kutoa mafunzo ya mazoezi ya kijeshi, kulipatia vifaa, zana, mitambo bora na ya kisasa pamoja na kuweka na kuimarisha miundombinu muhimu na ya kimkakati ili kuliwezesha jeshi kutekeleza jukumu lake la ulinzi wa mipaka ya nchi yetu. Vilevile Serikali imeweka alama za mipakani ili kuimarisha ulinzi na kulinda vema mipaka ya nchi.

Aidha, Jeshi la Wananchi linashirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, mamlaka za kiraia na mataifa mengine kupambana na matishio mapya ya kiusalama yakiwemo ugaidi, uharamia, uhamiaji haramu, biashara

haramu na dawa za kulevya na usafirishaji haramu wa binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu limeendelea kudumisha ushirikiano na nchi nyingine duniani kupitia mafunzo ya pamoja na *operation* za kikanda na kimataifa chini ya Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. Katika kutekeleza majukumu ya ulinzi wa amani, tarehe 7 Desemba, 2017 nchi yetu ilipoteza askari 15 huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo katika mashambulizi mabaya zaidi kuwahi kutokea kwa askari wetu wanaolinda amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine naomba kuungana na Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kuzipa pole familia za mashujaa hawa waliokuwa wakitekeleza majukumu yao ya ulinzi wa amani. Licha ya changamoto zinazojitokeza, Tanzania itaendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika kutekeleza majukumu ya ulinzi wa amani kwenye nchi mbalimbali duniani ili kuendelea kuifanya dunia kuwa mahala salama pa kuishi pamoja na kuyaongezea majeshi yetu uzoefu na mbinu za kisasa za ulinzi wa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa usalama wa raia, Serikali imelipatia Jeshi la Polisi vitendea kazi muhimu ikiwemo vifaa vya kisasa vya mawasiliano na uchunguzi ili liweze kupambana na majambazi na matukio mengine ya kihalifu nchini. Aidha, imejenga Kituo cha Kisasa cha Mawasiliano *(Call Centre)* Dar es Salaam ambacho kinawezesha wananchi kutoa taarifa ya matukio hayo kwa urahisi. Pia Serikali imehamasisha jamii kushiriki katika ulinzi wao na kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kwa lengo la kuwapatia taarifa za wahalifu na uhalifu. Natoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola ili kudhibiti matukio ya kihalifu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mradi wa Uhamiaji Mtandao ambapo mwezi Januari, 2018 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua pasi mpya ya kusafiria ya kielektroniki ya kimataifa ya Afrika Mashariki. Kuzinduliwa kwa pasi hii kutapunguza vikwazo vya kusafiri mipakani baina ya raia wa nchi wanachama na kuimarisha mahusiano na kuchochea shughuli za kiuchumi miongoni mwa raia wa Jumuiya. Natoa rai kwa Watanzania kuanza kutumia pasi hii na kuendelea kuchangamkia fursa mbalimbali za kiuchumi, kibiashara na ajira na elimu zinazopatika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua hiyo, Serikali imedhibiti wimbi la wakimbizi na wahamiaji haramu wanaoingia nchini kwa sababu mbalimbali. Aidha, ofisi tisa za uhamiaji zimefunguliwa katika wilaya ya Gairo, Iramba, Kakonko, Kilosa, Kiteto, Manyoni, Mvomero, Siha na Songwe kwa lengo la kuongeza udhibiti wa wahamiaji haramu. Katika mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kutekeleza awamu ya pili ya mradi wa uhamiaji mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 kumekuwa na Mikutano Mitatu ya Bunge ambapo masuala mbalimbali yalijadiliwa na kutolewa ufafanuzi na Serikali. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Mkutano huu wa Bajeti utakuwa unahitimisha idadi ya Mikutano Minne ya Bunge kwa mwaka huu wa fedha unaoishia Juni, 2018. Katika Mikutano Mitatu iliyopita, maswali ya msingi 359 na maswali ya nyongeza 1,002 yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Aidha, katika utaratibu wa maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu, maswali ya msingi 17 pamoja na mawili ya nyongeza yaliulizwa na kujibiwa. Miswada 15 ya Sheria ya Serikali iliwasilishwa, kujadiliwa na kupitishwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Bunge liliratibu na kusimamia shughuli za vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge, kutoa huduma za *Hansard*, utafiti, utawala na kutoa mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Ofisi ya Bunge. Pia Bunge lilijadili na kuridhia Maazimio matano yanayohusu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa. Katika

mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika kuongeza ufanisi wa utendaji wa mihimili wa Mahakama nchini. Katika mwaka 2017/2018 Mahakama imesikiliza na kukamilisha mashauri 494,525 kati ya 513,329, sawa na asilimia 96.3 ya mashauri yote katika ngazi zote za Mahakama. Hatua hii imesaidia kupunguza mlundikano wa mashauri katika mahakama zetu. Hali kadhalika katika kipindi hicho Serikali imeanza ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu katika mikoa ya Kigoma na Mara. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa Mahakama za Wilaya na za Mwanzo katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017 Serikali ilizindua Mfumo wa Kielektroniki wa Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Shughuli za Serikali. Mfumo huo unalenga kuongeza ufanisi katika uratibu wa shughuli za Serikali na kuiwezesha Serikali kufanya tathmini ya utoaji huduma kwa wananchi na mipango ya maendeleo. Mfumo huo umeanza kufanya kazi ambapo kwa sasa Wizara zote zinawasilisha utekelezaji wa shughuli zao kupitia mfumo huo. Katika mwaka 2018/2019 Serikali itaimarisha matumizi ya mfumo huo hasa katika ngazi za Mikoa na Halmashauri na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutekeleza jukumu la usimamizi na uhifadhi wa mazingira nchini. Katika mwaka 2017/2018 Serikali imeongeza hamasa na ushirikishwaji mkubwa wa wananchi katika suala la usafi, utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika maeneo yote ikiwemo makazi yao. Hatua hiyo imetokana na ushiriki mkubwa wa viongozi wa kitaifa, mikoa na watendaji wa ngazi zote katika shughuli za usafi na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha ukaguzi wa masuala ya hifadhi ya mazingira nchini, Serikali imeongeza idadi ya ukaguzi wa mazingira kutoka 62 hadi kufikia 512. Aidha, kaguzi 380 zimefanyika kwenye viwanda kwa lengo

la kufanya tathmini za mazingira pamoja na kutoa elimu na uelewa kuhusu uendeshaji endelevu wa viwanda unaozingatia utunzaji bora wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika Mkutano wa Kumi wa Bunge hili, napenda kusisitiza kwamba Halmashauri zote nchini ziweke mpango mahsusi wa kuhifadhi mazingira unaojumuisha kupanda na kutunza miti. Serikali itaweka utaratibu wa upimaji wa utendaji wa wakuu wote wa Mikoa na Wilaya pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri unaozingatia uendelezaji na utunzaji wa mazingira katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 Serikali imeimarisha utendaji wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kuipatia wataalamu, vifaa na kuongezea fedha. Aidha, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2015, imefanyiwa marekebisho ili kuondoa mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wake. Mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, ilikamata jumla ya watuhumiwa 11,071 na kati yao, watuhumiwa 3,486 ni wafanyabiashara wa dawa za kulevya ambao walifikishwa mahakamani. Watuhumiwa wengi waliokamatwa, walijihusisha na dawa za kulevya aina ya bangi, mirungi na *heroine*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, jumla ya tani moja na kilo 561.28 za dawa aina ya *heroine* zilikamatwa. Kati ya hizo, kilo 196.28 zilikamatwa kwenye eneo la maji ya Tanzania na nchi kavu na tani moja na kilo 365 zilikamatwa kwenye bahari kuu kwa kushirikiana na washirika wa kimataifa na kuteketezwa. Aidha, kilo 502 za *cocaine*, tani 47 za bangi na tani 7.4 za mirungi zilikamatwa. Mamlaka pia ilikamata lita 304,513 za vimiminika vya kemikali bashirifu na kilo 22,143 za kemikali bashirifu yabisi. Katika *operation* za uteketezaji wa mashamba ya bangi na mirungi, ekari 572.75 za bangi na ekari 64.5 za mirungi ziliteketezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeimarisha huduma za matibabu kwa watumiaji wa dawa za kulevya kwa kutumia *methadone* katika Hospitali za Taifa za Muhimbili, Mwananyamala, Temeke Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Vilevile Serikali imeanzisha vituo vya tiba hivyo kuwafikia waathirika wengi zaidi nchini ambapo kliniki saidizi za kutibu waathirika wa dawa za kulevya zimeanzishwa katika Hospitali za Rufaa za Mbeya na Mwanza. Hadi kufikia Januari, 2018 zaidi ya watumiaji 5,560 walikuwa wakipatiwa huduma za tiba ya *methadone* katika vituo mbalimbali nchini. Serikali pia imekuwa ikisimamia uanzishwaji wa nyumba za upataji nafuu *(Sober Houses)* ambazo hadi sasa idadi yake ni 22. Aidha, mwezi Februari, 2018 Serikali ilizindua mwongozo na uendeshaji wa *sober houses* unaolenga kuwawezesha wamiliki wa nyumba hizo kuwasaidia waathirika hao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Machi, 2018 nchi yetu ilishiriki katika Mkutano wa 61 wa Kimataifa wa *Commission for Narcotic Drugs* uliofanyika Vienna, Austria na kushirikisha zaidi ya nchi 150. Katika mkutano huo, Tanzania ilitambuliwa kama nchi ya mfano katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya Barani Afrika na kupewa heshima ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 28 wa Wakuu wa Vyombo vinavyopambana na Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya Duniani kutoka Afrika, utakaofanyika hapa nchini mwezi Septemba, 2018. Mkutano huo utatoa fursa kwa wataalam nchini kubadilishana taarifa, uzoefu, kujenga mahusiano na kujifunza mbinu zinazotumiwa na nchi nyingine katika kukabiliana na dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa viongozi na watendaji kuwaelimisha vijana kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, wananchi waendelee kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kutoa taarifa kuhusu wanaojihusisha na dawa hizo. Pia ni vema wazazi, walezi na jamii kuwa karibu na vijana wetu na kufuatilia nyendo zao ili kuwaepusha kuingia kwenye mkumbo wa matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kupambana na rushwa pamoja na ufisadi. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2017 hadi Machi, 2018, jumla ya majalada 325 yalifanyiwa uchunguzi na TAKUKURU na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ambapo majalada 214 kati ya hayo yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani. Aidha, kesi 727 ziliendeshwa mahakamani na kesi 219 ziliamuliwa na watuhumiwa 138 walipatikana na hatia na kuhukumiwa. Kutokana na *operations* zilizofanywa na TAKUKURU katika maeneo ya ukusanyaji mapato, uzuiaji wa malipo hewa na ukaguzi wa miradi ya maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 58.4 ziliokolewa na kurejeshwa Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAKUKURU pia imefuatilia miradi ya maendeleo 195 yenye thamani ya shilingi bilioni 154.1 katika sekta za elimu, afya, maji na ujenzi ili kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika kama zilivyokusudiwa na thamani ya fedha inapatikana. Katika ufuatiliaji huo, miradi 73 yenye thamani ya shilingi bilioni 30.9 ilibainika kuwa na kasoro katika utekelezaji wake. TAKUKURU imetoa mapendekezo ambayo yatafanyiwa kazi na Serikali na tayari hatua za kinidhamu na kisheria zimechukuliwa kwa wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI katika jamiii. Ili kutekeleza azma hiyo, Mpango wa Kuzuia Maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto umepewa kipaumbele. Aidha, elimu ya UKIMWI imetolewa kupitia vyombo vya habari, majarida na vipeperushi. Vilevile, elimu imetolewa kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo utoaji wa elimu rika pamoja na kuwashirikisha viongozi na watu mashuhuri, viongozi wa dini, sekta binafsi na kutekeleza programu za kupambana na UKIMWI mahali pa kazi. Kutokana na juhudi hizo, matokeo ya utafiti uliofanyika katika ngazi ya kaya kuanzia mwezi Oktoba, 2016 hadi Agosti, 2017 yanaonesha kuwa wastani wa kitaifa wa maambukizi ya VVU kwa watu wenye umri wa miaka 15 hadi 49 ni asilimia 4.7. Aidha, utafiti huo umebainisha kwamba kiwango cha maambukizi mapya ya VVU kwa mwaka ni asilimia 0.27.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatoa huduma za wananchi wanaoishi na virusi vya UKIMWI (WAVIU) nchini. Hadi kufikia Septemba 2017, WAVIU 972,127 sawa na asilimia 70 ya WAVIU wote walikuwa wanapatiwa dawa za kufubaza makali ya VVU. Katika mwaka 2017/2018 Serikali kwa kushirikiana na wadau wamechangia zaidi ya shilingi bilioni 1.5 kwenye Mfuko Maalum wa UKIMWI ili kupunguza utegemezi kutoka kwa wafadhili. Katika mwaka 2018/2019 Serikali itaanza utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Nne wa Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2018/2019 hadi mwaka 2022/ 2023. Vilevile kampeni maalum za kushawishi wanaume kushiriki katika kupima afya zao na vijana waweze kujitambua nazo zitaendeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuratibu shughuli za usimamizi wa maafa nchini kwa kuzuia, kupunguza madhara na kujiandaa kukabiliana na maafa pindi yanapotokea. Aidha, mfumo wa ufuatiliaji wa taarifa za mabadiliko ya tabianchi na upatikanaji wa taarifa za tahadhari za awali ili kupunguza madhara ya maafa umeshaboreshwa. Serikali pia imekamilisha kusimika mashine 36 za kisasa za kufuatilia taarifa za hali ya hewa katika Wilaya mbalimbali nchini kutokana pamoja na kuwaongezea uwezo wataalamu wa hali ya hewa. Jitihada hizi zimeongeza uhakiki na uhakika wa utabiri wa hali hewa nchini kufikia asilimia 87.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeimarisha ushirikiano katika masuala ya usimamizi wa maafa kupitia Umoja wa Afrika na jumuiya za *SADC*, *EAC* na *IGAD*. Ushirikiano huo umewezesha nchi wanachama kubadilishana taarifa za kuandaa utabiri wa hali ya hewa na matumizi yake katika kupunguza madhara ya maafa. Vilevile nchi hizo zinabadilishana uzoefu pamoja na kutoa mafunzo ya usimamizi wa maafa kwa wataalam wa nchi wanachama. Katika mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kuzijengea uwezo Kamati za Usimamizi wa Maafa za Mikoa na Wilaya na kuratibu shughuli za kupunguza madhara ya maafa na misaada ya kibinadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliratibu mbio za Mwenge wa Uhuru kwa lengo la kukuza mshikamano na kuhimiza shughuli za maendeleo. Katika mbio hizo ambazo kilele chake kilikuwa tarehe 14 Oktoba, 2017 Mjini Magharibi Zanzibar, miradi 1,512 yenye thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 1.06 iliwekewa mawe ya msingi na kuzinduliwa. Kati ya miradi hiyo, miradi 150 yenye thamani ya shilingi bilioni 568.8 ilikuwa ya viwanda. Uzinduzi wa mbio za mwenge kwa mwaka 2018 ulifanyika mkoani Geita tarehe 2 Aprili, 2018 na kilele chake kitafanyika mkoani Tanga tarehe 14 Oktoba, 2018. Ninawasihi wananchi kushiriki kwa wingi wakati wa mbio za Mwenge wa Uhuru kwani zinalenga kuleta umoja na mshikamano kwa wananchi pamoja na kuhimiza shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kuimarisha mahusiano na mataifa mengine duniani, mashirika ya kimataifa na washirika wetu wa maendeleo limeendelea kuwa kipaumbele cha Serikali katika kutekeleza Sera yetu ya Mambo ya Nje. Katika kufanikisha jukumu hilo kwa ufanisi, Serikali inafanya mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ili iweze kukidhi mahitaji ya matakwa ya sasa ya Tanzania katika kushughulikia siasa za kimataifa na diplomasia pamoja na masuala ya mtangamano wa kikanda na kuendeleza Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kutekeleza diplomasia ya uchumi kwa kuvutia wawekezaji na watalii; kutafuta fursa za mafunzo; kuendelea kuwashirikisha Watanzania waishio ughaibuni kuchangia katika maendeleo ya nchi yao pamoja na kutafuta ajira na masoko ya bidhaa za Tanzania nje. Aidha, Serikali itaimarisha sera ya ujirani mwema kwa lengo la kukuza mahusiano na kufungua milango ya ushirikiano katika utekelezaji wa miradi ya kitaifa ya kipaumbele hususan, reli, barabara, nishati na biashara na majirani zetu.

Vilevile Serikali itatoa msukumo kwa Mabalozi kutumia ushawishi wao kuitangaza vyema miradi ya kipaumbele na vivutio mbalimbali vilivyopo nchini na

kutangaza lugha ya Kiswahili ambayo ikitumika vizuri inaweza kuwa chanzo cha ajira kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanashuhudia mafanikio makubwa ya kiuchumi na kijamii katika kipindi kifupi cha takriban miaka miwili na nusu tangu Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iingie madarakani. Mafanikio hayo yanatoa matumaini kwa Watanzania kwamba yale yaliyoahidiwa ndani ya kipindi cha miaka mitano yatatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia malengo ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/2019 Serikali pamoja na mambo mengine, itaweka mkazo katika kudhibiti upotevu wa mapato; kuimarisha mfumo wa kukusanya mapato hususan kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na kudhibiti matumizi ya fedha na rasilimali nyingine za umma. Aidha, msukumo utawekwa katika kuhimiza uwajibikaji wa watendaji wa Serikali na kuimarisha ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wakati anazindua Bunge lako Tukufu tarehe 20 Novemba 2015, pamoja na mambo mengine aliweka wazi dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano kujenga uchumi wa viwanda kwa lengo la kutengeneza ajira nyingi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia azma hiyo, Serikali itaendelea kufanya yafuatayo:-

Moja, uimarisha na kudumisha amani, utulivu, mshikamano na umoja wa kitaifa uliopo ili kuleta maendeleo endelevu;

Mbili, uboresha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato na utoaji huduma;

Tatu, kujenga miundombinu muhimu ikiwemo reli inayoendelea kujengwa, bandari, viwanja vya ndege, barabara na madaraja yake;

Nne, kuimarisha uzalishaji na usambazaji wa nishati ya uhakika wa umeme sambamba na kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi, mashamba na maeneo ya makazi na viwanda;

Tano, kusimamia viongozi na watendaji wote ili kuondoa urasimu usio wa lazima pamoja na kuwahudumia wananchi wote bila ubaguzi wa aina yoyote; na

Sita, usimamia kikamilifu rasilimali zilizopo ili zitumike kwenye maeneo yanayochochea ukuaji uchumi na utoaji huduma bora kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa kila mwananchi kuendelea kuunga mkono jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kufanya kazi kwa bidii, weledi, uadilifu, uaminifu na kupiga vita rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2018/2019 Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizopo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni mia moja arobaini na tatu, milioni mia sita kumi na nane, mia saba sitini na mbili elfu na mia sita tisini na nane (shilingi 143,618,762,698). Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni sabini na nne, milioni mia tano ishirini na saba, mia tatu ishirini na moja elfu na mia sita tisini na nane (shilingi 74,527,321,698) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni sitini na tisa, milioni tisini na moja, mia nne arobaini na moja elfu (shilingi 69,091,441,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni mia moja ishirini na tano, milioni mia tano ishirini na moja, na mia moja elfu (shilingi 125,521,100,000) kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya

fedha hizo, shilingi bilioni mia moja kumi na saba, milioni mia mbili na tano, mia nne themanini na saba elfu (shilingi 117,205,487,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni nane, milioni mia tatu kumi na tano, mia sita kumi na tatu elfu (shilingi 8,315,613,000) ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI MKUU, MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB), KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2018/2019 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI zilizochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2017/2018 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2018/2019. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizopo chini yake pamoja na Mfuko wa Bunge kwa mwaka 2018/2019.

**2.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2017/2018 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2018/2019.

3. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutokana na fikra na uongozi wao makini katika ujenzi wa Taifa letu. Ni dhahiri kuwa juhudi zao katika kuongoza na kusimamia utekelezaji wa mipango ya Serikali, zinaleta manufaa makubwa kwa wananchi.

4. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** hivi karibuni tumewapata Waheshimiwa Wabunge wapya kutokana na chaguzi ndogo zilizofanyika. Nitumie fursa hii kuwapongeza sana Mhe. Dkt. Godwin Mollel (Mbunge wa Jimbo la Siha) na Mhe. Maulid Mtulia (Mbunge wa Jimbo la Kinondoni) kwa kuchaguliwa na kisha kuapishwa na Bunge lako Tukufu ili waendelee kuwatumikia wananchi wa majimbo yao na Watanzania kwa ujumla. Ni matumaini yangu kuwa Bunge lako Tukufu litaendelea kuwapatia ushirikiano wa kutosha ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

5. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Bunge lako lilimpoteza aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini, Mheshimiwa Leonidas T. Gama. Vilevile, baadhi ya waheshimiwa Wabunge na wananchi tunaowawakilisha walipata misiba ya ndugu, jamaa na marafiki. Aidha, kulitokea maafa na majanga ambayo yalisababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali. Pia, kumekuwepo na ajali za barabarani ikiwemo ajali mbaya iliyotokea tarehe 24 Machi 2018 wilayani Mkuranga na kugharimu maisha ya Watanzania 26. Ninaomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema waliopata majeraha. Aidha, ninatoa pole kwa ndugu jamaa na marafiki kwa misiba iliyotokea. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu mahali pema peponi. Amina!

6. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** napenda pia kutoa salamu za pole kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliopata majeraha mbalimbali kufuatia ajali ya gari tarehe 29 Machi 2018 walipokuwa wakitoka Dodoma kuelekea Dar es

Salaam. Wabunge hao ni Mheshimiwa Haji Ameir Haji (Mbunge wa Makunduchi), Mheshimiwa Khamis Ali Vuai (Mbunge wa Mkwajuni), Mheshimiwa Bhagwanji Maganlal Meisuria (Mbunge wa Chwaka), Mheshimiwa Makame Mashaka Foum (Mbunge wa Kijini) na Mheshimiwa Juma Othman Hija (Mbunge wa Tumbatu). Tuzidi kumuomba Mwenyezi Mungu awajalie afya wenzetu hawa ili waweze tena kuungana nasi kutekeleza majukumu yao katika Bunge lako hili Tukufu.

**7.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi kubwa ya kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kipekee, niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mhe. Mohammed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI inayoongozwa na Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini. Kamati hizo zimetoa mchango mkubwa wakati wa maandalizi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge. Aidha, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuaminika na kuchaguliwa kuongoza Kamati hizo.

**8.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Idara, Mashirika, Wakala na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na Taasisi zake kwa kutekeleza majukumu yao na kukamilisha kuandaa Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2018/2019.

**9.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kwa namna ya pekee kabisa, napenda kumshukuru Mhe. Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu; Mhe. Anthony Peter Mavunde, Mbunge wa Dodoma Mjini na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu; Mhe. Stella Alex Ikupa, Mbunge Viti Maalumu na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu; Makatibu Wakuu Bibi Maimuna K. Tarishi, Profesa Faustin R. Kamuzora, na Bwana Eric F. Shitindi, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Wafanyakazi wote kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**10.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** napenda pia kuwashukuru washirika wa maendeleo zikiwemo nchi marafiki, taasisi na mashirika ya kimataifa, madhehebu ya dini na mashirika yasiyo ya kiserikali, kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali katika kujenga uchumi wa viwanda na kuiletea nchi maendeleo.

**11.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kuniunga mkono na niwapongeze kwa kutekeleza shughuli za maendeleo jimboni kwa ufanisi, wakati mimi Mbunge wao nikitekeleza majukumu ya kusimamia utendaji wa Serikali. Kipekee, ninamshukuru mke wangu mpendwa, Mary na familia yangu kwa upendo wao, uvumilivu na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ya kitaifa. Nawashukuru sana.

## MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI

**12.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2018/2019 ni kuboresha utendaji wa Serikali na kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2018/2019. Aidha, Mpango na Bajeti umezingatia azma ya Serikali ya kufikia malengo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao umepangwa kuhitimishwa mwaka 2020/2021 ukiwa na dhima kuu ya "kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea ukuaji uchumi na maendeleo ya watu". Vilevile, Mpango huu umezingatia

azma ya kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 na utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizozitoa wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2015 pamoja na utekelezaji wa hotuba yake wakati akizindua Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015.

## MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO

**13.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** tukiwa tunaingia kwenye Bunge la tatu la bajeti kwa Serikali ya Awamu ya Tano, hatuwezi kumsahau Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kutimiza ndoto na matarajio ya Watanzania kwa kujenga nchi yenye uchumi imara. Katika kipindi hiki, tumeshuhudia mambo makubwa aliyoyafanya yakiwemo kujenga ari ya uzalendo kwa kuilinda na kuisemea nchi yetu bila woga; kudumisha amani, utulivu na mshikamano; kuimarisha ulinzi na usalama kwa kukomesha vitendo vya mauaji yaliyojitokeza Mwanza, Amboni (Tanga), Mkuranga, Kibiti, Rufiji (Pwani) pamoja na kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya.

**14.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kazi nyingine alizofanya ni kujenga nidhamu ndani ya utumishi wa umma na kukemea uzembe; kuendesha vita dhidi ya rushwa na ufisadi kwenye taasisi za umma; kuanzisha mahakama ya rushwa na ufisadi; kuimarisha ulinzi wa rasilimali za nchi zikiwemo za madini na maliasili. Aidha, amefufua Shirika la Ndege la Tanzania; ameanzisha ujenzi wa reli ya kisasa ya kiwango cha kimataifa (SGR); ameendeleza ujenzi wa barabara zikiwemo barabara za juu (flyovers) na amenunua meli na vivuko. Kazi nyingine ni ujenzi wa vyanzo vipya vya umeme kama vile Stiegler's Gorge; usambazaji umeme hadi vijijini na ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania).

**15.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** mambo mengine makubwa aliyoyafanya ni kuimarisha huduma za afya hususan upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaatiba katika vituo

vya kutolea huduma za afya; kutoa elimumsingi bila malipo kwa watoto wa Kitanzania; ujenzi wa miradi ya maji; na kuimarisha bei za mazao ya kibiashara. Aidha, Mheshimiwa Rais ametimiza ndoto ya Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya kuhamishia Makao Makuu ya Serikali mjini Dodoma. Haya ni baadhi tu ya mambo aliyoyafanya na yatatolewa ufafanuzi wa kutosha kupitia wizara za kisekta.

**HALI YA UCHUMI**

**16.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Tanzania ni miongoni mwa nchi tatu barani Afrika ambazo uchumi wake unakua kwa kasi. Viashiria vya kiuchumi vinaonesha kuwa katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba 2017, uchumi ulikua kwa asilimia 6.8, kiwango ambacho kilikuwa juu zaidi ikilinganishwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Uchumi wa Kenya ulikuwa kwa asilimia 6.1, Rwanda asilimia 6.0, Uganda asilimia 5.5, Burundi asilimia 0.0 na Sudan Kusini asilimia hasi 6.3. Hata hivyo, takwimu za hivi karibuni kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) zinaonesha kwamba katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2017, pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha asilimia 7.1 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2016. Shughuli zilizochangia ukuaji huo kwa viwango vikubwa ni pamoja na uchimbaji wa madini na mawe asilimia 17.5; huduma za usambazaji maji safi na majitaka asilimia 16.7; uchukuzi na uhifadhi wa mizigo asilimia 16.6; habari na mawasiliano asilimia 14.7 na ujenzi asilimia 14.1. Aidha, sekta ya kilimo, misitu na uvuvi ilikua kwa asilimia 3.6, kiwango ambacho hakijawahi kufikiwa tangu mwaka 2010.

**17.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kufikia Desemba 2017, deni la Taifa lilikuwa Dola za Marekani milioni 25,419.6. Viashiria vyote vya deni vinaonesha kuwa deni linahimilika kwani, thamani ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 19.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya deni la nje kwa uuzaji wa bidhaa nje ni asilimia 81.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 150; na thamani ya deni la nje kwa mapato ya ndani ni asilimia 117.1 ikilinganishwa na ukomo

wa asilimia 200. Kwa kuzingatia vigezo hivyo, bado tuna uwezo wa kuendelea kukopa kutoka ndani na nje ili kugharamia shughuli za maendeleo. Kwa ujumla, viashiria vya kuimarika kwa uchumi, vinatoa mwelekeo mzuri wa kufikiwa kwa malengo yetu ya kuwa nchi ya kipato cha kati inayoongozwa na uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

**SIASA**

**18.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** ni miaka 26 sasa imepita tangu mfumo wa siasa wa vyama vingi uanzishwe nchini. Katika kipindi hicho tumeona ushiriki wa Watanzania katika siasa ukiendelea kuongezeka na uhuru wa kujiunga na vyama vya siasa kwa kuridhishwa na itikadi za vyama hivyo pia ukiongezeka. Ni vyema tukajenga utamaduni wa kuheshimu wananchi pale wanapoamua kujiunga na chama cha siasa watakachokipenda. Jukumu letu kama viongozi wa siasa ni kunadi sera zetu kwa wananchi na kuhamasisha ujenzi wa demokrasia inayolenga kuleta maendeleo kwa wananchi wote bila ubaguzi wa aina yoyote pamoja na kudumisha amani, utulivu, mshikamano na kujenga umoja wa kitaifa.

**19.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, kumefanyika chaguzi ndogo za Wabunge katika majimbo matano na Madiwani katika kata 59 kujaza nafasi zilizoachwa wazi kutokana na sababu mbalimbali. Chaguzi hizi zilisimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa ufanisi. Katika chaguzi ndogo za ubunge zilizofanyika katika majimbo ya Songea Mjini, Singida Kaskazini, Longido, Kinondoni na Siha; Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilishinda majimbo yote. Vilevile, katika uchaguzi wa Madiwani, CCM ilishinda katika kata 58 na CHADEMA ilishinda katika Kata moja. Nichukue nafasi hii kuvipongeza vyama vyote vya siasa vilivyoshiriki katika chaguzi hizo na kipekee nakipongeza Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kupata ushindi mkubwa na wa kishindo katika maeneo mengi.

**20.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Ofisi ya Msajili imeendelea kuhakikisha kuwa demokrasia ya vyama vingi vya siasa inaimarika. Katika mwaka 2017/2018, Ofisi ya Msajili iliratibu

kikao cha Baraza la Vyama vya Siasa ambacho pamoja na kufanya uchaguzi wa Viongozi wa Kamati za Baraza hilo, kilijadili mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria Mpya ya Vyama vya Siasa na marekebisho ya Kanuni za Usajili wa Vyama vya Siasa. Vilevile, Ofisi ya Msajili inaendelea kukusanya maoni ya wadau kwa lengo la kuandaa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 pamoja na kanuni zake.

**MUUNGANO**

**21.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, kumefanyika vikao mbalimbali vya kisekta vya ushirikiano kati ya Wizara za SMT na SMZ kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali za Muungano wetu. Baadhi ya changamoto hizo ni masuala ya fedha, biashara na ajira katika taasisi za Muungano. Katika kipindi hicho, viongozi na wataalamu wa pande mbili za Muungano walikutana kwa ajili ya kujadili hoja zinazohusu sekta za fedha, biashara, viwanda na uwekezaji, ujenzi na uchukuzi, maliasili na utalii.

**SERIKALI KUHAMIA DODOMA**

**22.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali inaendelea kutekeleza zoezi la kuhamishia shughuli za Serikali Kuu Dodoma. Tangu utekelezaji wa zoezi hilo uanze mwezi Septemba 2016, jumla ya watumishi wa umma 3,829 kutoka Wizara na taasisi mbalimbali wamehamia Dodoma katika awamu ya kwanza na ya pili, na awamu ya tatu inaendelea. Katika kufanikisha azma hii, Serikali inaboresha miundombinu ya barabara, reli, uwanja wa ndege, umeme, mifumo ya maji safi na maji taka, ofisi, makazi na kuimarisha huduma za elimu, afya, mawasiliano na michezo.

**23.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imejipanga kuijenga Dodoma kuwa mji bora na wa kisasa unaoendana na mahitaji na mifumo ya miji bora duniani. Ili kufikia azma hiyo, Serikali inashirikiana na wadau ikiwemo sekta binafsi na mashirika ya kimataifa kuujenga Mji wa Dodoma. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye mara tu baada ya kuhamia Dodoma amezindua "Kampeni ya Kijanisha Dodoma" inayolenga kuifanya Dodoma kuwa ya kijani. Kampeni hiyo inahusisha kuendeleza, kutunza na kuhifadhi maeneo ya ukanda wa kijani.

**24.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** niupongeze Umoja wa Mataifa na mashirika yake kwa kufungua ofisi zake za muda mjini Dodoma mwezi Desemba 2017. Natoa wito kwa mashirika mengine ya kimataifa na mabalozi waige mfano huu wa kuhamishia ofisi zao Dodoma. Serikali itaendelea kutoa ushirikiano wa karibu kwa Mashirika ya Kimataifa na wanadiplomasia katika kurahisisha maandalizi yao ya kuhamia Dodoma. Aidha, natoa wito kwa wawekezaji wa ndani na nje kuendelea kuwekeza Dodoma kwani kuna fursa nyingi za uwekezaji ikizingatiwa nafasi yake kijiografia inayosaidia mikoa yote hapa nchini kufikika kwa urahisi na haraka zaidi. Nichukue fursa hii kuipongeza Kamati inayoratibu zoezi la Serikali kuhamia Dodoma inayosimamiwa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Bibi Maimuna K. Tarishi, Katibu Mkuu (Waziri Mkuu na Bunge).

## UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

**25.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali inatekeleza mipango mbalimbali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuunga mkono juhudi zinazofanywa na wananchi kujiletea maendeleo. Moja ya jitihada zilizofanywa na Serikali ni kuanzisha mifuko ya uwezeshaji ambayo inatoa mikopo kupitia vikundi vya vijana, wanawake, wazee, watu wenye ulemavu na makundi mengine yenye mahitaji maalum.

**26.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ulidhamini mikopo yenye thamani ya takriban shilingi bilioni 13 kwa SACCOS 58, VICOBA 172 na kampuni mbili. Aidha, Mfuko wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi umetoa mikopo ya Shilingi bilioni 62.8 kwa wajasiriamali 85,982. Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni

3.4 kwa vikundi 5,169 katika Halmashauri 153. Mfuko wa Kilimo Kwanza ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 62.7 kwa miradi 189 katika wilaya 76.

**27.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Vijana umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 783 ambapo vijana 840 kutoka Halmashauri mbalimbali walinufaika. Aidha, katika kipindi hicho, Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia asilimia 5 ya mapato yao ya ndani zilitenga shilingi bilioni 15 ikiwa ni mikopo ya masharti nafuu kwa vijana. Vilevile, Halmashauri 48 zilitenga ekari 217,882 kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali kwa vijana nchini. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kuwawezesha vijana kiuchumi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

**28.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** hivi sasa Serikali inaratibu jumla ya mifuko na programu 31 za uwezeshaji ambazo usimamizi wake upo katika taasisi mbalimbali za Serikali na za binafsi. Kila mfuko au programu imeanzishwa kwa sheria yake au taratibu maalumu zinazosimamia utendaji wa mfuko husika. Serikali imeona kuna umuhimu wa kupunguza idadi ya mifuko kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji wake ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Hivyo, tumeanza kufanya mapitio ya utendaji wa mifuko hiyo kwa nia ya kuunganisha baadhi ya mifuko yenye majukumu yanayofanana. Hatua hiyo, itasaidia kuwa na mifuko michache yenye tija ambayo itaharakisha kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

**Ukuzaji Ujuzi**

**29.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** suala la kukuza ujuzi wa nguvukazi tuliyonayo ni miongoni mwa ajenda muhimu ya kisera katika kuwezesha wananchi kujikwamua kiuchumi. Serikali inatoa msukumo wa kipekee kupitia Programu ya Ukuzaji Ujuzi nchini kwa lengo la kuwapatia ujuzi na stadi za kazi wananchi hasa kundi la vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ili waweze kumudu ushindani katika soko la ajira na hivyo kuwawezesha kushiriki katika ujenzi wa uchumi jumuishi wa viwanda.

**30.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** utafiti uliofanywa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi mwaka 2014, unaonesha kuwa asilimia 79.9 ya nguvukazi ni yenye kiwango cha chini cha ujuzi, asilimia 16.6 kiwango cha kati wakati ni asilimia 3.6 tu ndiyo yenye kiwango cha juu. Ili kufikia uchumi wa viwanda, Serikali imedhamiria kubadili mwenendo huo kwa kuhakikisha nguvukazi yenye kiwango cha juu cha ujuzi inafika asilimia 12 na kiwango cha kati asilimia 34. Kwa msingi huo, Serikali inaendelea kutekeleza programu ya kukuza ujuzi pamoja na programu nyingine ili kukidhi matakwa ya uchumi wa viwanda.

**31.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, jumla ya vijana 7,817 wamewezeshwa kupata ujuzi kupitia programu hiyo. Kati yao, vijana 220 walipata mafunzo kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na vijana 3,440 kupitia Taasisi ya Don Bosco. Mafunzo waliyopewa ni katika fani za ufundi stadi wa ushonaji nguo, useremala, uashi, TEHAMA, uchongaji wa vipuri, ufundi magari, umeme, bomba, vyuma, terazo, vigae na ujuzi wa kutengeneza bidhaa za ngozi. Aidha, kupitia VETA vijana 3,989 walipata mafunzo ya kurasimisha ujuzi uliopatikana kwa mfumo usio rasmi kwa fani za uashi, useremala, ufundi magari, upishi na uhudumu katika hoteli.

**32.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** mafunzo ya vitendo yalitolewa pia kwa wahitimu 168 kupitia viwanda na kampuni mbalimbali katika fani ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi. Vilevile, Serikali imeandaa na kuzindua Mwongozo wa Kitaifa wa Uanagenzi na Mwongozo wa Kitaifa wa Mafunzo ya Vitendo kwa wahitimu kwa lengo la kuweka utaratibu wa utoaji wa mafunzo hayo kwa wadau wote ili waweze kuajirika. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itatoa mafunzo ya ujuzi wa kujiajiri na stadi za kazi kwa vijana 10,500 katika fani mbalimbali. Ninazishukuru kampuni binafsi ambazo zinaendelea kutoa nafasi za mafunzo ya vitendo kwa wahitimu wetu. Serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika nyanja mbalimbali ili tuweze kukuza ujuzi wa rasilimali watu ya taifa.

## Ajira

**33.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Serikali imeendelea kuratibu juhudi za kukuza ajira nchini. Hadi kufikia Februari 2018, jumla ya ajira 482,601 katika sekta rasmi zimezalishwa nchini. Kati ya ajira hizo, ajira 345,547, sawa na asilimia 72 zimezalishwa kutokana na shughuli za umma ikiwemo miradi ya maendeleo ya Serikali kama vile ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na miradi ya TASAF; na ajira 137,054 sawa na asilimia 28 zimezalishwa katika sekta binafsi.

**34.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali inaandaa mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba Watanzania wazawa wanashiriki na kunufaika na miradi mikubwa ya kitaifa. Vikao kati ya Serikali na wafanyabiashara vimefanyika ili kuwaandaa kuwa sehemu ya utekelezaji wa mkakati huo. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kuratibu masuala ya ukuzaji ajira nchini ikiwa ni pamoja na kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Ajira ili iendane na mahitaji ya sasa ya soko la ajira.

## Masuala ya Kazi na Wafanyakazi

**35.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** ili kuhakikisha kwamba kunakuwepo tija, ufanisi na mahusiano mema mahali pa kazi, Serikali inasimamia Sheria Na.6 ya Ajira na Mahusiano Kazini na Sheria Na.7 ya Taasisi za Kazi. Sheria hizo zinalenga kuhakikisha haki na wajibu kwa mfanyakazi na mwajiri vinapatikana. Ili kufikia azma hiyo, Serikali imehimiza kuanzishwa kwa mabaraza ya wafanyakazi, kufunga mikataba ya hali bora pamoja na kufanya kaguzi mbalimbali mahali pa kazi ili kujiridhisha kuwa viwango vya kazi vinazingatiwa.

**36.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika kipindi cha Julai 2017 hadi Februari 2018, jumla ya kaguzi 102,860 zimefanyika katika maeneo mbalimbali ya kazi nchi nzima. Sambamba na

kaguzi hizo, elimu kuhusu sheria za kazi, wajibu na majukumu ya wajumbe wa baraza kwa waajiri na wafanyakazi kupitia vyama vyao ilitolewa. Jumla ya waajiri 640 na wafanyakazi 3,624 walipatiwa elimu hiyo. Aidha, mabaraza 441 ya wafanyakazi yaliundwa na 46 yalihuishwa upya.

**37.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali kupitia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ilipokea na kusajili migogoro ya kikazi 6,113 ambapo migogoro 4,816 sawa na asilimia 79, ilitatuliwa kwa njia ya usuluhishi na uamuzi. Katika mwaka 2017/2018, utafiti kuhusu sekta na vyanzo vinavyoongoza kwa migogoro ya kikazi umefanyika. Sekta ya usafirishaji iliongoza kwa kuwa na migogoro 547; ulinzi binafsi 512; viwanda 434; elimu 420; huduma za hoteli 399 na taasisi za umma 321. Aidha, aina ya vyanzo vinavyoongoza kusababisha migogoro ya kazi ni kuachishwa kazi bila kufuata taratibu sahihi; madai mbalimbali na kuvunjwa kwa mikataba isivyokuwa halali. Utafiti huu utaisaidia Serikali kwa kushirikiana na waajiri na vyama vya wafanyakazi kuweka mipango ya pamoja na kuzuia migogoro sehemu za kazi kabla haijatokea.

**38.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi na kuendeleza mijadala yenye tija ili kupunguza migogoro mahali pa kazi. Serikali pia itaendelea kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ikiwa ni pamoja na kufanya kaguzi, kusajili, kusuluhisha na kuamua migogoro katika maeneo ya kazi. Aidha, itashirikiana kwa karibu na vyama vya wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kufanya majadiliano ya mara kwa mara kwa lengo la kuongeza tija na kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

**SEKTA BINAFSI**

**39.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali inatambua mchango wa sekta binafsi katika kukuza uchumi wa Taifa letu. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na kuanzisha na kuboresha miundombinu wezeshi kama vile reli, barabara, umeme na maji. Hatua nyingine ni

kupunguza na kufuta baadhi ya kodi zinazoathiri ufanisi wa sekta binafsi; kuhuisha sera na sheria pamoja na kuimarisha majadiliano yenye manufaa baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Februari 2018, jumla ya miradi 175 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 4.4 ilisajiliwa kupitia Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC). Miradi hiyo inatarajiwa kutoa fursa za ajira 20,178.

**40.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa nia ya kuondoa changamoto zinazokwamisha maendeleo ya sekta binafsi. Katika mwaka 2017/2018, Serikali imefanya mikutano minne na wawakilishi wa sekta binafsi. Miongoni mwa mikutano hiyo, ni ule uliofanyika tarehe 19 Machi, 2018 ambao uliongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo kwa Wizara na Taasisi za umma kukutana na wawakilishi wa sekta binafsi ili kutatua kwa haraka changamoto zilizobainishwa katika mkutano huo. Serikali inawahakikishia wafanyabiashara na sekta binafsi kwamba inawathamini na itaendelea kushirikiana nao kutatua changamoto zinazowakabili ili kujenga uchumi wa viwanda.

**SEKTA YA HIFADHI YA JAMII**

**41.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii ikiwemo kutungwa kwa sheria inayounganisha Mifuko ya Pensheni ya PSPF, LAPF, PPF na GEPF na kuunda mfuko mmoja kwa ajili ya watumishi wa umma unaojulikana kama Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma. Sheria hiyo pia, imefanya marekebisho kwenye Sheria ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii ili kuufanya Mfuko huo uhudumie wafanyakazi wa sekta binafsi pamoja na kutoa huduma ya hifadhi ya jamii katika sekta isiyo rasmi.

**42.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kutungwa kwa sheria hiyo kutasaidia kuondoa changamoto iliyotokana na wingi wa mifuko ya hifadhi ya jamii inayolipa mafao yanayotofautiana

kwa watumishi wa umma wenye masharti ya kazi yanayofanana. Vilevile, sheria hiyo itasaidia kupunguza changamoto ya baadhi ya mifuko kutokuwa endelevu kutokana na idadi ndogo ya wanachama, ushindani usiokuwa na tija na gharama kubwa za uendeshaji. Sheria imeweka kipindi cha mpito cha miezi sita kitakachoanza tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hiyo. Lengo ni kuwezesha maandalizi ya utekelezaji wake kufanyika pasipo kuathiri shughuli na huduma muhimu kwa wanachama wa mifuko iliyounganishwa ikiwa ni pamoja na kupokea mafao yao. Napenda kuwataarifu Watanzania kupitia Bunge hili kwamba tayari Mheshimiwa Rais amesaini muswada huo kuwa sheria ya nchi. Utekelezaji wa sheria hii utaboresha mafao ya wafanyakazi.

**43.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Serikali itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003 na hivyo kuandaa Sera ya Taifa ya Kinga ya Jamii ambayo itakuwa jumuishi. Lengo la Serikali ni kuwezesha huduma za hifadhi ya jamii kuwafikia wananchi wengi zaidi hususan waliopo katika sekta isiyo rasmi na kurahisisha upatikanaji wa huduma hizo.

## Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu

**44.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali inaendelea kuimarisha uratibu na utekelezaji wa Sheria Na. 9 ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010, kwa kuhakikisha upatikanaji wa haki na fursa kwa watu wenye ulemavu. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imeunda kamati za watu wenye ulemavu katika mikoa 12 ya Geita, Kagera, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Njombe, Pwani, Singida, Rukwa, Shinyanga, Simiyu na Tabora. Ufuatiliaji unaendelea kufanyika ili kuhakikisha kuwa mikoa mingine nayo inaunda kamati hizo.

**45.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa vifaa saidizi kwa jamii ya watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kufanya shughuli zao bila utegemezi. Baadhi ya vifaa vilivyotolewa ni viti mwendo 240, bajaji 6, magongo ya kutembelea 350, kofia pana 128, fimbo

nyeupe 175, miwani maalum kwa wenye uoni hafifu 70, shime sikio 20, vyerehani 8, vifaa vya kukuzia maandishi 65, mafuta maalum ya kukinga ngozi dhidi ya mionzi ya jua 35, viti maalum vya kuogea 50 na nyenzo nyingine za kujimudu. Vilevile, Serikali imeendelea kuviboresha vyuo vya watu wenye ulemavu vya Yombo, Dar es Salaam na Sabasaba, Singida. Serikali pia inakamilisha uanzishwaji wa kanzidata ya wahitimu wenye ulemavu kutoka vyuo mbalimbali nchini ili iwe rahisi kuwaunganisha na fursa za ajira zinazopatikana kwenye sekta binafsi na umma.

**46.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali inatekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto kwa kutoa elimu ya ulinzi na usalama kwa watoa huduma katika vituo vinavyolea watoto wenye ulemavu wa ngozi kwenye mikoa ya Shinyanga, Mara, Tabora, Simiyu, Tanga, Mwanza, Kigoma na Singida. Lengo la utoaji elimu ni kuwajengea uelewa na kuwapa mbinu watoa huduma waendelee kuimarisha ulinzi kwa watoto pamoja na kuwahimiza wazazi, walezi na jamii waone umuhimu wa kulea watoto hao kwenye ngazi ya familia.

**47.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kukamilisha uanzishwaji wa Mfuko wa Taifa wa Maendeleo wa Watu wenye Ulemavu. Serikali pia itaendelea na zoezi la kuanzisha madawati ya watu wenye ulemavu na kuhamasisha sekta binafsi na umma kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu. Aidha, Serikali itahimiza waajiri wote nchini kuajiri watu wenye ulemavu wenye sifa kwenye nafasi mbalimbali na pia kutoa matangazo ya ajira yanayohamasisha wenye ulemavu kuomba nafasi zinazotangazwa. Vilevile, itahamasisha na kuelimisha jamii kuhusu mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu ikiwemo kuwaheshimu, kuwatambua, kuwathamini na kutowanyanyapaa.

**SEKTA ZA UZALISHAJI**

**Kilimo**

***Hali ya Upatikanaji wa Chakula***

**48.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** hali ya uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya chakula nchini imeendelea kuimarika. Katika msimu wa 2016/2017 na 2017/2018, uzalishaji ulifikia tani milioni 15.9 ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 13.3 ya chakula kwa kipindi hicho. Kutokana na uzalishaji huo, nchi ilikuwa na ziada ya tani milioni 2.6 za mazao yote ya chakula na hivyo, kujitosheleza kwa asilimia 120. Aidha, hadi kufikia Januari, 2018 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ulikuwa umenunua jumla ya tani 26,038 za mahindi na akiba ya chakula iliyopo ghalani ni tani 92,074.

***Mazao ya Biashara na Kuimarisha Ushirika***

**49.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imeamua kuweka mkazo maalum wa kuyaendeleza kwa kasi mazao matano ya biashara ambayo ni chai, kahawa, korosho, pamba na tumbaku. Lengo ni kuongeza mapato ya wakulima, kuwa chanzo cha kuaminika cha malighafi katika uchumi wa viwanda, na kuendelea kuwa chanzo kikuu cha ajira na fedha za kigeni. Uamuzi wa kuongeza usimamizi katika uzalishaji wa mazao hayo makuu ya biashara unatokana na ukweli kwamba, kwa kipindi kirefu uzalishaji ulishuka kutokana na changamoto kadhaa. Miongoni mwa changamoto hizo ni kupungua tija katika uzalishaji, baadhi ya wakulima kuacha kulima mazao hayo kutokana na kukata tamaa kwa sababu mbalimbali zikiwemo vyama vya ushirika kutotekeleza vema wajibu wao, wizi, dhuluma na pia ushiriki mdogo wa maafisa kilimo katika kusimamia kilimo cha kitaalamu.

**50.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** sababu nyingine za kushuka uzalishaji wa mazao hayo ni huduma zisizoridhisha za ugani na utafiti, ukosefu wa pembejeo bora, utitiri wa tozo na wingi wa vyama vya msingi na vyama vikuu vya ushirika. Kwa mfano, uzalishaji wa zao la pamba ulipungua kutoka tani 456,814 mwaka 2013/2014, hadi tani 282,809 mwaka 2015/ 2016. Kwa upande wa tumbaku, uzalishaji katika kipindi cha

miaka minne ulishuka kutoka tani 126,624 mwaka 2010/2011 hadi kufikia tani 60,929 mwaka 2015/2016.

**51.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imechukua hatua za kuimarisha utawala bora kwenye vyama vya ushirika kwa kusimamia chaguzi za vyama 2,537, chaguzi za viongozi wa bodi za vyama vya ushirika 532 na kufanya kaguzi katika vyama vya ushirika 2,896 vikiwemo vyama vikuu. Kazi za kusimamia vyama vya ushirika zinaendelea. Pamoja na hatua hiyo, Serikali inasimamia uendelezaji wa mazao hayo moja kwa moja kupitia maafisa kilimo na Bodi za Mazao. Hatua nyingine ni kufuta baadhi ya tozo zilizokuwa kero katika mazao makuu ya biashara pamoja na kuhakikisha kwamba mauzo yanafanyika kwa njia ya wazi na inayoleta ushindani.

**52.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kutokana na hatua zinazochukuliwa na Serikali kusimamia mazao makuu ya biashara, tayari tumeanza kuona matokeo chanya kwa kuongezeka uzalishaji wake. Kwa mfano, hadi mwezi Machi 2018, uzalishaji wa mazao ya asili ya biashara ulifikia tani 804,025. Uzalishaji huu unaashiria ongezeko la mavuno ikilinganishwa na mwaka 2016/2017. Ongezeko hilo la uzalishaji wa mazao ya biashara linakwenda sambamba na kuimarika kwa mwenendo wa bei za mazao hayo hususan korosho na kahawa.

**53.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kuimarisha vyama vya msingi vya ushirika vya mazao ya kilimo na masoko vinavyozalisha mazao ya kimkakati ya biashara ya pamba, kahawa, korosho, chai na tumbaku. Serikali inalenga kuimarisha masoko ya mazao hayo kwa kuhamasisha mfumo wa stakabadhi ghalani ambapo mazao hayo yatazalishwa na kuuzwa kupitia vyama vya ushirika kwa njia ya minada. Pamoja na hatua hizo, Soko la Bidhaa ambalo limeshaanzishwa, litasaidia sana kuimarisha masoko ya mazao kwani yatakuwa yanauzwa kwa njia ya ushindani mkubwa huku wakulima wanaozalisha kwa ubora wakinufaika na bei ya juu zaidi.

***Pembejeo za Kilimo***

**54.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imerahisisha upatikanaji wa mbolea kwa wakulima baada ya kuanza kuagiza mbolea kwa kutumia Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja. Hadi kufikia mwezi Machi 2018, upatikanaji wa mbolea hapa nchini ulikuwa tani 310,674, sawa na asilimia 64 ya mahitaji ya tani 485,000 kwa mwaka. Kwa upande wa mbegu bora za kilimo, upatikanaji umefikia tani 51,700, sawa na asilimia 86.2 ya mahitaji ya tani 60,000 kwa mwaka. Kwa mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kuboresha Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa pamoja ili uendelee kuleta ufanisi na tija iliyokusudiwa.

***Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo***

**55.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Serikali imekamilisha maandalizi ya awamu ya pili ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Programu hiyo itatekelezwa kwa miaka 10 katika vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaweka mkazo katika kutekeleza malengo makuu ya programu hiyo. Msukumo utawekwa kwenye kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo ya kipaumbele kwa kuimarisha upatikanaji na matumizi ya pembejeo na zana za kilimo; kuimarisha huduma za ugani; kuimarisha kilimo cha umwagiliaji; kuimarisha huduma za utafiti wa mazao ya kilimo na kuhakikisha matokeo ya utafiti yanawafikia wakulima; kuweka na kusimamia mipango ya matumizi bora ya ardhi ya kilimo; kuimarisha usindikaji wa mazao ya kilimo na kuwezesha upatikanaji wa masoko ya mazao.

**56.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tumeamua kwa dhati kusimamia kwa karibu sekta ya kilimo ambayo ndiyo inaajiri Watanzania wengi. Tutahakikisha kuwa mkulima ananufaika na kilimo chake kwa kuwafikishia wakulima pembejeo ikiwemo mbolea na mbegu kwa wakati; kuimarisha miundombinu ya kilimo na kuimarisha usimamizi wa vyama vya ushirika. Pia, Serikali itatoa kipaumbele katika kufungamanisha sekta ya kilimo na viwanda kwa lengo la kuongeza thamani na faida kwenye shughuli za kilimo.

### *Mifugo*

**57.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali inatambua kwamba mifugo bora na ya kisasa ni fursa kubwa ya kupunguza umaskini hapa nchini. Hata hivyo, ili mifugo hiyo iweze kuleta matokeo makubwa, hususan upatikanaji wa soko la uhakika ndani na nje ya nchi, hapana budi mifugo itambuliwe bayana. Kutokana na mahitaji hayo ya utambuzi, Serikali inatekeleza zoezi la utambuzi wa mifugo kwa njia ya chapa ya moto ambapo hadi Februari 2018, ng'ombe 16,408,022 wamepigwa chapa. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 94.4 ya ng'ombe 17,390,090 waliotegemewa kupigwa chapa. Zoezi hili ni endelevu na ninawaomba wadau watoe ushirikiano wa kutosha kwa Serikali ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

### *Maliasili na Utalii*

**58.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kutokana na umuhimu wa sekta ya maliasili na utalii katika ukuaji wa Pato la Taifa na kuongeza ajira, Serikali inaongeza juhudi za kulinda rasilimali za Taifa ikiwemo misitu, wanyamapori, malikale, ufugaji nyuki, uvuvi, pamoja na kuhakikisha rasilimali hizo zinanufaisha vizazi vya sasa na vijavyo. Serikali pia imechukua hatua za kuimarisha mifumo ya kukusanya mapato katika sekta hizo, kupambana na ujangili, kuzuia upotevu wa mazao ya misitu na kutatua migogoro ya mipaka kati ya vijiji na hifadhi. Katika mwaka 2017/2018, Serikali imeanza mapitio ya Sera za Taifa za Utalii, Misitu na Ufugaji Nyuki ili ziendane na mazingira ya sasa na kuimarisha zaidi ulinzi wa rasilimali hizo.

**59.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kutokana na juhudi zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha sekta ya utalii, idadi ya watalii walioingia nchini mwaka 2017 imeongezeka hadi kufikia watalii milioni 1.33 ikilinganishwa na watalii milioni 1.28 mwaka 2016. Pia, mapato yameongezeka na kufikia Dola za Marekani bilioni 2.19 mwaka 2017 ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 2.13 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia sita. Takwimu hizo zinabainisha kwamba, sekta ya utalii ina fursa kubwa ya kulipatia taifa fedha za kigeni na

kuzalisha ajira kwa wingi. Tutaendelea kuimarisha sekta hii kwa kuvutia wawekezaji zaidi na kuimarisha miundombinu ya maeneo ya utalii pamoja na kuhamasisha utalii wa ndani, utalii wa mambo ya kale na kihistoria katika miji ya zamani ikiwemo Bagamoyo, Kilwa na Mikindani.

***Viwanda***

**60.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** sote tunatambua kwamba kaulimbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kujenga uchumi wa Taifa unaotegemea viwanda. Hadi kufikia mwezi Februari 2018, viwanda vipya 3,306 vimeanzishwa. Aidha, Serikali inahamasisha uwekezaji katika viwanda kwa kutoa vivutio vya kodi na visivyo vya kodi kwa wawekezaji mahiri; kuendeleza na kuboresha miundombimu wezeshi kama vile barabara, reli, bandari, umeme na maji. Pia, kuhuisha sera, sheria na kanuni pamoja na kufuatilia utendaji wa viwanda vilivyobinafsishwa na kuchukua hatua stahiki kwa wamiliki walioenda kinyume na mikataba ya mauzo. Vilevile, Mikoa na Halmashauri zote nchini zimeelekezwa kutenga maeneo ya uwekezaji wa viwanda.

**61.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** sekta ya hifadhi ya jamii inashiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi wa viwanda ambapo, pamoja na miradi mingine, NSSF na PPF kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza wanatekeleza mradi mkubwa wa uzalishaji wa sukari mkoani Morogoro. Lengo la Mradi huo ni kuzalisha tani 250,000 za sukari na umeme MW 40. Mradi huo unatekelezwa katika shamba la Mkulazi lililopo Ngerengere lenye ukubwa wa hekta 63,000 na shamba la gereza la Mbigiri lenye ukubwa wa ekari 12,000 lililopo Dakawa. Hadi sasa ekari 2,000 za mashamba ya miwa zimetayarishwa katika eneo la Mkulazi na ekari 1,100 zimepandwa miwa. Lengo la Serikali ni kukamilisha awamu ya kwanza ya ufungaji wa mitambo ya kiwanda cha Mbigiri ifikapo mwezi Desemba, 2018 ili uzalishaji uanze mwaka 2019. Miradi hii itakapokamilika itazalisha zaidi ya ajira 100,000. Aidha, tangu kuanza kwa utekelezaji wa mradi huu mwezi Juni, 2017 ajira za moja kwa moja 780 na ajira zisizo za moja

kwa moja 24,000 ikijumuisha wakulima wadogo wa mbegu na kilimo cha nje zimezalishwa.

**62.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Serikali itatoa kipaumbele katika kutekeleza miradi ya kielelezo, uanzishwaji wa kanda maalum za kiuchumi pamoja na kuboresha mazingira ya biashara na kuvutia uwekezaji katika sekta ya viwanda. Vilevile, Serikali itaweka msisitizo katika kubuni mikakati ya uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vidogo na vya kati.

***Madini***

**63.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imeimarisha usimamizi katika sekta ya madini ili kuiwezesha sekta hiyo kuchangia kikamilifu katika uchumi wa nchi, kuongeza mapato ya Serikali na kuzalisha ajira. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kukusanya taarifa za uzalishaji wa madini, kuimarisha ukaguzi wa uzalishaji na mauzo kwenye migodi mikubwa na midogo na kufuatilia ukusanyaji wa maduhuli. Zoezi la ukaguzi limewezesha kukamatwa kwa madini yaliyokuwa yakitoroshwa yenye thamani ya Dola za Marekani takriban 898,523 na shilingi milioni 557.

**64.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018 maduhuli ya Serikali yaliyokusanywa kutoka sekta ya madini yalifikia shilingi bilioni 180.4. Pamoja na mambo mengine, mafanikio hayo yametokana na usimamizi makini katika sekta ya madini na uamuzi wa Serikali kufungua soko la *Tanzanite* nchini. Aidha, Serikali imeimarisha soko la madini nchini kwa kuhakikisha kuwa madini yanauzwa kwa ushindani.

**65.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** itakumbukwa kwamba, tarehe 20 Septemba 2017, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alielekeza ujengwe ukuta katika eneo linalozunguka mgodi wa *Tanzanite* uliopo Mererani ili kuimarisha ulinzi na kudhibiti utoroshaji wa madini hayo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa ukuta huo wenye mzunguko wa

kilomita 24.5 umekamilika. Nitumie fursa hii, kuwapongeza viongozi na watendaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kukamilisha kazi hiyo kwa wakati.

**66.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kujenga uwezo wa wazawa ili washiriki kikamilifu katika sekta ya madini. Uwezeshaji huo utakwenda pamoja na utoaji mafunzo kwa wachimbaji wadogo kuhusu teknolojia mbadala ya uchenjuaji dhahabu kwa lengo la kupunguza athari za mazingira na maafa katika maeneo ya migodi. Aidha, Serikali itakamilisha taratibu za kumpata mwekezaji atakayejenga mitambo ya kuchenjua madini nchini.

## HUDUMA ZA KIUCHUMI

### *Ardhi*

**67.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kutokana na umuhimu wa rasilimali ya ardhi kama kitovu cha uzalishaji mali, Serikali inachuka hatua madhubuti za kuiendeleza. Hatua hizo ni pamoja na kutekeleza Mpango Kabambe wa Majiji, Manispaa na Miji; udhibiti wa migogoro baina ya watumiaji wa ardhi na uimarishaji wa Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi nchini. Napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba Mipango Kabambe ya Manispaa za Iringa, Singida na Mji wa Kibaha imekamilika na mipango mingine 20 ipo katika hatua mbalimbali za uandaaji. Hadi sasa, michoro 1,110 ya mipango miji iliidhinishwa kati ya 1,148 iliyopokelewa kutoka Halmashauri za miji mbalimbali. Natoa wito kwa wananchi wote nchini wanapofanya shughuli za maendeleo kuzingatia mipango kabambe inayoandaliwa na mamlaka za upangaji miji.

**68.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imechukua hatua kadhaa za kukabiliana na changamoto ya migogoro ya ardhi miongoni mwa watumiaji ikiwemo migogoro ya mipaka ya vijiji, wakulima na wafugaji, wanavijiji na hifadhi na mapori ya akiba. Moja ya hatua zilizochukuliwa ni kuunda timu ya kisekta ya kushughulikia migogoro ya ardhi ambayo

imetembelea Mikoa ya Geita, Kagera, Katavi, Morogoro na Tabora na kufanya majadiliano na wadau 1,106. Hatua mbalimbali za utatuzi wa migogoro ya ardhi zinaendelea kuchukuliwa.

***Nishati***

**69.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imechukua hatua thabiti kuhakikisha kunakuwepo na umeme wa kutosha na wa uhakika kwa ajili ya uchumi wa viwanda. Hatua zilizochukuliwa zinalenga kuongeza uzalishaji, kuboresha miundombinu ya usafirishaji wa umeme na kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme vijijini na mijini. Katika mwaka 2017/2018, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mikubwa ya Kinyerezi I (MW 185), Kinyerezi II (MW 240) na Mradi wa Umeme wa Maji wa Mto Rufiji (Stiegler's Gorge) utakaozalisha MW 2,100.

**70.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali pia imepanua na kuboresha miundombinu ya kusafirisha umeme kwa kutekeleza miradi mbalimbali. Miradi hiyo ni pamoja na: Mradi wa Rufiji - Chalinze - Dodoma wenye msongo wa kV 400; Mradi wa Singida – Arusha – Namanga wenye msongo wa kV 400; na Mradi wa Makambako – Songea wenye msongo wa kV 220. Utekelezaji wa miradi hii umeongeza hali ya upatikanaji umeme nchini kufikia asilimia 67.5. Aidha, uunganishaji umeme kwa watumiaji umefikia asilimia 49.5.

**71.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali inatekeleza awamu ya tatu ya Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA) ambao umepangwa kufikisha huduma ya umeme kwenye vijiji 7,873 ambavyo havijapata umeme nchini. Kati ya hivyo, vijiji 7,697 vimepangwa kupatiwa umeme wa Gridi ya Taifa na vijiji 176 pamoja na visiwa vitapatiwa umeme nje ya gridi kwani ndiyo njia muafaka ya kuvipatia umeme kwa sasa. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaongeza fedha za mfuko wa REA ili kuhakikisha vijiji vilivyosalia pamoja na taasisi zinazotoa huduma za kijamii vijijini zinapata umeme. Serikali pia,

itaendeleza miradi ya kuunganisha Gridi ya Taifa na gridi za nchi jirani za Zambia, Kenya, Burundi na Rwanda.

***Bomba la Mafuta (Hoima – Tanga)***

**72.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** tarehe 5 Agosti 2017, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Rais wa Jamhuri ya Uganda, Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni waliweka Jiwe la Msingi la Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi bandari ya Tanga. Uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa mradi huo kwa upande wa Uganda ulifanyika katika eneo la Hoima tarehe 11 Novemba, 2017. Bomba hilo la kusafirisha mafuta ghafi litakuwa na urefu wa kilometa 1,445 ambapo kilometa 1,115 zitajengwa Tanzania. Mradi huo utakuwa na manufaa kwa wananchi wa pande zote mbili ambapo ajira takriban 10,000 zitazalishwa wakati wa ujenzi na ajira zaidi ya 1,000 wakati wa uendeshaji wake.

***Barabara***

**73.** **Mheshimiwa Naibu Spika,** Serikali inaendelea kuboresha mtandao wa barabara nchini. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Februari 2018, ujenzi wa Km. 776.45 za barabara kuu kwa kiwango cha lami umekamilika na Km. 1,760 zinaendelea kujengwa. Aidha, barabara zenye urefu wa Km. 17,054 zimekarabatiwa katika kipindi hicho. Vilevile, ujenzi wa madaraja ya Kilombero na Kavuu umekamilika na ujenzi wa madaraja ya Sibiti, Mto Mara, Lukuledi, Ruhuhu, Momba na Mlalakuwa unaendelea. Madaraja mengine 996 katika maeneo mbalimbali nchini yamekarabatiwa.

**74.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali inaendelea na jitihada za kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Hadi kufikia Februari 2018, ujenzi wa barabara ya juu katika eneo la TAZARA ulifikia asilimia 70 na ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Ubungo (Ubungo Interchange) umeanza. Aidha, maandalizi ya

Awamu ya Pili hadi ya Nne ya Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka yanaendelea. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imepanga kujenga kilometa 597 za barabara kuu na za mikoa kwa kiwango cha lami na kilometa 72 za kiwango cha lami zitakarabatiwa.

***Barabara za Vijijini na Mijini***

**75.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imeanzisha Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tanzania Rural and Urban Roads Agency – TARURA) kwa lengo la kurahisisha huduma za usafirishaji na kuongeza kasi ya wananchi kujiletea maendeleo. TARURA imepewa jukumu la kusimamia ujenzi na matengenezo ya mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometa 108,946.2 za vijijini na mijini. Katika mwaka 2017/2018, TARURA imesimamia matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 4,183.3, madaraja 35, makalavati makubwa 43 na madogo 364 na *drift* nne. Napenda kutumia nafasi hii kutoa wito kwa TARURA kuwaelimisha wananchi, viongozi na watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu majukumu na mfumo wa utendaji kazi wake.

***Reli***

**76.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa (Standard Gauge) itakayokuwa na urefu wa Km. 1,219. Hadi sasa, ujenzi wa kipande cha kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro chenye Km. 300 umeanza na unatarajiwa kukamilika Novemba, 2019. Aidha, tarehe 14 Machi 2018, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa kipande cha kutoka Morogoro hadi Makutupora chenye urefu wa kilomita 422. Ujenzi wa reli hii utasaidia kukuza sekta nyingine za kiuchumi kama vile kilimo, viwanda, madini, utalii pamoja na kutoa fursa nyingi za ajira. Utekelezaji wa mradi huu unakadiriwa kutoa ajira 30,000 za moja kwa moja na nyingine 600,000 zisizo za moja kwa moja.

***Bandari***

**77.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Serikali imeendelea kuboresha Bandari ya Dar es Salaam ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafiri wa majini. Uboreshaji huo utaanza na Gati Na. 1 – 7; kuongeza kina na upana wa lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli; kuimarisha mtandao wa reli bandarini pamoja na kujenga gati maalumu la kuhudumia meli za magari. Vilevile, Mamlaka ya Bandari Tanzania imefungua ofisi katika baadhi ya nchi jirani kwa lengo la kuongeza urahisi wa kutoa huduma. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea na uboreshaji wa bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Aidha, Serikali itatekeleza mradi wa dirisha moja la forodha (Tanzania Electronic Single Window System-eSWS) ili kuwaweka pamoja wadau wote wa kuondosha shehena bandarini na mipakani. Kukamilika kwa mradi huo, kutarahisisha na kupunguza muda na gharama za utoaji na upitishaji wa shehena bandarini.

***Mawasiliano***

**78.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Serikali imeendelea kutekeleza Awamu ya Tatu ya mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa mtandao wa miundombinu ya itifaki (Internet Protocol – Multiplier Label Switching) pamoja na ujenzi wa kituo cha kuhifadhi *data* ambacho hadi sasa mifumo ya taasisi 27 imeunganishwa ukiwemo mfumo wa ukusanyaji mapato wa TRA. Kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho kutaongeza usalama, usiri wa *data*, kujikinga na majanga na kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali na muingiliano wa mifumo katika Kituo cha *Data* cha Taifa na vituo vingine vitakavyojengwa nchini.

**79.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya kufikisha huduma ya mawasiliano vijijini ambapo vijiji 1,921 vimepatiwa huduma hiyo. Aidha, Serikali imeimarisha huduma za simu na intaneti katika taasisi za umma zikiwemo shule, vituo vya afya, vituo vya polisi na

ofisi za posta. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kupanua matumizi yake hadi katika ngazi ya wilaya. Vilevile, kuendelea kusimamia kampuni za simu nchini ili ziweze kutoa kumbukumbu sahihi kwa lengo la kukokotoa mapato yatokanayo na malipo ya huduma za simu za kitaifa na kimataifa.

## HUDUMA ZA JAMII

### *Elimu*

**80.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imetekeleza kwa mafanikio mpango wa utoaji wa elimu ya awali na elimumsingi bila malipo. Tangu kuanza kwa mpango huo, Serikali imekuwa inapeleka kwa wakati na moja kwa moja shuleni fedha zote za ruzuku ya elimumsingi. Kiasi cha shilingi bilioni 20.8 kinapelekwa kila mwezi kwa shule zote za msingi na sekondari nchini, ikijumuisha fedha za posho maalum kwa Walimu Wakuu, Waratibu wa Elimu Kata na Wakuu wa Shule.

**81.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** utekelezaji mzuri wa mpango wa elimumsingi bila malipo umechangia kuimarika kwa mahudhurio ya wanafunzi darasani; kuongezeka kwa ubora wa elimu inayotolewa shuleni kutokana na kuboreshwa kwa mazingira ya kujifunzia na kufundishia na kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi. Kwa mfano, idadi ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza imeongezeka kutoka 1,568,378 mwaka 2015 hadi 2,120,667 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 35.2. Kwa mwaka huu, idadi ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza ni 2,078,379. Vilevile, wanafunzi waliofaulu mtihani wa kuhitimu darasa la saba na kujiunga na kidato cha kwanza imeongezeka kutoka wanafunzi 448,826 mwaka 2015 hadi wanafunzi 538,826 mwaka 2016; na mwaka 2017 wanafunzi 562,695 wamechaguliwa kuingia sekondari.

**82.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Serikali imejenga na kukarabati miundombinu ya shule za msingi na sekondari ikiwemo ukarabati wa shule za sekondari

kongwe 89 ili kuboresha mazingira ya shule na kuinua ubora wa elimu. Aidha, Serikali imenunua na kusambaza vifaa vya maabara vyenye thamani ya shilingi bilioni 16.9 kwa shule za sekondari 1,696 kwa ajili ya kuimarisha ujifunzaji wa masomo ya sayansi kwa nadharia na vitendo. Vilevile, walimu 3,347 wa masomo ya sayansi na hisabati na mafundi sanifu wa maabara 386 wameajiriwa.

**83.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kutoa kipaumbele kwenye elimu, imeleta hamasa kubwa kwa wananchi kuchangia maendeleo ya elimu. Napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa wananchi na wadau mbalimbali kuendelea kuchangia kwa hiari maendeleo ya elimu kupitia Ofisi za Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri. Aidha, naziagiza Halmashauri zote nchini kuratibu na kusimamia ipasavyo michango ya hiari ya elimu inayotolewa na wananchi na matumizi yake, hususan kwa kuanzisha Mfuko Maalum wa Elimu katika Halmashauri husika ambao utasimamiwa na Bodi.

**84.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imeongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka shilingi bilioni 365 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 483 mwaka 2017. Hatua hiyo imewezesha idadi ya wanaonufaika na mikopo hiyo kuongezeka kutoka wanafunzi 98,300 mwaka 2015 hadi wanafunzi 119,435 mwaka 2017/2018. Serikali pia inaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya vyuo vya elimu ya juu nchini ili kuboresha mazingira ya vyuo hivyo na kuviwezesha kuzalisha wataalam mahiri wanaoweza kujiajiri au kuajiriwa katika soko la ajira. Natoa wito kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na vyuo vya elimu ya juu na wadau wa elimu kufanya tathmini na kuboresha mfumo wa ufundishaji wa wanafunzi wa elimu ya juu nchini ili kuwapatia mbinu zitakazowawezesha kujiajiri.

**85.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imeandaa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu wa mwaka 2017 hadi 2021 pamoja na mpango kazi wake unaolenga kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Utekelezaji wa

mpango huo wa sekta ya elimu utasaidia kuongeza idadi ya wataalam wenye ujuzi wa kati na wa juu ifikapo mwaka 2021. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kutekeleza awamu ya pili ya ukarabati wa shule kongwe, kujenga ofisi za udhibiti ubora katika wilaya mbalimbali nchini, kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya shule za sekondari na kujenga vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari.

## Maji

### *Huduma ya Maji Vijijini*

**86.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini kwa kujenga, kupanua na kukarabati miradi ya maji. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya miradi 71 imekamilishwa vijijini na mingine 366 inaendelea kutekelezwa. Utekelezaji wa miradi hiyo, umewezesha kuongezeka idadi ya wananchi wanaopata maji vijijini. Pia, Serikali imepanga kubadilisha mitambo inayotumia nishati ya dizeli kusukuma maji na kufunga mitambo inayotumia nishati ya jua ili kuwapunguzia wananchi gharama za uendeshaji na matengenezo.

**87.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2018/2019, Serikali itakamilisha ujenzi wa miradi ya maji 387 kwenye Halmashauri mbalimbali nchini na kuanza miradi mipya ya maji vijijini; kutekeleza miradi ya maji vijijini katika maeneo kame na yenye shida kubwa ya maji; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa mabwawa pamoja na upanuzi wa miundombinu ya maji kutoka kwenye mabwawa na visima vilivyochimbwa. Vilevile, Serikali itaendelea na ujenzi wa miradi mikubwa ya maji katika maeneo ya Tabora, Kigoma na Same - Mwanga- Korogwe.

### *Huduma ya Maji Mijini*

**88.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Serikali imejenga, kupanua na kukarabati miradi ya maji katika maeneo mbalimbali mijini ili kufikia

malengo yaliyowekwa. Juhudi hizo zimewezesha hali ya upatikanaji wa maji kwenye miji mikuu ya mikoa kufikia wastani wa asilimia 78. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam na maeneo yanayohudumiwa na DAWASA, upatikanaji wa maji umefikia asilimia 75. Aidha, upatikanaji wa maji katika miji mikuu ya wilaya, miji midogo na maeneo yanayohudumiwa na miradi ya kitaifa umefikia asilimia 60. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kukamilisha miradi mingi ya maji iliyopo.

## Afya

### *Utoaji wa Chanjo*

**89.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali inasimamia shughuli za utoaji wa chanjo nchini ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyowekwa kitaifa na kimataifa yanafikiwa. Hadi sasa, Tanzania imefikia kiwango cha juu cha asilimia 97 ya utoaji wa chanjo ya *pentavalent* kwa watoto inayokinga magonjwa ya kifaduro, dondakoo, pepopunda, homa ya ini na mafua. Kutokana na kufikia kiwango hicho, mwezi Desemba 2017, Serikali ya Tanzania ilipongezwa na Shirika la Afya Duniani kwa hatua hiyo kubwa. Lengo la Shirika la Afya Duniani ni kila nchi kufikia kiwango cha uchanjaji wa asilimia 90.

**90.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** mafanikio hayo yamefikiwa kutokana na usimamizi madhubuti wa Serikali katika utoaji wa chanjo. Niwapongeze sana viongozi na watendaji wa sekta ya afya pamoja na mamlaka zote zinazohamasisha na kutoa huduma za chanjo hapa nchini.

### Upatikanaji wa Dawa, Vifaa na Vifaa Tiba

**91.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imeimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya. Bajeti kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa dawa, chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi imeongezwa kutoka shilingi bilioni 252 mwaka 2016/2017 na kufikia shilingi bilioni 269 mwaka 2017/2018. Kutokana na

ongezeko hilo, upatikanaji wa aina 135 ya dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini umeimarika na kufikia asilimia 89.6.

### *Huduma za Tiba za Kibingwa*

**92.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imeboresha na kuimarisha upatikanaji wa huduma za matibabu ya kibingwa nchini. Huduma zilizoimarishwa ni pamoja na upandikizaji wa figo na vifaa vya kuongeza usikivu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, upasuaji kwa kutumia tundu dogo na kufungua kifua katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete. Vilevile, Serikali imeimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ambapo dawa zinapatikana na muda wa kupata huduma ya mionzi ya saratani umepungua. Kutokana na maboresho hayo, idadi ya wagonjwa waliopewa rufaa ya matibabu nje ya nchi imepungua kutoka wagonjwa 304 mwaka 2016/2017 na kufikia 103 mwaka 2017/2018. Hatua hiyo imesaidia kupunguza gharama kubwa ambazo Serikali ingetumia kuwapeleka wagonjwa hao nje ya nchi.

### ULINZI NA USALAMA

**93.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** hali ya mipaka ya nchi yetu ni salama. Katika mwaka 2017/2018, Serikali imeendelea kuliimarisha Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kutoa mafunzo na mazoezi ya kijeshi, kulipatia vifaa, zana, mitambo bora na ya kisasa pamoja na kuweka na kuimarisha miundombinu muhimu na ya kimkakati ili kuliwezesha jeshi kutekeleza jukumu lake la ulinzi wa mipaka ya nchi yetu. Vilevile, Serikali imeweka alama za mipakani ili kuimarisha ulinzi na kulinda vema mipaka ya nchi. Aidha, Jeshi la Wananchi linashirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, mamlaka za kiraia na mataifa mengine kupambana na matishio mapya ya kiusalama yakiwemo ugaidi, uharamia, uhamiaji haramu, biashara haramu za dawa za kulevya na usafirishaji haramu wa binadamu.

**94.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Jeshi letu limeendelea kudumisha ushirikiano na nchi nyingine duniani kupitia mafunzo ya pamoja na operesheni za kikanda na kimataifa chini ya Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. Katika kutekeleza majukumu ya ulinzi wa amani, tarehe 7 Desemba 2017 nchi yetu ilipoteza askari 15 huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo katika mashambulizi mabaya zaidi kuwahi kutokea kwa askari wetu wanaolinda amani. Kwa mara nyingine, naomba kuungana na Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kuzipa pole familia za mashujaa hawa waliokuwa wakitekeleza majukumu yao ya ulinzi wa amani. Licha ya changamoto zinazojitokeza, Tanzania itaendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika kutekeleza majukumu ya ulinzi wa amani kwenye nchi mbalimbali duniani ili kuendelea kuifanya dunia kuwa mahali salama pa kuishi pamoja na kuyaongezea majeshi yetu uzoefu na mbinu za kisasa za ulinzi wa amani.

**95.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kwa upande wa usalama wa raia, Serikali imelipatia Jeshi la Polisi vitendea kazi muhimu ikiwemo vifaa vya kisasa vya mawasiliano na uchunguzi ili liweze kupambana na ujambazi na matukio mengine ya kihalifu nchini. Aidha, imejenga Kituo cha Kisasa cha Mawasiliano (Call Centre) Dar es Salaam ambacho kinawezesha wananchi kutoa taarifa ya matukio hayo kwa urahisi. Pia Serikali imehamasisha jamii kushiriki katika ulinzi wao na kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kwa lengo la kuwapatia taarifa za wahalifu na uhalifu. Natoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola ili kudhibiti matukio ya kihalifu nchini.

**96.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali inatekeleza mradi wa Uhamiaji Mtandao *(e-immigration)* ambapo mwezi Januari 2018, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Pasi Mpya ya Kusafiria ya Kielektroniki ya Kimataifa ya Afrika Mashariki. Kuzinduliwa kwa pasi hii kutapunguza vikwazo vya

kusafiri mipakani baina ya raia wa nchi wanachama, kuimarisha mahusiano na kuchochea shughuli za kiuchumi miongoni mwa raia wa Jumuiya hii. Natoa rai kwa Watanzania kuanza kutumia pasi hii na kuendelea kuchangamkia fursa mbalimbali za kiuchumi, kibiashara, ajira na elimu zinazopatika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**97.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** pamoja na hatua hiyo, Serikali imedhibiti wimbi la wakimbizi na wahamiaji haramu wanaoingia nchini kwa sababu mbalimbali. Aidha, ofisi tisa mpya za uhamiaji zimefunguliwa katika wilaya za Gairo, Iramba, Kakonko, Kilosa, Kiteto, Manyoni, Mvomero, Siha na Songwe kwa lengo la kuongeza udhibiti wa wahamiaji haramu. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kutekeleza awamu ya pili ya mradi wa uhamiaji mtandao.

**BUNGE**

**98.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, kumekuwa na mikutano mitatu ya Bunge ambapo masuala mbalimbali yalijadiliwa na kutolewa ufafanuzi na Serikali. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Mkutano huu wa Bajeti utakuwa unahitimisha idadi ya mikutano minne ya Bunge kwa mwaka huu wa fedha unaoishia Juni, 2018. Katika mikutano mitatu iliyopita, maswali ya msingi 359 na maswali ya nyongeza 1,002 yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Aidha, katika utaratibu wa maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu, maswali ya msingi 17 pamoja na mawili ya nyongeza yaliulizwa na kujibiwa. Miswada 15 ya Sheria ya Serikali iliwasilishwa, kujadiliwa na kupitishwa na Bunge.

**99.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** vilevile, Bunge liliratibu na kusimamia shughuli za vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge, kutoa huduma za *hansard*, utafiti, utawala na kutoa mafunzo kwa Waheshimiwa wabunge na watumishi wa Ofisi ya Bunge. Pia, Bunge lilijadili na kuridhia Maazimio matano yanayohusu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake ya kikatiba.

## MAHAKAMA

**100.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika kuongeza ufanisi wa utendaji wa mhimili wa Mahakama nchini. Katika mwaka 2017/2018, Mahakama imesikiliza na kukamilisha mashauri 494,525 kati ya 513,329, sawa na asilimia 96.3 ya mashauri yote katika ngazi zote za Mahakama. Hatua hii imesaidia kupunguza mlundikano wa mashauri katika mahakama zetu. Hali kadhalika, katika kipindi hicho Serikali imeanza ujenzi wa majengo ya Mahakama Kuu katika mikoa ya Kigoma na Mara. Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa Mahakama za Wilaya na za Mwanzo katika maeneo mbalimbali nchini.

## MASUALA MTAMBUKA

### *Mfumo wa Ufuatiliaji wa Shughuli za Serikali*

**101.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Serikali ilizindua Mfumo wa Kielektroniki wa Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Shughuli za Serikali. Mfumo huo unalenga kuongeza ufanisi katika uratibu wa shughuli za Serikali na kuiwezesha Serikali kufanya tathmini ya utoaji huduma kwa wananchi na mipango ya maendeleo. Mfumo huo umeanza kufanya kazi ambapo kwa sasa Wizara zote zinawasilisha utekelezaji wa shughuli zao kupitia mfumo huo. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaimarisha matumizi ya mfumo huo hasa katika ngazi za Mikoa na Halmashauri na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.

### Hifadhi ya Mazingira

**102.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza jukumu la usimamizi na uhifadhi wa mazingira nchini. Katika mwaka 2017/2018, Serikali imeongeza hamasa na ushirikishwaji mkubwa wa wananchi katika suala la usafi, utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika maeneo yote ikiwemo makazi yao. Hatua hiyo imetokana na ushiriki mkubwa wa viongozi wa kitaifa, mikoa na watendaji wa ngazi zote katika shughuli za usafi na uhifadhi wa mazingira.

**103.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** ili kuimarisha ukaguzi wa masuala ya hifadhi ya mazingira nchini, Serikali imeongeza idadi ya Wakaguzi wa Mazingira kutoka 62 hadi kufikia 512. Aidha, kaguzi 380 zimefanyika kwenye viwanda kwa lengo la kufanya tathmini za mazingira pamoja na kutoa elimu na uelewa kuhusu uendeshaji endelevu wa viwanda unaozingatia utunzaji bora wa mazingira.

**104.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kama nilivyoeleza katika Mkutano wa Kumi wa Bunge hili, napenda kusisitiza kwamba halmashauri zote nchini ziweke mpango mahsusi wa kuhifadhi mazingira unaojumuisha kupanda na kutunza miti. Serikali itaweka utaratibu wa upimaji wa utendaji wa wakuu wote wa mikoa na wilaya pamoja na wakurugenzi wa halmashauri unaozingatia uendelezaji na utunzaji wa mazingira katika maeneo yao.

### Vita Dhidi ya Dawa za Kulevya

**105.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Serikali imeimarisha utendaji wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kuipatia wataalamu, vifaa na kuongezea fedha. Aidha, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2015, imefanyiwa marekebisho ili kuondoa mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wake. Mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, ilikamata jumla ya watuhumiwa 11,071 na kati yao, watuhumiwa 3,486 ni wafanyabiashara wa dawa za kulevya ambao walifikishwa mahakamani. Watuhumiwa wengi waliokamatwa, walijihusisha na dawa za kulevya aina ya bangi, mirungi na *heroine*.

**106.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika kipindi hicho, jumla ya tani moja na kilo 561.28 za dawa aina ya *heroin* zilikamatwa. Kati ya hizo, kilo 196.28 zilikamatwa kwenye eneo la maji ya Tanzania na nchi kavu na tani moja na kilo 365 zilikamatwa kwenye bahari kuu kwa kushirikiana na washirika wa kimataifa na kuteketezwa. Aidha, kilo 5.2 za *cocaine,* tani 47.7 za bangi na tani 7.4 za mirungi zilikamatwa.

Mamlaka pia ilikamata lita 304,513 za vimiminika vya kemikali bashirifu na kilo 22,143 za kemikali bashirifu yabisi. Katika operesheni za uteketezaji wa mashamba ya bangi na mirungi, ekari 572.75 za bangi na ekari 64.5 za mirungi ziliteketezwa.

**107.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imeimarisha huduma za matibabu kwa watumiaji wa dawa za kulevya kwa kutumia *methadone* katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Mwananyamala na Temeke jijini Dar es Salaam. Vilevile Serikali imeanzisha vituo vipya vya tiba hiyo ili kuwafikia waathirika wengi zaidi nchini ambapo kliniki saidizi za kutibu waathirika wa dawa za kulevya zimeanzishwa katika hospitali za rufaa za mikoa ya Mbeya na Mwanza. Hadi kufikia Januari 2018, zaidi ya watumiaji 5,560 walikuwa wakipatiwa huduma za tiba ya *methadone* katika vituo mbalimbali nchini. Serikali pia imekuwa ikisimamia uanzishwaji wa nyumba za upataji nafuu (Sober House) ambazo hadi sasa idadi yake ni 22. Aidha, mwezi Februari 2018, Serikali ilizindua mwongozo wa uendeshaji wa *sober houses* unaolenga kuwawezesha wamiliki wa nyumba hizo kuwasaidia waathirika hao ipasavyo.

**108.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** mwezi Machi 2018, nchi yetu ilishiriki katika Mkutano wa 61 wa Kimataifa wa *Commission for Narcotic Drugs (CND*) uliofanyika Vienna, Austria na kushirikisha zaidi ya nchi 150. Katika mkutano huo, Tanzania ilitambuliwa kama nchi ya mfano katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya barani Afrika na kupewa heshima ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 28 wa Wakuu wa Vyombo vinavyopambana na Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya Duniani (HONLEA) kutoka Afrika, utakaofanyika Septemba 2018. Mkutano huo utatoa fursa kwa wataalam nchini kubadilishana taarifa, uzoefu, kujenga mahusiano na kujifunza mbinu zinazotumiwa na nchi nyingine katika kukabiliana na dawa za kulevya.

**109.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** natoa rai kwa viongozi na watendaji kuwaelimisha vijana kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, wananchi waendelee kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na

Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kutoa taarifa kuhusu wanaojihusisha na dawa hizo. Pia ni vema wazazi, walezi na jamii kuwa karibu na vijana wetu na kufuatilia nyendo zao ili kuwaepusha kuingia kwenye mkumbo wa matumizi ya dawa za kulevya.

**Vita dhidi ya Rushwa**

**110.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kupambana na rushwa pamoja na ufisadi. Katika kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya majalada 325 yalifanyiwa uchunguzi na TAKUKURU na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ambapo majalada 214 kati ya hayo yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani. Aidha, kesi 727 ziliendeshwa mahakamani na kesi 219 ziliamuliwa na watuhumiwa 138 walipatikana na hatia na kuhukumiwa. Kutokana na operesheni zilizofanywa na TAKUKURU katika maeneo ya ukusanyaji mapato, uzuiaji wa malipo hewa na ukaguzi wa miradi ya maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 58.4 ziliokolewa na kurejeshwa Serikalini.

**111.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** TAKUKURU pia imefuatilia miradi ya maendeleo 195 yenye thamani ya shilingi bilioni 154.1 katika sekta za elimu, afya, maji na ujenzi ili kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika kama zilivyokusudiwa na thamani ya fedha inapatikana. Katika ufuatiliaji huo, miradi 73 yenye thamani ya shilingi bilioni 30.9 ilibainika kuwa na kasoro katika utekelezaji wake. TAKUKURU imetoa mapendekezo ambayo yanafanyiwa kazi na Serikali na tayari hatua za kinidhamu na kisheria zimechukuliwa kwa wahusika.

**Mapambano Dhidi ya UKIMWI**

**112.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imedhamiria kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI katika jamiii. Ili kutekeleza azma hiyo, Mpango wa Kuzuia Maambukizi ya VVU kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto umepewa kipaumbele. Aidha, elimu ya UKIMWI imetolewa kupitia vyombo vya habari, majarida na vipeperushi. Vilevile,

elimu imetolewa kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo utoaji wa elimu rika pamoja na kuwashirikisha viongozi na watu mashuhuri, viongozi wa dini, sekta binafsi na kutekeleza programu za kupambana na UKIMWI mahali pa kazi. Kutokana na juhudi hizo, matokeo ya utafiti uliofanyika katika ngazi ya kaya kuanzia mwezi Oktoba 2016 hadi Agosti 2017 yanaonesha kuwa wastani wa kitaifa wa maambukizi ya VVU kwa watu wenye umri wa miaka 15 hadi 49 ni asilimia 4.7. Aidha, utafiti huo umebainisha kwamba kiwango cha maambukizi mapya ya VVU kwa mwaka ni asilimia 0.27.

**113.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali inatoa huduma kwa wananchi wanaoishi na virusi vya UKIMWI (WAVIU) nchini. Hadi kufikia Septemba 2017, WAVIU 972,127 sawa na asilimia 70 ya WAVIU wote walikuwa wanapatiwa dawa za kufubaza makali ya VVU (ARV's). Katika mwaka 2017/2018, Serikali kwa kushirikiana na wadau wamechangia zaidi ya shilingi bilioni 1.5 kwenye Mfuko Maalum wa UKIMWI ili kupunguza utegemezi kutoka kwa wafadhili. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaanza utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Nne wa Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2018/2019 hadi 2022/2023. Vilevile, kampeni maalum za kushawishi wanaume kushiriki katika kupima afya zao na vijana kujitambua zitaendeshwa.

**Uratibu wa Maafa**

**114.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu shughuli za usimamizi wa maafa nchini kwa kuzuia, kupunguza madhara na kujiandaa kukabiliana na maafa pindi yanapotokea. Aidha, mfumo wa ufuatiliaji wa taarifa za mabadiliko ya tabianchi na upatikanaji wa taarifa za tahadhari za awali ili kupunguza madhara ya maafa umeboreshwa. Serikali pia imekamilisha kusimika mashine 36 za kisasa za kufuatilia taarifa za hali ya hewa katika wilaya mbalimbali nchini pamoja na kuwaongezea uwezo wataalamu wa hali ya hewa. Jitihada hizi zimeongeza uhakika wa utabiri wa hali hewa nchini kufikia asilimia 87.

**115.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali imeimarisha ushirikiano katika masuala ya usimamizi wa maafa kupitia

Umoja wa Afrika na jumuiya za SADC, EAC na IGAD. Ushirikiano huo, umewezesha nchi wanachama kubadilishana taarifa za kuandaa utabiri wa hali ya hewa na matumizi yake katika kupunguza madhara ya maafa. Vilevile, nchi hizo zinabadilishana uzoefu pamoja na kutoa mafunzo ya usimamizi wa maafa kwa wataalam wa nchi wanachama. Katika mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kuzijengea uwezo Kamati za Usimamizi wa Maafa za Mikoa na Wilaya na kuratibu shughuli za kupunguza madhara ya maafa na misaada ya kibinadamu.

### Mbio za Mwenge wa Uhuru

**116.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali iliratibu mbio za Mwenge wa Uhuru kwa lengo la kukuza mshikamano na kuhimiza shughuli za maendeleo. Katika mbio hizo ambazo kilele chake kilikuwa tarehe 14 Oktoba 2017 Mjini Magharibi Zanzibar, miradi 1,512 yenye thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 1.06 iliwekewa mawe ya msingi na kuzinduliwa. Kati ya miradi hiyo, miradi 150 yenye thamani ya shilingi bilioni 568.8 ilikuwa ya viwanda. Uzinduzi wa mbio za mwenge kwa mwaka 2018 ulifanyika mkoani Geita tarehe 2 Aprili 2018 na kilele chake kitafanyika mkoani Tanga, tarehe 14 Oktoba 2018. Ninawasihi wananchi kushiriki kwa wingi wakati wa mbio za Mwenge wa Uhuru kwani zinalenga kuleta umoja na mshikamano kwa wananchi pamoja na kuhimiza shughuli za maendeleo.

## MAHUSIANO YA KIMATAIFA

**117.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** jukumu la kuimarisha mahusiano na mataifa mengine duniani, mashirika ya kimataifa na washirika wetu wa maendeleo limeendelea kuwa kipaumbele cha Serikali katika kutekeleza Sera yetu ya Mambo ya Nje. Katika kufanikisha jukumu hilo kwa ufanisi, Serikali inafanya mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ili iweze kukidhi mahitaji na matakwa ya sasa ya Tanzania katika kushughulikia siasa za kimataifa na diplomasia pamoja na masuala ya mtangamano wa kikanda na kuendeleza Umoja wa Afrika.

**118.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kwa mwaka 2018/2019, Serikali itaendelea kutekeleza diplomasia ya uchumi kwa kuvutia wawekezaji na watalii; kutafuta fursa za mafunzo; kuendelea kuwashirikisha Watanzania waishio ughaibuni kuchangia katika maendeleo ya nchi yao pamoja na kutafuta ajira na masoko ya bidhaa za Tanzania nje. Aidha, Serikali itaimarisha sera ya ujirani mwema kwa lengo la kukuza mahusiano na kufungua milango ya ushirikiano katika utekelezaji wa miradi ya kitaifa ya kipaumbele hususan, reli, barabara, nishati na biashara na majirani zetu.

Vilevile, Serikali itatoa msukumo kwa Mabalozi kutumia ushawishi wao kuitangaza vyema miradi ya kipaumbele na vivutio mbalimbali vilivyopo nchini na kutangaza lugha ya Kiswahili ambayo ikitumika vizuri inaweza kuwa chanzo cha ajira kwa Watanzania.

**HITIMISHO**

**119.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** wananchi wanashuhudia mafanikio makubwa ya kiuchumi na kijamii katika kipindi kifupi cha takriban miaka miwili na nusu tangu Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iingie madarakani. Mafanikio hayo yanatoa matumaini kwa Watanzania kwamba yale yaliyoahidiwa ndani ya kipindi cha miaka mitano yatatekelezwa.

**120.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** ili kufikia malengo ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/2019, Serikali pamoja na mambo mengine, itaweka mkazo katika kudhibiti upotevu wa mapato; kuimarisha mfumo wa kukusanya mapato hususan kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na kudhibiti matumizi ya fedha na rasilimali nyinginezo za umma. Aidha, msukumo utawekwa katika kuhimiza uwajibikaji wa watendaji wa Serikali na kuimarisha ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.

**121.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Mheshimiwa Rais wakati anazindua Bunge lako Tukufu tarehe 20 Novemba 2015, pamoja na mambo mengine aliweka wazi dhamira ya

Serikali ya Awamu ya Tano kujenga uchumi wa viwanda kwa lengo la kutengeneza ajira nyingi kwa Watanzania.

Ili kufikia azma hiyo, Serikali itaendelea kufanya yafuatayo:

**Mosi:** Kuimarisha na kudumisha amani, utulivu, mshikamano na umoja wa kitaifa uliopo ili kuleta maendeleo endelevu;

**Pili:** Kuboresha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato na utoaji huduma;

**Tatu:** Kujenga miundombinu muhimu ikiwemo reli, bandari, viwanja vya ndege, barabara na madaraja;

**Nne:** Kuimarisha uzalishaji na usambazaji wa nishati ya uhakika sambamba na kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi, mashamba na maeneo ya makazi na viwanda;

**Tano:** Kusimamia viongozi na watendaji wote ili kuondoa urasimu usio wa lazima pamoja na kuwahudumia wananchi wote bila ubaguzi wa aina yoyote; na

**Sita:** Kusimamia kikamilifu rasilimali zilizopo ili zitumike kwenye maeneo yanayochochea ukuaji uchumi na utoaji huduma bora kwa wananchi.

**122.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** natoa wito kwa kila mwananchi kuendelea kuunga mkono jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kufanya kazi kwa bidii, weledi, uadilifu uaminifu na kupiga vita rushwa.

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2018/2019**

***122.*** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kwa mwaka 2018/2019, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizopo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Moja**

**Arobaini na Tatu, Milioni Mia Sita Kumi na Nane, Mia Saba Sitini na Mbili Elfu na Mia Sita Tisini na Nane (Shilingi 143,618,762,698)**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Sabini na Nne, Milioni Mia Tano Ishirini na Saba, Mia Tatu Ishirini na Moja Elfu na Mia Sita Tisini na Nane (Shilingi 74,527,321,698)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida **na Shilingi Bilioni Sitini na Tisa, Milioni Tisini na Moja, Mia Nne Arobaini na Moja Elfu (Shilingi 69,091,441,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

**123.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** vilevile, naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Moja Ishirini na Tano, Milioni Mia Tano Ishirini na Moja, na Mia moja Elfu (Shilingi 125,521,100,000)** kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Mia Moja Kumi na Saba, Milioni Mia Mbili na Tano, Mia Nne Themanini na Saba Elfu (Shilingi 117,205,487,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Tatu Kumi na Tano, Mia Sita Kumi na Tatu Elfu (Shilingi 8,315,613,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

**124.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Kwa hivyo tutaendelea na utaratibu wetu. Nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyenijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu. Lakini pili niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Rufiji kwa kuendelea kuniombea dua na kuendelea kuniamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kuniamini na kwa kunirejesha kwenye Kamati tena hii ya Katiba na Sheria lakini kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kunichagua tena kwa mara nyingine kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 6(2)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari mwaka 2016, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Aidha, Kanuni ya 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo nchini iliyotengewa na kupokea fedha katika mwaka wa fedha 2017/2018 kuanzia tarehe 14 hadi 18 Machi, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti za Wizara na taasisi inayosimamia kuanzia tarehe 23 hadi 29 Machi, 2018 ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu ina Mafungu sita ya bajeti kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu;

(ii) Fungu 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu;

(iii) Fungu 65 – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu;

(iv) Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA);*

(v) Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi; na

(vi) Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

(i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

(ii) Kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018;

(iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2018/2019; na

(iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Orodha ya miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(a) Mradi Na. 6351 – Ujenzi wa Majengo (Fungu 37);

(b) Mradi Na. 6575 – Kujiandaa na Kukabili Maafa (Fungu 37);

(c) Mradi Na. 5306 - Kuimarisha Taarifa za Mabadiliko ya Tabia nchi na Mifumo ya Tahadhari (Fungu 37);

(d) Mradi Na. 4944 - Programu ya Kuendeleza Ushindani wa Sekta Binafsi (Fungu 37);

(e) Mradi Na. 4494 - Programu ya Uendelezaji Mifumo ya Masoko na Huduma za Kifedha Vijijini (Fungu 37);

(f) Mradi Na. 6207 – Programu ya Kusaidia Uchaguzi Tanzania (Fungu 61); na

(g) Miradi Na. 6218, 6581 na 4952 - Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (Fungu 65).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 tarehe 29 na 30 Machi, 2017 naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili, 2017 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi, 2018. Katika robo ya tatu ya mwaka huu wa fedha 2017/2018 uchambuzi huu pia ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 na kiasi cha fedha kilichopokelewa katika miradi ya maendeleo hadi kufikia mwezi Machi, 2018 lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu muelekeo wa mpango wa bajeti hii kwa mapato na matumizi ya Serikali katika mwaka wa fedha 2018/2019 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa maduhuli kwa

kulinganisha kiasi kilichokusanywa hadi mwezi Machi, 2018 na lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti mwezi Aprili, 2017. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya maduhuli Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake kama kutazama hali halisi ya kila taasisi kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Bunge liliidhinisha makadirio ya makusanyo ya maduhuli yenye jumla ya shilingi bilioni thelathini na sita, milioni hamsini na nne, laki saba themanini na nne elfu (36,054,784,000/=) hadi kufikia Februari, 2018 kiasi cha maduhuli kilichokusanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake ni shilingi bilioni ishirini na moja, milioni mia mbili sitini na moja na elfu sabini na nane mia mbili na nane (21,261,078,208/=) sawa na asilimia 58.9 ya lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 mafungu yaliyosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa shilingi bilioni sitini na saba, milioni tatu, laki saba na elfu tisa mia tatu thelathini na sita (67,003,709,336/=) kwa ajili ya matumizi ya kawaida hadi kufikia mwezi Februari, 2018 taasisi hizo zilipokea kiasi cha shilingi bilioni arobaini na tatu, milioni mia tatu arobaini na mbili na elfu ishirini na moja, mia tatu tisini na tatu (43,342, 021,393/=) sawa na asilimia 64.7 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa uwiano wa bajeti iliidhinishwa na upatikanaji wa fedha ya matumizi ya kawaida hadi kufikia mwezi Februari 2018 umeainishwa katika jedwali namba moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi huu unaonesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila fungu. Aidha, fedha iliyoongezeka katika bajeti ya Fungu 61 - Tume ya Taifa ya

Uchaguzi hadi kupokea zaidi ya asilimia 100 ya fedha zilizoidhinishwa ni kutokana na gharama za chaguzi ndogo zilizohitaji kiasi hicho cha fedha ili kukamilisha chaguzi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ili kurahisisha usimamizi wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi. Kwa hatua hii Kamati inaipongeza Hazina na Serikali kwa ujumla kwa kutoa fedha kwa wakati kama zilivyoidhinishwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Waziri Mkuu iliidhinishiwa fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha shilingi bilioni tisini na tatu, milioni mia tano sitini na tano, laki tatu sabini na mbili na mia saba sitini na tatu (93,565,372,763/=)ambapo kiasi cha shilingi bilioni sitini na moja, milioni mia tano sitini na tano, laki tatu sabini na mbili, mia saba sitini na tatu (61,565,372,763) ambazo ni sawa na Asilimia 65.8 ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa fedha za nje na shilingi bilioni thelathini na mbili (32,000,000,000/=) za bajeti ya maendeleo zilikuwa ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Februari, 2018 fedha za miradi zilizopokelewa ni shilingi bilioni arobaini na sita, milioni mia tano thelathini na mbili, laki tano arobaini na tano na mia tisa sabini na tisa tu (46,532,545,979/=) ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo, kati ya fedha hizo zilizopokelewa, fedha za ndani ni shilingi bilioni nne na milioni ishirini na tatu elfu, laki sita ishirini na tatu na mia moja (4,023,623,100) ambazo ni sawa na asilimia 6.54 ya fedha iliyokuwa imetengwa kama bajeti ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufafanuzi zaidi kuhusu mchanganuo wa mwenendo wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ilitegemea kwa kiasi kikubwa fedha za nje kwa mwaka wa fedha 2017/2018 jambo ambalo likiendelea linaweza kukwamisha utekelezaji wa maendeleo ya nchi hasa ukizingatia unyeti wa Ofisi hii. Kamati inaishauri Serikali kutafuta vyanzo mbadala vya ndani ya nchi katika kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2018/2019 tarehe 27 na 28 mwezi Machi 2018. Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 - 2020/2021). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2018/2019 umeainisha maeneo 23 ya vipaumbele yakiwemo;

(i) Kuchapa nyaraka mbalimbali za uendeshaji wa shughuli za Serikali Kuu, Bunge na Serikali za Mitaa;

(ii) Kujenga uwezo wa Serikali kukabiliana na maafa;

(iii) Kuratibu utekelezaji wa mpango wa ushiriki wa Watanzania kwenye uwekezaji *(Local Content);*

(iv) Kuratibu shughuli za Bunge na kushughulikia kero na malalamiko ya wananchi;

(v) Kuboresha mifumo ya uchaguzi;

(vi) Kumwezesha Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ndani na nje ya nchi pamoja na kuongoza shughuli za Serikali katika Mikutano ya Bunge;

(vii) Kuboresha Daftari la Kudumu la Kupiga Kura;

(viii) Kuhakiki maeneo ya uchaguzi *(Delimitation);*

(ix) Kuratibu na kusimamia masuala ya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia, kufariki au kupata madhara ya kiafya wakiwa kazini;

(x) Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini;

(xi) Kuratibu utekelezaji wa sera, sheria na mikakati ya kukuza ajira nchini na kuongeza nafasi za ajira za Watanzania nje ya nchi;

(xii) Kuratibu na kusimamia uwezeshaji na maendeleo kwa vijana;

(xiii) Kusimamia, kuratibu na kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu; na

(xiv) Kusimamia taasisi za umma zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliridhishwa na vipaumbele viliyowekwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa mwaka 2018/2019. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yapo katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, utaratibu wa chaguzi mbalimbali nchini na kukamilisha mipango ya Serikali kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vipaumbele hivyo Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi kaulimbiu ya Serikali

ya Awamu ya Tano ya kuwa na Tanzania yenye viwanda ili kuweza kutengeneza ajira kwa wananchi wengi na kuongeza fursa mbalimbali za biashara na mapato ya nchi na wananchi kwahivyo kupunguza utegemezi mkubwa wa bajeti kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Waziri Mkuu inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi bilioni thelathini na tisa, milioni mia nane tisini na saba, laki nane hamsini na tano na mia moja themanini na saba (39,897,855,187). Kiasi hicho kimeongezeka zaidi ya bilioni 3.84 ukilinganisha na maduhuli yaliyopangwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kamati imeridhishwa na nia thabiti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu kuongeza uwezo wa ukusanyaji Maduhuli katika kuchangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maduhuli haya yatakusanywa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu Na. 37), Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Fungu Na. 61), Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, (Fungu Na. 65) na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa (Fungu Na. 27). Sehemu kubwa ya makadirio ya maduhuli haya yanatokana na shughuli za Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali katika kuchapa nyaraka mbalimbali za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, pamoja na nyaraka za matukio maalum. Sehemu nyingine inayotegemewa kutoa maduhuli zaidi ni Fungu Na. 65 ambalo linahusisha taasisi mbalimbali zilizo katika sekta ya kazi, vijana, ajira na wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila fungu husika ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na.3

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba jumla ya shilingi bilioni sitini na sita, milioni mia moja sitini na mbili, laki saba themanini na tisa, na mia sita tisini na nane (66,162,789, 698) kwa ajili ya Katumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni kumi na tisa, milioni mia mbili, laki tano sabini na mbili na mia tano tisini na nne

(19,200,572,594) ni kwa ajili ya mishahara, na shilingi bilioni ishirini na tatu, milioni mia nane Ishirini na tisa, laki nne sitini na sita na hamsini na moja (23,829,466,051) ni ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Msajili wa Vyama vya Siasa. Shilingi bilioni ishirini na tatu, milioni mia Moja ishirini na tatu, laki saba na hamsini na moja na senti hamsini na tatu (23, 123, 751, 053) ni fedha za matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchanganuo wa mapato na matumizi kwa mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, mafungu ambayo yametengewa fedha nyingi kuliko mengine katika mwaka wa fedha ujao ni Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa (Fungu Na. 27) ambalo limetengewa shilingi bilioni kumi na tisa, milioni mia nne na sita, laki tatu arobaini na moja, (19,406, 341,000), Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu Na. 37) ambalo limetengewa shilingi bilioni kumi na saba, milioni mia nne Ishirini na saba, laki saba na elfu kumi na nne (17, 427, 714,000) na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ni (Fungu 65) ambalo limetengewa shilingi bilioni kumi na tatu, milioni mia sita arobaini na nne, na elfu sitini na saba, mia sita tisini na nane (13,644, 067,698).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake zimeombewa shilingi bilioni hamsini na nane, milioni mia saba tisini na moja, laki nne na elfu arobaini na moja (58,791, 441,000) kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizi shilingi bilioni thelathini na moja (31,000,000,000) ni fedha za ndani na shilingi bilioni ishirini na saba, milioni mia saba tisini na moja, laki nne na elfu arobaini na moja (27,791,441,000) ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha fedha za ndani kinachoombwa kwa miradi ya maendeleo ni kikubwa kuliko kiasi cha fedha za nje ukilinganisha na bajeti ya miradi ya maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2017/ 2018 ambapo kiasi cha fedha za nje kilikuwa ni kikubwa kuliko fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii ni ya kupongeza kwani inaonyesha nia ya kupunguza utegemezi wa fedha za nje katika kufadhili miradi ya maendeleo ambapo wakati mwingine upatikanaji wa fedha hizo huwa siyo wa uhakika na hivyo kukwamisha utekelezaji wa mipango ya Serikali kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, fedha inayotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2018/2019 ni pungufu kwa zaidi ya shilingi bilioni thelathini na nne (34,000,000,000), pungufu ambayo ni asilimia 37.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hiyo iliyotengwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu katika bajeti ya miradi ya maendeleo unatokana na kukamilika kwa ujenzi wa makazi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kiasi kikubwa hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika miradi ya maendeleo katika mwaka huu wa fedha umelenga katika maeneo saba yakiwemo:-

(i) Kujenga uwezo wa Serikali kukabiliana na maafa;

(ii) Kutekeleza mpango wa kukuza ujuzi na stadi za kazi katika viwanda, kilimo, biashara, utalii, usafirishaji, TEHAMA, madini, mafuta na gesi asilia;

(iii) Kuwajengea uwezo wa kiuchumi vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Vijana;

(iv) Kuratibu upatikanaji wa kazi na ajira na staha nchini;

(v)Kuratibu Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko na Huduma ya Kifedha Vijijini;

(vi) Kuendeleza ujenzi wa makazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mlimwa Dodoma; na

(vii) Kuimarisha upatikanaji wa taarifa ya mabadiliko ya tabianchi na mifumo ya tahadhari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na taarifa za Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 wa Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake. Aidha, maoni na ushauri wa Kamati umezingatia pia taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu; Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika mwaka wa fedha uliopita. Aidha, Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge kuhakikisha kwamba Kamati inafanya ziara za kikazi kukagua hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa makazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ili kujiridhisha na uthamini wa makazi hayo na kiasi cha fedha kilichotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha miundombinu ya kazi katika Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, Ofisi hiyo iendelee kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wake na kutoa taarifa kwa Kamati kuhusu hatua za utekelezaji zinazofikiwa. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba fedha zote zinazoombwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ofisi hii muhimu zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa haraka na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri zabuni za ujenzi wa miradi ya maendeleo zitolewe kwa uwazi

*(transparency and competitive bidding process)* na kipaumbele kitolewe kwa makampuni ya ndani ya wakandarasi yaliyokidhi vigezo na yenye uwezo wa kutekeleza na kukamilisha miradi kwa wakati na kwa mujibu wa mikataba ya miradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi yote ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha uliopita wa bajeti (2017/2018) na ile iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha ujao (2018/2019), Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe kwamba fedha zote za miradi ya maendeleo zinatumika kwa tija na kwa kuzingatia kanuni ya thamani ya fedha kwa miradi husika *(value for money).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendeleza jitihada zake za kuhakikisha inapunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa fedha za nje katika miradi ya maendeleo. Hatua hiyo inawezekana kama Serikali itaongeza vyanzo vipya vya mapato, ujenzi wa uendelezaji wa viwanda nchini, kuimarisha mifumo ya udhibiti na usimamizi wa mapato ya Serikali na kudhibiti matumizi ya maliasili za nchi kwa manufaa ya wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa; Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuchukua jitihada za kutosha kusuluhisha mgogoro kati ya Chama cha Wananchi (CUF) ili kuepusha athari kubwa zinazoweza kujitokeza katika Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inashauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na weledi katika usimamizi na utoaji wa ruzuku kwa vyama vya siasa na kuhakikisha kwamba taratibu husika zinafuatwa katika utoaji wa ruzuku hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ifanye ufuatiliaji na ukaguzi wa matumizi ya ruzuku kwa vyama vya siasa ili kuhakikisha kuwa matumizi ya ruzuku hizo yanazingatia madhumuni yaliyokusudiwa na ikibainika

ruzuku hizo zinatumika tofauti na madhumuni hayo, chama husika kisipewe ruzuku hiyo ili kutoa fundisho kwa vyama vyote kuzingatia matumizi stahiki ya fedha za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri na kusisitiza kwamba Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ihakikishe kunakuwepo na usimamizi wa karibu kwa kufuatilia na kuchunguza mienendo inayoharibu sifa na vigezo vya vyama vya siasa nchini na kwamba Msajili asisite kufutia usajili chama chochote cha siasa kitakachokiuka sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa vyama vya siasa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitarudia, Kamati inaishauri na kusisitiza kwamba Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ihakikishe kunakuwepo na usimamizi wa karibu kwa kufuatilia na kuchunguza mienendo inayoharibu sifa na vigezo vya vyama vya siasa nchini na kwamba Msajili asisite kufutia usajili chama chochote cha siasa kitakachokiuka sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa vyama vya siasa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF)* kuhakikisha kwamba unatoa elimu ya kutosha kwa waajiri na wafanyakazi hususani vyama vya wafanyakazi kwa lengo la kuhakikisha kwamba waajiri wote nchini wanazingatia matakwa ya sheria katika kuhakikisha wanajiandikisha kwenye mfuko, wanalipa ada/ michango stahiki kwa wakati na kutoa taarifa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri mfuko kuweka mkazo zaidi katika ulipaji fidia kwa wafanyakazi ambalo ndilo lengo kuu la mfuko na kuwepo mfumo mzuri wa kufanya tathmini za fidia kwa wafanyakazi wanaopata ajali kazini na kuhakikisha kwamba malipo ya fidia yanafanyika kwa haraka na kwa kila mfanyakazi aliyetimiza vigezo vya fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 65 - Kazi na Ajira; pamoja na Kamati kuipongeza Serikali kwa kutunga sheria

ya kuunganisha mifuko ya pensheni, Kamati inaendelea kushauri kuwa haki na maslahi ya wanachama wa mifuko iliyofutwa zilindwe na kutolewa kwa wakati bila usumbufu wowote. Aidha, Serikali ihakikishe ajira za wafanyakazi zinalindwa na taarifa za mabadiliko ya mifuko zitolewe haraka na kwa wakati kwa kila mfanyakazi na mnufaika bila usumbufu wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuishauri Mamlaka ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) kuendelea kusimamia afya na usalama mahala pa kazi na hasa kwa wafanyakazi wanaofanya kazi katika maeneo hatarishi kama migodini au viwandani na kuchukua hatua kali za kisheria kwa waajiri wote wasiozingatia masuala ya afya na usalama wa wafanyakazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuendelea kuboresha Daftari la Wapiga Kura na kuchukua jitihada za kutosha katika kuboresha daftari hili. Hatua hii ijumuishe utoaji wa elimu ya uraia hususani uandikishaji wa wapiga kura kwa vijana wengi zaidi ili waweze kutumia haki yao ya Kikatiba ya kupiga na kupigiwa kura. Hali hii itaongeza idadi ya Watanzania wengi zaidi watakaokuwa na sifa na vigezo vya kupiga kura katika chaguzi mbalimbali zinazokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Tume kujitahidi kufanya kazi kwa weledi ili kuendelea kuaminika kwa Wadau wake wa uchaguzi. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba, inawashirikisha wadau wa uchaguzi wakati wa uhuishaji wa Daftari la Wapiga kura ili kuepuka migogoro isiyokuwa na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba Tume ihakikishe inafuatilia wasimamizi wake wa uchaguzi na kuwawajibisha pale wanapofanya uzembe unaosababisha madhara ambayo yangeweza kudhibitiwa mapema na msimamizi aliye makini na anayetambua na kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria. Kamati yangu pia imeipongeza Tume kwa kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi wa hali ya juu. Nimshukuru pia kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Napenda nimpongeze pia kwa umahiri wake katika kasi ya kuliendesha Bunge hili katika kutekeleza kaulimbiu ya Hapa Kazi Tu na Tanzania ya Viwanda kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya wananchi na Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa weledi na umahiri wako katika kusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge wote kwa kazi nzuri kwanza kwa kuteuliwa siku ya jana, lakini pia kwa kazi yao nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya njema katika kutekeleza majukumu yenu mliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru sana Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Bunge, Sera, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Naibu Waziri, Mheshimiwa Antony Mavunde, *a.k.a* Tony, Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, Makatibu Wakuu na wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee kabisa napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu. Naomba majina yao yote kama yalivyo katika taarifa hii yaingie katika *Hansard.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati yangu kukamilisha kazi yake bila kukwama.

Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Stanslaus Kagisa, Ndugu Dunford Mpelumbe na Msaidizi wa Kamati Ndugu Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii kwa wakati. *(Makofi)*

Napenda pia kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* Ndugu Hanifa Masaninga na watendaji wote wa Idara hiyo kwa kuhakikisha kwamba taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Bunge, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI WA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge la 11.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 (2)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu. Aidha, Kanuni ya 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo nchini, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kuanzia tarehe 14 hadi 18 Machi 2018. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kuanzia tarehe 23 hadi 29 Machi, 2018 ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu ina Mafungu 6 ya bajeti kama ifuatavyo;

i) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu,
ii) **Fungu 25** - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu,
iii) **Fungu 65** – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu,
iv) **Fungu 15** - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA),
v) **Fungu 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), na
vi) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na;

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati

## 2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/ 2018

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Orodha ya Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

**a) Mradi Na. 6351** – Ujenzi wa Majengo **(Fungu 37)**

**b) Mradi Na. 6575** – Kujiandaa na Kukabili Maafa **(Fungu 37)**

**c) Mradi Na.5306** - Kuimarisha Taarifa za Mabadiliko ya Tabia nchi na Mifumo ya Tahadhari **(Fungu 37)**

**d) Mradi Na. 4944-** Programu ya Kuendeleza Ushindani wa Sekta Binafsi **(Fungu 37)**

**e) Mradi Na. 4494-** Programu ya Uendelezaji Mifumo ya Masoko na Huduma za Kifedha Vijijini **(Fungu 37)**

**f) Mradi Na.6207** –Programu ya Kusaidia Uchaguzi Tanzania **(Fungu 61)**

**g) Miradi Na.6218, 6581 na 4952-** Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi **(Fungu 65)**

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA OFISI YA WAZIRI MKUU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa fedha 2018/2019, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 tarehe 29 na 30 Machi, 2017. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2017 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi 2018 katika Robo ya Tatu ya Mwaka huu wa fedha 2017/2018. Uchambuzi huu pia ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kiasi cha Fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Machi 2018. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa hadi Machi 2018 na lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi

Aprili 2017. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake kama kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

## 3.2 Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Bunge liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Thelathini na Sita, Milioni Hamsini na Nne, Laki Saba Themanini na Nne Elfu (36,054,784,000/=).** Hadi kufikia Februari , 2018 kiasi cha Maduhuli kilichokusanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake ni **Shilingi Bilioni Ishirini na Moja, Milioni Mia Mbili Sitini na Moja, Sabini na Nane Elfu na Mia Mbili na Nane tu (21,261,078,208)** sawa na **asilimia 58.9** ya lengo lililokusudiwa.

## 3.3 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Mafungu yanayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa **Shilingi Bilioni Sitini na Saba, Milioni Tatu,Laki Saba na Tisa Elfu na Mia Tatu Thelathini na Sita (67,003,709,336 /=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Februari 2018 Taasisi hizo zilipokea **Shilingi Bilioni Arobaini na Tatu, Milioni Mia Tatu Arobaini na Mbili na Ishirini na Moja Elfu, Mia Tatu Tisini na Tatu (43,342, 021,393) sawa na asilimia 64.7% ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.**

Uchambuzi wa uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha ya Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari 28, 2018 umeainishwa katika **Jedwali Na. 1**

**JEDWALI NA. 1: Uchambuzi wa Uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari, 2018**

| NA. | FUNGU | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | FEDHA ILIYOPATIKANA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 37-OFisi ya Waziri Mkuu | 21,819,483,336 | 10,204,275,965 | 46.8 |
| 2 | 25- Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 5,923,228,000 | 4,228, 560,201 | 71.4 |
| 3 | 65 – Kazi, Ajira ,Vijana na Wenye Ulemavu | 11,561,196,000 | 7,239,972,429 | 62.6 |
| 4 | 27- Msajili wa Vyama vya Siasa | 19,525,938,000 | 12,768,806,400 | 65.4 |
| 5 | 15-Tume ya Usuluhishi na Uamuzi | 3,409, 750,000 | 1,991,892,331 | 58.4 |
| 6 | 61- Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 4,764,294,000 | **6,908,514,067** | **145** |
| | **JUMLA** | **67,003,889,336** | **43,342,021,393** | **64.7** |

**Chanzo: Taarifa ya WN-OWM, tarehe 27 Machi, 2018**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na Mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu. Aidha, Fedha iliyoongezeka katika Bajeti ya Fungu 61(Tume ya Taifa ya Uchaguzi) hadi kupokea zaidi ya asilimia 100% ya fedha zilizoidhinishwa, ni kutokana na gharama za Chaguzi ndogo zilizohitaji kiasi hicho cha fedha ili kukamilisha chaguzi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upataikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ili kurahisisha usimaimizi na Utekelezaji wa Shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi. Kwa hatua hii, Kamati inaipongeza Hazina na Serikali kwa Ujumla kwa kutoa Fedha kwa wakati kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

### 3.4 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018,

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Ofisi ya Waziri Mkuu iliidhinishiwa Fedha za Miradi ya Maendeleo

kiasi cha **Shilingi Bilioni Tisini na Tatu, Milioni Mia Tano Sitini na Tano, Laki Tatu Sabini na Mbili Elfu , Mia Saba Sitini na Tatu(93, 565, 372, 763 )** ambapo kiasi cha **Shilingi Bilioni Sitini na Moja, Milioni Mia Tano Sitini na Tano, Laki Tatu Sabini na Mbili Elfu, Mia Saba Sitini na Tatu (61, 565, 372, 763)** ambazo ni sawa na **Asilimia 65.80%** ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa Fedha za Nje na **Shilingi Bilioni Thelathini na Mbili (32, 000,000,000), ambayo ni sawa na Asilimia 34.20%** ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Februari, 2018 Fedha za Miradi zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni Arobaini na Sita, Milioni Mia Tano Thelathini na Mbili, Laki Tano Arobaini na Tano Elfu, Mia Tisa Sabini na Tisa (46, 532, 545, 979) sawa na asilimia 49.7%** tu ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo, kati ya fedha hizo zilizopokelewa, fedha za ndani ni **Shilingi Bilioni Nne na Milioni Shirini na Tatu Elfu, Laki Sita Ishirini na Tatu, Mia Moja( 4, 023, 623, 100)** ambazo ni sawa na **asilimia 6.54%** ya Fedha iliyokuwa imetengwa kama bajeti ya Ndani.

**Mheshimiwa Spika,** ufafanuzi zaidi kuhusu mchanganuo wa mwenendo wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni kama inavyoainishwa katika Jedwali lifuatalo, **(Jedwali Na.2):-**

**JEDWALI NA.2: Mwenendo wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo hadi Februari, 2018**

| FUNGU | NA.YA MRADI | JINA LA MRADI | FEDHA ZILIZOIDHINISHWA 2017/2018 | | FEDHA ZILIZOPOKELEWA HADI FEB.2018 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani | Fedha za Nje | F/Ndani | F/Nje | Asilimia % |
| 37 | 6351 | Ujenzi wa Majengo-OWM | 5,000,000,000 | 0 | 4,023,623,100 | | 80.5 |
| | 6575 | Mradi wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa | 0 | 440,000,000 | 0 | 0 | 0 |
| | 5306 | Mradi wa Kuimarisha Taarifa za Mabadiliko ya Tabianchi na Mifumo ya Tahadahari | 0 | 1,021, 618,000 | 0 | 283,986,200 | 27.80 |
| | 4944 | Programu ya Kuendeleza Ushindani wa Sekta Binafsi | 300,000,000 | 16,258,594,844 | 0 | 0 | 0 |
| | 4494 | Programu ya Uendeezaji Mifumo ya Masoko na Huduma za Kifedha Vijijini | 700,000,000 | 42,445,159,919 | 0 | 40,957,778,948 | 95 |
| 61 | 6207 | Programu ya Kusaidia Uchaguzi Tanzania | 10,000,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 65 | 6218 | Mradi Unaotekelezwa kwa Pamoja na ILO | 0 | 1,400,000,000 | | 319,505,139 | 23 |
| | 6581 | Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini | 15,000,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 4952 | Mfuko wa Maendeleo ya Vijana | 1,000,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| JUMLA | | | **32,000,000,000** | **61,565,372,763** | **4,023,623,100** | **42,508,922,878** | |
| | | | **93,565,372,763** | | **46,532,545,979** | | **49.7** |

**Chanzo: Taarifa ya WN-OWM, tarehe 27 Machi, 2018**

### 3.5 Yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ilitegemea kwa kiasi kikubwa fedha za Nje kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 jambo ambalo likiendelea linaweza kukwamisha utekelezaji wa maendeleo ya nchi hasa ukizingatia unyeti wa Ofisi hii. Kamati inashauri Serikali kutafuta vyanzo mbadala vya ndani ya nchi katika kugharamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 tarehe 27 na 28 Machi 2018. ***Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021).***

### 4.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 umeainisha maeneo 23 ya viapumbele yakiwemo;

i) Kuchapa Nyaraka mbalimbali za Uendeshaji wa Shughuli za Serikali Kuu, Bunge na Serikali za Mitaa,

ii) Kujenga uwezo wa Serikali kukabiliana na Maafa;

iii) Kuratibu Utekelezaji wa Mpango wa Ushiriki wa Watanzania kwenye Uwekezaji (Local Content);

iv) Kuratibu Shughuli za Bunge na kushughulikia kero na malalamiko ya Wananchi;

v) Kuboresha Mifumo ya Uchaguzi,

vi) Kumwezesha Waziri Mkuu kutekeleza Majukumu yake kwa ufaninisi Ndani na Nje ya Nchi pamoja na kuongoza Shughuli za Serikali katika Mikutano ya Bunge

vii) Kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura,

viii) Kuhakiki Maeneo ya Uchaguzi (Delimitation)

ix) Kuratibu na Kusimamia Masuala ya Fidia kwa Wafanyakazi wanaoumia, kufariki au kupata madhara ya kiafya wakiwa kazini,

x) Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini,

xi) Kuratibu Utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati ya Kukuza Ajira nchini na kuongeza nafasi za Ajira za Watanzania nchi za nje,

xii) Kuratibu na kusimamia Uwezeshaji na Maendeleo ya Vijana,

xiii) Kusimamia, Kuratibu na kutoa huduma kwa Watu wenye Ulemavu, na

xiv) Kusimamia Taasisi za Umma zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na Vipaumbele viliyowekwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2018/2019. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yapo katika Ofisi ya Waziri

Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Uratibu wa Chaguzi mbalimbali nchini na kukamililisha mpango wa Serikali kuhamia Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na vipaumbele hivyo Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi Kauli Mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na Tanzania yenye Viwanda ili kuweza kutengeneza Ajira kwa Wananchi wengi na kuongeza fursa mbalimbali za biashara na mapato kwa nchi na Wananchi na hivyo kupunguza utegemezi mkubwa wa kibajeti kutoka nje ya Nchi.

### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Ofisi ya Waziri Mkuu inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni Thelathini na Tisa, Milioni Mia Nane Tisini na Saba, Mia Nane Hamsini na Tano na Mia Moja Themanini na Saba (39,897,855,187/=).** ***Kiasi hicho kimeongezeka zaidi ya Bilioni 3.84 ukilinganisha na Maduhuli yaliyopangwa kukusanywa kwa mwaka wa Fedha 2017/2018. Kamati imeridhishwa na nia thabiti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu kuongeza uwezo wa ukusanyaji Maduhuli katika kuchangia pato la Taifa.***

**Mheshimiwa Spika,** Maduhuli haya yatakusanywa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu **(Fungu 37),** Tume ya Taifa ya Uchaguzi (**Fungu 61),** Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, **(Fungu 65)** na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa (**Fungu 27).** Sehemu kubwa ya Makadirio ya Maduhuli haya yatatokana na shughuli za Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali katika kuchapa Nyaraka mbalimbali za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, pamoja na Nyaraka za matukio maalumu. Sehemu nyingine inayotegemewa kutoa Maduhuli zaidi ni Fungu 65 ambalo linahusisha Taasisi mbalimbali zilizo katika Sekta ya Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila Fungu Husika ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali lifuatalo **(Jedwalu Na.3);- Jedwali Na.3; Makisio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

| FUNGU | TAASISI HUSIKA | MADUHULI YALIYOIDHINISHWA 2017/2018 | MAKADIRIO YA MADUHULI 2018/2019 |
|---|---|---|---|
| 27 | Msajili wa Vyama vya Siasa | 175,000 | 175,000 |
| 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 1,010,003,000 | 1,000,000,000 |
| 61 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 15,000,000 | 15,000,000 |
| 65 | Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu | 35,029,605,100 | 38,882,855,187 |
| **JUMLA** | | **36,054,7883, 100** | **39,897,855,187** |

## 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba jumla ya **Shilingi Bilioni Sitini na Sita, Milioni Mia Moja Sitini na Mbili, Laki Saba Themanini na Tisa, Mia Sita Tisini na Nane (66,162,789, 698/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Mbili, Laki Tano Sabini na Mbili Elfu, Mia Tano Tisini na Nne (19,200,572,594/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Nane Ishirini na Tisa, Laki Nne Sitini na Sita Elfu na Hamsini na Moja(23,829,466,051/=)** ni Ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Msajili wa Vyama vya Siasa na **Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Moja Thelathini na Mbili, Laki Saba Hamsini na Moja Elfu na Hamsini na Tatu (23, 132, 751, 053/=**) ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa Mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mafungu ambayo yametengewa fedha nyingi kuliko mengine katika Mwaka wa Fedha ujao ni Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa **(Fungu 27)** ambalo limetengewa **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Nne na Sita,Laki Tatu**

**Arobaini na Moja Elfu, (19,406, 341,000/=)**, Ofisi ya Waziri Mkuu **(Fungu 37)** ambalo limetengewa **Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Nne Ishirini na Saba, Laki Saba Kumi na Nne Elfu (17, 427, 714,000/=)** na Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu**(Fungu 65)** ambalo limetengewa **Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Sita Arobaini na Nne, Sitini na Saba Elfu na Mia Sita Tisini na Nane(13,644, 067,698).**

### 4.4 Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake zimeombewa **Shilingi Bilioni Hamsini na Nane, Milioni Mia Saba Tisini na Moja, Laki Nne Arobaini na Moja Elfu(58,791, 441,000/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizi **Shilingi Bilioni Thelathini na Moja (31,000,000,000/=)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Mia Saba Tisini na Moja, Laki Nne Arobaini na Moja Elfu (27,791,441,000/=)** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kiasi cha Fedha za Ndani kinachoombwa kwa Miradi ya Maendeleo ni kikubwa kuliko kiasi cha Fedha za Nje ukilinganisha na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka 2017/2018 ambapo kiasi cha Fedha za Nje kilikuwa kikubwa kuliko Fedha za Ndani.

**Mheshimiwa Spika,** hatua hiyo ni ya kupongezwa kwani inaonyesha nia ya kupunguza utegemezi wa Fedha za Nje katika kufadhili Miradi ya Maendeleo ambapo wakati mwingine upatikanaji wa fedha hizo huwa siyo wa uhakika na hivyo kukwamisha utekelezaji wa Mipango ya Serikali kwa Wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, fedha iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 ni pungufu kwa zaidi ya **Bilioni 34** , pungufu ambayo ni **asilimia 37%** ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, Upungufu katika Bajeti ya Miradi ya Maendeleo unatokana na kukamilika kwa Ujenzi wa Makazi ya Waziri Mkuu kwa kiasi kikubwa hapa Mjini Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Miradi ya Maendeleo katika Mwaka huu wa Fedha umelenga katika **maeneo 7** yakiwemo:-

i) Kujenga Uwezo wa Serikali kukabiliana na Maafa
ii) Kutekeleza Mpango wa Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi katika Viwanda, Kilimo, biashara, Utalii, Usafirishaji, TEHAMA, Madini, Mafuta na Gesi Asilia,
iii) Kuwajengea Uwezo wa Kiuchumi Viajana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana,
iv) Kuratibu upatikanaji wa Kazi na Ajira na Staha Nchini,
v) Kuratibu Programu ya kuendeleza Mifumo ya Masoko na Huduma ya Kifedha Vijijini, na
vi) Kuendeleza Ujenzi wa Makazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mlimwa Dodoma, na
vii) Kuimarisha Upatikanaji wa Taarifa za Mabadiliko ya Tabianchi na Mifumo ya Tahadhari.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake. Aidha, Maoni na Ushauri wa Kamati umezingatia pia Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

## 5.1 FUNGU 37- Ofisi ya Waziri Mkuu

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Mwaka wa Fedha uliopita. Aidha Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge

kuhakikisha Kamati inafanya Ziara ya kikazi kukagua hatua iliyofikiwa katika Ujenzi wa Makazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ili kujiridhisha na uthamani wa Makazi hayo na kiasi cha fedha kilichotumika.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha Miundombinu ya kazi katika Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, Ofisi hiyo iendelee kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi wake na kutoa taarifa kwa Kamati kuhusu hatua za utekelekelezaji zitakazofikiwa. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa fedha zote zinazoombwa na kuidhininshwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii muhimu zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa haraka na kwa ufanisi.

iii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Zabuni za ujenzi wa Miradi ya Maendeleo zitolewe kwa uwazi (Transparent and Competitive Bidding Process) na kipaumbele kitolewe kwa Makampuni ya Ndani ya Wakandarasi yaliyokidhi vigezo na yenye uwezo wa kutekeleza na kukamilisha Miradi kwa wakati na kwa mujibu wa Mikataba ya Miradi husika.

iv) **Mheshimiwa spika**, katika Miradi yote ya Maendeleo iliyotengewa fedha Mwaka uliopita wa Bajeti (2017/2018) na ile iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha ujao (2018/2019), Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe fedha zote za Miradi ya Maendeleo zinatumika kwa tija na kwa kuzingatia Kanuni ya thamani ya fedha kwa miradi husika *(Value For Money).*

v) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuendeleza jitihada zake za kuhakikisha inapunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa Fedha za Nje katika Miradi ya Maendeleo. Hatua hiyo inawezekana kama Serikali itaongeza vyanzo vipya vya Mapato, Ujenzi na Uendelezaji wa Viwanda nchini, kuimarisha Mifumo ya Udhibiti na usimamizi wa Mapato ya Serikali na kudhibiti Matumizi ya Maliasili za nchi kwa manufaa ya Wengi.

## 5.2 Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuchukua jitihada za kutosha kusuluhisha migogoro katika Chama cha Wananchi - CUF ili kuepusha athari kubwa zinazoweza kujitokeza katika Muungano.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inashauri Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na weledi katika usimamizi na utoaji wa ruzuku kwa vyama vya siasa na kuhakikisha kwamba taratibu husika zinafuatwa katika utoaji wa ruzuku hizo.

iii) **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ifanye ufuatiliaji na ukaguzi wa Matumizi ya Ruzuku kwa Vyama vya Siasa ili kuhakikisha kuwa matumizi ya Ruzuku hizo yanazingatia madhumuni yaliyokusudiwa na ikibainika Ruzuku hizo zinatumika tofauti na madhumuni hayo, Chama husika kisipewe Ruzuku ili kutoa fundisho kwa vyama vyote kuzingatia matumizi stahiki ya fedha za Wananchi.

iv) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri na kusisitiza kwamba, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ihakikishe kunakuwepo na Usimamizi wa karibu kwa kufuatilia na kuchunguza mienendo inayoharibu sifa na vigezo vya Vyama vya Siasa nchini na kwamba Msajili asisite kufuta Usajili wa Chama Chochote cha Siasa kitakachokiuka Sheria, Kanuni na Taratibu za Uendeshaji wa Vyama vya Siasa hapa nchini.

## 5.3 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)

i) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Mfuko kuhakikisha unatoa Elimu ya kutosha kwa Waajili na Wafanyakazi hususan vyama vya Wafanyakazi kwa lengo la kuhakikisha kuwa Waajili wote nchini wanazingatia matakwa ya Sheria katika kuhakikisha Wanajiandikisha kwenye Mfuko, wanalipa Ada/Michango stahiki kwa wakati na kutoa taarifa sahihi.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Mfuko kuweka mkazo zaidi katika ulipaji fidia kwa Wafanyakazi ambalo ndilo lengo kuu la Mfuko na kuweka Mfumo mzuri wa kufanya tathmini za fidia kwa Wafanyakazi wanaopata ajali kazini na kuhakikisha kwamba malipo ya fidia yanafanyika kwa haraka kwa kila Mfanyakazi aliyetimiza vigezo vya fidia.

5.4 **FUNGU 65 - Kazi na Ajira**

i) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuipongeza Serikali kwa kutunga Sheria ya Kuunganisha Mifuko ya Pensheni, Kamati inaendelea kushauri kuwa, haki na maslahi ya Wanachama wa Mifuko iliyofutwa zilindwe na kutolewa kwa Wakati bila usumbufu wowote. Aidha, Serikali ihakikishe ajira za Wafanyakazi zinalindwa na taarifa za Mabadiliko ya Mifuko zitolewe haraka na kwa Wakati kwa kila Mfanyakazi na Mnufaika bila usumbufu wowote.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Mamlaka ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) kuendelea kusimamia Afya na Usalama wa Wafanyakazi Mahali Pa Kazi na hasa kwa Wafanyakazi wanaofanya kazi katika maeneo hatarishi kama Migodini au Viwandani na kuchukua hatua kali za kisheria kwa Waajili wote wasiozingatia masuala ya Afya na Usalama wa Wafanyakazi wao.

5.5 **FUNGU 61-Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuendelea kuboresha Daftari la Wapiga Kura na kuchukua jitihada za kutosha katika uboreshaji wa Daftari hili. Hatua hizi zijumuishe utoaji Elimu ya Uraia hususan uandikishaji wa Wapiga Kura kwa Vijana wengi zaidi ili waweze kutumia haki yao ya Kikatiba ya kupiga au kupigiwa kura. Hali hii itaongeza idadi ya Watanzania wengi zaidi watakaokuwa na sifa na vigezo vya kupiga kura katika chaguzi mbalimbali zinazokuja.

ii) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Tume kujitahidi kufanya kazi yake kwa Weledi ili kuendelea kuaminika kwa Wadau wake wa Uchaguzi. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba, inawashirikisha Wadau wa Uchaguzi wakati wa uhuishaji wa Daftari la Wapiga kura ili kuepuka migogoro isiyokuwa na tija kwa Taifa.

iii) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kwamba, Tume ihakikishe inafuatilia Wasimamizi wake wa Uchaguzi na kuwawajibisha pale wanapofanya uzembe unaosababisha madhara ambayo yangeweza kudhibitiwa mapema na msimamizi aliye makini na anayetambua na kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Napenda nikupongeze pia kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge hili katika kutekeleza Kauli Mbiu ya **HAPA KAZI TU** na **TANZANIA YA VIWANDA** kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge Kazi, Ajira, Vijana, na Watu wenye Ulemavu, Mhe. Jenista J. Mhagama, (Mb) Naibu waziri, Mhe. Antony Mavunde, (Mb), Mhe.Stella Alex Ikupa, (Mb), Makatibu Wakuu na Wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu. **Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie Katika Hansard:-**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Najma murtaza Giga, Mb – Makamu/Mwenyekiti
3. Mhe. George Simbachawene, Mb – Mjumbe;
4. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb – Mjumbe;
5. Mhe. Ally Saleh Ally, Mb – Mjumbe
6. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb – Mjumbe;
8. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb – Mjumbe;
9. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb – Mjumbe;
10. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb – Mjumbe;
11. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb – Mjumbe;
12. Mhe. Nimrod Elirehema Mkono, Mb – Mjumbe;
13. Mhe. Suzan Peter Maselle, Mb – Mjumbe;
14. Mhe. Alfredina Apilinary Kahigi, Mb – Mjumbe;
15. Mhe. Latiffah Hassan Chande, Mb – Mjumbe
16. Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb – Mjumbe;
17. Mhe. Ally Abdulla Saleh, Mb – Mjumbe;
18. Mhe. Jacquiline Kandidus Ngonyani Msongozi, Mb-Mjumbe;
19. Mhe. Bupa nelson Mwakang'ata, Mb – Mjumbe;
20. Mhe. Sixtus Raphael mapunda, Mb – Mjumbe;
21. Mhe. Hassan Selemani Kaunje, Mb – Mjumbe;
22. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb – Mjumbe;
23. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb – Mjumbe;
24. Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mb – Mjumbe;
25. Mhe. Emmanuel A. Mwakasaka, Mb – Mjumbe;
26. Mhe. Dkt Damas Daniel ndumbaro, Mb – Mjumbe;

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Makatibu wa Kamati hii, Ndg.

Stanslaus Kagisa, Ndg. Dunford Mpelumbe na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) Ndg. Hanifa Masaninga na Watendaji wote wa Idara hiyo kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

4 APRILI, 2018

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchengerwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa ushauri mzito ulioutoa humu, nina amini nakala ya hii taarifa atapewa Msajili wa Vyama ili azingatie ukurasa wa 18 na 19. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Hawa Abdulahman Ghasia. *(Makofi)*

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya

Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Sera, Bunge, kazi, Vijana, Ajira na Walemavu pamoja na Katibu wa Bunge na kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019. Mashauriano haya yamefanyika kwa mujibu kifungu cha 71(b) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mapitio ya utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia Machi 15, 2018 ya mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi yanayojumuisha vipaumbele na masuala muhimu yaliyopendekezwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Mfuko wa Bunge – Fungu 42 uliidhinishiwa kiasi cha shilingi 121,652,262,000 kati ya fedha hizo shilingi 24,454,715,000 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 89,997,547,000 kwa ajili ya matumizi ya mengineyo na shilingi 7,200,000,000.00 kwa ajili ya mpango wa maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo shilingi 7, 000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 200,000,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mpango kazi na mtiririko wa fedha kwa mwaka 2017/2018, Mfuko wa Bunge ulipanga kutumia fedha za matumizi ya Kawaida kiasi cha shilingi 80,317,810,250 hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2018. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi 18,341,036,250 ni mishahara na shilingi 61,976,774,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018 Ofisi ya Bunge ilikuwa imepokea fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha shilingi 81,479,720,100.09; kati ya fedha hizo shilingi 64,734,612,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 16,740,080,100

kwa ajili ya mishahara. Hivyo, fedha za matumizi mengineyo iliyopokelewa ni sawa na asilimia 104.4 wakati fedha za mishahara ni sawa na asilimia 91.2 ya fedha zilizopangwa kutumika hadi tarehe 31 Machi, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mpango kazi na mtiririko wa fedha kwa mwaka 2017/2018; Mfuko wa Bunge ulipanga kutumia fedha za maendeleo kiasi cha shilingi 6,885,000,000 hadi kufikia 31 Machi, 2018. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018, Mfuko ulikuwa umepokea kiasi cha shilingi 115,980,000 sawa na asilimia mbili ya fedha zote ziliyopangwa kutumika katika kipindi cha robo ya tatu. Aidha, fedha hizo za nje ni kwa ajili ya kutekelezaji wa shughuli za Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha. Mfuko haujapokea fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Bunge, usimikaji wa Studio ya Bunge, ujenzi wa *lift* katika jengo la utawala na ununuzi za mtambo wa kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Mfuko wa Bunge ulipanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha shilingi 42,500,000 makusanyo hayo yalipangwa kutokana na marejesho ya masurufu na malipo ya kodi ya pango. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018, Ofisi ya Bunge ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi 15,720,000 ambacho ni sawa na asilimia 36.9 ya bajeti ya maduhuli iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Bunge kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na mipango mizuri waliyojiwekea kwa mwaka huu wa fedha. Ni matumaini ya Kamati kuwa katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Bunge itajitahidi kufikia malengo yake kwa usahihi na kwa wakati. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018, Ofisi ya Bunge ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Bunge, Fungu 42, uligharamia uratibu wa shughuli za Kamati kama ifuatavyo:-

(a) Kuwezesha na kuratibu ziara za Kamati za Kisekta kwa ajili ya kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha, 2017/2018;

(b) Kuwezesha na kuratibu ziara za kamati mbili za kusimamia matumizi ya fedha za umma kwa ajili ya kufuatilia thamani halisi ya matumizi ya fedha za umma katika maeneo mbalimbali;

(c) Kuwezesha na kuratibu ziara za Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili kufuatilia miradi ya uwekezaji inayotekelezwa kwa mitaji ya umma;

(d) Kuwezesha na kuratibu utayarishaji na uwasilishaji wa taarifa za mwaka za shughuli za Kamati kumi na sita; na

(e) Kuwezesha na kuratibu vikao vya wiki mbili kabla ya Mkutano wa Nane, Mkutano wa Tisa na Mkutano wa Kumi vya Kamati Kumi na Saba za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mfuko wa Bunge uliwezesha uratibu wa Shughuli za Kamati Maalum zifuatazo:-

(a) Kamati Maalum ya Ushauri kuhusu Mfumo wa Uchimbaji, Usimamizi na Udhibiti wa Madini ya Tanzanite;

(b) Kamati Maalum ya Ushauri kuhusu Mfumo wa Uchimbaji, Usimamizi na Umiliki wa Udhibiti wa Madini ya Almasi nchini;

(c) Kamati Maalum ya Ushauri kuhusu Mfumo wa Usimamizi na Udhibiti wa shughuli za Uvuvi katika Bahari Kuu; na

(d) Kamati Maalum ya Ushauri kuhusu namna ya kuliwezesha Taifa kunufaika na Mapato yatokanayo na Sekta Ndogo ya Gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Bunge - Fungu 42 umefanikisha Mikutano midogo mitatu ya Bunge kwa ufanisi

ambapo mambo mbalimbali yamefanyika kama yanavyoonekana katika kitabu chetu cha hotuba kuanzia ukurasa wa tisa hadi ukurasa wa kumi na moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mfuko wa Bunge umewezesha ushiriki wa Bunge katika Mikutano ya Kimataifa. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018 Mfuko wa Bunge umewezesha Wabunge kushiriki kwenye michezo ya michuano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyofanyika Dar es Salaam. Aidha, viongozi wa Bunge na Wabunge wanaoliwakilisha Bunge la Tanzania kwenye Mikutano ya Kimataifa ambayo Bunge letu ni mwanachama waliweza kushiriki kwenye mikutano hiyo kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la Afrika, Umoja wa Wabunge wa Jumuiya ya Madola, Kanda ya Afrika, *CPA-International, Africa Caribbean Pacific and European Union,* Jukwaa la Kibunge la Jumuiya ya Maedeleo Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC- PF),* Bunge la Afrika Mashariki na Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)* pia wameweza kushiriki katika Mkutano wa Shirikisho la Wabunge Duniani *(Global Parliamentarian Conference)* pamoja na Mkutano wa mwaka wa Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF).*

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018, Mfuko wa Bunge umeweza kutoa elimu kwa umma kuhusu Bunge kwa njia mbalimbali, mojawapo ikiwa ni kuelimisha wageni mbalimbali wanaolitembelea Bunge pamoja na kufanya ziara katika Mikoa ya Mbeya, Tanga na Mara na pia kushiriki kwenye Maonesho ya Saba Saba na Nane Nane ya kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/2019 Mfuko wa Bunge umepanga kutumia kiasi cha shilingi 125,521,100,000; kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi 24,441,023,000 ni fedha za mishahara; shilingi 92,764,464,000.00 ni fedha za matumizi mengineyo na shilingi 8,315,613,000.00 ni fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika fedha za maendeleo, kiasi cha shilingi 5,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 3,315,613,000 ni fedha za nje ambapo kiasi cha shilingi 3,015,613,000 ni kwa ajili ya Mpango wa Kuliwezesha Bunge ambao umekuwa ukiwajengea uwezo Waheshimiwa Wabunge kupitia semina na mafunzo mbalimbali na kiasi cha shilingi 300,000,000 zimetengwa kwa ajili ya Maboresho ya Fedha za Umma kwa ajili ya kujenga mifumo bora ya takwimu zinazotumika na Bunge zinazohusu bajeti na uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Bunge inatarajia kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 61,000,000.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Ghasia kabla hujaanza hiyo nyingine naomba urudi ukae kidogo.

Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kuwezesha Kamati ya Bajeti kumaliza hotuba yake, nalazimika kutumia Kanuni 28(2) ya kuongeza nusu saa na fasili hii inanitaka niwahoji Waheshimiwa Wabunge ili kama mnakubaliana na hiyo hoja. Kwa hivyo, nitawahoji.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Walioafiki wameshinda, kwa hiyo tutaendelea, Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 fedha zilizokasimiwa zimetengwa katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linatekeleza majukumu yake ya Kikatiba. Baadhi ya majukumu ambayo yamepangwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 ni kama yafuatayo:-

(a) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mkutano wa Bajeti na Mikutano midogo mitatu ya Bunge;

(b) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano minne ya Kamati za Kudumu za Bunge;

(c) Kuratibu na kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge,

(d) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Wabunge na uchambuzi wa Miswada;

(e) Kutoa huduma za utafiti kwa Wabunge;

(f) Kuwezesha Wabunge kushiriki kwenye Mikutano ya Kimataifa ambayo Bunge ni wanachama;

(g) Kuandaa vipindi vya televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;

(h) Kuratibu shughuli mbalimbali za utawala na pia kuwajengea Wabunge uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao Kikatiba kupitia Mpango wa Kuliwezesha Bunge;

(i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ukarabati na ununuzi wa mitambo ya usalama, kusimika kituo cha matangazo ya Bunge katika Ukumbi wa Bunge, ujenzi wa makazi ya viongozi wa Bunge - Dodoma na ukarabati wa Ukumbi wa Msekwa, Ukumbi wa Bunge pamoja na majengo ya Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati:-

Kwa kuwa mara kadhaa kumeibuka umuhimu wa kuteuliwa kwa Kamati Maalum ili kushughulikia mambo muhimu yenye maslahi ya kitaifa; Na kwa kuwa mara zote Kamati hizo Maalum huwa hazikutengewa bajeti yake kwa mwaka wa fedha husika hivyo kuathiri bajeti ya ofisi;

Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inarejesha mapema fedha ambazo zitatumika kutoka katika Bajeti ya Mfuko wa Bunge endapo yatajitokeza masuala muhimu zikiwemo Kamati Maalum ili kutoathiri Bajeti ya Mfuko kwa mwaka husika.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe kwa kumshukuru Mheshimiwa Spika na wewe mwenyewe kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Namshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Aidha, Kamati inamshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu) kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu bajeti ya Mfuko wa Bunge. Ninaomba majina yao yote yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama yalivyoandikwa katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa ushauri wa kitaalam ambao wamekuwa wakiipa Kamati ambao umewezesha kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge – Fungu 42, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Sera, Bunge, kazi, Vijana, Ajira na Walemavu pamoja na Katibu wa Bunge na kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19. Mashauriano haya yamefanyika kwa mujibu kifungu cha 71 (b) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mapitio ya utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia Machi 15, 2018 ya mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi yanayojumuisha vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Bajeti ya Mwaka wa fedha 2018/ 2019.

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, Kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 Mfuko wa Bunge –Fungu 42 uliidhinishiwa kiasi cha **Sh. 121,652,262,000.00**. Kati ya fedha hizo **Sh.24,454,715,000.00** ni

kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh.89,997,547,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Mengineyo (OC) na **Sh. 7,200,000,000.00** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo **Sh.7,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Sh. 200,000,000.00** ni fedha za nje.

### 2.1 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Mpango Kazi na Mtiririko wa Fedha kwa Mwaka 2017/2018 (Cash Flow and Action Plan), Mfuko wa Bunge ulipanga kutumia fedha za Matumizi ya Kawaida kiasi cha **Sh.80,317,810,250.00** hadi kufikia Machi 31, 2018. Kati ya fedha hizo kiasi cha **Sh.18,341,036,250** ni Mishahara na **Sh.61,976,774,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Hadi kufikia Machi 15, 2018 Ofisi ya Bunge ilikuwa imepokea fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha **Sh.81,479,720,100.09.** Kati ya fedha hizo **Sh.64,739,612,000.09** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh.16,740,080,100.00** kwa ajili ya Mishahara (PE). Hivyo, fedha za matumizi mengineyo (OC) iliyopokelewa ni sawa na **asilimia 104.4** wakati fedha za mishahara ni sawa na **asilimia 91.2** ya fedha zilizopangwa kutumika hadi Machi 31, 2018.

### 2.2 Matumizi ya Fedha za Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Mpango Kazi na Mtiririko wa Fedha kwa Mwaka 2017/18; Mfuko wa Bunge ulipanga kutumia fedha za Maendeleo kiasi cha **Sh.6,885,000,000** hadi kufikia Machi 31, 2018. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 15 Machi 2018, Mfuko umepokea kiasi cha **Sh.115,980,000** ambazo ni sawa na asilimia **2** ya fedha zote ziliyopangwa kutumika katika kipindi cha Robo ya Tatu. Aidha, fedha hizo za nje ni kwa ajili ya kutekelezaji wa shughuli za Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP). Mfuko haujapokea fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Bunge, usimikaji wa Studio ya Bunge, ujenzi wa lifti katika jengo la utawala na ununuzi za mtambo wa kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge.

### 2.3 Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Mfuko wa Bunge ulipanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha

**Sh.42,500,000** Makusanyo hayo yalipangwa kutokana na marejesho ya masurufu (Recovery of Public Money) na malipo ya kodi ya Pango. Hadi kufikia Machi 15, 2018, Ofisi ya Bunge ilikuwa imekusanya kiasi cha **Sh.15,720,000** ambacho ni sawa na asilimia **36.9** ya bajeti ya maduhuli iliyoidhinishwa.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Bunge kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na mipango mizuri waliyojiwekea kwa Mwaka huu wa Fedha. Ni matumaini ya Kamati kuwa katika mwaka huu wa Fedha 2017/18; Ofisi ya Bunge itajitahidi kufikia malengo yake kwa usahihi na kwa wakati. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018, Ofisi ya bunge ilitekeleza majukumu yafuatayo;

### 3.1 Uratibu wa shughuli za Kamati za Bunge hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018.

Mfuko wa Bunge, Fungu 42, uligharamia uratibu wa shughuli za Kamati kama ifuatavyo:-

a) Kuwezesha na kuratibu ziara za Kamati za Kisekta kwa ajili ya kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha, 2017/2018;

b) Kuwezesha na kuratibu ziara za Kamati Mbili (2) za kusimamia matumizi ya fedha za Umma kwa ajili ya kufuatilia thamani halisi ya matumizi ya fedha za Umma katika Maeneo mbalimbali;

c) Kuwezesha na kuratibu ziara za Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili kufuatilia miradi ya uwekezaji inayotekelezwa kwa mitaji ya umma;

d) Kuwezesha na kuratibu utayarishaji na uwasilishaji wa Taarifa za Mwaka za Shughuli za Kamati Kumi na Sita (16);

e) Kuwezesha na kuratibu vikao vya wiki mbili (2) kabla ya Mkutano wa nane, Mkutano wa Tisa na Mkutano wa Kumi vya Kamati Kumi na Saba za Bunge;

Aidha, Mfuko wa Bunge uliwezesha Uratibu wa Shughuli za Kamati Maalum zifuatazo:-

(e) Kamati Maalum ya Ushauri kuhusu Mfumo wa Uchimbaji, Usimamizi na Udhibiti wa Madini ya Tanzanite;

(f) Kamati Maalum ya Ushauri kuhusu Mfumo wa Uchimbaji, Usimamizi na Umiliki wa Udhibiti wa Madini ya Almasi Nchini;

(g) Kamati Maalum ya Ushauri kuhusu Mfumo wa Usimamizi na Udhibiti wa shughuli za Uvuvi katika Bahari Kuu; na

(h) Kamati Maalum ya Ushauri kuhusu namna ya kuliwezesha Taifa kunufaika na Mapato yatokanayo na Sekta Ndogo ya Gesi.

**3.2 Uratibu wa Shughuli za Mikutano Midogo Mitatu ya Bunge hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018.**

Mfuko wa Bunge, Fungu – 42 umefanikisha Mikutano Midogo Mitatu ya Bunge kwa ufanisi ambapo mambo mbalimbali yamefanyika kama ifuatavyo:-

(a) Wabunge Kumi na Mbili (12) waliapa kiapo cha Uaminifu;

(b) Taarifa za Mwaka za Taasisi/Mashirika manne (4) ziliwasilishwa Bungeni

(c) Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake Arobaini na Nne (44) yaliwasilishwa Bungeni;

(d) Maswali ya kawaida Mia Tatu Themanini na Tatu (383) yaliulizwa Bungeni na kujibiwa na Serikali;
(e) Waziri Mkuu aliweza kujibu maswali kumi na sita (16) ya papo kwa papo kutoka kwa Wabunge katika kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu;

(f) Bunge lilikaa kama Kamati ya Mipango kwa ajili ya kupokea, kujadili na kushauri kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2018/2019;

(g) Miswada Kumi na Nne (14) ilipokelewa na Katibu wa Bunge ambapo yote ilisomwa kwa hatua zote na kupitishwa na Bunge;

(h) Maazimio manne (4) yaliridhiwa na Bunge;

(i) Kauli Moja (1) ya Waziri ilitolewa Bungeni;

(j) Hoja za Kamati za Bunge (15) zilijadiliwa na kupitishwa Bungeni;

(k) Mbunge mmoja (1) alitoa maelezo binafsi;

(l) Jumla ya machapisho 20,412 yalichapishwa ambapo kati ya hayo vitabu vya Taarifa Rasmi (426), Taarifa za Kamati za Bunge (10,000), Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (6,750), Sheria za Kusaini Mhe. Rais (84), Machapisho mbalimbali (2,827), Kamati Maalum ya Bunge ya Ushauri kuhusu mfumo wa Udhibiti wa Shughuli za Bahari Kuu Nchini (95), Taarifa Rasmi ya Kamati Maalum ya Bunge ya Ushauri kuhusu namna ya kuliwezesha Taifa kunufaika na mapato yatokanayo na sekta ndogo ya Gesi (80) na Maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa za Kamati Kumi na Sita za Kudumu za Bunge (150).

### 3.3 Kuwezesha ushiriki wa Bunge katika Mikutano ya Kimataifa

Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018, Mfuko wa Bunge umewezesha Wabunge kushiriki kwenye michezo ya michuano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyofanyika Dar es Salaam. Aidha, Viongozi wa Bunge na Wabunge wanaoliwakilisha Bunge la Tanzania kwenye Mikutano ya Kimataifa ambayo Bunge letu ni mwanachama waliweza kushiriki kwenye mikutano hiyo kama ifuatayo:-

(a) Bunge la Afrika (PAP);

(b) Umoja wa Wabunge wa Jumuiya ya Madola (CPA), Kanda ya Afrika, *CPA- International;*

(c) *Africa Caribbean Pacific and European Union (ACP/EU);*

(d) Jukwaa la Kibunge la Jumuiya ya Maedeleo Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC- PF);

(e) Bunge la Afrika Mashariki; na

(f) Umoja wa Mabunge Duniani ( IPU).

(g) Mkutano wa Shirikisho la Wabunge Duniani (Global Parliamentarian Conference) pamoja na Mkutano wa Mwaka wa Benki ya Dunia (World Bank) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

### 3.4 Kutoa Elimu kwa Umma kuhusiana na masuala ya Kibunge

Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018, Mfuko wa Bunge umeweza kutoa elimu kwa Umma kuhusu Bunge kwa njia ya:

a) Kuelimisha wageni mbalimbali wanaolitembelea Bunge pamoja na kufanya ziara katika Mikoa ya Mbeya, Tanga na Mara; na

b) Kushiriki kwenye maonesho ya Saba Saba na Nane Nane ya Kitaifa.

## 4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### 4.1 Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/19

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mpango na Bajeti ya Mwaka 2018/ 2019 Mfuko wa Bunge umepanga kutumia kiasi cha

**Sh.125,521,100,000.00** Kati ya fedha hizo kiasi cha **Sh.24,441,023,000.00** ni fedha za Mishahara; **Sh.92,764,464,000.00** ni fedha za Matumizi mengineyo na **Sh.8,315,613,000.00** ni fedha za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** katika fedha za Maendeleo, kiasi cha **Sh.5,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Sh.3,315,613,000.00** ni fedha za nje ambapo kiasi cha **Sh. 3,015,613,000.00** ni kwa ajili ya Mpango wa Kuliwezesha Bunge (*Legislative Support Program)* ambao umekuwa ukiwajengea uwezo Waheshimiwa Wabunge kupiti Semina na Mafunzo mbalimbali. Na kiasi cha **Sh. 300,000,000.00** kimetengwa kwa Programu ya Maboresho ya Fedha za Umma (*Public Finance Reform Program)* kwa ajili ya kujenga mifumo bora ya takwimu zinazotumika na Bunge zinazohusu Bajeti na Uchumi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2018/19 Ofisi ya Bunge inatarajia kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 61,000,000.00.**

### 4.2 Shughuli zitakazotekelezwa Katika Mwaka wa Fedha 2018/19

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa Fedha 2018/19, fedha zilizokasimiwa zimetengwa katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linatekeleza majukumu yake ya Kikatiba. Baadhi ya majukumu ambayo yamepangwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2018/19 ni kama yafuatayo:

(a) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mkutano wa Bajeti na Mikutano Midogo Mitatu (3) ya Bunge;

(b) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano Minne (4) ya Kamati za Kudumu za Bunge;

(c) Kuratibu na kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard);

(d) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Wabunge na uchambuzi wa miswada;

(e) Kutoa huduma za Utafiti "Information Research" kwa Wabunge;

(f) Kuwezesha Wabunge kushiriki kwenye Mikutano ya Kimataifa ambayo Bunge ni Mwanachama.

(g) Kuandaa vipindi vya Televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;

(h) Kuratibu shughuli mbalimbali za utawala (huduma kwa Wabunge, ununuzi wa vifaa vya Ofisi, malipo ya maji, umeme na simu, usafi na ulinzi);

(i) Kuwajengea Wabunge uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kikatiba kupitia Mpango wa Kuliwezesha Bunge;

(j) Kuratibu na Kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ikiwa ni pamoja na:

- Ukarabati na ununuzi wa mitambo ya usalama;
- Kusimika Kituo cha Matangazo ya Bunge *(Broadcasting Studio)* katika Ukumbi wa Bunge
- Ujenzi wa Makazi ya Viongozi wa Bunge - Dodoma; na
- Ukarabati wa Ukumbi wa Msekwa, Ukumbi wa Bunge pamoja na majengo ya Ofisi ya Bunge;

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**5.1 Kwa kuwa**, mara kadhaa kumeibuka umuhimu wa kuteuliwa kwa Kamati Maalum ili kushughulikia mambo muhimu yenye maslahi ya Kitaifa, na kwa kuwa mara zote Kamati hizo Maalum huwa hazikutengewa Bajeti yake kwa mwaka wa fedha husika hivyo kuathiri Bajeti ya Ofisi;

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inarejesha mapema fedha ambazo zitatumika kutoka katika Bajeti ya Mfuko wa Bunge endapo yataibuka masuala muhimu zikiwemo Kamati Maalumu ili kutoathiri Bajeti ya Mfuko kwa Mwaka husika.

## 6.0 HITIMISHO.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kumshukuru Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu) kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo;

1) Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
2) Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb - Makamu Mwenyekiti
3) Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
4) Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
5) Mhe. Abdallah Majura Bulembo, Mb
6) Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
7) Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
8) Mhe. Dalali Peter Kafumu, Mb
9) Mhe. David Ernest Silinde, Mb
10) Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
11) Mhe. Hasna Sadi Kalunda Mwilima, Mb
12) Mhe. Dkt. Immaculate Swale Semesi, Mb
13) Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali Raza, Mb
14) Mhe. Makame Kassim Makame, Mb

15) Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
16) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
17) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
18) Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb
19) Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
20) Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
21) Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
22) Mhe. Stephen Julius Masele, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa ushauri wa kitaalamu ambao wamekuwa wakiipa Kamati ambao uwezesha kukamilisha taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge – Fungu 42, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Hawa A. Ghasia, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**
04 APRILI, 2018

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti amemaliza kwa wakati, na hapa tulikuwa tumeshahojiana kuhusu kuongeza nusu saa, tumebakiza Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI. Kwa hiyo, hiyo nusu saa yetu tuliyoiongeza tutamaliza na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI. Kwa hiyo, nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI aje atusomee na yeye hotuba yake. Mheshimiwa Mukasa. *(Makofi)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na kutuleta hapa. Lakini kwa namna ya pekee nishukuru Ofisi ya Spika, wewe ukiwa ni mmoja wao, kwa kunipa fursa kunirudisha kwenye Kamati ya Masuala ya UKIMWI na hivyo nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya UKIMWI kwa kuniamini na kunichagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho ingawa sio kwa umuhimu, namshukuru mke wangu na familia kwa kunivumilia kwa kazi ninazozifanya, na kwa bahati zuri leo ninaye hapa ananishuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99...

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako, kama unaweza kumruhusu mke wangu mpendwa Aleswa Swai Mukasa asimame wamuone. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mukasa, inabidi mimi ndiyo nimuite maana la sivyo haruhusiwi kusimama humu ndani. *Mrs. Mukasa* amekaa upande gani jamani, watu wanataa kumuona wifi yao humu ndani. *(Makofi)*

Karibu sana wifi yetu, karibu na siku nyingine hata kama hazungumzi yeye hapa mbele. *(Makofi)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya – Fungu 91 na Tume ya Kudhibiti UKIMWI – Fungu 92 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na maoni ya Kamati

kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 10 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Masuala ya UKIMWI imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa shughuhuli za Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI ikiwa ni kuchambua Bajeti ya Taasisi hizo, Kanuni ya 10(d).

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 25 Machi, 2018 Kamati ilipokea na kuijadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 na kufanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2018/2019 Fungu 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa taarifa za mafungu hayo mawili, naomba kutoa taarifa ya Kamati inayofafanua mambo makubwa sita kama ifuatavyo:-

(i) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI;

(ii) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya;

(iii) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI;

(iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2018/2019;

(v) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya mafungu 91 na 92; na

(vi) Hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2017/2018, kwa fungu 92, Kamati ilifanya mapitio ya utekelezaji wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa wakati wa kupitisha Bajeti ya mwaka wa 2017/2018. Jumla ya mapendekezo manne yaliyotolewa na Kamati, mapendekezo yote Serikali imeyachukua na kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilipewa jumla ya mapendekezo manne likiwemo:-

(i) Mamlaka kuongeza vituo vya tiba ya *methadone* angalau kwa kila mkoa ili kuhakikisha wananchi wa mikoa yote wananufaika;

(ii) Utoaji wa elimu mipakani ili kuongeza nguvu katika udhibiti wa uingizwaji wa dawa nchini na utoaji wa elimu wa dawa za kulevya kwa jamii kwa ujumla;

(iii) Mamlaka kwa kushirikiana na Serikali imeendelea kutekeleza mapendekezo hayo kwa kuweka mbinu mbadala kama vile uanzishwaji wa dirisha maalumu katika idara ya magonjwa ya akili katika hospitali zote za rufaa za mikoa za magonjwa ya akili pamoja na miongozo ya kuanzisha na kuendesha nyumba za upataji nafuu *(sober houses).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuufanyia kazi ushauri wa Kamati katika kuendeleza juhudi za kupambana na dawa za kulevya. Aidha, ni maoni ya Kamati kuwa mamlaka iendelee kuongeza nguvu za kupambana na dawa za kulevya ikiwemo kudhibiti, kuwatambua na kuwasaidia wadau wote wa dawa za kulevya ikiwemo jamii ya Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Tume ya Kudhibiti UKIMWI (Fungu 92) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Fungu 91) haikuwa na makadirio ya makusanyo ya maduhuli yaliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti (Fungu 92) kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za *TACAIDS* kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kama ambavyo ziliidhinishwa na Bunge lako tukufu ili kuona matumizi yake. Ilikuwa ni matarajio ya Kamati kupata taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa walau asilimia 75 kwa mafungu yote mawili ya mwaka mzima ikizingatiwa kwamba wakati wa uchambuzi wa taarifa ya tume ilikuwa ni mwezi Machi, 2018 ambayo ni robo ya tatu ya mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo katika uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Fungu 92, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 kiasi cha fedha kilichokuwa kimepokelewa ilikuwa ni asilimia 57.8 ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge. Aidha, uchambuzi wa Kamati unaonesha kwamba asilimia hiyo iliyopokelewa inabebwa na fedha za miradi ya maendeleo ambayo kwa asilimia kubwa ni fedha za wafadhili wa nje. Kamati imebaini kwamba fedha za *UNDAP* zilitolewa kwa asilimia 552 na fedha za *Global Fund* zilitolewa kwa asilimia 401. Aidha, fedha za Serikali zilitolea kwa asilimia 56.7 ambazo ni fedha za matumizi ya kawaida tu zikiwemo fedha za mishahara ya watumishi ambayo kwa namna yoyote ile ni lazima itolewe ili watumishi waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaona kwamba utekelezaji wa shughuli za tume kwa kiasi kikubwa unategemea sana fedha kutoka kwa wafadhili. Kutokana na hali hiyo ni dhahiri kuwa endapo ufadhili huu utakoma basi Tume itashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika ajenda nzima ya muitikio wa mapambano dhidi ya UKIMWI ikiwemo kusambaza taarifa, kutetea haki za binadamu walioambukizwa na kuathirika na VVU pamoja na kuhimiza hali ya kuishi vizuri kwa matumaini pamoja na shughuli nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaliomba Bunge kuihimiza Serikali kukamilisha upelekaji wa fedha hasa za ndani kwa tume ili iweze kukamilisha utekelezaji wa shughuli zake kabla mwaka wa fedha wa 2017/2018 haujakamilika.

Fedha nyingi zilizotolewa ni za wafadhili ikilinganishwa na fedha za ndani ambazo siyo fedha za maendeleo; rejea Jedwali Namba 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Fungu 91), iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 4.015 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 3.448 sawa na asilimia 85.8 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, na shilingi milioni 567.360 ambayo ni asilimia 14.2 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa mamlaka. Kwa mujibu wa taarifa mamlaka iliyowasilisha mbele ya Kamati inaonyesha kuwa hadi kufikia Februari, 2018 mamlaka ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 2.707, sawa na asilimia 67.2 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya mwaka wa fedha wa 2017/2018; kati ya fedha hizo shilingi milioni 543.527 sawa na asilimia 95.7 kwa ajili ya mishahara ya watumishi na bilioni 2.163 sawa na asilimia 62.7 kwa ajili ya matumizi mengineyo kama ilivyoonesha kwenye Jedwali Namba 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Tume ya Kudhibiti UKIMWI ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 3.455 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambazo ni za wahisani. Hadi kufikia wakati Kamati inapokea taarifa ya utekelezaji mwezi Machi, 2018 kiasi cha bilioni 2.028, sawa na asilimia 58.7 tu ndicho kilichokuwa kimepokelewa ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1.915 kilitumika.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kulikuwa na matumizi makubwa ya fedha ikilinganishwa na kile kilichokuwa kimeidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kiwango hicho kikubwa cha matumizi ni kutokana na bakaa ya fedha za *Global Fund* za mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo Tume ilizipokea mwishoni mwa mwaka 2017. Aidha, fedha nyingine zilipokelewa na Tume chini ya Mradi wa Umoja wa Mataifa wa Kuhuisha UKIMWI kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa ambazo zilitolewa mwezi Desemba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania inatekeleza miradi yake ya maendeleo kwa utegemezi wa fedha kutoka kwa wafadhili kwa asilimia100. Serikali inagharamia matumizi ya kawaida ikiwemo mishahara ya watumishi na matumizi mengineyo. Ni maoni ya Kamati kuwa mwenendo huu wa utegemezi wa fedha za miradi ya maendeleo siyo jambo sahihi endapo nia ya Serikali ni kudhibiti UKIMWI kama jina la Tume linavyojibainisha sambamba na malengo yake kwa ujumla. Kamati inasikitishwa sana na hali hii ya kutotengwa kwa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Tume kwani hii ndiyo tume pekee inayoshughulika na masuala ya UKIMWI hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya haikutengewa kabisa fedha za miradi ya maendeleo. Kamati inaona kwamba hali hii haifai kwani ajenda ya kupambana na dawa za kulevya ni kubwa na pana kuliko inavyochukuliwa kwa sasa.

Kamati inajiuliza ufanisi wa Tume hii katika kupambana na janga hili utapatikana kwa njia gani kama Serikali haioni umuhimu wa kuipa Tume fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo! Mfano wa miradi ya maendeleo inayoweza kunufaika na fedha za maendeleo ni pamoja na uongezaji wa vituo vya kupata nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya, kufanya uraghabishi kwa jamii wa namna ya kupambana na kudhibiti dawa za kulevya na hata kuikinga jamii kushiriki katika mapambano kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa mfumo maalum kwa ngazi ya jamii kwa ajili ya kuwatambua warahibu wa madawa ya kulevya na hivyo kuweza kuwashirikisha na kuwasaidia ni kikwazo kikubwa katika muitikio wa kitaifa wa kupambana na tatizo hili. Upo ushahidi kuwa watu hawa hurudi baada ya muda mfupi katika hali yao ya awali ya kutumia dawa za kulevya endapo wataendelea kuwa na ukaribu na watu wanaotumia dawa

za kulevya na endapo watakaa kwa angalau miezi sita bila ya kupata fursa ya kushiriki kwenye shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Tume haipatiwi fedha za maendeleo, na kwa kuzingatia kwamba kuna kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu wanaolazimika kuacha matumizi ya dawa za kulevya kutokana na kampeni kubwa inayoendelea, na kwa kuwa kuna ushahidi kwamba watu hawa hutumia tena dawa za kulevya kama hakuna mpango endelevu, basi ni dhahiri kuwa utoaji wa pesa za matumizi ya kawaida ikiwemo kampeni za kukamata wahusika wa madawa ya kulevya bila ya uwepo wa fedha za maendeleo ni sawasawa na mfuaji wa nguo ambaye huitumbukiza nguo hiyo kwenye tope mara tu baada ya kuifua badala ya kuitafutia mahali pa kuikausha, kuipiga pasi na kuihifadhi mahali stahiki na hivyo kuendeleza mzunguko usiokwisha wa ufuaji na kuchafuka tena kwa nguo hiyo bila ukomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo ni maoni ya Kamati kwamba utoaji na utumiaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida bila kuambatana na mifumo na mipango ya kimkakati inaleta matokeo ya kuendeleza mzunguko wa kupunguza idadi ya watumiaji, lakini na kuwarudisha tena kwenye utumiaji baada ya muda mfupi *(vircious circle).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo Kamati inapendekeza Serikali itenge fedha za maendeleo ambazo zinaweza kutoa fursa kwa tume kuanza kujenga mifumo itakayojumuisha jamii nzima kimkakati katika kuwapokea, kuwatambua, kuwashirikisha na kuwasaidia watu waliowahi kutumia madawa ya kulevya na hivyo kuiwezesha tume kupata matokeo yenye manufaa ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imepanga kujikita katika kuongeza juhudi za utoaji uongozi wa kimkakati katika Mwitikio wa Taifa wa UKIMWI. Tume imeainisha maeneo

matano ambayo itaweka mkazo katika mwaka wa fedha 2018/2019; rejea kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tume iliainisha maeneo matatu ya kuweka mkazo zaidi, hasa katika kipindi cha kati kwa kuzingatia ufinyu wa rasilimali fedha, maeneo hayo ya kipaumbele ni kama yalivyorejewa kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia maeneo ambayo tume iliainisha na kuyaridhia kwa kuwa yalioneka kuwa na tija katika suala zima la uboreshaji wa mapambano dhidi ya UKIMWI, pia maeneo hayo yanashabihiana na mipango na mikakati mbalimbali yakiwemo makubaliano ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kupambana na maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijiridhisha kwamba tume imepanga kutekekeleza mipango ambayo imeainishwa katika miongozo mbalimbali ikiwemo Malengo ya Maendelao Endelevu *(Sustainable Development Goals).* Aidha, utekelezaji wa shughuli hizo zote unalenga katika kuhakikiasha tisini tatu (90-90-90) zinapatikana ikiwemo kwamba hakuna mtu au watu wenye maambukizi wanafariki kutokana na UKIMWI. Kwa kutekeleza haya yote kutasababisha kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi wa jamii kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imejipangia madhumuni ya kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya, kudhibiti upatikanaji wa dawa za kulevya pamoja na utekelezaji wa masuala ya kinga na tiba kwa watu wanaotumia dawa za kulevya. Mamlaka imepanga kufikia madhumuni hayo kwa kuweka mikakati mitatu ambayo imeainishwa katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijadili mikakati hii na kuona kwamba ina tija kwa taifa zima kama mikakati hii itatekelezwa kwa wakati. Utekelezaji wake unategemea na

upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini. Ni imani ya Kamati kwamba Mamlaka itashirikiana na wadau wengine wa dawa za kulevya katika kutekeleza mikakati hiyo na kuendeleza mapambano dhidi ya dawa za kulevya ili kupunguza madhara ya dawa hizo kwa jamii na kujenga Taifa lenye afya bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kupitia Fungu 92 inaomba jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 12.901 ikiwa ni makadirio ya matumizi yake; kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 10.3 sawa na asilimia 79.7 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na shilingi bilioni 2.609 sawa na asilimia 20.2 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio haya ya matumizi ya mwaka 2018/2019 ni ongezeko la takribani shilingi bilioni 6.926 ambayo ni sawa na asilimia 53.6 ikilinganishwa na bajeti ya matumizi ya mwaka uliotangulia. Ni maoni ya Kamati kuwa kwa ongezeko la bajeti hii kwa tume linaleta matumaini yanayoletwa na Serikali katika kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI kwa Taifa la Tanzania, ikizingatiwa kwamba hapo mwanzo bajeti ilikuwa inatekelezwa na misaada ya wahisani. Kamati inaendelea kuipongeza Serikali kwa kuonesha nia ya kujali afya ya wananchi wake, kwani kwa mujibu wa taarifa mbalimbali inaonesha kwamba hakuna Mtanzania ambaye hajaathirika na janga la UKIMWI kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imekadiria matumizi ya kiasi cha shilingi bilioni 5.755 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4.948 sawa na asilimia 85.9 ya fedha yote inayoombwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, na shilingi milioni 806.549 sawa na asilimia 14.1 kwa ajili ya mishahara. Makadirio haya yameongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.74 sawa na asilimia 30.2 ikilinganishwa na makadirio ya matumizi kwa mwaka uliotangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa Kamati ilibainika kwamba Tume haijatenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kama ambavyo ilijitokeza kwa mwaka uliotangulia. Mwendelezo huo wa kutotenga fedha za maendeleo unaashiria kutolitazama tatizo hili kimkakati na *by the way* kutakuwa na madhara makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika,Kamati inatambua majukumu ya Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya ni dhahiri ni udhibiti wa matumizi wa dawa za kulevya, kufanya uelimishaji wa jamii na kufanya afua za kupunguza madhara ya dawa za kulevya kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba jukumu la pili na la tatu ni la kimkakati kuliko vinginevyo. Ni maoni ya Kamati kuwa kuna umuhimu wa mamlaka na kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya kuanza kutenga fedha kwenye bajeti yake kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kujenga mfumo bora wa kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini kwa upana wake ikiwa ni pamoja na kujenga jamii ya Watanzania isiyokuwa na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati; moja, ni kuhusu Tume ya Kudhibiti UKIMWI. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, Tume ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 5.983 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2018 Tume ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 3.462 sawa na asilimia 57.8 tu ya fedha zote zilizotakiwa kutolewa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inapeleka fedha hizo Tume ya Kudhibiti UKIMWI kabla ya mwaka wa fedha haujaisha na kuanza mwaka mwingine wa fedha ili Tume iweze kukamilisha utelezaji wa mipango iliyokuwa imejiwekea kwa mwaka uliotangulia. Ni dhahiri kwamba kila mwaka unakuwa na mpango na malengo yake mahususi kulingana na wakati husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bajeti utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Tume imekuwa ikitekelezwa kwa kutegemea wafadhili kwa asilimia mia moja. Uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali haikutenga kabisa kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni tatu tu, sawa na asilimia 29.1 ya fedha yote iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Tume kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Pamoja na utengaji huo wa fedha, utegemezi huu bado ni mkubwa ikizingatiwa upelekaji wa fedha katika Tume huwa haufanyiki kama vile ambavyo inategemewa. Rejea jedwali namba tano 1(1).

Mheshimiwa Naibu Spika, mapambano dhidi ya UKIMWI yanategemea sana utengefu wa rasilimali fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa afua mbalimbali za UKIMWI kwa wananchi wote wa Tanzania, kwani UKIMWI haubagui. Ni imani ya Kamati kwamba Serikali haitatekeleza afua za UKIMWI kwa kuwalenga watu wenye maambukizi ya UKIMWI peke yao bali hata wale ambao hawajapata maambukizi ya VVU ili kuweza kuwakinga wasipate maambukizi. Aliyekuwa Rais wa Marekani aliwahi kusema kama ifuatavyo; nanukuu:-

*"We live in a completely interdependent world which simply means we can not escape from each other. How we respond to AIDS depends in part on whether we understand this interdependence. It is not someone's problem but this is everybody's problem."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba tunaishi katika dunia ya kutegemeana kwa maana ya kwamba hatuwezi tukakimbiana. Jinsi tutakavyopambana na virusi vya UKIMWI inategemea kama tunaelewa namna tunavyotegemeana; na hili siyo tatizo la mtu mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya kupambana na tatizo hili la ugonjwa wa UKIMWI. Aidha, Serikali iweke mpango mkakati wa kupata vyanzo vingine vya mapato vya kujiwezesha kutenga fedha zaidi kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Itakuwa jambo jema endapo suala la UKIMWI litapata angalau asilimia 50 za maendeleo ya Tume iwe ni fedha za ndani na asilimia 50 nyingine itokane na wafadhali wa nje, kwa kuwa tatizo hili ni la wananchi wote na Tanzania nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianzisha Mfuko wa UKIMWI wa Taifa mwaka 2015 kwa ajili ya kuongeza nguvu za kupambana na tatizo hili. Mfuko huu ulizinduliwa mwezi Desemba, 2016 ambapo mgeni rasmi alikuwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu. Pamoja na malengo mengine, Mfuko huu ulilenga kuwezesha nchi kujisimamia yenyewe ambapo ilitegemewa kwamba ndani ya miaka miwili Serikali iweze kuwa na fedha zake za ndani angalau asilimia 30. Aidha, siku ya uzinduzi ya mfuko huu, zilipatikana shilingi milioni 348. Aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, Hayati Nelson Mandela aliwahi kusema, nanukuu:-

*"History will surely judge us harshly if we do not respond with all the energy and resources that we can bring to bear in the fight against HIV/AIDS."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba historia itatuhukumu vibaya endapo hatutapambana kwa nguvu na kutumia rasilimali zetu dhidi ya VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kamati kwamba upo umuhimu wa utekelezaji wa haraka wa mipango iliyopo kwa ajili Mfuko huu kama ambavyo ilikuwa imekusudiwa, ikizingatiwa kwamba wadau wa maendeleo walikuwa wameiwezesha Serikali kutekeleza shughuli za masuala ya UKIMWI wanaendelea kujitoa na dalili zinaonesha kwamba tatizo hili bado lipo na kuna umuhimu wa kuendelea kukabiliana nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mkakati wa Serikali wa kupata tisini tatu kwa maana ya kwamba asilimia 90 ya watu wanaokadiriwa kuishi na virusi vya UKIMWI wapime, asilimia 90 kati yao watumie dawa za kufubaza na asilimia 90 ya hao wanaotumia, watumie vizuri ili kufubaza, ni dhahiri kuwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI ni wadau muhimu katika mapambano haya. Hata hivyo ili waweze kushiriki kwa ukamilifu, ni vizuri wakapata msaada kwa ajili ya kujikimu kiuchumi na vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inafanya jukumu la kutoa dawa za kufubaza makali ya UKIMWI bila malipo, ni wajibu wa wadau hawa kushiriki katika jitihada za kuimarisha afya zao kwa kushiriki katika nyanja za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kuwa Serikali inayo furusa ya kuwasaidia kimkakati wadau hawa katika kuwezesha uchumi wa watu katika kaya zao na mmoja mmoja; na kwa kuzingatia kwamba upo ushahidi kwamba unapopatikana muunganiko sahihi wa uratibu na rasilimali fedha kidogo *(seed money)* yanapatikana matokeo chanya kupitia vikundi vya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mfano mmoja. Kipo kikundi kimoja Wilayani Mbozi, Mkoa wa Songwe kilichowezeshwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mtaji wa shilingi milioni moja na kikapewa uratibu na usimamizi bora uliofanywa na Baraza la Taifa la watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Kikundi kilifanyia kazi kiasi hicho cha pesa na uratibu na matokeo baada ya miaka mitatu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuna ungezeko la watu walijitokeza katika kijiji hicho kujiweka wazi kwamba wanaishi na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na wamejiunga na sasa wako wanachama 46 kutoka wanachama 14 waliokuwepo mwanzo; pili kikundi kwa ujumla wake kilipata miradi ya kilimo na ufugaji; tatu, kila mwana kikundi amepata miradi ya kilimo na ufugaji kwa ngazi ya kaya yake; nne, kila mwanakikundi na familia yake wameweza kupata bima ya afya kwa mwaka mzima; na tano, kikundi kina akiba ya

shilingi milioni tisa kutokana na uwekezaji wa uratibu na milioni moja miaka mitatu iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfumo huu, Kamati inaona ni mafanikio makubwa ambayo yametokana na uwezeshaji wa fedha na hivyo ni maoni ya Kamati kuwa sambamba na uwezeshaji huo wa kifedha, Serikali itumie mfumo wa konga wa vikundi ndani ya konga kama njia rasmi ya Serikali kuweza kuvitambua vikundi hivi.

Kamati inatoa maoni kwamba Halmashauri zitenge asimilia moja ama zaidi ya fedha ya mapato ya ndani kwa ajili ya kutumika kama *seed money* ambayo itaunganishwa na uratibu unaotolewa kwenye ngazi za Halmashauri kwa ajili ya kupata matokeo makubwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutumika kwa mfumo huu kutasaidia upatikanaji wa Bima ya Afya miongoni mwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI kwa kutumia jitihada zao wenyewe na hivyo kuipunguzia Serikali matumizi makubwa ya dawa kwa ajili ya magonjwa nyemelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Serikali kuwa Halmashauri zote nchini zitenge asimilia moja tu ya mapato ya ndani katika asimilia kumi ambayo imeshatengwa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ambayo itatolewa na mfumo kwa mkopo wa riba nafuu ili kuweza kuongeza nguvu katika mwitikio wa kitaifa wa UKIMWI kwani watu wanaoishi na VVU ni sehemu ya jamii ambayo pia inahitaji kuwezeshwa na kuweza kushiriki katika mapambano haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie kuhusu hali ya upatikanaji ya dawa katika Bohari Kuu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mukasa, kwa muda wako uliobaki, nadhani uhitimishe. Mengine yote yaliyoko humu, wewe zungumza hapo kwamba yaingie kwenye *Hansard*.

**MHE. OSCAR R. MUKASA-MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako, naomba yote yaliyopo kwenye ripoti yaingie kwenye *Hansard* kwa ajili ya kumbukumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue furusa hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ambao wameorodheshwa kwenye ripoti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe pia kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa muda wa kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Wakuu, (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu), Mheshimiwa Jenista Mhagama, pamoja na Manaibu Waziri wake kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoendelea kuutoa. Aidha, napenda kushukuru Mkurugenzi Mtendaji wa *TACAIDS* na yule wa Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya kipekee kabisa, nawashukuru Wajumbe wa Kamati kama walivyoorodheshwa. Nashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Ndugu Stephen Kagaigai. Nawashukuru Makatibu wa Kamati wakiongozwa na Ndugu Asia Msangi, Ndugu Happiness Ndalu na Ndugu Agness Nkwera. Vile vile nawashukuru Msaidizi wa Katibu wa Bunge, Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge na Ndugu Dickson Bisile.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti *UKIMWI (TACAIDS)* Fungu 92, jumla ya Sh.12,909,431,000/= na Fungu 91, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya, jumla ya Sh.5,755,101,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mukasa.

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA NA MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 NA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya – **Fungu 91** na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* **– Fungu 92** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 10 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Masuala ya UKIMWI imepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa shughuli za Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) ikiwa ni kuchambua Bajeti ya Taasisi hizo, Kanuni ya 10(d).

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe Tarehe 25 Machi, 2018 Kamati ilipokea na kuijadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 na kufanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na **Fungu 92** – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS).

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Uchambuzi wa kina wa Taarifa za (Fungu 91 &92), naomba kutoa taarifa ya Kamati inayofafanua mambo makubwa sita (6) yafuatayo:-

1.2.1 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)

1.2.2 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018;

1.2.3 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019*;*

1.2.4 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya Tanzania kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019*;*

1.2.5 Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati wa Fungu 91 na Fungu 92; na

1.2.6 Hitimisho.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA KAMATI

### 2.1 Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati – TACAIDS

**Mheshimiwa Spika,** Katika kufanya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2017/2018, kwa Fungu 92, Kamati ilifanya mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo yaliyotolewa wakati wa kupitisha Bajeti ya Tume hii kwa mwaka wa 2017/2018. Jumla ya Mapendekezo manne (4) yaliyotolewa na Kamati, Mapendekezo yote Serikali imeyachukua na kuyafanyia kazi ikiwemo kufanya ukaguzi wa fedha zinazotolewa kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI kwa asasi zisizo za Serikali ili kuhakikisha fedha hizo zinafanya kazi iliyokusudiwa, Aidha, Serikali inaendelea na mchakato wa kubuni vyanzo vya mapato kwa ajili ya Mfuko wa UKIMWI wa Taifa (AIDS TRUST FUND). Kamati

inaipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati na inaiomba Serikali kuendeleza utekelezaji huo ili mapendekezo hayo yaweze kutoa matokeo chanya kwa ajili ya kuendeleza juhudi za Udhibiti wa UKIMWI hapa nchini.

### 2.2 Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati-Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, ilipewa jumla ya Mapendekezo manne (4) likiwemo mamlaka kuongeza vituo vya tiba ya Methadone angalau kwa kila mkoa ili kuhakikisha wananchi wa mikoa yote wanafikiwa na huduma hii, utoaji wa elimu mipakani ili kuongeza nguvu katika udhibiti wa uingizwaji wa dawa nchini na utoaji wa elimu wa dawa za kulevya kwa jamii kwa ujumla. Mamlaka kwa kushirikiana na Serikali imeendelea kutekeleza mapendekezo hayo kwa kuweka mbinu mbadala kama vile uanzishwaji wa dirisha maalumu katika idara ya magonjwa ya akili katika hospitali zote za rufaa za mikoa za magonjwa ya akili pamoja na miongozo ya kuanzisha na kuendesha nyumba za upataji nafuu (Sober House).

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuufanyia kazi ushauri wa Kamati katika kuendeleza juhudi za kupambana na Dawa za Kulevya. Aidha, ni maoni ya Kamati kuwa, Mamlaka iendelee kuongeza nguvu za kupambana na dawa za kulevya ikiwemo kudhibiti, kuwatambua na kuwasaidia wadau wote wa dawa za kulevya ikiwemo jamii nzima ya Tanzania.**

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2018/2019

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa BajetI kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 (Fungu 91 & 92)

#### 3.1.1 Makusanyo ya Maduhuli

Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 Tume ya Kudhibiti UKIMWI (Fungu 92) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Fungu 91) haikuwa na Makadirio ya makusanyo ya maduhuli yaliyoidhinishwa na Bunge.

### 3.1.2 Upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti (Fungu 92) ambayo ilitengewa Tume kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama ambavyo ziliidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili kuona matumizi yake. Ilikuwa ni matarajio ya Kamati kupata taarifa ya upatikanaji wa fedha walau **asilimia 75** (Fungu 91 & 92) ya mwaka mzima ikizingatiwa kwamba wakati wa uchambuzi wa taarifa ya Tume ilikuwa ni mwezi Machi, 2018 ambayo ni robo ya tatu ya mwaka wa fedha wa 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo katika Uchambuzi wa taarifa ya Utekelezaji wa Fungu 92, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 kiasi cha fedha kilichokuwa kimepokelewa ilikuwa ni **asilimia 57.8** ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa Fedha wa 2017/2018. Aidha, uchambuzi wa Kamati unaonesha kwamba asilimia hiyo iliyopokelewa inabebwa na fedha za Miradi ya maendeleo ambayo kwa asilimia kubwa ni fedha za wafadhili wa nje. Kamati imebaini kwamba fedha za UNDAP zilitolewa kwa **asilimia 552.0** na fedha za *Global Fund* zilitolewa kwa **asilimia 401**. Aidha, fedha za Serikali zilitolea kwa **asilimia 56.7** ambazo ni fedha za matumizi ya kawaida tu zikiwemo fedha za mishahara ya Watumishi ambayo kwa namna yoyote ile ni lazima itolewe ili watumishi waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona kwamba utekelezaji wa shughuli za Tume kwa kiasi kikubwa unategemea sana fedha kutoka kwa wafadhili. Kutokana na hali hiyo ni dhahiri kuwa endapo ufadhili huu utakoma basi Tume itashindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika ajenda nzima ya muitikio wa mapambano dhidi ya UKIMWI ikiwemo kusambaza taarifa, kutetea haki za binadamu walioambukizwa na kuathirika na VVU pamoja na kuhimiza

hali ya kuishi vizuri kwa matumaini, uratibu wa tafiti mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusaidia juhudi za kutafuta chanjo na tiba ya VVU, uhamasishaji wa kitaifa na kimataifa kwa kushirikiana na wadau wote wa masuala ya UKIMWI pamoja na shughuli nyingine.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaiomba Bunge kuihimiza Serikali kukamilisha upelekaji wa fedha hasa za ndani kwa Tume ili iweze kukamilisha utekelezaji wa shughuli zake kabla mwaka wa fedha wa 2017/2018 haujamalizika. Fedha nyingi zilizotolewa ni za wafadhili ikilinganishwa na fedha za ndani ambazo siyo fedha za maendeleo. Rejea Jedwali Na. 1**

Jedwali Na. 1: **Ulinganifu wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha Fedha zilizopatikana 2017/2018 (FUNGU 92)**

| BAJETI ILIYOIDHINISHWA | | UPATIKANAJI WA FEDHA | |
|---|---|---|---|
| **MGAWANYO** | **KIASI KILICHOIDHINISHWA** | **Kiasi kilichopokelewa hadi Feb 2018** | **Asilimia** |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA (FEDHA ZA NDANI)** | | | |
| Mishahara | 1,715,858,000.00 | 1,064,292,000.00 | 62.0 |
| Kawaida (OC) | 812,746,000.00 | 369,723,600.00 | 45.4 |
| Mfuko wa UKIMWI (ATF) | 0.00 | **0.00** | 0 |
| **JUMLA NDOGO** | **2,528,604,000.00** | **1,434,015,600.00** | 56.7 |
| **MAENDELEO (FEDHA ZA NJE)** | | | |
| UNDAP | 132,922,955.00 | 733,763,853.00 | 552.0 |
| ATF | 3,000,000,000.00 | 0.00 | 0 |
| GLOBAL FUND | 322,420,045.00 | 1,295,177,821.00 | 401.7 |
| **JUMLA NDOGO** | 3,455,343,000.00 | 2,028,941,674.00 | 58.7 |
| **JUMLA KUU** | **5,983,947,000.00** | **3,462,957,274.00** | **57.8** |

**Chanzo.** ***Taarifa ya Tume (TACAIDS) ya Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2018/2019***

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Fungu 91), iliidhinishiwa kiasi cha shilingi **Bilioni 4.015** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi **Bilioni 3.448** sawa na **asilimia 85.8** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi **Milioni 567.360 asilimia 14.2** kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Mamlaka. Kwa mujibu wa Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilionesha kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Tume ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **Bilioni 2.707** sawa na asilimia 67.2 ya fedha yote iliyoidhinishwa na bunge kwa ajili ya matumizi ya mwaka wa Fedha wa 2017/2018. Kati ya fedha hizo shilingi **Milioni 543.527 sawa** na **asilimia**

**95.7** kwa ajili ya mishahara ya watumishi na **Bilioni 2.163** sawa na **asilimia 62.7** kwa ajili ya matumizi mengineyo **Rejea Jedwali Na. 2**

Jedwali Na. 2: **Ulinganifu wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha Fedha zilizopatikana 2017/2018 (FUNGU 91)**

| **BAJETI ILIYOIDHINISHWA** | | **UPATIKANAJI WA FEDHA** | |
|---|---|---|---|
| **MGAWANYO** | **KIASI KILICHOIDHINISHWA** | **Kiasi kilichopokelewa hadi Feb 2018** | **Asilimia** |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA (FEDHA ZA NDANI)** | | | |
| Mishahara | 567,360,000.00 | 543,527,370.00 | 95.7 |
| Kawaida (OC) | 3,448,552,991.00 | 2,164,211,867.00 | 62.7 |
| Miradi ya Maendeleo | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | **4,015,912,991.00** | **2,707,739,437.00** | 67.4 |

***Chanzo:** Taarifa ya Mamlaka Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2017/2018*

### 3.1.3 Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Tume ya Kudhibiti UKIMWI ilitengewa jumla ya shilingi **Bilioni 3.455** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambazo ni za wahisani**.** Hadi kufikia wakati Kamati inapokea taarifa ya Utekelezaji mwezi Machi, 2018 kiasi cha Shilingi **Bilioni 2.028** sawa na **asilimia 58.7 tu** ndicho kilichokuwa kimepokelewa ambapo kiasi cha shilingi **Bilioni 1.915** kilitumika. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kulikuwa na matumizi makubwa ya fedha ikilinganishwa na kile kilichokuwa kimeidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kiwango hicho kikubwa cha matumizi ni kutokana na bakaa ya Fedha za Global Fund za mwaka wa fedha wa 2016/17 ambapo Tume ilizipokea mwishoni mwa mwaka 2017. Aidha, fedha nyingine zilipokelewa na Tume chini ya Mradi wa Umoja wa Mataifa wa Kuhuisha UKIMWI kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa ambazo zilitolewa mwezi Desemba 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania inatekeleza Miradi yake ya Maendeleo kwa utegemezi wa fedha kutoka kwa wafadhili kwa **asilimia100**. Serikali inagharamia matumizi ya kawaida ikiwemo mishahara ya watumishi na

matumizi mengineyo ya Tume. Ni maoni ya Kamati kuwa, mwenendo huu wa utegemezi wa fedha za Miradi ya Maendeleo siyo jambo sahihi endapo nia ya Serikali ni kudhibiti UKIMWI kama jina la Tume linavyofahamika sambamba na malengo yake kwa ujumla. Kamati inasikitishwa sana na hali hii ya kutotengwa kwa fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Tume kwani hii ndiyo Tume pekee inayoshughulika na masuala ya UKIMWI hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya haikutengewa kabisa fedha za Miradi ya Maendeleo. Kamati inaona kwamba hali hii haifai kwani ajenda ya kupambana na Dawa za kulevya ni kubwa na mapana kuliko inavyochukuliwa kwa sasa. Kamati inajiuliza ufanisi wa Tume hii katika kupambana na Dawa za kulevya utapatikana kwa njia gani kama Serikali haioni umuhimu wa kuipa Tume fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo? Mfano wa miradi ya maendeleo inayoweza kunufaika ma fedha za maenedeleo ni pamoja na uongezaji wa vituo vya kupata nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevya, kufanya uraghabishi kwa jamii wa namna ya kupambana na kudhibiti dawa za kulevya na hata kuikinga jamii ili isishiriki katika njia yoyote ya matumizi ya dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika**, kukosekana kwa mfumo maalumu kwa ngazi ya jamii kwa ajili ya kuwatambua warahibu wa madawa ya kulevya na hivyo kuweza kuwashirikisha na kuwasaidia ni kikwazo kikubwa katika muitikio wa kitaifa wa kupambana na tatizo hili. Upo ushahidi kuwa watu hawa hurudia baada ya muda mfupi hali yao ya awali ya kutumiadawa za kulevya endapo wataendelea kuwa na ukaribu na watu wanaotumia madawa ya kulevya na endapo watakaa kwa angalau miezi sita bila ya kupata fursa ya kushiriki kwenye shughuli za uzalishaji mali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa sasa tume haipatiwi fedha za maendeleo, na kwa kuzingatia kwamba kuna kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu wanaolazimika kuacha

matumizi ya madawa ya kulevya kutokana na kampeni kubwa inayoendelea, na kwa kuwa kuna ushahidi kwamba watu waliowahi kutumia madawa ya kulevya hurudia katika hali hiyo ndani ya muda mfupi endapo wataendelea kuwa na ukaribu na watu wanaotumia madawa ya kulevya na pia watakaa kwa miezi sita bila ya kupata fursa ya kushiriki kwenye shughuli za uzalishaji mali, basi ni dhahiri kuwa utoaji wa pesa za matumizi ya kawaida ikiwemo kampeni za kukamata wahusika wa madawa ya kulevya bila ya uwepo wa fedha za maendeleo ni sawasawa na mfuaji wa nguo ambaye huitumbukiza nguo hiyo kwenye tope mara tu baada ya kuifua badala ya kuitafutia mahali pa kuikausha, kuipiga pasi na kuihifadhi mahali stahiki na hivyo kuendeleza mzunguko usiokwisha wa ufuaji na kuchafuka tena kwa nguo hiyo bila ukomo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa maana hiyo ni maoni ya Kamati kwamba utoaji na utumiaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida bila kuambatana na mifumo na mipango ya kimkakati inaleta matokeo ya kuendeleza mzunguko wa kupunguza idadi ya watumiaji wa madawa ya kulevya na wakati huo huo kuwarudisha kwa kasi ile ile au zaidi watu hao kwenye hali yao ya awali (Vircious cycle).

**Mheshimiwa Spika**, **Kwa sababu hiyo ni maoni ya Kamati kwamba fedha za maendeleo zinaweza kutoa fursa kwa tume kuanza kujenga mifumo itakayo jumuisha jamii nzima kimkakati katika kuwapokea, kuwatambua, kuwashirikisha na kuwasaidia watu waliowahi kutumia madawa ya kulevya na hivyo kuiwezesha tume kupata matokeo yenye manufaa ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.**

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2018/2019

### 4.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya ikilinganishwa na Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/ 2019

#### 4.1.1 Vipaumbele vya Tume ya Kudhibiti UKIMWI

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 imepanga kujikita katika kuongeza juhudi za utoaji uongozi wa kimkakati wa mwitikio wa Taifa wa UKIMWI. Tume imeainisha maeneo ambayo itaweka mkazo kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019. Maeneo hayo ni pamoja na;

i. Kutafuta rasilimali za UKIMWI kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi;

ii. Kutayarisha na kusambaza miongozo ya UKIMWI kwenye sekta na mikoa ya kipaumbele;

iii. Kuimarisha majadiliano ya kisekta na wadau wa UKIMWI;

iv. Kuongeza jitihada katika kusambaza matokeo ya tafiti za UKIMWI kwa wadau; na

v. Kujenga uwezo wa watumishi ili kuongeza uwajibikaji na ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

Aidha, Tume iliainisha maeneo matatu (3) ya kuweka mkazo zaidi hasa katika kipindi cha kati kwa kuzingatia ufinyu wa rasilimali fedha, maeneo hayo ya kipaumbele zaidi ni pamoja na haya yafuatayo;

i. Kupunguza utegemezi wa wafadhili katika kugharamia programu za UKIMWI nchini;

ii. Kuongeza utumiaji wa huduma za UKIMWI kwa vijana wenye umri wa miaka 15-24 na makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi; na

iii. Kuongeza jitihada za kupeleka huduma za UKIMWI kwenye Mikoa 14 ya vipaumbele ukiwemo mkoa wa Iinga, Kagera, Katavi, Mbeya, Mwanza, Njombe, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Tabora, Dodoma, Geita na Songwe.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia maeneo ambayo Tume iliainisha na kuyaridhia kwa kuwa yalioneka kuwa na tija katika sual zima la uboreshaji wa mapambano dhidi ya VVU/ UKIMWI pia maeneo hayo yanashabihiana na Mipango na Mikakati mbalimbali yakiwemo makubaliano ya kitafa na kimataifa yenye lengo la kupambana na maambukizi ya UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijiridhisha kwamba, Tume imepanga kutekekeleza malengo ambayo yameainishwa katika miongozo mbalimbali ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo ya Muda wa kati 2017/2018-2020/20121, Malengo ya Maendelao endelevu (Sustainable Development Goals 2030). Aidha, utekelezaji wa shughuli hizo zote unalenga katika kuhakikiasha tisini tatu (90-90-90) zinapatikana ikiwemo hakuna mtu au watu wenye maambukizi wanafariki kutokana na UKIMWI. Kwa kutekeleza haya yote kutapelekea kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi wa jamii ambao utachangia jamii isiyo na maambukizi ya VVU.

### 4.1.2 Vipaumbele vya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 imejipangia madhumuni ya kudhibti matumizi ya dawa za kulevya, kudhibiti upatikanaji wa dawa za kulevya pamoja na utekelezaji wa masuala ya kinga na tiba kwa watu wanaotumia dawa za kulevya. Mamlaka imepanga kufikia madhumuni hayo kwa kuweka mikakati mitatu (3) ifuatayo;

i. Kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya katika nchi yetu (Supply Reduction);

ii. Kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya (Demand Reduction);

iii. Kupunguza madhara yanayosababishwa na utumiaji wa dawa za kulevya (Harm Reduction);

**Mheshimiwa Spika,** kamati iliijadili mikakati hii na kuona kwamba ina tija kwa taifa zima kama mikakati hii itatekelezwa kwa wakati. Utekelezaji wa ke unategemea na upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini. Ni imani ya Kamati kwamba, Mamlaka itashirikiana na wadau wengine wa dawa za kulevya katika kutekeleza mikakati hiyo na kuendeleza mapambano dhidi ya dawa za kulevya ili kupunguza madhara ya dawa hizo kwa jamii na kujenga taifa lenye afya bora.

## 4.2 **Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

### 4.2.1 Tume ya Kudhibiti UKIMWI

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa Fedha wa 2018/2019 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kupitia **Fungu 92** inaomba jumla ya kiasi cha shilingi **12.909** ikiwa ni makadirio ya matumizi yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi Bilioni 10.300** sawa **na asilimia 79.7** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na shilingi **Bilioni 2.609** sawa na **asilimia 20.2** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha mishahara ya watumishi.

**Mheshimiwa Spika**, makadirio haya ya matumizi ya mwaka 2018/2019 ni ongezeko la takribani shilingi **Bilioni 6.926** sawa na **asilimia 53.6** ikilinganishwa na bajeti ya matumizi ya Tume kwa mwaka wa Fedha wa 2017/2018. Ni maoni ya Kamati kuwa kwa ongezeko la bajeti hii kwa Tume inaleta matumaini makubwa yanayoletwa na Serikali katika kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI kwa taifa la Tanzania, ikizingatiwa kwamba hapo mwanzo bajeti ilikuwa inatekelezwa na misaada ya wahisani. Kamati inaendelea kuipongeza Serikali kwa kuonesha nia ya kujali afya ya wananchi wake, kwani kwa mujibu wa taarifa mbalimbali inaonesha kwamba hakuna mtanzania ambaye hajaathirika na janga la UKIMWI kwa maana ya kwamba kama mtu hajaambukizwa basi amepata athari za UKIMWI kwa maana ya kufiwa na mtu wake wa karibu akiwemo ndugu, rafiki, jirani n.k.

### 4.2.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 imekadiria kufanya matumizi ya kiasi cha Shilingi **Bilioni 5.755** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni **4.948 sawa na asilimia 85.9** ya fedha yote inayoombwa ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo na Shilingi **806.549** sawa na **asilimia 14.1** kwa ajili ya Mishahara. Makadirio haya yameongezeka kwa kiasi cha shilingi **Bilioni 1.74** sawa na **asilimia 30.2** ikilinganishwa na makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wa Kamati, ilibainika kwamba Tume haijatenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa Fedha wa 2018/2019 kama ambavyo ilijitokeza kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018. Muendelezo huu wa kutotenga fedha za maendeleo unaashiria kutolitazama tatizo hili kimkakati na baade kutakuwa na madhara makubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua majukumu ya Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya ambayo ni udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevya, kufanya uelimishaji kwa jamii na kufanya afua za kupunguza madhara ya dawa za kulevya kwa jamii. Ni dhahiri kwamba jukumu la pili na la tatu ni ya kimkakati kuliko vinginevyo

**Mheshimiwa Spika**, **ni maoni ya Kamati kuwa kuna umuhimu wa Mamlaka ya kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuanza kutenga fedha kwenye Bajeti yake kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kujenga mfumo bora wa kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini kwa upana wake ikiwa ni pamoja na kujenga jamii ya Watanzania isiyotumia dawa za kulevya na kutoshiriki katika biashara na matumizi ya dawa za kulevya.**

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Kamati kufanya Uchambuzi wake wa kina wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 na Makadirio ya matumzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Mamlaka ya Kupambana na kudhibiti Dawa za kukevya, Kamati ina Maoni, Mapendekezo na Ushauri katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo;

### 5.1 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania

### 5.1.1 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Tume ilitengewa kiasi cha shilingi **Bilioni 5.983** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia tarehe 28, Februari 2018 Tume ilipokea kiasi cha shilingi **Bilioni 3.462,** sawa na **asilimia 57.8** tu ya fedha zote zilizotakiwa kutolewa na Serikali kwenda katika Tume hii.

**Mheshimiwa Spika**, **Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inapeleka fedha hizo Tume ya Kudhibiti UKIMWI kabla ya mwaka wa fedha haujaisha na kuanza mwaka mwingine wa fedha ili Tume iweze kukamilisha utekelezaji wa mipango iliyokuwa imejiwekea kwa mwaka 2017/2018. Ni dhahiri kwamba kila mwaka unakuwa na mipango na malengo yake ingawa mipango hiyo huwa ni endelevu.**

### 5.1.2 Utegemezi wa Fedha za Wahisani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa** Spika, Bajeti ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Tume imekuwa ikitekelezwa kwa kutegemea fedha za wahisani kwa **asilimia 100**. Uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa katika mwaka wa Fedha wa 2017/2018 Serikali haikutenga kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya

utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha kwa mwaka wa Fedha wa 2018/2019, Serikali imetenga kiasi cha shilingi **Bilioni 3** tu sawa na **asilimia 29.1** ya fedha yote iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya maendeleo ya Tume kwa mwaka wa Fedha 2018/2019. Pamoja na utengaji huo wa fedha utegemezi huu bado ni mkubwa ikizingatiwa upelekaji wa fedha katika Tume huwa haufanyiki kama vile ambavyo unategemewa (**Rejea 5.1.1**).

**Mheshimiwa Spika,** mapambano dhidi ya UKIMWI yanategemea sana utengefu wa rasilimali fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa afua mbalimbali za UKIMWI kwa wananchi wote wa Tanzania kwani UKIMWI haubagui. Ni imani ya Kamati kwamba Serikali haitekelezi afua za UKIMWI kwa kuwalenga watu wenye maambukizi peke yao bali hata wale ambao hawajapata maambukizi ya VVU ili kuweza kuwakinga wasipate maambukizi hayo. Aliyekuwa Rais wa Marekani aliwahi kusema nanukuu ***"We live in a completely interdependent world which simply means we cannot escape each other. How we respond to AIDS depends in part on whether we understand this interdependence. It is not someone else's problem, this is everybody's problem".*** Kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba, tunaishi katika dunia inayotegemeana kwa maana ya kwamba hatuwezi tukakimbiana. Jinsi tunavyopambana na Virus ivya UKIMWI inategemea kama tunaelewa namna tunavyotegemeana, siyo tatizo la mtu mmoja bali ni tatizo la kila mmoja wetu.

**Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI kwa wananchi wake. Aidha, Serikali iweke mpango mkakati wa kupata vyanzo vingine vya mapato vya kujiwezesha kutenga fedha zaidi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Itakuwa jambo jema endapo ya UKIMWI angalau asilimia 50 ya fedha ya maendeleo ya Tume iwe ni fedha za ndani na asilimia 25 tu itokane na wafadhili wa nje kwa kuwa tatizo hili ni la wananchi wote wa Tanzania na si wale wenye maambukizi pekee.**

### 5.1.3 Mfuko wa UKIMWI wa Taifa (AIDS Trust Fund)

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilianzisha Mfuko wa UKIMWI wa Taifa mwaka 2015 kwa ajili ya kuongeza nguvu za kupambana na UKIMWI hapa nchini. Mfuko huu ulizinduliwa Mwezi Disemba, 2016 siku ya UKIMWI Duniani ambapo mgeni rasmi alikuwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Pamoja na malengo mengine mfuko huu ulilenga kuwezesha nchi kuwa na uwezo wa kifedha wa kupambana na UKIMWI ambapo ilitegemewa kwamba ndani ya miaka miwili Setikali iweze kuwa na fedha zake za ndani kwa ajili ya masuala ya UKIMWI kwa asilimia 30.

Aidha, siku ya uzinduzi wa mfuko huu zilipatikana kiasi cha shilingi **milioni 348** na Serikali iliahidi kutenga kiasi cha shilingi **Bilion 5.5** kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 fedha ambazo mpaka sasa hazijatolewa na kuufanya mfuko huu ushindwe kutekeleza malengo yake. Aliyewahi kuwa Rais wa Afrika Kusini Hayati Nelson Mandela aliwahi kusema, nanukuu "***History will surely judge us harshly if we do not respond with all the energy and resources that we can bring to bear in the fight against HIV/AIDS".*** Kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba, historia itatuhukumu vibaya kama hatupambani kwa nguvu na kwa kutumia rasilimali zetu zote dhidi ya VVU na UKIMWI. Kamati inatambua jitihada za serikali katika jambo hili ikiwa ni pamoja na kuwanza hatua za awali za kutafuta chanzo cha ukahika na kwa ajili ya Mfuko wa UKIMWI wa Taifa.

**Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kwamba, upo umuhimu wa utekelezaji wa haraka wa mipango iliyopo kwa ajili ya Mfuko huo kama ambavyo ilikuwa imekusudiwa kuanzishwa kwake, ikizingatiwa wadau wa maendeleo waliokuwa wanaiwezesha Serikali kutekeleza shughuli za masuala ya UKIMWI wanaendelea kujitoa na hali ya maambukizi mapya ya UKIMWI bado ni hatarishi. Njia za upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Mfuko wa UKMWI zinazotumika mpaka sasa zinadhihirisha hamasa ya kutosha katika kutafuta fedha lakini zinapungukiwa ubora na uthabiti wa mikakati kwa kiasi kikubwa.**

### 5.1.4 Uwezeshwaji kiuchumi kwa Watu wanaoishi na Mambukizi ya Virusi vya UKIMWI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Mkakati wa Serikali wa kupata **Tisini tatu 90 -90-90** kwa maana ya kwamba **asilimia 90** ya watu wote wanaokisiwa kuishi na Virusi Vya UKIMWI wanatambua hali zao za maambukizi, **asilimia 90** kati yao wanatumia dawa za kufubaza makali ya Virusi Vya UKIMWI *(ARVs)* na **asilimia 90** ya hao wanaotumia dawa kwa usahihi ili kufubaza Virusi vya UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa watu wanaoishi na VVU ni miongoni mwa wadau muhimu wa Mkakati huu kuweza kufikia malengo ya Tisini tatu. Hata hivyo, ili waweze kushiriki kwa ukamilifu na ufanisi wanahitaji ustawi wa hali zao kwa ujumla ikiwemo kiafya na kiuchumi. Kwa kuwa Serikali, inafanya jukumu la kutoa dawa za kufubaza makali ya UKIMWI bila malipo, ni wajibu wa wadau hao kushiriki katika kuendeleza jitihada za kuimarisha afya zao kwa kushiriki katika nyanja za kiuchumi ili waweze kujipatia kipato kwa ajili ya kutunza afya zao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kuwa, Serikali inayo fursa ya kuwasaidia kimkakati katika jukumu la kuwawezesha kiuchumi watu wanaoishi na maambukizi ya VVU kwa kuzingatia upo ushahidi kwamba unapopatikana muunganiko sahihi wa uratibu na rasilimali fedha kidogo yaani ***Seed Money*** yanapatikana matokeo chanya kupitia vikundi vya watu waaoishi na VVU.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa mfano wa kikundi kimoja katika wilaya ya Mbozi Mkoa wa Songwe kilichowezeshwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mtaji wa kiasi cha Shilingi **Milioni moja** (1,000,000/=) na kikapewa uratibu na usimamizi bora uliofanywa na Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na VVU. Kikundi kiliifanyia kazi kiasi hicho cha fedha kwa muda wa miaka mitatu (3) na matokeo yamekuwa kama ifuatavyo;

(a) Kuongezeka kwa watu waliojiweka wazi hali zao za maambukizi ya VVU na kujiunga na kikundi (kutoka watu 14 mpaka 46);

(b) Kikundi kwa ujumla wake kilipata miradi ya kilimo na ufugaji;

(c) Kila mwana kikundi amepata mradi wa kilimo na ufugaji kwa ngazi ya kaya yake;

(d) Kila mwanakikundi na familia yake wameweza kupata Bima ya afya kwa mwaka mzima; na

(e) Kikundi kina akiba ya shilingi Milioni Tisa (9,000,000), ikiwa ni miaka 3 baada ya uwezeshaji wa awali wa uratibu na fedha kidogo (seed money)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mfano huu Kamati inaona ni mafanikio makubwa ambayo yametokana na uwezeshwaji wa fedha kidogo na uratibu mzuri kwa kikundi hiki cha watu wanaoishi na VVU katika Halmashauri hiyo na vikundi vingine vinafanya hivyo pia katika halmashauri nyingine ingawa ni kwa uchache.

**Mheshimiwa Spika**, ni maoni ya Kamati kuwa sambamba na uwezeshaji huo wa kifedha (seed money) Serikali itumie mfumo wa KONGA na vikundi ndani ya Konga kama njia rasmi ya Serikali kuweza kuwatambua, kuwashirikisha na kuwasaidia watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI kwa namna yenye tija. Kwa kuwa mfumo huo umetumika kwa mafanikio huko Mbozi na kwingineko na kuwa Tume ya Taifa inafanya kazi tayari na Baraza la Taifa la watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (NACOPHA), na kwa kuwa kwa kupitia Baraza lao la NACOPHA watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI wameweza kushirikiana na halimashauri katika kudhihirisha matokeo chanya kwenye baadhi ya maeneo hapa nchini, ni maoni ya Kamati kuwa Serikali inayo fursa ya kutumia mfumo ambao umejaribiwa na kutoa matokeo chanya kwa manufaa ya watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI nchini kote na taifa zima kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, kutumika kwa mfumo huu kutasaidia upatikanaji wa bima ya afya miongoni mwa watu wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI kwa kutumia jitihada zao wenyewe na

hivyo kuipunguzia Serikali matumizi makubwa ya dawa kwa ajili ya magonjwa nyemelezi kwani watu hawa watakuwa wanapata tiba kwa wakati muafaka na kwa upana (comprehensively) na hivyo afya zao kuimarika kila mara. Faida hii ni sambamba na faida ya watu hawa kupata lishe bora kutokana na miradi yao ya maendeleo na hivyo kupunguza kushambuliwa na magonjwa nyemelezi na kupunguza gharama za matumizi ya madawa kwa ajili ya magonjwa hayo.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa Halmashauri zote nchini zitenge asilimia 1 tu ya mapato ya ndani kutoka katika asilimia 10 ambayo imekwisha kutengwa kwa ajili ya mfuko wa Maendeleo ya Jamii ambayo itatolewa kwa mfumo wa mkopo wa riba nafuu ili kuweza kuongeza nguvu katika mwitikio wa kitaifa wa UKIMWI kwani watu wanaoishi na VVU ni sehemu ya jamii ambayo pia inahitaji uwezeshwaji wa kiuchumi kwa ajili yao binafsi na taifa kwa ujumla.**

### 5.1.5 **Hali ya upatikanaji wa Dawa kutoka Bohari Kuu ya Dawa**

**Mheshimiwa Spika,** Bohari ya Dawa ndiyo inayohusika katika uagizaji na usambazaji wa Dawa hapa nchini. Licha ya taarifa ya Bohari Kuu ya Dawa (Machi, 2018) kuonesha kwamba usambazaji wa Dawa katika vituo vya kutolea huduma ya afya ni **asilimia 89.6** imekuwa ikilalamikiwa kutotekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kutopeleka Dawa katika vituo vya kutolea huduma ya afya kwa wakati hususan dawa za kuzuia magonjwa nyemelezi aina ya ***Septrin,*** hivyo kuwasababishia WAVIU kukosa huduma hiyo kwa wakati na kupata gharama za kununua dawa hizo.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa ushauri kwamba Halmashauri zote nchini zishirikiane na Bohari Kuu ya Madawa kuhakikisha kuwa dawa za kuzuia magonjwa nyemelezi zinapatikana na kusambazwa kwa wakati ili kuwapunguzia gharama WAVIU ikizingatiwa kwamba WAVIU wengi wapo katika kundi la watu ambao hawajapata huduma ya Bima**

**ya afya hivyo kuwasababishia kuingia gharama za kifedha za kununua dawa hizo ili hali kupata dawa hizi bila malipo ni haki yao ya kisera.**

### 5.1.6 Uratibu wa Mashirika yasiyo ya kiserikali *(NGOs)* yanajishughulisha na Masuala ya UKIMWI

**Mheshimiwa Spika**, Mapambano dhidi ya UKIMWI yanafanyika na wadau mbalimbali wa UKIMWI wakiwemo wadau wa ndani na nje, wadau wa Serikali na wadau wasio wa kiserikali ambao wote kimsingi wanahitajika kuratibiwa ili mapambano hayo yatoe matokeo chanya kwa walengwa na jamii kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kuna baadhi ya Mikoa na Halmashauri zimeshindwa kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za taasisi na mashirika yasiyo ya kiserikali *(NGOs)* katika maeneo yao ambayo yanajishughulisha na masuala ya UKIMWI hivyo kupelekea kuwepo kwa baadhi ya vikundi kupata wafadhili zaidi kuliko vikundi vingine ndani ya mkoa au halmashauri moja.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia uongozi wa mkoa na halmashauri katika ngazi za uratibu ufanye usimamizi na uratibu bora wa wadau wa masuala ya UKIMWI ili kuhakikisha rasilimali zote za masuala ya UKIMWI zinazokuja kwa jina la watanzania zinagawanywa kwa usawa katika utekelezaji wa afua za UKIMWI ili kupunguza upendeleo usiokuwa wa lazima ambao unakwamisha malengo ya kupata Tisini tatu za mafanikio (90-90-90).**

## 5.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

### 5.2.1 Serikali itenge Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti na kupambana na Dawa za Kulevya

ambayo ni udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevya, kufanya uelimishaji kwa jamii na kufanya afua za kupunguza madhara ya dawa za kulevya kwa jamii. Ni dhahiri kuwa jukumu la pili na la tatu ni ya kimkakati zaidi ikilinganishwa na jukumu la kwanza.

**Mheshimiwa Spika,** Ni maoni ya Kamati kuwa, upo umuhimu sasa wa Serikali kuiwezesha Mamlaka hii kwa kutenga fedha kwenye Bajeti yake kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kujenga mfumo bora wa kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini pamoja na kujenga jamii ya Watanzania isiyotumia dawa za kulevya na kutoshiriki katika biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika**, **Kamati inaishauri Serikali kuipa nguvu Mamlaka hii kifedha ili iweze kuwa kufanya miradi ya maendeleo ambayo itaiwezesha mamlaka kuwa karibu na wananchi katika kushiriki wa kupambana na kudhibiti dawa za kulevya kwani vita hii ni ngumu na siyo ya mtu mmoja wala mamlaka peke yake.**

### 5.2.2 Utolewaji wa Elimu ya dawa za kulevya kwa Jamii

**Mheshimiwa Spika,** dawa za kulevya ni tatizo linaloongezeka kwa kiwango kikubwa katika jamii yetu siku hadi siku na linaathiri vijana wengi ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa. Kamati imebaini kuwa bado elimu kuhusu matumizi na madhara ya dawa za kulevya haijawafikia wanajamii kwa kiasi kikubwa kama ilivyofanyika kwa mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU/ UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha Mamlaka na wadau wengine wa dawa za kulevya wanatoa elimu jamii ya kutosha kuanzia ngazi ya Kaya, Vijijini, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa zima kwa ujumla. Elimu hii ilenge kuelimisha umma kuhusu madhara ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya kwa kufanya hivyo mapambao haya ya dawa za kulevya yatakuwa shirikishi kwa manufaa ya taifa zima. Kazi hii itaweza kufanyika kwa ufanisi**

**endapo tu itatengenezwa mikakati badala ya matangazo kwa mtindo wa zima moto.**

### 5.2.3 Mfumo wa Taasisi katika Utekelezaji wa shughuli za Masuala ya Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikiendeleza mapambano dhidi ya udhibiti na upambanaji wa Dawa za kulevya nchini ikishirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo taasisi zisizo za kiserikali. Kwa mujibu wa uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa, zipo baadhi ya NGOs na Taasisi zinazojihusisha na masuala ya dawa za kulevya nchi ambazo hazina muundo na mifumo rasmi wa jinsi gani zinawasaidia watumiaji wa dawa za kulevya. Watumiaji wa dawa za kulevya wamegawanyika katika makundi mbalimbali wakiwemo wanaotumia dawa kwa kuvuta na wale wanaotumia kwa kujidunga na sindano (IDUs) wakiwemo wanawake na wanaume.

Kamati imebaini kuwa, zipo taasisi na asasi ambazo zinatekeleza shughuli zake kwa kuwabagua watumiaji wa dawa hizo mfano zinazo wahudumia wanawake peke yake, wale wanaojidunga kwa sindano na mara nyingine wale wanaotumia kwa kuvuta. Ikumbukwe kwamba watumiaji wengi wanaotumia kwa kujidunga ni wale ambao wamepita katika hatua ya kuvuta kwanza na ndipo anakwenda katika hatua ya kujidunga. Ni maoni ya Kamati kuwa, kwa kufanya ubaguzi huu wa makundi ya watumiaji kunazidi kuhatarisha jamii kwani yule ambaye angeweza kufikiwa katika hatua ya kuvuta dawa za kulevya angeweza kuzuiwa kwa kupata huduma kabla ya kufika katika hatua ya kujidunga.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa, kupitia Mamalaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya pamoja na Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia kitengo chake cha uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali wafanye zoezi la utambuzi na uratibu wa asasi zote zinazojishughulisha na Dawa za Kulevya ili kuangalia malengo yao pamoja na kazi zinazofanywa na asasi hizo na kuwawekea mfumo rasmi wa utekelezaji wa shughuli zao ili**

**kuhakikisha kuwa walengwa wanafaidika na uwepo wa asasi hizi kwani fedha zinakuja kwa jina la watanzania mfano mzuri wa uratibu wa aina hiyo ni ule wa wadau wa mwitikio wa UKIMWI nchini.**

### 5.2.4 Uanzishwaji wa Vikundi vya Watu walioathirika na Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,** tafiti zinaonesha kuwa, watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) wamefanikiwa kupitia mabaraza yao yajulikanayo kama (KONGA) ambayo yalianzishwa kuanzia ngazi ya Kata hadi Wilaya. Kupitia mfumo huo wameweza kupata taarifa zote za mwitikio wa Masuala ya UKIMWI pamoja na kujikwamua kiuchumi na kuhakikisha hukuna vifo vinavyotokana na VVU/UKIMWI kutokana na usimamizi unaofanywa na wao wenyewe kupitia uongozi rasmi.

**Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa ni wakati sasa wa Serikali kushirikiana na Asasi zisizo za kiserikali kubuni namna sahihi na ya kimkakati ya kuwafikia watu walioathirika na Dawa za Kulevya ili iwe njia rahisi ya kuwatambua, kuwashirikisha na kuwasaidia waathirika wa dawa za kulevya katika mwitikio wa kitaifa wa janga hili. Njia hii inaweza kusaidia kuwafatilia kwa ukaribu mienendo yao ili kuacha matumizi ya dawa hizo, kupunguza unyanyapaa miongoni mwa jamii, kuwawezesha kufanya shughuli nyingine za kiuchumi pamoja na kupata takwimu sahihi ya warahibu. Kwa kufanya hivi tutajenga Taifa ambalo ni imara na haya yote yanaweza kufanywa chini ya uratibu wa uongozi wa Halmashauri husika kama ambavyo imefanikiwa kwa upande wa UKIMWI.**

### 5.2.5 Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2015

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya chini ya Kifungu Namba 4 na 5 ya Mwaka 2015. Aidha, Sheria

hii ni miongoni mwa Sheria ambazo zimetambulika na nchi nyingine kuwa ni Sheria nzuri ya Kupambana na Dawa za Kulevya. Licha ya ubora wa Sheria hii kuna changamoto katika kuitekeleza kwani kumekuwa na changamoto ya namna ya kuitumia endapo mtuhumiwa akipatikana upande wa pili wa Muungano hasa mipakani hivyo kupelekea kuwa na mianya mingi ya uingizaji wa Dawa za Kulevya nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mamlaka ziko dalili dhahiri kuwa kuna ongezeko la uhalifu unaohusiana na Dawa za Kulevya Tanzania visiwani ikilinganishwa na Tanzania Bara hasa kutokana na ukali wa sheria na utekelezwaji wake kwa upande wa huku Bara. Aidha, Mamlaka ilieieleza Kamati kwamba hii inatokana na kukosekana na utofauti (**Synergy**) wa Sheria ya Udhibiti na kupambana na Dawa za Kulevya katika maeneo haya mawili kunaleta changamoto ya udhibiti wa tatizo hili ndani ya mipaka ya Tanzania kwa ujumla wake.

**Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa, kuna umuhimu wa Serikali kuitazama tena Sheria hii ili iweze kuipa nguvu zaidi Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ili kutokomeza biashara ya dawa za kulevya na kuinusuru nchi yetu.**

## SEHEMU YA SITA

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa muda wa kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi  Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama (Mb) pamoja na Manaibu Waziri Mheshimiwa Antonny Peter Mavunde (Mb) na Mheshimiwa Stella Alex Ikupa (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa wanaondelea kuutoa kwa Kamati wakati wote wa shughuli za Kamati. Vilevile napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu Ofisi ya Waziri Mkuu wa Sera na Uratibu Ndg. Prof. Faustin Kamuzora na Katibu Mkuu Waziri Mkuu na Bunge Ndg.

Maimuna Tarishi pamoja na Maafisa Waandamizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Ndg Rogers William Siyanga, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati hii ili kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa nafasi ya kipekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI , kwa kazi nzuri walioifanya ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Pamoja na ufinyu wa muda wajumbe hawa lakini walikuwa tayari kutekeleza jukumu hili kubwa na kwa wakati. Kwa heshima kubwa nomba kuwatambua kwa majina Waheshimiwa wafuatao:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb | **M/Mwenyekiti** |
| 3. | Mhe. Dkt. Haji Hussein Mponda, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Salma Rashid Kikwete | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Zainab Matitu Vullu , Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Kemirembe Julius Lwota, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe Albert Obama. Ntabaliba | Mjumbe |
| 9. | Mhe Rose Cyprian Tweve | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Yussuf Haji Khamis | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Masoud Abdallah Salim , Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Godfrey William Mgimwa, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Mattar Ali Salum, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Amina Nassor Makilagi, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Edward Franz Mwalongo, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Omar Ahmad Badwel, Mb | Mjumbe |

20. Mhe. Prof. Norman Adamson King Sigalla, Mb Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, wakiongozwa na Ndugu Stephen Kagaigai Katibu wa Bunge, Ndg. Athuman Hussein Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge na Ndugu Dickson Bisile Mkurugenzi Msaidizi kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kipekee nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndg. Asia Msangi, Ndg. Happiness Ndalu na Ndg. Agnes Nkwera na msaidizi wao wa Kamati Ndg. Grace Mwenye kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania **Fungu 92** jumla ya shilingi **Bilioni Kumi Na Mbili, Milioni Mia Tisa Na Tisa, Laki Nne Na Thelathini Na Moja Elfu** **(12, 909,431,000/=)** na **Fungu 91** Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya jumla ya Shilingi **Bilioni Tano, Milioni Mia Saba Hamsini Na Tano, Laki Moja Na Moja Elfu (5,755,101,000/=)**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.



Mhe. Oscar R. Mukassa, (Mb)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa mawasilisho ambayo yako chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, mchana tutaendelea na uchangiaji.

Wachangiaji wa mchana japokuwa tunatarajia vyama vilete majina, lakini kwa upande wetu Bunge, tunayo majina hapa ya vyama kwa Wabunge walioomba kuchangia Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na tutawataja wachache wale ambao wataanza mchana. Uwiano utakuwa CCM asilimia 70, CHADEMA asilimia 18 na *CUF* asilimia 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakichangia Wabunge 10 wa CCM watachangia watatu wa CHADEMA, atachangia *CUF* mmoja. Kwa hiyo, ndiyo uwiano utakaokuwa unachukuliwa kadri tunavyoendelea kuchangia.

Wachangiaji wetu wa mchana ama wale ambao wameomba Wizara hii; ni Mheshimiwa Munira Mustapha Khatibu, Mheshimwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mheshimiwa Ally Seif Ungando na Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa. Wengine wataendelea kutajwa kadri michango itakavyokuwa mchana.

Tunao pia Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye na Mheshimiwa Khatib Said Haji. Kwa hiyo, hawa mchana ndiyo watakaoanza halafu wengine watakuwa wakiitwa kwa kadri tunavyoendelea. Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka sasa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.36 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala. Tunaanza na Mheshimiwa Deo Sanga halafu Mheshimiwa Anne Malecela na Mheshimiwa Deodorus Buberwa Kamala wajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niwe mtu wa kwanza kuanza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli pamoja na Makamu wa Rais na Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kazi nzuri wanazozifanya kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la elimu. Naishukuru tena Serikali kwa namna ambavyo imeanzisha mpango wa elimu bure, hivi sasa wanafunzi wamekuwa ni wengi sana katika mashule yetu. Kuna shule kwenye Halmashauri yangu ya Mji wa Makambako; Shule ya Ikwete, Shule ya Mashujaa na Shule za Juhudi. Shule hizi ni za siku nyingi, zimechakaa sana majengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa namna ya kipekee kabisa ikishirikiana na wananchi nami Mbunge wao pamoja na Waheshimiwa Madiwani, tuone namna gani tunajiimarisha kuweza kujenga shule hizi ili zifanane na shule nyingine ambazo zipo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la pili la afya. Naipongeza sana Serikali kwa dhati kabisa kwa kazi nzuri inayofanya katika maeneo yetu kwa kutenga fedha nyingi kupeleka katika Vituo vya Afya, Zahanati na Hospitali. Kazi hiyo ni nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, katika Halmashauri ya Mji wangu wa Makambako tuna Kituo cha Afya kimoja, kinachoitwa Lyamkena. Tunaomba na sisi pia tupewe fedha kama ambavyo zimepewa Halmashauri nyingine ili nasi Kituo cha Afya hiki kiweze kufanya kazi za upasuaji na kama ambavyo vituo vingine vinafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kutenga fedha ambazo wamenipa kwa ajili ya kujenga

Hospitali ya Mji wa Makambako. Naishukuru sana. Pia katika Hospitali ya Mji wa Makambako niiombe Wizara au Serikali, Kituo cha Afya kilipandishwa hadhi tangu mwaka 2013 na kuwa hospitali, lakini mgao wa dawa bado tunapata kama Kituo cha Afya wakati ni hospitali. Naiomba sana Serikali itupe mgao wa dawa kama hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni maji. Naipongeza Serikali kwa dhati kwa namna ambavyo imenipa fedha za miradi katika Kijiji cha Ibatu, Usetule, Mtulingala, Mahongole na Mbugani - Nyamande, Kiumba na Ikelu. Hivi sasa shughuli za maji kule zinaendelea. Naipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo inataka kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Serikali, kuna mradi mkubwa ule wa fedha za kutoka India ambazo zilitengwa kwenye bajeti. Mradi ule wa miradi 17, Tanzania Bara miradi 16 na Zanzibar mradi mmoja (1). Katika miradi hiyo na Makambako ipo na Njombe Mjini ipo na Wanging'ombe ipo. Naomba kujua, ni kitu gani kinakwamisha mradi huu usianzishwe? Kwa sababu tulipata taarifa wakati fulani, alikuja Waziri wa India pale Ikulu, alisaini mkataba huu. Tatizo ni nini? Kimekwamisha kitu gani mradi huu hauanzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ione namna ambavyo itaanzisha mradi huu wa fedha za kutoka India ili kutatua tatizo la Mji wa Makambako katika suala hili la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu ujenzi. Alipokuja Mgombea ambaye ni Rais sasa, katika Mji wa Makambako, alituahidi kutupa kilomita sita za lami katika Mji wa Makambako. Mpaka sasa hata kilomita moja haijaanza. Kila nikiongea na Mheshimiwa Waziri, amekuwa akiniambia kwamba safari hii ilitengwa kilomita mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali angalau wangeanza kwa kilomita mbili hizi, angalau katika

Mji wetu wa Makambako, ungekuwa ni mji unaopendeza kupitia barabara zake za lami. Siyo hivyo tu, naiomba pia *TARURA,* katika Mji wa Makambako kuna barabara ya kutoka pale Makambako kwenda Maguvani. Maguvani ni eneo la sekondari, pana korongo kubwa katikati. Naiomba Serikali itupe fedha za dharura kwa sababu hivi sasa wanafunzi wanaotoka ng'ambo kwenda katika shule hii ya Sekondari ya Maguvani wanazunguka Mjini Makambako ambako ni kilomita 10 wakati pale ni kilomita moja na nusu tu. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ione namna ya kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *TARURA* vile vile, tuna stendi ya Mji wa Makambako. Stendi ile ndiyo stendi kubwa lakini maji yote yanapotiririka yanakwenda kwenye majumba ya watu na nyumba kadhaa zimeanguka. Naiomba Serikali ituwekee makalavati ambayo yatanusuru nyumba hizi za wananchi katika stendi kuu ya Makambako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipokuja Rais katika Mji wa Makambako alituahidi kutujengea uwanja wa mpira. Tumeshaandaa uwanja na mpaka sasa hakuna kinachoendelea. Naiomba sana Serikali kuona namna ya kutimiza ahadi hii ya Mheshimiwa Rais kwa wananchi. Kila wakati tumekuwa tukiwaambia kwamba muda bado, tunaiomba sasa Serikali ichukue jukumu la kuhakikisha uwanja huu unajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwenye suala la umeme kwa nchi nzima na hususan katika Halmashauri yangu. Vijiji vingi sasa Mkandarasi yuko *site* anaendelea kuweka nguzo. Naipongeza sana Serikali kuona sasa katika vijiji vyote vya Halmashauri ya Mji wa Makambako vitapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, katika Kijiji cha Kifumbe kwenda Kijiji cha Mtanga ni kilomita tano mpaka sita. Shughuli hii Mkandarasi anayoendelea nayo, kijiji kitakachobaki katika ukanda huo ni hicho peke yake. Kwa

hiyo, naiomba sana Serikali, ione namna ya kuona kijiji hicho nacho kinaunganishwa katika awamu hii inayoendelea hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ione namna ya kuanzisha mashamba kwa ajili ya mbegu mbalimbali za kilimo hasa mahindi katika ukanda wetu. Tatizo la mbegu limekuwa ni kubwa sana. Utaona wakati fulani baadhi ya watu wamekuwa wakichakachua mbegu, ni kwa sababu mbegu hizi ni chache. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ione namna ya kuanzisha mashamba kwa ajili ya mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna Mawakala waliosambaza pembejeo. Hivi sasa ni zaidi ya miaka mitatu, hawajalipwa. Naiomba Serikali kama kuna baadhi ambao walifanya kazi nzuri katika kufuatilia na katika kuhakiki, basi walipwe. Wale ambao walichakachua wakafanya udanganyifu waambiwe kwamba ninyi hamlipwi kwa sababu mmefanya udanganyifu, lakini wale waliofanya vizuri walipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu fidia kwa soko la Kimataifa, Makambako. Wale watu sasa imekuwa ni tatizo kubwa. Naiomba Serikali, wakati fulani wameandamana, wamejaa kwenye mafuso kwenda Dar es Salaam na wakasema watashuka pale Ikulu, kama kuuawa wauawe. Nilimwambia Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nilimwambia, nikawasihi. Naiomba sana Serikali, chonde chonde tuone namna ya kuwalipa fidia hawa watu. Zaidi ya miaka 21 sasa hawajalipwa fidia, kwa hiyo, imekuwa ni tatizo kubwa sana. Naomba sana walipwe fidia watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati nachangia suala la Mambo ya Ndani, naomba niseme kama ifuatavyo: Makambako ndiyo *center.* Unapozungumzia kwenda Mbeya, Makambako ndiyo *center;* unapozungumzia kwenda Songea, Makambako ndiyo *center;* unapokwenda Iringa,

Makambako ndiyo *center.* Ni *center* wakati fulani baadhi ya wahalifu ndiyo wanakimbilia pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie Waheshimiwa Wabunge, hata wale waliokuwa wanafanya uhalifu kule Kibiti walipatikana baadhi ya wawili, watatu pale Makambako. Nikaenda mimi pale Polisi wakaniambia Mheshimiwa Mbunge njoo uwaone watu hao. Walikimbia kumbe wakaenda Songea. Walipoona Songea msako mkali, wakakimbilia Makambako. Kwa hiyo, naomba sana, tuone katika magari yatakayokuja ambayo Mheshimiwa Waziri jana alisema, katika mgao tuone... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Kamala ajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ya pili kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Ofisi yake. Nitachangia maeneo matatu tu. Nitaanza na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, nitakuja Wizara ya Afya na mwisho nitamalizia Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nitakalolizungumza, nafikiri ni jambo ambalo linamgusa kila Mbunge hapa ndani na nina uhakika linamkera kila Mbunge hapa ndani; suala la kuchoma nyavu za kuvulia samaki. Kwanza naomba niipongeze Serikali sana. Serikali inafanya kazi nyingi, inafayanya kazi nzuri sana na Watanzania wanaridhika na mwenendo wa ufanyaji kazi, kwa jinsi ambavyo Serikali inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la uvuvi haramu, linanipa taabu kidogo. Wavuvi ni wafanyabiashara. Wanapokwenda kuvua na nyavu zao, mtaji wao ni nyavu zao. Suala linalonisumbua kwenye Serikali, jamani Serikali naomba mnisaidie, wavuvi hawa wananunua nyavu

madukani. Wao ndio watumiaji wa mwisho. Wanapotumia kuvua wanakamatwa na zile nyavu ambazo zinazaa uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu najiuliza kila wakati, kwani hizi nyavu wamezipata wapi? Suala linalonisumbua, hizi nyavu wamezipata wapi? Kikatiba Serikali Kuu ndiye anayetakiwa asimamie maendeleo ya wananchi. Aangalie wananchi wanavyopambana katika kujitafutia maendeleo. Serikali Kuu inatakiwa ihakikishe wakulima wanapata pembejeo, wanapata mbolea lakini mbolea sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inashindwaje kutafuta chanzo cha nyavu hizi ambazo ndizo zinazozaa uvuvi haramu? Swali liko hapo, kwa sababu mvuvi yule kwa ufahamu wangu mdogo, maana yake kule kwetu Same sisi hatuko kama watu wa kwenye Ziwa Victoria. Nina imani kwamba mvuvi anakwenda kununua nyavu, lakini nina uhakika Serikali inapaswa kuangalia zile nyavu kama ambavyo inaangalia pembejeo na mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inanisumbua. Inakuwaje Waziri wa Mifugo anakwenda Ziwa Victoria, anakuta nyavu zilizotumika Ziwa Victoria asilimia 90 ya nyavu zile eti ni haramu? Zinatoka wapi hizi nyavu? Hawa wavuvi wanatengeneza wenyewe? Ndiyo kitu kinanisumbua. Naiomba Serikali sasa kwa sababu hili la kuchoma nyavu za wavuvi, kwanza tunachoma mtaji wa mvuvi yule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mfanyabiashara, ukinichomea mtaji wangu unaniua mimi. Naiomba Serikali ifanye kila njia idhibiti nyavu hizi ambazo ndiyo zinazaa uvuvi haramu. Iangalie hizi nyavu kule zinakotengenezwa; ina maana Serikali haijui nyavu zimetoka wapi? Kama zinaingia kwenye nchi kutoka nje, kwa nini inaruhusu nyavu ambazo zitazaa uvuvi haramu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona tusikimbilie kuchoma hizi nyavu zikiwa kwa mtumiaji wa mwisho.

Tuziwahi hizi nyavu zinapoingia nchini. Nafikiri Serikali imenielewa. Tutamwonea mvuvi, *unless* kama hawa wavuvi wana viwanda vyao wenyewe vya kutengeneza hizi nyavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itakapokuja kutujibu, itoe jibu ambalo litatatua hili tatizo. Mwisho kabisa, tusisikie nyavu zinachomwa. Tusikie huko kwenye viwanda vya hizo nyavu au huko bandarini, nyavu zinarudishiwa huko huko. Nimeeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili linahusu Wizara ya Afya. Mimi ni mwanamke ambaye nimepata watoto mara nne. Nashukuru kwa Sheria ya Nchi yangu kila nilipopata mtoto nilipata M*aternity Leave* ya siku 84. Namshukuru Mungu kwamba nilizaa watoto wangu salama. Sasa sheria ya nchi hii kwenye *Maternity Leave* iko sahihi, unajifungua mtoto, unapata siku 84 za kumwangalia mtoto mpaka anapata nguvu na wewe unarudi kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sheria iangaliwe upya, kwa sababu kuna mwanamke anazaa watoto wawili, kuna mwingine anazaa pacha watatu, kuna mwingine anazaa pacha wanne, kuna mwingine bahati mbaya anazaa mtoto mwenye kichwa kikubwa, kuna mwingine anazaa mgongo wazi, watoto hawa wanahitaji uangalizi wa zaidi ya siku 84. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu aliyepata mtoto mmoja, tena mwenye afya ni tofauti sana na mtu aliyezaa kitoto njiti. Ni tofauti na mwanamke aliyezaa mtoto ambaye mgongo uko wazi. Ni tofauti na mwanamke aliyezaa mtoto mwenye kichwa kikubwa, anahitaji uangalizi wa zaidi ya siku 84. Naiomba Serikali ikaingalie hii sheria upya kuliko inavyo-*generalize* kwamba kila mwanamke akijifungua, *84 days* anapumzika. Je, wale waliozaa njiti? Je, ambaye Mungu amempa watoto wanne? Je, ambaye amepewa watoto wawili, wameungana na wana matatizo kichwani? Siku 84 hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, turudi tuangalie hii sheria upya tena kwa uharaka, maana yake juzi nimemwona yule mwanamke aliyetoka pale *Aga Khan,* amejifungua watoto watatu na ameajiriwa na Serikali hii iliyopo madarakani, hii Serikali yetu. Hivi huyu siku 84 na watoto watatu hawa zinamtosha? Hapo nitaomba Serikali iangalie vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye Wizara ya Ardhi. Hapa nazungumzia Kata ya Ndungu. Hii kata iko Wilaya ya Same. Mimi naishi *next door* na Kata ya Ndungu. Kata ya Ndungu ni kata yenye *population,* tukienda kwenye sensa ya mwaka 2012, *population* yake ni wananchi 16,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kata, nakwenda kwenye ardhi kwa sababu kwa vipindi viwili nimekaa hapa Bungeni nikitetea wananchi wa Jimbo la Same Mashariki. Hili suala nilikuwa naliongea, kwamba nusu ya ardhi ya Kata ya Ndungu, ardhi yake ina mwekezaji sijui wa mkonge lakini ule mkonge hauendelezwi. Nililalamika hapa Bungeni, Waziri wa Uwekezaji wa kipindi kile Mheshimiwa Mama Maria Nagu, akaja akaona ile shida, akaona kwamba kwa kweli pale kuna tabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 60 ya wananchi 16,000 ni vijana, hawana ardhi, hawana mashamba, hawana makazi, ardhi yote iko kwa mwekezaji ambaye ule mkonge hauendelezi, upo tu. Namsihi Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, yupo Mheshimiwa Mama Angelina, aje Ndungu akaione ile ardhi ambavyo iko pale, hakuna kinachotokea, vijana wa Kata ya Ndungu hawana nyumba, wanaishi na wazazi wao. Anaoa mke, anakaa na mama yake na baba yake. Ndoa itavunjika ile; gubu la mama mkwe! Anataka ajenge nyumba yake, hana mahali pa kujenga. Mkonge umekufa, nusu ya ardhi ya Kata ya Ndungu. Nafikiri Serikali imenisikiliza. Sikuwa mtata sana, nimeeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kamala halafu, Mheshimiwa Ibrahim Hassanali Mohammedali na Mheshimiwa Nuru Bafadhili, wajiandae. Mheshimiwa Kamala, hayupo, Mheshimiwa Ibrahim Hassanali Mohammedali

**MHE. HASSANALI MOHAMEDALI IBRAHIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa Bungeni salama nikiwa na afya nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri aliyowasilisha leo asubuhi hapa Bungeni. Kabla sijakwenda huko, kwanza nitakuwa mwizi wa fadhila kama sijachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli. Haya tunayozungumza hapa Bungeni kujadili bajeti mbalimbali za Wizara zote, huu ni mkakati ya Mheshimiwa Rais kwa kukusanya kodi. Ndiyo maana leo tuko hapa kifua mbele kuzungumzia bajeti zetu za Wizara mbalimbali ikiwepo bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Rais kwamba sisi Wabunge wa CCM tuko nyuma yake na tutakuwa nyuma yake mpaka atakapomaliza kipindi chake 2025. Nasema hivi kwa sababu gani? Sisi wote hapa ni mashahidi wa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli anapofanya kazi kwa bidii, upendo na uzalendo katika kuwasaidia Watanzania waliokuwa wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa sababu siwezi kuyataja mambo yote, nitaje mambo mawili matatu ambayo Mheshimiwa Rais katika kipindi kifupi alichokuwa madarakani ameweza kununua ndege *ATC*, ameanza vilevile kutujengea reli ya *SGR* (*Standard Gauge Railway);* ukusanyaji wa pesa wa mapato ambayo ni historia katika nchi hii katika awamu zote zilizopita, Awamu hii ya Tano, kwa kweli pesa zinazokusanywa na *TRA* kwa sababu mwenyewe Mheshimiwa Rais anafuatilia hilo suala, limekuwa historia ya *TRA* wanakusanya pesa kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika ujenzi wa bomba la mafuta, tumeona Mheshimiwa Rais alivyojitahidi na vilevile ufuaji wa umeme ambapo hata juzi hapa Mheshimiwa Rais amekwenda kuzindua Kinyerezi ambayo tutapata megawati 2,500. Hayo ni baadhi ya mambo tu, siwezi kuyataja yote lakini nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mambo haya anayofanya naweza kuwaambia Wapinzani 2020 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli hana upinzani nchi hii. Kwa utabiri wangu huu Waheshimiwa Wabunge wa CCM watakuja kuniambia, Mheshimiwa Raza kweli asilimia ambayo Mheshimiwa Rais atapata ni zaidi ya 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mambo anayofanya Mheshimiwa Rais, vilevile nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kumteua ndugu yangu Mheshimiwa Kassim Majaliwa kuwa Waziri Mkuu wa Awamu hii ya Tano. Niseme kwa sababu gani nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Waziri Mkuu; kwanza Waziri Mkuu wetu *masha Allah* ni *handsome. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua Mheshimiwa Waziri Mkuu ana hadhi ya kipekee ninapokwenda popote, basi huna haja ya kumwambia mtu huyu ndio Waziri Mkuu wa Tanzania, anajulikana tu. Sifa nyingine ambayo Waziri Mkuu anayo, kwanza ni mtu makini sana, mwenye busara, mwenye upendo, mchapa kazi, kwa ufupi tunaita kwa kizungu *all-rounder*. Mheshimiwa Waziri Mkuu hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze vilevile dada yangu Mama Mary kwa kukupata mtu kama wewe, hii pia ni sifa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuje katika bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nimefuatilia bajeti hii, nimeona ni bajeti ambayo ni ya matumaini na hususan Mheshimiwa Waziri Mkuu nakupongeza kwa kusimamia masuala ya mbolea na mbegu bora. Kama tunavyojua, nchi yetu ya Tanzania asilimia kubwa

sana ni wakulima na wafugaji. Kwa hiyo, naomba vilevile haya masuala ya upatikanaji wa mbolea yawe ni endelevu kwa sababu tukiwa na mbolea nzuri na mbegu nzuri, tutapata matunda mazuri na wakulima watapata nguvu na watakuwa na imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka nipongeze kwa kuongezwa bajeti kwenye Wizara ya Afya kwa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu. Hapa nimesoma na nimeona kwamba imeongezwa mpaka kufikia shilingi bilioni 269. Hii inaonesha Serikali ilivyokuwa makini katika kuwasaidia Watanzania ambao ni wanyonge na maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa umeme, napongeza vilevile kwa sababu umeme ni kitu muhimu sana katika nchi hii. Bila umeme hakuna viwanda, hakuna chochote. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais anapokwenda na *speed* hii na naamini Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko nyuma yake kumsaidia ili kuona kwamba baadhi ya vijiji ambavyo havijapata umeme, natumaini mpaka mwaka 2020 hivyo vijiji vitafikiwa na umeme ili wananchi wetu nao wapate kumwona Mheshimiwa Rais angalau katika kuangalia *TV* zao na kusikiliza redio zao. Hiyo ni moja katika maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dar es Salaam, naweza kusema ni kioo cha Tanzania, kwa sababu watalii wote, wafanyabiashara wakubwa wote wanakuja katika Jiji la Dar es Salaam. Leo Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna baadhi ya sehemu Dar es Salaam huwezi ukapita usiku kama hujaziba pua. Kwa sababu kuna watu wanalala, kuna watu wanaoga, kuna watu wanafanya choo hapo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao ushahidi kwenye simu yangu kwamba watu katika mitaa fulani Dar es Salaam wanachafua mazingira kabisa, yaani mazingira yanakuwa machafu sana. Sehemu hiyo siyo kwamba wanalala watu wawili au watatu, wanalala watu 50 na kuendelea. Ushahidi huo ninao kwenye simu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Jiji letu la Dar es Salaam liangaliwe kuhusiana na mazingira yetu kwani haya mambo yamepita kiasi. Watu wanaoga kabisa, wanachukua maji wanachota wanaoga hapo hapo, wanafanya haja zao; haileti picha nzuri sana. Naona iko haja kwa Mkurugenzi wetu wa Jiji Dar es Salaam kuliona hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kama atanipa nafasi kuwa Mkurugenzi wa Jiji wa Dar es Salaam kwa muda wa wiki mbili au tatu, nitafanya kazi hiyo kwa wiki tatu na mtaiona Dar es Salaam itakavyokuwa safi. Naamini huyu Mkurugenzi aliyekuwepo sasa hivi, baada ya kusikia maneno haya, atajirekebisha na atafanya yale ambayo yanastahiki katika jiji letu la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi ya kuzungumza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. HASSANALI MOHAMEDALI IBRAHIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nuru Bafadhili, halafu Mheshimiwa Riziki Said Lulida na Mheshimiwa Mwalongo ajiandae.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa nikiwa katika afya nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na bajeti hii nitazungumzia kuhusu elimu na afya. Nikianzia na suala zima la elimu, hivi karibuni tulimsikia Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamini William Mkapa, akilalamikia ufaulu mdogo wa wanafunzi wetu katika shule zetu za Serikali. Ni kweli wanafunzi wetu katika shule za Serikali wanapata

elimu lakini haifanani na wanafunzi wa shule za binafsi. Kwa sababu shule za sekondari za Serikali utakuta darasa moja lina wanafunzi 45, 50 mpaka 60; ni sekondari nayo hiyo. Shule za binafsi utakuta labda *form one* wako 20, *form two* wako 25, lakini hawazidi 40 na Walimu wapo wa kutosha ambao wanawafundisha wale wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitaaluma mimi ni mwalimu. Mwalimu unatakiwa katika muda wa dakika 40 unazopewa, uzungukie wanafunzi wote wa darasani kwako ili ujue kosa lake; amefanya nini katika kazi uliyompa au anahitaji msaada gani? Sasa utakuta darasa lina wanafunzi 70 au 80, utawazungukiaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali iangalie pia uwiano wa wanafunzi katika madarasa yetu. Walimu wanafanya kazi, wanajitahidi, lakini madarasa yanajaa wanafunzi kiasi ambacho msaada unakuwa ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali iwaangalie sana wanafunzi wetu. Kila siku mimi natamka, nasema, "mwanafunzi mwenye njaa, hafundishiki." Kuna wanafunzi wengine, pengine amekula saa 11.00; asubuhi hajala chochote anaambiwa aende shule. Kwa kweli mwanafunzi yule kwake itakuwa ni vigumu sana kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu kule shule za watu binafsi, au wenzetu Wazungu wanasema za *private,* utakuta wanafika kule saa 4.00 kuna kantini, mzazi kampa mtoto wake pesa, anajinunulia chakula. Mchana vilevile anajinunulia chakula. Sisi watoto wetu, anaondoka nyumbani pengine hata uji hakunywa asubuhi na hata senti 20 au Sh.50/= za kwenda kumuwezesha kununua chochote cha kutafuna, hakupewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa akili itakuwa kwenye kusoma au atawaza njaa? Mara nyingi wanafunzi wa namna ile, utakuta hawashiki lolote katika akili zao, kwa sababu anawaza nikitoka hapa nitakwenda kula nini? Kwa hiyo,

Serikali ifanye utaratibu wa kuwawezesha angalau wapate uji. Saa 4.00 mwanafunzi akipata uji, atajua kuwa nikifika shuleni nitapata uji, nitakunywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuzungumzia kuhusu Walimu. Walimu kweli wanafanya kazi, lakini kuna maneno. Sisi tulipoanza kazi ya Ualimu tuliambiwa Ualimu ni wito kama Shehe, Padri, *Sister* au Askofu. Imani ile sisi ilituingia. Sasa hivi tuna Walimu wenye matatizo. Mwalimu amekwenda shule, asubuhi tayari ameshalewa. Hivi mwanafunzi atakwenda kusoma nini kwa Mwalimu yule ambaye amelewa? Au Mwalimu usiku anakwenda kwenye mabaa mwingine anajiuza. Mpaka wanafunzi wanafikia kumdharau Mwalimu darasani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali ihakikishe kuwe na utaratibu maalum au kuwe na *circular* maalum inayowafanya Walimu wawe wanaiheshimu ile kazi ya Ualimu, kama sisi tulivyoambiwa kuwa Ualimu ni wito. Ndiyo maana viongozi wengi hapa ni Walimu kwa sababu walikuwa na nidhamu nzuri sana. Kwa hiyo, tuwaangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuangalie stahiki za Walimu. Kuna Mwalimu anapandishwa daraja lakini anaweza kukaa miaka miwili hajapewa pesa zake. Kwa hiyo, Walimu nao wanachoka, ndio wanafanya kazi vilevile wanavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu suala la afya. Nitazungumzia kuhusu hospitali yangu ya Mkoa ya Rufaa ya Tanga, Bombo. Kwa kweli ile hospitali inapokea wagonjwa kutoka sehemu mbalimbali, lakini ile hospitali ina tatizo moja; Hospitali ya Bombo haina lifti ya kuwapandisha wagonjwa katika jengo la *Galanos*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wagonjwa inabidi wapandishwe kwa kutumia mabaunsa. Kuna watu maalum wenye miili mikubwa wamekaa pale, unawalipa ndio wanakupandishia mgonjwa wako juu ili aende wodini

akalazwe. Kwa hiyo, Serikali iangalie jinsi gani itaitengeneza ile lifti ya Hospitali ya Bombo ukizingatia hospitali ile ndiyo Hospitali yetu ya Rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuzungumzia kuhusu Hospitali ya Wilaya. Sisi kama Wilaya ya Tanga nasema hatuna Hospitali ya Wilaya. Hospitali ya Wilaya huwezi kuifananisha na Kituo cha Afya kimoja kinaitwa Makorora, kingine kinaitwa Ngamiani, kingine kinaitwa Pongwe katika Kata ya Pongwe. Vile vituo huwezi kuvilinganisha na hospitali yetu ya Wilaya. Nimeitembelea ile Hospitali ya Wilaya, nimekuta vile vyumba ni kama mabweni ya wanafunzi wa sekondari, yaani kabisa haikujengwa kihospitali ya Wilaya. Ni ili mradi tuambiwe Tanga tuna Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali hiyo ya Wilaya haikuzingatia miundombinu ya walemavu. Kuna ghorofa ya kupanda huko juu. Sasa mlemavu akiambiwa apande juu, atapanda vipi? Hospitali hiyo ya Wilaya pia hatuna *ambulance* ya Wilaya. Kwa hiyo, watu wa Tanga Hospitali ya Wilaya pia tunategemea pia hivyo Vituo vya Afya na vilevile tunategemea Hospitali ya Rufaa ya Bombo. Kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe Tanga na sisi tunapata hospitali yetu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya iliyojengwa, inaelekea kama ilijengwa kwa mshtuko sijui; imejengwa labda kisiasa au vipi, kwa sababu tulikuwa na kiwanja chetu cha hospitali kiko sehemu za Mwakibila Kata ya Tangasisi. Miaka kati ya 2007 mpaka 2010, kiwanja kile kiliuziwa mwekezaji. Mwekezaji yeye hakujenga chochote, badala yake kikahamishwa kiwanja kilichokuwa kijengwe hospitali kikapelekwa hiyo sehemu ambayo inaitwa Masiwanishamba, lakini miundombinu ya kwenda huko Masiwanishamba pia hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali hiyo hiyo tunayoambiwa ni Hospitali ya Wilaya, ikifika saa 9.30 hospitali

inafungwa. Ina maana wagonjwa wanaambiwa wasiugue tena hapo mpaka kesho tena saa moja na nusu, kunakuwa hakuna tena huduma ya hospitali. Kwa hiyo, naiomba Serikali itusaidie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie suala zima la kuhusu madawa ya kulevya. Kama tulivyoona kwenye vitabu vyetu tulivyopewa kuhusu masuala mazima ya dawa za kulevya, ni dhahiri kwamba vijana wengi wanaotumia dawa za kulevya wakipelekwa kwenye *Sober House* wanatulia vizuri wanakuwa wazuri, lakini wanaporudi tu kwenye maeneo yao na akikutana na wale wengine, wanarudia tena kazi yao. Kwa hiyo, inakuwa ni kama kumpigia mbuzi gitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Serikali kama itawezekana ihakikishe tujengewe *Sober Houses* kwa ajili ya vijana wetu wale ambao wameathirika na dawa za kulevya. Pia katika hizo *Sober Houses* tuhakikishe wakifika kule *at least* wanapata mafunzo mbalimbali ya kazi za mikono. Kuna mwingine atafundishwa labda useremala, mwingine atafundishwa kushona cherehani, kwa hiyo, akirudi huku uraiani anaweza akaajirika pengine akipewa nyezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika hii Serikali ni sikivu. Kwa hiyo, tuhakikishe wale tunaowapeleka katika *Sober Houses,* tuhakikishe tunawapatia mafunzo maalum. Siyo tu yale mafunzo ya kuwazuia wasile unga, lakini wapate mafunzo ya kuhakikisha kwamba wanapata mafunzo ya kazi za mikono ili akirudi aende akajitegemee mwenyewe katika maisha yake anayoishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie kuhusu rushwa sasa. Hii rushwa yaani imekuwa kama ni donda ndugu, kwa sababu mtu anaambiwa kabisa hapa hatupokei rushwa, lakini ukimaliza anakwambia unaniondoaje...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Mwalongo na Mheshimiwa Daudi Silanga wajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru nakushukuru. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema nami kuchangia katika hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunahitaji amani na amani haichezewi. Watu wanajaribu kuangalia ubinafsi bila kuiangalia nchi inakwenda wapi. Popote panapotokea vita wahanga ni wanawake na watoto. Leo wanasema usipoziba ufa utajenga ukuta. Tumeiona Libya sasa hivi wanawake na watoto wanahangaika. Tumeiona Iraq, wanawake na watoto wanahangaika, tunaiona Somalia, wanawake na watoto wanahangaika, tumeiona Rwanda, wanawake na watoto walihangaika, wanakuja mpaka Tanzania kama wakimbizi na Burundi hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo chokochoko ndogo ndogo zinazoanza ziwe za kidini, ziwe za kisiasa. Wachungaji, Maaskofu na Mashehe watangaze dini. Nia ya kupewa nafasi hiyo kutangaza uadilifu, kuitangaza amani kwa wananchi wao. Wakianza Maaskofu, Mashehe kujiingiza katika siasa, siasa ni *propaganda*. Sasa wanataka kutangaza mchezo wa *propaganda* waingize katika dini, haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Serikali isimamie kikamilifu. Kwa mfano, mimi hapa mlemavu, ikianza vita mtakimbia humu nyote, mtaniacha mimi niko humu ndani. Hivyo mhanga namba moja ni mlemavu. Wagonjwa waliokuwa mahospitalini watakuwa wahanga wa vita. Wazee watakuwa wahanga wa vita. Watanzania hatutaki vita. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, kama wana hoja, iletwe hoja patafutwe ufumbuzi na usuluhishi. Kutumia majukwaa

ya dini kutangaza mazungumzo ambayo yatawafanya vijana wapate mihemko, waingie mtaani wafe wao wakimbie, haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kuna *clip* ya mtoto amekimbia Syria, ameokotwa na *UN* ameshika nguo ya mama yake na dada yake, anasema nakwenda kumshtakia Mungu, mama yangu anauawa namwona hivi hivi, baba amekimbia. Wanaume hawana uvumilivu na watoto. Pakianza vita, wanaume wote wanakimbia wanaacha akinamama wanahangaika hapa. Wanawake Tanzania nzima, tuungane tupinge hii kitu. Tutakaoathirika ni wanawake. Haikubaliki na wala haitakubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunashiba kwa vile pana amani hapa. Tunataka maji hapa kwa vile pana amani. Mnataka barabara kwa vile pana amani hapa. Bila amani hakuna maji wala barabara. *Bodyguard* anamkimbia Rais, *bodyguard* anamkimbia Waziri Mkuu, kila mmoja anatafuta taharuki, anakimbia anakwenda anakokwenda kwake. Tusilichukue kama ni kitu cha mzaha, ni kitu hatari. Watanzania nimewaangalia leo nilikuwa nasikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais Nyerere akisema hivi: "Kuna watu wanaangalia maslahi ya mabepari na kuna watu wanaangalia haki za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hao wanaoangalia haki za mabepari waangaliwe kwa macho mawili ili wasituingize katika mgogoro." Hata hiyo amani isimamiwe kwa ukamilifu. Kama kuna wanaovunja amani upande huu na upande wa pili vile vile ushughulikiwe. Msumeno unakata mbele na nyuma, haukati sehemu moja. Italeta furaha na faraja kuona wale wanaotaka kuleta uharibifu wa amani nchi hii wanashughulikiwa bila kuangalia anatoka wapi? Anaelekea wapi? Amani ni amani tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie miradi na mikopo ya Tanzania. Kwa muda mrefu Tanzania ina madeni makubwa, tena madeni makubwa sana lakini madeni haya yalisababishwa na mikataba ambayo

haikufanyiwa *analysis.* Nitatoa mfano, anakuja *World Bank,* anatoa mradi wa *Selous,* ule mkopo nitalipa kwa miaka 25, lakini anakupa *condition* ambayo badala ya kusema utafaidika, anafaidika yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikuja kututawala, sasa hivi wanatutawala kwa kupitia mikopo. Mkopo wa shilingi bilioni 500 anakwambia utalipa kwa miaka 25. Kila mwaka kwa maana hiyo nitalipa shilingi bilioni 20. Shilingi bilioni 20 nikichukua mwakani riba inarudi pale pale mpaka miaka 100 mkopo huo hauishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile wao wanacheza na akili yetu bila kuangalia sisi wenyewe kama hicho wanachokifanya kina usahihi gani katika kufanya *analysis?* Analeta mkopo wa shilingi bilioni 500, anaweka na *conditions* za pembeni. Watakuja kufanya kazi ma-*expatriate* wetu, watalala katika nyumba kubwa, wanataka wafanyakazi wanne, mshahara wake kwa mwezi dola 20,000; kila mwisho wa mwezi atakwenda Mikumi au Serengeti. Ile mikataba ya pembeni ukiisoma inatia kinyaa kabisa. Haiifanyi nchi hii kama itaweza kukwamuka kwa kupitia hii mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiulize, ilijengwa reli ya kati, kutoka Kigoma mpaka Dar es Salaam kwa kodi za vichwa za Watanganyika wakati ule. Kila Mtanganyika aliambiwa atoe kodi; na waliijenga reli kwa hela zetu kutoka Kigoma mpaka Dar es Salaam. Matokeo yake ilikuwa ni wao kuja kuchukua madini, wao kuchukua pembe na wamefaidika wamekuwa matajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutajirika, wamekuja na *system* ya pili ya mikopo. Naomba, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mwenye dhamana na Mawaziri, waiangalie mikopo kwa umakini sana. Nina imani kuwa hii kazi ndugu yangu anaiweza. Awaokoe Watanzania ambao wanaangamia na mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkopo wa Selous, umeletwa mkopo maeneo ya Udzungwa, Mikumi na Ruaha, zote ziko

chini ya *TANAPA.* Wanataka kujenga viwanja vya ndege, barabara kutoka Lindi kwenda Liwale hakuna. Kwa nini wasituambie tunataka mkopo huu ukajenge barabara ya Liwale ili watalii waende Liwale? Kwa nini wasijenge barabara ya kwenda Namtumbo ili watu waende Namtumbo? Wanatupa *conditions* ambazo zinatufanya tunakwazika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mradi huu utapita, najua kweli hii Serikali siyo sikivu na nitaufuatilia. Kama Serikali ni sikivu, mkopo wa *World Bank* unaokwenda Selous ufanyiwe kazi ili mwananchi wa mikoa mitano hii ikiwemo Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ambayo tumeiacha kwa muda mrefu kwa miradi mikubwa, kwa kweli sitakubaliana nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mradi wa *SAGCOT. SAGCOT* ni *Sothern Agriculture Corridor of Tanzania.* Lindi, Mtwara na Ruvuma tuliachwa. Hii ni mikakati ya makusudi ya kutufanya Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma tuendelee kuwa maskini. Sasa wamelala waliolala, sisi bado tuko macho. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu ameturudisha tena kuja kuangalia haya, je, wataendelea kutukandamiza Mikoa ya Kusini? Kama unataka kuleta msaada wa utalii kusini, unaiachaje Kilwa, wakati Kilwa katika *heritage* ilikuwa namba 21? Naomba mradi huu wa *World Bank* utushirikishe Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma kwa kikamilifu ili tuwe *beneficiary* kwa mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia barabara. Hata Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi katika kutembelea mikoa yote; Mikoa ambayo iko nyuma ni Lindi, Mtwara na Ruvuma katika barabara. Sasa uwiano wa maendeleo, kuna wengine wanapaishwa kwa maendeleo, wengine wanawekwa nyuma, haikubaliki. Watanzania ni Watanzania wote tunahitaji kula hii keki. Leo Mkoa wa Lindi, Mtwara na Ruvuma tuna *produce* korosho ya kutosha; uchumi wa nchi uko juu; leo umwambie mtu twende Liwale, hawezi kufika. Mwambie mtu aende Milola sasa hivi hafiki. Hakuna barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba bajeti itakayokuja ya Wizara ya Ujenzi iangalie mikoa ambayo imeachwa kwa muda mrefu ipewe *priority.* Hii itatufanya na sisi tufarijike kujiona na sisi tuko ndani ya keki ya Watanzania. Tunawaona wenzetu Kaskazini wanavyosaidiwa huko, nasi tunataka Kusini iende sambamba na mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi, nimekuja kuzungumza hayo machache kuitangaza amani, amani hii itatusaidia katika kilimo, afya na elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwalongo na Mheshimiwa Daudi Silanga jiandae.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, nianze kwa kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali jinsi inavyofanya kazi. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Watendaji wote wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri Mkuu imeeleza kwamba bado tuna nafasi ya kuweza kukopa kama Watanzania kwa sababu deni letu ni himilifu. Naomba sasa tukope ili kusudi miradi ya maendeleo ambayo katika Jimbo la Njombe Mjini haitekelezeki, sasa itekelezeke. Mradi wa kwanza ni ujenzi wa barabara ya Itoni – Manda. Barabara hii miaka yote imekuwa ikiambiwa itajengwa ili kwenda Mchuchuma na Liganga, lakini haijengwi. Amewekwa mkandarasi kilometa 50. Kutoka Njombe ni kilometa 50 ndani ya Jimbo la Ludewa, lakini mkandarasi yule hana nguvu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande cha kuanzia Njombe mpaka linapoishia Jimbo la Njombe Mjini hakijaanza. Sasa tuombe kama fedha hiyo ya kukopa ipo. Kama Serikali

ina fedha ya kutosha, iweke mkandarasi mwingine aanze kutengeneza barabara kutoka Itoni kwenda Manda ili kusudi tunaposema kwamba tuna mradi kielelezo wa Liganga, basi hata barabara iendane. Maana barabara ile ina uchumi mkubwa kwa wananchi lakini vile vile ina madini hayo yaliyopo huko ambayo tunahitaji yachangie uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni maji. Maji katika Jimbo la Njombe Mjini ni tatizo kubwa sana. Miradi ya maji haitekelezeki. Wakandarasi wako *site* lakini malipo yanachelewa sana. Yuko Mkandarasi anafanya kazi katika mradi wa Igongo, malipo yake yanachelewa sana; na tunajua kabisa kwamba hela ya maji ni hela ambayo wote tunachangia kupitia mafuta na kadhalika. Kwa hiyo, naomba sana, kama Wakandarasi wako *site* na wanafanya kazi, basi walipwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, ni msikivu na anajitahidi kufanya kazi vizuri, lakini tunajua kabisa kwamba matatizo yapo kwa Watendaji, lakini kwake kama Waziri na Naibu wake wanafanya kazi vizuri mpaka wanajitwisha na ndoo. Hii ni dalili kwamba kazi wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la maji ya Njombe Mjini. Mradi wa maji Njombe Mjini leo hii nasimama hapa Bungeni kwa mara ya tatu na kila bajeti inapokuja ya mwaka wanataja mradi wa Njombe Mjini tutapata maji kutoka Mto Hagafilo, lakini mradi ule haujatekelezwa mpaka leo. Tumeambiwa upo kwenye miradi ya miji 17, tunataka tuambiwe safari hii shida ni nini? Vinginevyo, tuambiwe kabisa kwamba mradi ule haupo ama upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kabisa kwamba iko miradi mikubwa katika mikoa mingine inatekelezwa na watu wanapata maji, lakini sisi pale Njombe maji yapo kilometa tisa yanatakiwa yafike katikati ya mji, tunashindwa kuyapata yale maji, kila siku tunaambiwa fedha ipo, tutafanyiwa lakini hatufanyiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la afya. Naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri inayofanya. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, sisi katika Jimbo la Njombe Mjini tumepewa shilingi milioni 500, tunajenga Kituo cha Afya pale Ihalula, lakini pamoja na ujenzi huo wa Kituo cha Afya, wananchi kwa kushirikiana na Halmashauri wanajenga kituo kizuri sana cha afya katika Kata ya Makoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Makoo, Kata ya Ihalula na Kata ya Utalengoro ni Kata ambazo ziko mbali sana na mjini. Tunaomba, tutakapokuwa tumekamilisha kazi hizi, basi tupewe magari ya wagonjwa, lakini tupewe Waganga wa kutosha katika vituo hivi vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, iko Hospitali ya Mkoa ambayo inajengwa. Naishukuru sana Serikali kwa kutujengea Hospitali ya Mkoa. Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika, aliiona ile hospitali nzuri kabisa inayojengwa pale, lakini hospitali ile bado haijakamilika. Kwa sasa tunatumia Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, ndiyo imechukuliwa kama Hospitali ya Mkoa, lakini ina upungufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chumba cha upasuaji, wagonjwa wa aina zote wanapasuliwa chumba hicho hicho. Hebu niambie, huku unapasua mtu labda amevunjika mguu halafu kuna dharura ya mama mjamzito, unafanyaje? Unamtoa huyu mgonjwa unayempasua mguu umwingize mama mjamzito? Kwa hiyo, tunaomba pale Hospitali ya Kibena, tujengewe angalau *theatre* ya ziada ili kusudi angalau tuweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndiye Mbunge wa watu wenye UKIMWI. Naiomba sana Serikali, kama sisi Njombe tuna UKIMWI na tumekuwa tukitangazwa kwamba hata *data* zetu ziko juu sana, basi tuhudumiwe. Huduma tunayoiomba, kwanza kabisa hatuna mashine ya kupima virusi vya UKIMWI *(viral load).* Sisi ndio tunaoonekana kwamba ndio waathirika wa kwanza, lakini inabidi tubebe sampuli za damu tupeleke Mbeya au tupeleke Iringa kwa ajili ya kupima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Njombe tupewe mashine hiyo ya kupima *viral load* ili tupime pale Njombe. Vile vile tupewe dawa kwa ajili ya magonjwa nyemelezi. Kama kweli Serikali inatutambua sisi kweli ni waathirika wa kwanza katika nchi hii kwa maradhi ya UKIMWI, basi tupewe dawa za kutosha za magonjwa nyemelezi na vitendanishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine unaenda kufanya vipimo unaambiwa vitendanishi hakuna. *MSD* hawatoi vitendanishi, vitendanishi wanatakiwa kutoa Wizara ya Afya na Wizara ya Afya inachelewa kutoa. Linapokuja suala la kugawa Waganga, sisi tunaoumwa zaidi, tupewe zaidi Waganga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana tupo mjini, tunaambiwa ah, Hizi Halmashauri za Mjini tusiwape Waganga wa kutosha, lakini sisi tunaomba mtambue kwamba sisi ni wagonjwa zaidi na tunakiri hilo na tunaomba mtusaidie. Msiendelee kututangaza tu kwamba sisi ni wagonjwa zaidi, lakini hamtusaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Njombe Mjini hakuna hata kijiji kimoja ambacho umeme wa *REA* umewaka. Wakandarasi wanakuja, wanaulizia wanaondoka. Naomba sana, najua ndugu yangu Waziri wa Nishati yuko makini na tunawasiliana naye kwa karibu. Hebu awasimamie hawa watu wafanye ile kazi kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la elimu. Hapa nazungumzia habari ya mikopo ya elimu ya juu. Mikopo ya elimu ya juu inanyanyasa wanafunzi. Anakopeshwa mwanafunzi mwaka wa kwanza, mwaka wa pili hakopeshwi, atapata wapi fedha ya kuendelea kujisomesha? Matokeo yake wanaanza kuzurura mitaani, wanaomba misaada. Mara waje kwa Waheshimiwa Wabunge, mara waende wapi. Kwa hiyo, naomba Bodi ya Mikopo ikimkopesha mwanafunzi mkopo mwaka wa kwanza, ihakikishe kwamba huyo mwanafunzi anakwenda naye mpaka mwaka wa nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu bila malipo ni zuri sana na linawasaidia sana wananchi huko vijijini na wananchi wote kwa ujumla, lakini tatizo lake kubwa ni kwamba elimu bila malipo ingewekewa kiwango maalum kwamba kiwango cha chini kabisa ambacho Serikali itatoa kwa shule ni kiasi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuna shule ambazo zina wanafunzi wachache. Kuna shule zina wanafunzi 150. Kwa hiyo, ukichukua ile namba ya wanafunzi na kutoa ile fedha ya Serikali, unajikuta kwamba fedha ya matengenezo na michezo haipatikani pale shuleni. Kwa hiyo, naomba sana kuwe na angalau kiwango cha chini ambacho kinaanzia angalau kuweza kulipia zile gharama za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile liko suala la elimu msingi. Elimu msingi, watoto sasa hivi wako darasa la nne na watoto hawa kila nikisimama hapa wanasema kwamba itafika mahali tutakuwa na *form one* mbili; tutakuwa na *form one* waliosoma miaka saba, lakini tutakuwa na *form one* waliosoma miaka sita. Je, maandalizi yetu yakoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile suala la kuandaa Walimu kwa ajili ya elimu msingi limekwama. Ilikuwepo *NACTE* na *NECTA,* sasa zimeingia kwenye ushindani, kwamba Mabaraza haya mawili ya Mitihani yanavutana jinsi ya kutoa elimu kwa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itoe maamuzi, kama tuliamua kwamba Taasisi ya Elimu ya Ufundi wajibu wake ni kusimamia mitihani yote ya ufundi ikiwemo ya Majeshi, Polisi na kadhalika, basi isimamie. Isirudi tena Wizara ya Elimu ikatoa mitihani mingine ikairudisha Baraza la Mitihani. Huku ni kuleta mkanganyiko na kuwavuruga Watendaji. Vilevile wapo wawekezaji katika masuala ya elimu, nao wanapata shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la Polisi. Nimetembelea Gereza la Njombe pale mjini. Pale kuna mahabusu wana miaka sita, saba mpaka kumi wanalalamikia

suala la Polisi kwamba upelelezi unachelewa. Naomba sana, wanaotuhumiwa kwa mauaji upelelezi ukamilike ili kusudi kesi zao ziweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile liko suala la Mahakama. Mahabusu wa Gereza la Njombe wanailalamikia sana Mahakama. Moja, Njombe hatuna Mahakama Kuu, inakuja kwa vikao. Ikikaa kikao Njombe, haimalizi kesi, matokeo yake mahabusu wamelundikana sana katika Mahakama ya Njombe na wanasababisha ile mahabusu ionekane ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama inapokuwa haifanyi vikao na ikakamilisha zile kesi, ina maana inasababisha mlundikano wa mahabusu pale Magereza, matokeo yake kunakuwa na watuhumiwa wengi sana, halafu Gereza linaonekana ni dogo. Kwa hiyo, naomba sana, Idara ya Mahakama, namwona Mwanasheria Mkuu yuko hapa, tuone, tupeleke Mahakama Kuu Njombe ili kusudi Vikao vya Mahakama Kuu vifanyike Njombe. Kwa sababu Mheshimiwa Rais ameshawadhihirishia Watanzania kwamba fedha katika nchi hii siyo tatizo. Kwa hiyo, naomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la mawakala wa pembejeo. Mawakala wa pembejeo waliosambaza mbolea mwaka 2015/2016 wamepekuliwa mara nane. Hesabu zao zimepitiwa mara nane, lakini hakuna Wakala hata mmoja aliyepewa jibu. Jamani, huu siyo uungwana. Kama watu hawa wamepekuliwa hivi, wapewe majibu.

*(Hapa kengele ililiakuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Daudi Shilanga na Mheshimiwa Deo Ngalawa ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa

Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya hasa katika suala zima la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kusimamia suala zima la kilimo hususan pamba, tumbaku na kahawa, lakini kazungumzia pamba. Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoka kwenye 120,000 kwa miaka mitatu mfululizo ya nyuma, tumevuka sasa hivi tunatarajia kuvuna 600,000, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali hususan katika suala zima la pembejeo, katika mikakati hii mikubwa tunayoifanya, basi ni vema iende sambamba na pembejeo ili kusudi mazao haya yasiendelee kuathirika kwa kukosa pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Waziri Mkuu, mazao haya mengi tumeyapata, lakini wale tunaokaa kandokando na uhifadhi, tunalo janga la tembo. Tembo wamekuwa wakivamia sana katika maeneo hayo na kusababisha maafa makubwa katika jamii. Basi nalo hilo katika suala zima la ulinzi iwe sehemu ya kipaumbele, hususan maeneo ya Itilima, maeneo ya Nyasosi na maeneo ya Mwalali na Nkuyu na Longalombogo, basi viwekwe vituo ili tembo hawa wasiendelee kuja kuharibu mazao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu kwa vijana, Mheshimiwa Waziri Mkuu Wizara yake inayo dhamana ya elimu. Naomba na kuishauri Serikali, hususan katika vijiji vipya na mikoa mipya na Wilaya mpya zilizoanzishwa, kumekuwa na changamoto ya kutokuwa na shule katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika baadhi ya maeneo wananchi wamekuwa wakijenga madarasa, lakini katika Sheria ya Elimu wanasema lazima tuwe na madarasa sita. Sasa mimi kama mwakilishi wa wananchi, wananchi wananiuliza, hivi tutaanzaje kuwa na majengo sita wakati

kuna darasa la kwanza litapita, la pili mpaka la tatu na la nne? Kwa nini tusiwe na manne halafu tuendelee na mwendelezo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, vijana wengi wako kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, ni vyema Wizara ya Elimu ikashauriwa kuwa na mipango ambayo siyo ya kubana sana ili watoto wetu waweze kupata elimu kama tunavyotarajia katika Awamu hii ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara katika Mkoa wetu wa Simiyu. Aliahidi katika Wilaya yangu ya Itilima, nilikuwa sina jengo la utawala, lakini leo ukiingia Itilima mambo yanakwenda vizuri, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la kuanzisha Wakala wa Barabara *(TARURA),* mimi nishauri katika sehemu ya *TARURA,* ni vyema hawa *TARURA* sasa waweze kushiriki katika vikao vya Halmashauri kusudi wapate mawazo kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao. Tutakapofanya hivyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu tutakuwa na uboreshaji mkubwa na ufanisi mkubwa katika kutekeleza majukumu yao. Siyo kama inavyofanya sasa, inafanya yenyewe, wananchi hawajui kinachoendelea katika maeneo husika, lakini katika suala zima, kazi inakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia suala la juzi alilokuwa anazungumzia kuhusu la wanunuzi wa pamba hususan katika kuanzisha Vyama vya Ushirika. Vyama vya Ushirika mwendelee kuviimarisha ili kusudi wanunuzi hao wasije wakapoteza fedha zao pindi msimu utakapofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la vijana kuhusu mkopo. Nimeingia Bungeni leo ni mwaka wa tatu. Nimekuwa nikisikiliza humu ndani Waheshimiwa Wabunge tukizungumzia habari ya asilimia 10. Naiomba Wizara itengeneze mfumo wa fedha hizi kuwa na kapu moja ili vijana katika Halmashauri zetu nchi nzima wawe wanakopa kwa

pamoja na kurudishwa ili hizi fedha ziwe na mzunguko katika maeneo mbalimbali ya vijana na *generation* ya vijana wanaokuja. Siyo hivi inavyokwenda, fedha hizi zinakuwa nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita, nilikuwa napitia katika Mkoa wa Dar es Salaam. Mkoa wa Dar es Salaam mwaka 2017 umekopesha shilingi bilioni 3.9, lakini *collection* ni shilingi milioni 400. Utaona sasa kizazi kinachokuja huku nyuma, kitakuta fedha hazipo na hizo fedha zitapotea, lakini tukizisimamia vizuri nina imani kwa usimamizi wenu mahiri Mheshimiwa Waziri Mkuu, akilisimamia hili nina imani fedha zile zitasaidia kizazi kijacho na katika mfumo mzima wa uchumi wa viwanda, vijana wetu wanaweza wakajiajiri na wakafanya kazi kubwa sana katika maeneo yetu husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala zima la afya. Naiomba Serikali ya Awamu ya Tano, miongoni mwa Wilaya 67 na Itilima imo kwa kupata Hospitali ya Wilaya. Ninazo Zahanati 28 zimejengwa ndani ya Serikali ya Awamu ya Tano, chini ya Mheshimiwa Dokta Magufuli na wewe mwenyewe Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba zile Zahanati basi Serikali Kuu wazimalizie kwa maana ya kwamba wananchi wameshajenga mpaka hatua za mwisho, lakini ziko Zahanati tatu ambazo zimeshakamilika. Nyumba ya Mganga na kila kitu. Tunachosubiri tu ni kupeleka Wauguzi na tuna tatizo na suala zima la watumishi. Itilima inahitaji watumishi katika kada ya Afya watumishi 630, tulionao ni 120; lakini tuna wakazi 342,000. Kwa hiyo, utaona adha hii inayowapata wananchi wa Itilima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, alipofanya ziara yake ya kwanza katika Mkoa wetu wa Simiyu mwaka 2016, alipita akaahidi barabara. Leo wakandarasi wako *site* na wanafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika ziara yake aliahidi ujenzi wa mabwawa katika Wilaya yangu ya Itilima na kule Mwapalala, sasa bwawa limekamilika na maji yanatoka kwa asilimia mia moja. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya. Kweli anaitendea nchi haki na kiapo alichoapa, kweli Watanzania wote tunaamini kazi anayoifanya ni kubwa na nzuri zaidi. Nchi yetu ilikuwa haina usafiri, leo ina ndege tatu na nyingine zinaendelea kuja. Hiyo ni hatua kubwa ya maendeleo.

Ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge tuendelee kumuunga mkono Rais wetu kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Mwenye macho haambiwi tazama. Naungana na maneno ya Mheshimiwa Azza, amesema 2020 wataisoma. Wataisoma kweli kweli kwa sababu kazi iliyofanywa ni kubwa na inaonekana na Watanzania wote wanaikubali kazi mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mambo mengi ambayo mmeyafanya Serikali ya Awamu ya Tano, lakini kubwa zaidi kuweza kujitegemea sisi wenyewe kuliko kuwa manamba wa kuendelea kukopa katika nchi za nje. Unapokuwa mkopaji hata heshima ya nchi haipo, lakini sasa wameshika adabu yao na ndege juzi ilipoteremka kila mtu nadhani alinyamaza kimya ambaye alikuwa haiombei nchi yetu mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngalawa, halafu Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Dau Mbaraka wajiandae.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niongee katika Bunge lako Tukufu. Kwanza nianze na pongezi kwa Serikali yetu na kufuatia ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pale Ludewa tarehe 26 Januari, 2017, imeleta matokeo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofika Ludewa aliambiwa juu ya taabu kubwa ya barabara, hasa ile barabara inayotoka Mkiyu kuja Madaba ambayo inapita kwenye mradi wa Liganga na Mchuchuma na pia kuna ile barabara ambayo inatoka Mchuchuma kwenda Liganga. Mpaka hivi ninavyozungumza, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umeanza toka ile Julai, 2017 na unaisha mwezi Oktoba mwaka huu. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napongeza miradi ya *REA* inayoendelea katika Jimbo langu. Wakandarasi wapo na wanaendelea na kazi hivi ninavyozungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Serikali katika miradi hii ya Vituo vya Afya. Zile shilingi milioni 500 tumepata katika Vituo vya Afya viwili; Vituo vya Afya vya Manda na kule Mlangali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, alipita Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Nditiye, tumeona *impact* ya ile ziara. Sasa hivi ninavyozungumza, minara nane ya mitandao ya mawasiliano ya *Halotel* imeanza kujengwa. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa hatua ambazo inachukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie na mambo mengine yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna huu Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Mradi huu wa Liganga na Mchuchuma ni mradi wa kimkakati. Napenda sasa kuiomba Serikali kwamba

hii miradi lazima tuiwekee programu. Kwa sababu ni miaka mitano, lazima tuwe tunajua mwaka wa kwanza tunafanya kitu gani? Mwaka wa pili tunafanya kitu gani? Mpaka ile miaka mitano itakapofika na iweze ku-*take off. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa naamini kwamba, hizi barabara zinazotengenezwa sasa kuelekea kwenye hii miradi miwili ni miundombinu wezeshi kuelekea huo mradi kuanza. Pia, tuna ule mradi wa Makambako – Songea, Madaba – Ludewa, kwa maana ya Gridi ya Taifa na yenyewe sasa hivi tayari imeshafika Ludewa, bado tu muda kidogo uende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali itupe ule mpango kwamba sasa tutakapokuwa tumemaliza *stage* hii tunakuja *stage* hii, ili tuweze kuzifanyia *assessment,* hata tunapokuja katika Bunge hili, tuna uwezo wa kusema kwamba, *okay,* kwa namna tunavyokwenda basi, mradi huu utakuwa umekamilika kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi jinsi tulivyo, tunashindwa kufanya *assessment* kwamba sasa huu mradi umefikia wapi? Labda ningependa tu Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hili, tujue kwamba sasa huu mradi hasa hasa unaanza lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, kuna changamoto ambazo huwa zinaelezwa kwenye hotuba mbalimbali za Waheshimiwa Mawaziri, mwaka 2016/2017 na 2017/2018, lakini naamini kwamba zile changamoto ziko ndani ya uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali ifanye jitihada na safari hii ije na majibu kwamba sasa mradi huu unaenda kwa *stage* hizi, mpaka itakapofikia muda fulani huo mradi utaanza, kwa sababu maswali yamekuwa mengi sana. Ikumbukwe tunaambiwa kwamba huu mradi ni wa kimkakati. Kwa hiyo, naamini mradi wa kimkakati ni lazima upewe kipaumbele kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi tulivyo hatuna uwezo hata wa kutoa majibu sahihi kwa wananchi wetu wanapokuwa wanatuuliza kwamba huu mradi utaanza lini? Kwa hiyo, naamini kwamba Serikali itakapokuja basi, itakuja na majibu ili kuona namna gani ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunao mradi wa barabara ya Itoni – Njombe, Ludewa – Manda. Mradi huu vilevile una *impact* katika ile miradi mikubwa ya makaa ya mawe Mchuchuma na chuma cha Liganga, lakini unaenda kwa utaratibu mno. Hii barabara imepangiwa *lots* nne; mpaka sasa hivi tupo kwenye ile *lot* ya kwanza tu. Kwa hiyo, unakuta sasa inatuchukua mwaka wa pili ule mradi toka uanze, lakini barabara hii bado haijakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa sababu hii barabara ni muhimu kwa ajili ya kufungua uchumi wa nchi, Serikali sasa itupatie na *lot* nyingine, hasa ile *lot* ya kuanzia pale Njombe kuja Lusitu ili tuweze kuona kwamba sasa ile miradi tunayoizungumzia ya Mchuchuma na Liganga inaweza ika-*take off* kirahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuimarika kwa miundombinu hiyo ya barabara itawezesha wananchi kujiandaa na ujio wa hiyo miradi. Kwa sababu *impact* ya miradi ile inatarajia kuleta watu wasiopungua 300,000 ndani ya Ludewa na Mkoa wa Njombe kwa ujumla wake. Kwa hiyo, maana yake ita-*stimulate* uchumi, mazao ya wakulima wetu yatapata tija, kwa maana ya bei na kwa maana ya mzunguko wa biashara. Kutakuwepo na usafirishaji wa aina nyingi na barabara zitakazotumika ndiyo hizi ambazo tunazizungumzia sasa hivi na pia tutaanzisha hivyo viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kuongeza thamani ya bidhaa ambazo tutakuwa tunazizalisha kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuisihi Serikali na kuiomba kwa moyo mkunjufu kabisa, ituongezee *lot* ya pili kwenye barabara ya Itoni – Njombe, Ludewa – Manda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye eneo la afya. Kwenye eneo la afya tuna upungufu mkubwa sana wa wahudumu au wafanyakazi wa afya. Kwa kweli, tatizo hili limeshakuwa kubwa na bahati mbaya zaidi ni kwamba hata ujenzi unaoendelea kwenye maeneo mbalimbali bado unahitaji sana nguvu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, sasa hivi kule kwetu Ludewa tunajenga Vituo vya Afya 17 na sasa hivi vipo kwenye viwango mbalimbali; na hizo zote ni nguvu za wananchi. Wananchi wale wana uwezo wa kujenga mpaka kufikia kuezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali sasa hebu itupie jicho kule, ikiwezekana iwasaidie hawa wananchi na wadau mbalimbali ambao wanashughulika na ujenzi wa hivyo Vituo vya Afya. Wananchi wameingiwa na hamasa kubwa kwa ajili ya utekelezaji ambao Serikali inaufanya. Kwa hiyo, naamini kwamba wakiungwa mkono ile sera au Ilani ya Chama cha Mapinduzi inayozungumzia Kituo cha Afya Kila Kata, ina uwezo wa kutekelezwa kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye upande wa elimu, bado tuna upungufu mkubwa wa Walimu katika nchi nzima. Tuna upungufu wa Walimu 90,000 nchi nzima kwa *data* ambazo tunazo sasa hivi. Kwa hiyo, Serikali ijaribu kuona uwezekano wa kupata Walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la juu ya ubora wa elimu ambayo inatolewa sasa hivi. Ukijaribu kuangalia kwa kiasi kikubwa, matokeo mabaya yanayoipata nchi sasa hivi kutokana na hii mitihani ya *NECTA,* vilevile inachangiwa kwa kiasi kikubwa na ubovu wa Walimu. Kwa hiyo, wakati mwingine tunaweza tukawalaumu wanafunzi, lakini vilevile kuna tatizo la msingi kwa Walimu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuishauri Serikali, umeshafika muda sasa kwa sababu, elimu ni

*profession* kama zilivyo *professions* nyingine za Uhasibu au Sheria, tuunde sasa chombo madhubuti, *Teachers' Profession Board,* ambacho kila Mwalimu atakapokuwa ame-*graduate,* lazima apite huko kwa ajili ya kupata utaalam zaidi na kupimwa, kufanyiwa *assessment* kabla hajaenda kuwafundisha watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini tukishafanya hivyo, tutapata *quality* ya Walimu ambao ni wazuri na *product* itakayotoka kwa wanafunzi wetu, itakuwa ni *product* nzuri. Ilishafika wakati kwamba Ualimu ilikuwa ni kimbilio la kila mmoja. Kwa hiyo, lile kimbilio la kila mmoja nadhani sasa hivi wakati wake umeshapita. Kwa hiyo, nashauri tupate chombo madhubuti kitakachosimamia *quality* ya elimu. Kwangu nashauri tuwe na *Teachers' Profession Board.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado miundombinu ya shule zetu ni chakavu. Wananchi wanajitahidi na wanaendelea vizuri na ile dhana ya kusema elimu bure imeleta sokomoko kubwa kwa wananchi wetu. Hivyo, bado naiomba Serikali na sisi Waheshimiwa Wabunge kwa umoja wetu, tujaribu kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili baadhi ya yale mambo ambayo hayapo kwenye elimu bure, basi wananchi wetu wayachukue na ile itawatengenezea ile *sense* ya *ownership.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimwambia mtu elimu bure kila kitu, anaondoka na anaacha kila kitu. Tukitengeneza ile *sense* ya *ownership,* maana yake mtu anajua kile kitu ni chake na atakuwa na uwezo wa kukisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja na ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lupembe na Mheshimiwa Dau ajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa ninaombanimshukuru Mungu aliyetupa uzima na uhai tumeweza kufika kwenye Bunge hili ambalo ametupa kibali yeye. Hatukuja kwa uwezo wetu tumekuja kwa uwezo wa Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kuwatumikia Watanzania, tunaona jitihada zake ni nzuri mno kupita kiasi maana yake bajeti hii ni ya kupongeza tu kwa sababu kazi kubwa inafanyika na tunaona jinsi Serikali inavyowatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze sana Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya katika nchi yetu. Vile vile naomba nimpongeze Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kazi kubwa anayoifanya. Tunaiona kazi yake, juzi alikuwa Geita kwenye Mwenge, tumekuona dada yetu mpendwa umefanya kazi nzuri sana. Pia niwapongeze Naibu Mawaziri kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa najua ajira ni shida sana, lakini naiomba Serikali yangu sikivu najua mpaka sasa hivi kweli kuna watendaji ambao walikuwa darasa la saba lakini watendaji hawa wametufanyia kazi kubwa sana Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata wamefanya kazi kubwa wemetujengea shule, wametujengea *dispensary* na vituo vya afya. Tunaomba watendaji hawa warudishwe kazini wasubiriwe muda ambao wataweza kustaafu ili waweze kupata haki zao. Najua Serikali yangu sikivu mmesikia mnaweza kutenda kitendo hicho ili hawa watu waweze kurudi makazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze tena kwa ndege ambayo imefika tumeona uzinduzi wake. Nasi Mkoa wetu wa Katavi tuna uwanja mkubwa sana wala hatuombi uwanja leo. Sisi tayari tuna uwanja, lakini hauna ndege. Hivyo, tunaomba sasa kwa sababu kuna ndege

nyingine imefika mpya na sisi sasa Serikali mtupangie ratiba ili na sisi wananchi wa Katavi sasa tuweze kufaidi matunda ya Serikali ya Awamu ya Tano, kwa sababu jitihada ni kubwa tunaziona kwa macho na wananchi wa Katavi wana maeneo ambayo watajivunia kwa sababu wana eneo kubwa sana la utalii, tuna Mbuga ya Katavi, sasa watalii wataweza kufika Katavi kwa urahisi kwa sababu uwanja wa ndege tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali yangu kwa *route* zitakazopangwa sasa hivi ya ndege hii mpya, basi na Katavi mtuangalie kwa jicho la huruma ili na sasa na sisi tuweze kupata watalii na Serikali yetu iweze kuingiza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua ndani ya nchi yetu kuna mikoa ambayo tuliongeza Katavi, Njombe, Geita pamoja na Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Mikoa mpaka leo hawajapata makazi, hawajengewa nyumba za kuishi pamoja na Ofisi zao. Kwa mfano, ndani ya Mkoa wetu wa Katavi Mkuu wa Mkoa mpaka leo anatumia jengo la Halmashauri ya Manispaa. Naomba basi sasa hivi tupange mikakati mizuri tuweze kuwajengea ofisi kwa sababu Mkuu wa Mkoa anahitajika apate ofisi yake ili aweze kufanya kazi vizuri. Vilevile akipata makazi atakaa vizuri sana na akafanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tuangalie Mkoa wa Katavi kwa sababu hana nyumba wala hana ofisi na siyo vizuri hawa watu kuhangaika hangaika, wanatakiwa wapate sehemu ya kukaa mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mawasiliano, naomba niipongeze sana Serikali kwa jitihada ya kuweka mawasiliano katika maeneo mengi. Mkoa wa Katavi bado kuna maeneo mawasiliano hayajafika kabisa na mazingira yetu Mkoa wa Katavi ni magumu. Ukiangalia kama Kata ya Ilunde. Ilunde jiografia yake ni ngumu sana, vilevile Ilunde kuna biashara nyingi ambazo zinafanyika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yangu iangalie basi Kata ya Ilunde iipeleke mawasiliano, wakipata Kata ya Ilunde na kuna Kata jirani inaitwa Kata ya Ilela, Kata ya Ilela nayo watapata mawasiliano kwa urahisi. Naomba sana maeneo haya ni maeneo ya biashara wanalima karanga, wanavuna asali, kuna vitu vingi vinavyofanyika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengine ya Utende, kuna maeneo mengine Wilaya ya Tanganyika, maeneo ya Sibwesa, kuna biashara, wanalima mpunga na wanafanya shughuli nyingi za kijamii ambazo zinaingiza mapato ndani ya Serikali yetu. Naomba katika maeneo haya mtandao uweze kufika, kwa sababu mtandao sasa hivi ni maisha, kwa sababu mtandao ukipiga simu biashara kila kitu kinakuja kwa wepesi zaidi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika maeneo ya Ilela pamoja na Ilunde wanatamani sana na wenyewe wapate *TBC Radio*, hakuna usikivu wa radio yetu ya Serikali. Wanatamani sana waweze kusikia matangazo ya *TBC*. Naomba sana upande wa radio basi tupate mawasiliano hayo ili nasi tusikie matangazo ya Kitaifa, Kimataifa pamoja na Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niipongeze Mifuko ya jamii *PPF, LAPF* pamoja na *NSSF*. Wamekuwa miongoni mwa jamii kwa asilimia kubwa sana. Wanasaidia sana maendeleo ndani ya jamii zetu, vilevile kusaidia jinsi gani wananchi wanavyofanya kazi zao na wenyewe wanawasaidia kupitia maombi ambayo yanafika katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kabisa ni jinsi gani kupitia elimu bure wananchi wengi wamehamasika kupeleka watoto mashuleni. Sasa hivi ndani ya maeneo yetu ndani ya vijiji vyetu na vitongoji vyetu wananchi wengi wamehamasika kujenga majengo, wamehamasika kujenga vitu vingi ambavyo Serikali inaenda kuwahamasisha, unakuta maboma yale yanaishia kwenye lenta.

Mheshimiwa Mwenyekiti,aiomba sana Serikali yetu kupitia Halmashauri zetu yale maboma wananchi walikoyafikisha basi waweze kumaliza kwa sababu watoto wetu wengi sana wanasoma kwenye miti wengine, hatuna vyoo vya kutosha, najua kwa sababu wanafunzi wamekuwa wengi ndani ya madarasa na maeneo yetu, vyoo tulivyovijenga kupitia wananchi vimekuwa havitoshi, basi naomba Serikali yangu sikivu, tuweke mikakati maalum, kwa sababu tumeona jinsi gani sasa hivi Serikali yetu ilivyokumbuka zile shule za Sekondari za zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Elimu. Waziri wa Elimu amesimamia vizuri sana, shule zile kongwe zote zimeboreshwa zimekuwa nzuri sana kusema kweli, lazima tupongeze kwa hili, kwa sababu tumekwenda kwenye shule kongwe tumeona jinsi gani matengenezo yalivyotengezwa, basi tunaomba Serikali kupitia shule za misingi sasa, kwa sababu shule nyingi za misingi zimeharibika mazingira yake siyo rafiki kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri mtoto akikaa kwenye mazingira rafiki atasoma vizuri. Hivyo, naiomba Serikali yangu sasa ichukue jukumu hili, kupitia TAMISEMI tuanze kuboresha shule zetu za msingi pamoja na mazingira yao ya kwenda maeneo nyeti ili watoto wale waweze kusoma vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme, ndani ya Mkoa wetu wa Katavi *REA* III haijafanyika kabisa kwa sababu Mkandarasi sijui alipelekwa Mahakamani, hakuna kitu chochote kinaweza kufanyika. Sasa wananchi wa Mkoa wa Katavi wanahitaji umeme, maeneo mengi tukipita kwenye Kata zetu hakuna umeme na kuna sehemu zingine ni za biashara, watu wanajishughulisha na mambo mengi, sasa unakuta umeme hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu sikivu, sasa hivi katika bajeti hii najua bajeti hiyo imeshapita ya wakati ule *REA* III, lakini bado tuna nafasi ya kuweka tena mikakati mipya ili Mkoa wa Katavi katika yale maeneo yote

*REA* III haijapita, tunaomba iweze kufanyika kwa sababu wananchi wa Mkoa wa Katavi kupitia maeneo mengi wanahitaji nao waweze kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jeshi la Polisi. Najua Jeshi la Polisi tunalipenda sana wanatulinda usiku na mchana, basi nao tuwawekee vizuri mazingira yao. Unakuta kwenye kituo cha Kata ukienda kuona nyumba ya Askari wetu ni nyumba ya udongo inasikitisha. Naomba basi tujitahidi kuwawekea mazingira mazuri, wanafanya kazi vizuri tuwawekee mazingira mazuri ili waweze kufanya kazi vizuri na kuendeleza amani ndani ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Malizia, unga mkono hoja.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga Mkono hoja. Nashukuru kwa barabara inayoanzia Tabora – Mpanda, nashukuru sana na Wakandarasi wako *site,* hongera sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mheshimiwa Azza Hillal na Mheshimiwa Jitu Soni, wajiandae.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba hii nzuri leo asubuhi, nielekeze pia na pongezi zangu kwa Mheshimiwa Rais kwa namna anavyokitendea haki Kiti chake nasi Watanzania tunampa pongezi nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu Septemba, 2016, alifanya ziara katika Kisiwa cha Mafia, ziara yake kwa kweli imetuletea faraja kubwa sana na changamoto nyingi sana ambazo zilikuwa zinatukabili katika kisiwa chetu aliweza kuzifanyia kazi na kuzitatua. Hata hivyo, alipoondoka aliacha viporo kama vitatu, vinne hivi na tukakubaliana kwamba atatuita Ikulu twende tukaongee kuyamaliza haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nianze kwa kumkumbushia Mheshimiwa Waziri Mkuu viporo hivyo. Suala la kwanza leo asubuhi lilizungumzwa hapa. Suala la tatizo la *X-Ray* la Kisiwa cha Mafia unaingia sasa mwaka wa sita Mafia hakuna *X-Ray* na unaingia sasa mwaka wa pili toka Mbunge wa Mafia anayeongea sasa hivi alete *X-Ray* yake mwenyewe mpya ambayo haijafungwa mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri asubuhi hapa ameliambia Bunge lako kwamba Kampuni ya *Philips* italeta mashine za *X-Ray* kwa ajili ya hospitali za mikoa mwezi Juni na wao ndiyo wanawajibika katika kuzi-*maintain* kwa maana ya kufanyia matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingetaka kwenda mbali sana, namwomba sana Mheshimiwa Waziri badala ya kusubiri hizo *X-Ray* za ku-*import* kutoka nje awaambie *Philips* kwanza wakatengeneze *X-Ray* ya Mafia mwaka wa sita huu haijatengenezwa. Hili halihitaji kusubiri Juni kama wao wapo hapa basi waende wakaitengeneze *X-Ray* ya Mafia, kwa sababu imekuwa haifanyi kazi kwa miaka sita na mimi leo ndiyo mara yangu ya mwisho kulisema hili jambo ndani ya Bunge hili, nitakachokifanya baada ya hapa nakijua mimi mwenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu tulimfikishia kilio chetu ni tatizo la mgogoro baina ya hifadhi ya bahari ya Mafia na Halmashauri ya Mafia. Ningeomba sana ndugu yangu Mheshimiwa Ulega nilimwona Mheshimiwa Waziri Mpina ametoka, lakini Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Abdallah Ulega namwona naomba anisikilize vizuri kwa sababu alikuja Mafia ameliona hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mafia ni Halmashauri ndogo sana na maskini, ina vyanzo vya mapato vichache sana, kuna Taasisi inaitwa Hifadhi ya Bahari. Ni taasisi ambayo *staffing* yake haizidi hata watu 15 lakini wanakusanya mapato kwa maana ya maduhuli kutokana na watalii wanaokuja kutembelea Kisiwa cha Mafia zaidi ya

milioni 700 kwa mwaka na Halmashauri ya Mafia tunapewa asilimia 10. Halmashauri ya Mafia yenyewe kwenye vyanzo vyake vingine vyote inakusanya shilingi milioni 600. Utaona pana tatizo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi ndogo tu ambayo *staffing* yake haizidi hata watu 15 inakusanya shilingi milioni 700 lakini Serikali kwa maana ya Halmashauri ya Wilaya ya Mafia ambayo ndiyo inawajibika na shule, inawajibika na Zahanati, inawajibika na Hospitali na wakati ule barabara na mambo mengine maji na vitu kama hivyo tunakusanya shilingi milioni 600. Eneo la utawala la Mafia limepunguzwa na Taasisi ya Hifadhi ya Bahari ya Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachokitaka na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja tuliliongea hili na akaahidi kwamba tutakutana Ikulu pale tuliongee tulimalize pamoja na Mawaziri wanaohusika. Ningeomba kwa namna ya kipekee sana hatuombi jambo kubwa, tunachoomba kwamba ule mgao basi angalau uwe wenye kufanana. Sisi ambao tuna mambo makubwa ya kuendesha tupate mgao mkubwa tupate asilimia 60 na hii hifadhi ya bahari ipate asilimia 40, kwa sababu kuna hatari Halmashauri ya Mafia ikapelekwa kule kwa Mheshimiwa Ungando, Kibiti kwa sababu hatuwezi kufikia malengo ya kukusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa zote zinakwenda kwenye Taasisi ya Hifadhi ya Bahari ambao hawawajibiki na jambo lingine lolote la maendeleo ya Mafia zaidi ya uhifadhi na Halmashauri nayo pia inafanya kazi ya uhifadhi. Ningeomba kwa namna ya kipekee sana kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu suala hili la kikao kile, tukutane ili tuliweke sawa na suala la kanuni wala siyo suala la sheria ni Waziri mwenye dhamana ya uvuvi na mifugo abadilishe kanuni tuanze kupata sasa Halmashauri asilimia 60 na Hifadhi ya Bahari asilimia 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine, tulilalamika kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu Hifadhi ya Bahari wanaacha kazi yao msingi ya uhifadhi na wameiingia katika

masuala ya kuuza na kumiliki maeneo na wameuza visiwa. Kisiwa cha Shungimbili kimeuzwa na sasa pale kuna hoteli ya nyota saba kwa usiku mmoja ni dola elfu kumi (10,000). Kwa taarifa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Halmashauri ya Mafia haipati hata *single cent* kwenye mapato haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo mambo ambayo tungependa tukae na Mheshimiwa Waziri Mkuu tuyaongee, haiwezekani wao kazi yao kuhifadhi badala ya kuhifadhi wanauza maeneo na wanapouza maeneo hata huo mrabaha sijui kitu gani ambacho pengine Halmashauri tungestahili kupata hatupati hata kitu kimoja. Huu sasa unafika mwaka wa pili toka uwekezaji ule ufanywe pale na Halmashauri ya Mafia hatujapata hata senti tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitoa kilio chetu cha usafiri Mafia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na naamini Waziri Mbarawa sijamwona lakini nimemuona Mheshimiwa Injinia Nditiye hapa. Nilikwenda kwake, tuna dhiki ya usafiri katika kisiwa cha Mafia, maeneo mengine tunaona watu wanajengewa vivuko na Serikali, tumejitahidi sana kuishawishi *private sector* watuletee boti zao binafsi hawajavutika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali kwa namna ya kipekee kabisa ichukue nafasi yake watutengenezee chombo, kule tuna *sege* tuko kama kwenye *cage* hatuwezi kutoka lazima tuvuke bahari. Hata hivyo, wanawajengea vivuko watu wengine sitaki kuwataja hapa wanajenga vivuko maeneo mengine ambayo yanapitika kwa barabara, sisi hatuna namna ya kutoka au kuingia Mafia lazima tupite kwenye kivuko, kivuko ambacho kinagharimu bilioni mbili mpaka tatu, hawataki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mbarawa ameniahidi kwamba kwenye bajeti hii ataingiza hilo. Sasa nataka atakapokuja kujibu hotuba hii aniambie na Mheshimiwa Nditiye nimemwona watuambie watajenga kivuko mara hii au hawajengi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha atusaidie katika hilo kwa sababu imeshafika wakati sasa ni wakati

wowote kule ni kama *timing bomb,* yale magogo tunayosafiria yale ambayo siyo salama wakati wowote yatazama na watu watapoteza maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifikia hapo tunasema Mheshimiwa Nditiye, Mheshimiwa Mbarawa, Waziri wa Fedha mtakuwa *masuulu, masuulu* ni neno la Kiarabu, maana yake mtakuwa *responsible* na hiyo dhambi, kwa sababu wanawapandisha watu katika magogo, pesa wanatenga katika maeneo ambayo hayana ulazima wa kupata vivuko vya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lingine pale, Mafia ni eneo dogo sana, kuna viboko wametoka kwa Mheshimiwa Ungando wamekuja Mafia pale, wameshafikia 40 sasa hivi. Kilio hiki tumekisema toka alipokuwa Waziri Mheshimiwa Maghembe, wanakula mipunga ya watu, wanakula mazao ya watu na kilio tumekileta Wizarani.*(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi wiki mbili zilizopita, Mwenyekiti wangu wa Kata wa CCM, Kata ya Ndagoni ameuawa na kiboko. Tumetoa taarifa mpaka leo wataalam wamekwenda pale badala ya kuwafanya utaratibu wa kuwavuna au kuwafanyia *relocation* wale kwa sababu Mafia eneo ni dogo hawawezi kukaa. Wapigeni sindano walale muwahamishe muwapeleke huko Rufiji, ndiko kwenye *origin* yao, pale sisi nafasi yetu ni ndogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa wamekuja wataalam pale wameishia kupiga picha, je, nami namwuliza Mheshimiwa Hasunga anasubiri mpaka watu wangapi wafe na viboko ndiyo watakuja kuwaondoa wale viboko pale Mafia. Hili nalo pia na yeye pia utakuwa *masuulu*. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme na nashukuru nyuma yangu yupo Profesa hapa. Suala la umeme vijijini, Profesa alituahidi lakini leo hayupo, naamini Serikali ni

moja. Walituahidi kwamba visiwa vidogodogo vyote vitapata umeme unaotumia nguvu ya jua kwa maana ya *solar*. Kisiwa cha Jibondo, Kisiwa cha Bwejuu, Kisiwa cha Juani na Kisiwa cha Chole. Mheshimiwa Dkt. Kalemani ahadi hii naye alinihakikishia kwamba tutapata umeme mpaka sasa sijaona dalili zozote, naye pia atakuwa *masuulu*. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la barabara, Kisiwa cha Mafia siyo kidogo hivyo, kuna barabara ambayo ina urefu zaidi ya kilometa sitini pale.....

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dau. Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, jiandae Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na hatimae nimesimama humu ndani kuweza kuchangia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan; Mheshimiwa Waziri Mkuu, Majaliwa Kassim Majaliwa; na Baraza lote la Mawaziri na Watendaji wote wa Serikali kwa kazi kubwa wanayoifanya. Hongereni sana, kazi inaonekana, chapeni kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba nianze na kituo cha Buhangija, Kituo cha Watoto wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali mwaka huu wa fedha wametupa shilingi milioni mia mbili themanini na sita na laki sita ambazo zimeweza kujenga madarasa manne, mabweni mawili na matundu 18 ya vyoo. Tunaishukuru sana Serikali kwa kukiona kituo hiki, lakini kituo hiki bado kina upungufu mwingine ambao unahitaji kukamilishwa na hata mwaka jana nilivyokuwa nachangia nilisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha watoto wenye ulemavu Buhangija kina upungufu wa watumishi. Kina upungufu wa Walimu wa watoto wasiosikia. Kituo hiki mahitaji yake ni Walimu nane lakini kina Walimu wawili tu. Mheshimiwa Jenista hata mwaka jana nilisema naomba akitazame kituo hiki. Walimu wawili tu hawatoshelezi kuwafundisha watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo hiki kina walezi wawili tu wakati mahitaji ni walezi nane. Kituo hiki cha Buhangija hakina Mpishi hata mmoja, wapishi wanaopika pale ni kwa kujitolea na wanalipwa kama vibarua. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kulifanyia kazi pamoja na kuboresha mazingira hayo lakini watumishi hawa waweze kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie sekta ya afya; niishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa ambayo imeendelea kufanya katika sekta ya afya. Katika Mkoa wangu wa Shinyanga imeweza kuwezesha ujenzi na uboreshaji wa vituo sita vya afya. Kituo cha Afya cha Iyenze kilichopo Halmashauri ya Mji Kahama, Kituo cha Afya cha Chela kilichopo Halmashauri ya Msalala, Kituo cha Afya cha Ukune kilichopo Halmashauri ya Ushetu na Kituo cha Afya Tinde na Samuye Halmashauri ya Shinyanga Vijijini pamoja na Kituo cha Afya cha Songwa kilichopo Halmashauri ya Kishapu. Tunaishukuru Serikali na tunaipongeza kwa kazi kubwa wana kazi inaonekana, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uboreshaji wa vituo hivi, kuna matatizo mengine ambayo yanastahili wagonjwa hawa kupewa rufaa. Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu haina Hospitali ya Wilaya. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini huu ni mwaka wa nane sasa naiongelea Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini. Tulishaanza ujenzi lakini ujenzi huu umekuwa ukisuasua kwa sababu hatupewi fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali yangu sikivu, nimemsikia asubuhi Mheshimiwa Naibu Waziri akisema kwa

mwaka huu wa fedha kuna hospitali za Wilaya 67 ambazo zitakwenda kujengwa. Namwomba na nina hakika kwamba Hospitali ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini na Hospitali ya Wilaya ya Ushetu zitakuwepo katika orodha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijatendea haki Mkoa wangu wa Shinyanga nisipoongelea Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga. Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga unakwenda taratibu na hii ni kwa sababu fedha ambayo inatengwa imekuwa ikitengwa fedha kidogo na hivyo kufanya ujenzi huu usikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga kuna upungufu mkubwa wa watumishi. Mahitaji ya Hospitali ya Mkoa wa shinyanga watumishi ni 474, lakini waliopo ni 285 tu. Kwa takwimu zilizopo watumishi 30 ndani ya miaka miwili hii wanakwenda kustaafu, hivyo niiombe Serikali kuweza kuongeza watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kusema na mwaka jana kwenye bajeti nilisema Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga ina uhitaji wa Madaktari Bingwa 21, lakini mpaka hivi ninavyoongea kuna Madaktari Bingwa wanne tu. Daktari Bingwa wa Magonjwa ya akinamama mmoja, Daktari wa Watoto mmoja, Daktari wa Upasuaji mmoja na hivyo kufanya tatizo la Madaktari Bingwa katika hospitali hii linakuwa ni sugu, niombe hospitali iweze kuletewa Madaktari hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa elimu. Nitumie fursa hii kuishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, Serikali sikivu ya Awamu ya Tano imeweza kufanya mambo makubwa katika Mkoa wa Shinyanga. Nianze na Halmashauri ya Wilaya ya Msalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ilipata milioni mia moja sabini na kwenda kujenga hosteli ya Sekondari ya Burige na Sekondari ya Ntobo Sekondari, tunaishukuru sana Serikali. Halmashauri ya Ushetu imepeleka fedha katika Shule ya Msingi Nonwe milioni mia

moja tisini na mbili na Shule ya Msingi Bugomba milioni mia moja tisini na mbili na hivyo kufanya mazingira ya shule hizi kuwa mazuri na kuwavutia watoto na uandikishaji kuendelea kuwa mkubwa katika shule zetu hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niingie katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Halmashauri ambayo Mimi ni Diwani na ni Halmashauri ambayo nahudhuria vikao vyake vya Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Shinyanga Vijijini ina Shule ya Sekondari ya Zunzuri, shule hii ni kongwe, shule hii ina kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne lakini Halmashauri tulikaa kwenye Baraza la Madiwani tukakubaliana shule hii tuweke kidato cha tano na cha sita. Baadhi ya miundombinu tumekwishaiweka katika shule hii, vimebaki vitu vichache ambavyo havijakamilika bwalo la chakula, bweni moja, ukarabati wa maabara tatu pamoja vifaa vyake na vitanda 48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa naomba niseme kwenye shule hii ya sekondari. Hazina walikuwa wanapeleka fedha katika shule moja inaitwa *Tinde Day* wakifikiri kwamba ile shule ni ya *Boarding*. Kwa hiyo fedha zile zilikuwa zinakwenda pale kimakosa, Halmashauri na Mkurugenzi wakachukua jukumu la kuiandikia barua Hazina kuomba kubadilisha fedha zile kuzipeleka kwenye Shule ya Sekondari ya Zunzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI walijibu barua ile wakakubali kuruhusu kubadilisha fedha hiyo na baada ya TAMISEMI kutoa barua kuruhusu kubadilisha fedha hiyo Halmashauri ilianza kutumia fedha hizo. Kwa masikitiko makubwa Hazina wameandika barua kumzuia Mkurugenzi asiendelee kutumia fedha hizo kwa matumizi ya Shule ya Sekondari Zunzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa Hazina ni nani na TAMISEMI ni nani! TAMISEMI wameruhusu na fedha ile ikaanza kutumika ili kuboresha maeneo haya na kidato cha

tano kiweze kuanza kufanya kazi, lakini leo hii Hazina wameandika barua kumzuia Mkurugenzi na wanamtaka Mkurugenzi arudishe fedha ile. Naomba majibu ya Serikali, Serikali ni moja, Halmashauri ni moja ni kwa nini wanazuia matumizi ya fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusemea Shule ya Sekondari ya Zunzuri, naomba niisemee Shule ya Sekondari ya Wasichana iliyopo Tinde. Shule ya Wasichana ya Tinde ni ya kidato cha tano na sita. Shule hii ina miundombinu mizuri, nyumba za Walimu za kutosha, madarasa ya kutosha, maabara, lakini shule hii haina bwalo wala ukumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha unapokuwa katika mazingira yale kama mvua inanyesha wanafunzi wanakula nje wakati mwingine wananyeshewa na mvua. Mheshimiwa Waziri wa Elimu nilimwomba na narudia tena kumwomba leo hii humu, chonde chonde aitizame Shule ya Wasichana ya Tinde. Yeye ni mama nina hakika anajua akimwelimisha mwanamke, akimwelimisha binti atafika na yeye hapo alipofika yeye, naomba aitizame Shule ya Wasichana ya Tinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado niko katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Sasa naomba niongelee Shule ya Msingi Masunula iliyopo katika Kata ya Usule. Shule ya Masunula ipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Shule hii imekuwa ikifanya vizuri kwa miaka mitatu mfululizo, imekua ikiongoza ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa shule hii haina nyumba hata moja ya Mwalimu. Hivi tunawatazamaje Walimu hawa ambao kwa miaka mitatu mfululizo wameweza kutufundishia watoto wetu na shule ile kuweza kuongoza kwa ufaulu. Niiombe sana Serikali tunaomba waitizame shule ya Msingi ya Masunula waweze kutujengea nyumba za watumishi kwa sababu shule hii haina nyumba hata moja ya mtumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya

Wilaya ya Shinyanga fedha za maendeleo, kwa masikitiko makubwa hili naomba niliseme. Mwaka 2016/2017 tuliidhinishiwa fedha za maendeleo bilioni 1.6, lakini fedha ambayo Halmashauri ilipokea ni milioni 420 tu. Fedha zingine zote hazikuweza kufika. Mwaka wa fedha 2017/2018 tuliidhinishiwa bilioni 1.7; mpaka hivi ninavyoongea Halmashauri haijapokea kiasi chochote cha fedha ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naomba sana Serikali ilitazame kwa macho mawili, ni kwa nini halmashauri yetu tunakuwa tunaidhinishiwa pesa, lakini fedha hizi hazifiki. Naomba nipate majibu ya kutosha ni kwa nini Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga mpaka sasa hivi hatujapata fedha ya Maendeleo hata shilingi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisemee suala la Watendaji. Suala la Watendaji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jitu Soni, halafu jiandae Mheshimiwa Allan Kiula.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu pia naomba niipongeze Serikali hasa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri wanayofanya kwa kufanya uratibu mbalimbali na kuhakikisha kwamba shughuli zote za Serikali zinaenda. Kuna maeneo mbalimbali ambapo ningependa kushauri na naamini kabisa ushauri utazingatiwa kama ilivyokuwa siku zote unazingatiwa ili shughuli ya maendeleo iende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilikuwa naomba kwanza suala hili la *budget process* ya kwetu tuangalie

namna Serikali iangalie nasi tuendelee kushauri tubadilishe mfumo wetu wa *budget circle* kwa sababu mengi tunayozungumza leo tayari *ceiling* zimeshawekwa na maeneo mengi watu wameshapanga bajeti zao, kufumua na kuiandaa upya inakuwa ni ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa ni vizuri sisi tungekuwa tunajadili mambo mengi, nini kipande nini kishuke, mabadiliko gani yaje yawe yanafanyika kuanzia mwezi wa Nane mpaka mwezi wa kumi na moja ili watu wanapoandaa bajeti zao basi shughuli hizi zote ziweze kuendana na *budget circle* na kama kuna mabadiliko tuweze kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuwe na mfumo, kwanza tujue kabisa mapato yetu ni shilingi ngapi ili kutokana na yale makusanyo ndiyo tupange matumizi yake. Hapo tukiweza kufanya ninaamini kabisa hili suala la kusema fedha hazijatosha, hazijaenda kule kutokana na hii *cash budget* itakuwa tatizo hilo tumeondokana nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naomba niipongeze kwanza Sheria ya Manunuzi tumeifanyia mabadiliko mara kadhaa na inaenda vizuri, tumeona mafanikio makubwa katika sekta kwa kutumia *force account* katika sekta ya elimu, afya. Hata hivyo, bado hiyo hiyo Sheria ya Manunuzi inatumika vibaya na fedha zote tunazokusanya bado matumizi ni mabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tukienda kwenye manunuzi ambapo tunaendelea kutoa *tender* na wale wanaopokea zile *tender* bado bei zao ziko juu. Kwa mfano, ukienda *TEMESA, TEMESA* ni chaka moja ambapo mahali manunuzi yale bado ni tatizo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha nyingi za Serikali zinapotea pale *TEMESA, TBA* na taasisi nyingi

za Serikali ambazo zinatoa huduma, unakuta gharama zao ni kubwa kuliko ya *private sector* na pesa zetu nyingi zinapotea huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kwenye viwanda. Naomba kwamba tuna sera nzuri tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda lakini tusipoangalia kwa undani tukafanya uchambuzi wa kina kwamba gharama za uzalishaji ambazo zinakuwa ni kubwa kuliko bei ya bidhaa ambayo inatoka nje, bado hatutaweza kuwa nchi ya viwanda na utakuta bado tutakuwa tunaagiza vitu kutoka nje. Sehemu kubwa inatokana na utitiri wa masuala ya tozo, ushuru, ada na kodi. Hayo yakifanyiwa kazi nina uhakika kwamba viwanda vyetu vya ndani vinaweza vikafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Serikali haswa kwa upande wa miundombinu; huko Babati Madaraja yameendelea kujengwa. Daraja la Magara, daraja la Mtogiheri na madaraja mengine yamejengwa vijijini ambayo hata barabara za *trunk roads* hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la barabara ningeomba Serikali iangalie upya suala la mgao wa fedha zile ambazo zinaenda *TANROAD* na ambazo zinaenda *TARURA*. Ningeshauri kwamba tuwe *fifty fifty* kwa sababu *TARURA* ndiyo ina kilometa nyingi za barabara na hiyo ingefanya barabara za vijijini pia ifanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kwenye suala la elimu hasa elimu stadi. Katika Bunge lililopita tuliweza kupitisha hapa sheria ambayo ilichukua *skills development levy* ile asilimia nne tukagawa mbili kwa mbili. Mbili zikaenda kwenye Bodi ya Mikopo kwa dharura kwa muda wa mwaka mmoja, lakini naona kwamba sasa bado imeendelea kubaki huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba ile pesa yote asilimia nne irudi iende sasa kwenye ufundi stadi, *VETA* kwa sababu *VETA* yetu pia inataka mabadiliko makubwa. Leo tukitaka uchumi wa viwanda, viwanda vyote siku hizi ni

mambo ya *ICT* na tusipobadilika na mfumo huo kwa kufundisha vijana wetu masuala ya *ICT* bado wale watakaokuwa wanapata mafunzo pale itakuwa hawajafikia hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la maji. Naomba Serikali ijitahidi kuhakikisha kwamba Wakala wa Maji Vijijini ianzishwe mapema ili miradi ya maji iweze kwenda vizuri. Pia pesa ambayo inatengwa kutokana na ile shilingi hamsini tuliyoweka, basi yote ile iende kwa ajili ya maji vijijini, lakini tunaomba kwenye bajeti hii basi Serikali ifikirie kuongeza shilingi hamsini nyingine iwe mia ili Mfuko wa Maji uweze kutuna wananchi vijijini waweze kupata maji. Niihakikishie Serikali wananchi wote hawatajali kupanda kwa gharama zingine ili wananchi wenzao wa vijijini waendelee kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine la upande wa Kilimo. Naiomba Serikali sasa ijitahidi kuhakikisha kwamba Benki ya Kilimo iwezeshwe ule mtaji ambao waliahidi kwamba itawezeshwa ili wakulima waweze kukopa kule na suala la utafiti pia tuwe na fedha za kutosha kuhakikisha kwamba tafiti mbalimbali zinaendelea kufanyika, kile chombo ambacho tumeanzisha *Tanzania Agricultural Research Institute* iweze kuanza kazi yake mara moja na fedha zake ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni muhimu sana leo hii fedha za *OC* zinaenda vizuri ambazo zinajumuisha mishahara na gharama zingine za kawaida, lakini fedha za maendeleo zinaenda kutokana na pesa inavyopatikana. Ningeomba kwamba kama kuna uwezekano tuangalie kama tunaweza kupanga kwa uwiano kwamba fedha asilimia fulani zikienda za *OC* basi na za maendeleo ziwe zinaenda zinafanana. Nasema hivi kwa sababu kama *OC* imeenda asilimia 100 na za maendeleo imeenda asilimia 10 wanaenda kusimamia nini kwa sababu ile fedha tunaendelea kupoteza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo zote ziendane na

kama tunaona kwamba hatuna fedha za kutosha kwa maendeleo kwa miradi yote, basi tuweke vipaumbele mwaka huu itakuwa Wizara kadhaa tunawekeza fedha huko zote halafu *OC* kwenye hizo Wizara ambazo hazipati fedha za maendeleo tupunguze kabisa zote ziende kwenye suala la maendeleo ili *value for money* iweze kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningeomba Serikali huko ndani ya Serikali suala la *PPP* bado halijaeleweka vizuri. Ningeomba kwanza papatikane elimu ya kutosha na semina mbalimbali kwa Wabunge, lakini pia kwa Watumishi wote ili tukikaa pamoja vizuri naamini kwamba suala hili la *PPP* inaweza kutusaidia na tukapata mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni muhimu ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na mifumo mbalimbali kwa mfano kwenye madini. Kwenye Sekta ya Madini ningependekeza niwapongeze Serikali kwa kazi nzuri iliyofanyika, lakini pia kile kituo cha Arusha ambacho kinatoa mafunzo kwa kufundisha watu wa kuchakata madini kutengeneza *jewellery* na vito, basi fedha za kutosha ziwekezwe ili tuweze kuzalisha wataalam wa humu ndani nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho, ni kwenye masuala ya maafa. Ningeomba Serikali pia tujipange, maeneo mengi haya maafa yangeweze tukaepukana nayo kwa kupanga. Tukiwa na *master plan* ambayo hasa Miji yetu na katika maeneo ambayo yanakuwa sasa miji midogo tuwe na *master plan* ili tuweze kuepuka masuala mbalimbali ya maafa. Pia katika maeneo yote ambapo yanatokea mafuriko tuhakikishe kwamba Serikali tujipange na tujue chanzo cha mafuriko ni nini tuweze kuzuia yale mafuriko ili tusitumie fedha nyingi kwenye masuala ya maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeomba Taasisi zote za Serikali kwa mfano *Fire*, watu wa *Traffic* wakusanye mapato yao yote kwa njia ya kielektroniki na hiyo itaziba

mianya hii ya pesa ambazo zinaendelea kupotea na tukipata fedha nyingi Mfuko wa Serikali ukiwa umetuna vizuri nina uhakika kabisa kwamba fedha za maendeleo pia zitakuwa zinatoka na tunaweza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la muhimu, tuendelee kuangalia suala hilo la Sheria ya Manunuzi na pia suala hilo la viwanda namna ya kukaa pamoja na kuhakikisha kwamba sera yetu inakaa vizuri, lakini pia gharama zote za uzalishaji wote tuzielewe. Tukiwa tunaelewa kwa pamoja naamini kabisa kwamba bidhaa zote ambazo tunaagiza kutoka nje, hasa za kilimo na bidhaa zingine za mifugo nyama, samaki hizo zote ambazo tunaweza kuzalisha nchini tungewekeza basi huko tuzalishe bidhaa zote, sisi ndio tuwe tunapaleka nje na *exports* ziwe kubwa kuliko *imports* hasa kwa vitu ambavyo vinawezekana ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake ya Mawaziri, Naibu Mawaziri, lakini pia Watendaji wote huko Serikalini wanaweza kujipanga na haya yote ambayo tunashauri wakafanikisha kwamba tuweze kupanga na mambo yakaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo naomba ni suala zima la migogoro ya ardhi, Tume mbalimbali zimeundwa, naomba haswa kwa mfano kule Babati, migogoro ya ardhi kwa hifadhi zile mbili za Tarangire na Manyara, Vijiji vya Hayamango, Gedamar, Gedejabong lakini pia Vilimavitatu migogoro ile na yale mashamba ya Kiru tufike mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya migogoro ile ina miaka zaidi ya 25, hivyo tumalize ili watu waishi kwa amani, wafanye kazi ya maendeleo kwa sababu tayari nishati imefika katika maeneo mengi, barabara zimeboreshwa na wapo tayari kufanya kazi, kitu kinachozuia ni hiyo migogoro michache ambapo tukiweza kuwekeza suala zima ya maendeleo huko tutakuwa tunaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala zima la uratibu pia katika ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala zima la kusaidia watu wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum kwamba Mfuko ule wa UKIMWI utafutiwe chanzo cha kudumu cha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Allan Kiula, jiandae Mheshimiwa Ntimizi.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba hii muhimu jioni ya leo. Kwanza kabisa niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa juhudi inazochukua ili kuweza kukuza uchumi, tumeona kwamba uchumi unakua kwa asilimia 6.8 na Tanzania ni moja miongoni mwa nchi tano za Afrika ambazo uchumi wake unakua vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye taarifa tumeelezwa zaidi ya viwanda 3,000 vimeweza kuanzishwa. Kwa hiyo hiyo ni hatua nzuri na ni dhamira ambayo Serikali ilivyoingia madarakani ilionesha kwamba jambo hilo litaweza kufanyika. Juzi tumeshuhudia pia uzinduzi wa *lot two* ya ujenzi wa *standard gauge*, hiyo ni hatua kubwa ya kuweza kuimarisha uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia Waziri Mkuu akizunguka maeneo mbalimbali kuhimiza suala la kilimo, kilimo cha pamba kinakwenda vizuri, korosho zimepanda bei na mazao mengine ambayo yameainishwa hapa mazao ya kimkakati. Sasa pamoja na pongezi hizo yapo mambo machache ambayo Wabunge inabidi tushauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianzia na kilimo, ule wigo wa mazao ya kimkakati uko umuhimu wigo huo

ukapanuliwa. Kwa mfano, juzi Rais alizindua kiwanda cha mafuta cha alizeti Singida. Sasa zao la alizeti na lenyewe linatakiwa lipewe mkakati Dodoma, Singida na Shinyanga tuweze kulima zao la alizeti na tukilima zao la alizeti kwa wingi tunaweza kusaidia kuokoa fedha za kigeni ambazo zinatumika kuagiza mafuta nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu Bungeni huwa tunalumbana sana suala la kusema mafuta nje yasiagizwe, lakini mbegu zilizopo ndani ya nchi zinakuwa hazitoshi, sasa ni lazima uwekwe mkakati ikiwepo, kuwepo na ruzuku ya mbegu na mbolea ili zao hilo liweze kuzalishwa kwa wingi na tuweze kuvuna mazao ambayo yataleta tija kwenye viwanda vyetu, kwa sababu viwanda hivi vinategemea sana sekta ya kilimo. Kwa hiyo, sekta ya kilimo ikiimarishwa tutaweza kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nimeambiwa kwamba kuna malighafi ngano inaagizwa nje ya nchi na baadhi ya Wawekezaji ndani ya nchi humu, lakini zamani *NAFCO* walikuwa wanalima sana ngano na ilikuwa ni ya . Kwa hiyo, ni lazima mazao kama ngano na yenyewe yaweze kuangaliwa na tuweze kuyawekea mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo napenda kuzungumza ni suala la elimu, nitazungumza kidogo sana kwa sababu kila siku tumekuwa tunazungumza na Wabunge wamekuwa wakizungumza suala la ubora wa elimu. Nimejaribu kufanya utafiti tu hasa katika Wilaya mpya hizi. Katika Wilaya mpya unakuta kwanza miundombinu yenyewe haitoshi, unakuta Wakaguzi na Waratibu Kata wapo, lakini Waratibu na Wakaguzi hawana usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya kama ya Mkalama haina gari la Wakaguzi, sasa huo ubora wa elimu wameachiwa Mkuu wa Shule na Walimu, kama utaratibu ulikuwa umeweka kuwepo na Wakaguzi wa Wilaya na Waratibu wa Kata ilikuwa ni muhimu kuhakikisha kwamba na mambo yanayohusiana na kusimamia ubora wa elimu yanawekwa vizuri ilikuwa ni jambo la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la Walimu hawatoshi katika ngazi ya shule za msingi na sekondari na pia tukizingatia kwamba suala la elimu bila malipo limeongeza udahili wa wanafunzi. Pia tunaomba suala la *VETA* liimarishwe, kuna tozo iliwekwa hapa, tumetembelea *VETA* hivi karibuni tukaona kwamba pesa zile hazirudi, kwa hiyo tunaishauri Serikali iweze kurudisha ile tozo iliyokuwa inatozwa kwa maana ya kupelekwa *VETA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* ni chombo kizuri kimeanzishwa, kinafanya kazi vizuri tuna imani nacho, lakini wenzangu wamezungumzia suala la uwakilishi wa *TARURA* kwamba wapi tunakutana na *TARURA* ili tuweze kutoa mawazo yetu. Ni jambo la muhimu inabidi kuangaliwa. Pia bajeti ya asilimia 30 kwa 70 *TANROAD* na *TARURA* bado inaleta mashaka ufanisi wa *TARURA, TARURA* itakuwepo pale lakini haitakuwa na ufanisi sana kwa sababu pesa zinazopelekwa kule zitakuwa hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tunaomba Serikali iweze kuangalia namna ya kuipatia pesa zaidi *TARURA* ili kubadilisha mfumo wa mgawanyo labda iwe 40 kwa 60. Tunafahamu kwamba barabara za lami ni gharama na barabara ikishakuwa ya lami inatakiwa iendelee kuwa ya lami lakini bado tunahitaji barabara za vijijini ili ziweze kutoa mazao vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya afya niipongeze Serikali kwa kutoa pesa kuimarisha vituo vya afya Tanzania nzima ikiwemo Mkalama tulipata milioni 300 za kununua vifaa na kasi ya ujenzi inaendelea vizuri na sasa wananchi watapata tiba na Serikali itaonekana kwamba ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi ambayo bado ipo hapa ni suala la Wilaya mpya ikiwepo Wilaya ya Mkalama. Sasa Wilaya mpya hazina hospitali za Wilaya, kwa hiyo kwa maelezo ama jibu ambalo lilitolewa na Naibu Waziri wa Afya asubuhi natumaini na Mkalama nayo mwaka huu itapata hospitali ya Wilaya. Bado tunasisitiza kwamba Wilaya

mpya zote ziweze kupata hospitali, hilo ni jambo muhimu na ule mnyororo wa tiba uweze kukaa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme tunaipongeza Serikali kwa kuweka mikakati ya kuongeza umeme katika gridi ya Taifa, kuanzisha *Stieglers Gorge* na miradi mingine kama Kinyerezi I, II na III. Ni jambo zuri kuleta umeme ambao utasaidia viwanda na viwanda bila umeme haviwezi kuwa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiunganisha na hapo, suala la *REA, REA* inafanya kazi nzuri lakini bado katika baadhi ya Mikoa *speed* yake ni ndogo na *scope* yake kwa maana ya kwamba nguzo ngapi zinakaa katika kijiji ni jambo muhimu ambalo inabidi liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri muhusika kwa sababu alifika katika Mkoa wetu wa Singida na bahati nzuri alifika Mkalama na alifanya kazi nzuri na kuna mahali umeme umewaka lakini bado tunataka kwenye miradi ya *REA II* ambayo ilikuwa haijakamilishwa iweze kukamilishwa, maana yake nguzo zipo kule na waya zipo wananchi wanaangalia, sasa wanaanza kusema umeme tutauona lini, wanaanza kukata tamaa, lakini kwa juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano nafikiri jambo hili litakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala moja la msingi, suala la maji vijijini. Hotuba ya Waziri Mkuu imezungumzia suala la maji vijijini, lakini katika bajeti tuliona kwamba kulikuwa na mradi wa vijiji 10, visima hivyo virefu vimechimbwa vipo lakini havijajengwa na ukiangalia bajeti nyingi kwenye Wilaya wanatoa milioni 400 mpaka milioni 600. Mradi mmoja kujenga ni milioni 400, ina maana kama umechimba visima 10 itachukua miaka 10 kuweza kujenga miradi hiyo ya maji. Kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo inabidi litafakariwe upya na liweze kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba tuanzishe Wakala wa Maji, tumeanzisha Mfuko wa Maji lakini sasa ianzishwe Wakala wa Maji kama vile *REA* inavyofanya kazi.

Wakala wa Maji akianzishwa atakuwa na kazi ya kutafuta pesa na kutekeleza miradi na kukabidhi miradi. Jambo hilo litakuwa mwarobaini wa upatikanaji wa maji hasa vijijini. Kwa hiyo, jambo hilo na lenyewe tunashauri Serikali iweze kulichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kupongeza baadhi ya taasisi, nipongeze *TEA* kwa sababu wanasaidia sana katika sekta ya elimu, wamefanya kazi kubwa sana na hata Jimboni kwangu wameweza kufanya kazi kubwa sana. Pia nipongeze TAMISEMI kwa kusaidia miundombinu na kuleta watumishi inagwaje bado tunahitaji watumishi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa sababu inatekeleza sasa ili kuunganisha Mkoa kwa Mkoa. Daraja la Sibiti linaendelea vizuri na kabla ya kuja huku nilifika Sibiti na wananchi wana matumaini sana na daraja la Sibiti, tukimaliza Daraja la Sibiti sasa tunatarajia kwamba barabara hiyo itajengwa barabara ya lami na kuweza kurahisisha usafiri wa mizigo na raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Ntimizi, ajiandae Mheshimiwa Boniphace Getere.

**MHE. MUSSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nianze kwa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya. Amefika Jimboni kwangu Igalula, ametatua kero za tumbaku katika Jimbo langu la Igalula sasa wakulima wa tumbaku wanaanza kupata kile ambacho wanategemea kutokana na zao lao la tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, MheshimiwaJenista na Naibu Waziri mdogo wangu Mheshimiwa Anthony Mavunde na Dada

yangu Stella Alex Ikupa kwa kazi kubwa wanayomsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu, mambo yanakwenda vema na sisi tunaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati alivyokuja Jimboni kwangu hakuondoka hivi hivi, aliniachia mchango katika kituo changu cha afya na sasa tunakwenda vizuri. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani zangu kwa Serikali hasa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Alivyokuja Jimboni kwangu Igalula nilimweleza matatizo ya miundombinu katika Jimbo letu la Igalula, barabara yangu ya Chaya – Nyahua na aliniahidi baada ya mwezi mmoja Mkandarasi atakuwa *site* na hivi ninavyozungumza Mkandarasi yupo *site* na barabara imeanza kutengenezwa. Nashukuru sana kwa kazi nzuri anayofanya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Igalula unapozungumzia reli ya kati, ujenzi unaofanyika sasa wa *standard gauge* unatugusa sisi kwa asilimia 100. Wananchi wetu kusafiri wanategemea sana reli katika Mkoa wa Tabora na kusafirisha mazao yetu kutoka Tabora kwenda sokoni kunategemea sana usafiri wa reli. Kwa hiyo, ujenzi wa *standard gauge* kwa sisi wananchi wa Tabora tunapongeza kwa kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunamwomba aendelee kuwa na afya njema ili ujenzi huu uweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kidogo suala la Watendaji wa Vijiji na Kata. Nashukuru baadhi ya Wabunge wamelizungumzia, kuna waraka umetoka Watendaji wetu wa Vijiji na Kata ambao wana elimu ya darasa la saba ambao wengi wao wameajiriwa takribani miaka 20 iliyopita leo wanatakiwa waondoke kwenye ajira, wanapoteza mafao yao na kazi zao. Baadhi yao wana takribani miaka miwili wanaelekea kwenye kustaafu, mtu

aliyefanya kazi kwa miaka 20, leo anaambiwa anaondoka kwenye kazi hana mafao na hajui ataenda kuishi vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watendaji hawa ndio tuliwatumia kujenga shule zetu za msingi, tuliwatumia kujenga shule za sekondari, kujenga nyumba za Walimu, tumewatumia kusimamia ulinzi na usalama katika maeneo yao, wamefanya mambo mengi kwa miaka 20, leo malipo yake ni haya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu na namuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu waliangalie hili kwa macho mawili ili tuwasaidie watendaji hawa ambao wengi wao baada ya miaka miwili mitatu wanaondoka kwenye utumishi, tusubiri waweze kumaliza muda wao tuanze upya utaratibu wa kuajiri watu wengine baada ya hawa kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la afya. Ilani yetu inazungumzia kila Kijiji kiwe na zahanati lakini kila Kata iwe na kituo cha afya. Haya yote tunataka kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata huduma bora na salama za afya. Tunataka kuhakikisha kwamba mama na mtoto wanajifungua salama, wanapata huduma zilizo bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Igalula hatuna kituo hata kimoja cha afya katika Jimbo zima. Tunazo zahanati lakini *referral* ya kutoka kwenye zahanati ni hospitali yetu ya Kitete iliyopo Tabora Mjini takribani kilomta 100 toka Jimboni Igalula. Mama mjamzito anapopata tatizo la kujifungua kutoka Igalula kwenda kwenye Hospitali ya Serikali ya Kitete takribani kilomita 100, asiyekuwa na uwezo wa kusafiri wanapata matatizo, wengine wanapoteza maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuingia madarakani sisi tuliliona tatizo hili, tumeanza kujenga vituo vya afya katika kila Kata, lakini Kata zetu tano za Jimbo la Igalula tumeshafika katika eneo la lenta tunasubiri sasa

Serikali iweze kutusaidia. Tunaomba waliopata milioni 500 na sisi tuangaliwe tuweze kusaidiwa kupata fedha hizo kujenga vituo vya afya katika Jimbo la Igalula ili kuondokana na tatizo la vifo vya mama na mtoto kama Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la maji na umwagiliaji ambalo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ipo katika ukurasa wa 27 ikiambatana na upatikanaji wa chakula kwa wananchi wetu. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya kuondoa kero ya maji katika maeneo yetu. Wamefanya haya kwa bajeti tuliyowapitishia mwaka jana ya Sh.50 tuliyoiongeza katika lita moja ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nnaomba kama waliweza kufanya mambo makubwa haya kwa Sh.50 tulizoziweka kwenye bajeti iliyopita, kama kuna uwezekano tuwaongezee Sh.50 tena katika lita ya mafuta iwe Sh. 100 iingie katika Mfuko wa Maji, nina hakika kero kubwa ya maji katika maeneo yetu itakwisha. Niombe Waheshimiwa Wabunge tusimamie hili sisi tunaotoka vijijini tunaiona kero kubwa ya maji. Tulisema tutamtua mama ndoo kichwani, tutekeleze kwa vitendo kwa kumwongezea bajeti ili aweze kutekeleza. Tusipoweka bajeti ya kutosha haya yote hayawezi kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la upatikanaji wa chakula linaendana na kuboresha miradi ya umwagiliaji katika maeneo yetu. Tukitengeneza miradi mizuri ya umwagiliaji suala la upatikanaji wa chakula katika maeneo mengi halitakuwa tatizo. Tunapowaambia wananchi wasiseme kama kuna njaa wakati hatutengenezi mazingira bora ya umwagiliaji tunakuwa hatutendi haki, lakini yapo maeneo mengi ambayo miradi hii ipo inaweza ikafanyika na ikasaidia upatikanaji wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu kuna miradi miwili mikubwa, Goweko kuna mradi wa umwagiliaji

umeshatengenezewa *feasibility study,* umeshafanyiwa usanifu na imeshapatikana hati ya mazingira. Katika Kata ya Loya tumeshapata hati ya mazingira na usanifu umefanyika. Katika bajeti ya mwaka 2016/2017, iliwekwa miradi hii iweze kutekelezeka, lakini mpaka leo haijaweza kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ili wananchi wetu wasiwe na shida ya chakula, miradi hii iweze kuangaliwa kwa makini iweze kutengewa fedha, ikiweza kutekelezeka hatutakuwa na shida ya chakula. Wananchi wetu watapata fedha za kuchangia miradi ya maendeleo, Halmashauri zetu zitapata kodi na mwisho wa siku hata uchumi wa viwanda tutakwenda nao vizuri huko tunapokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la barabara. Nilipoanza kushukuru barabara yangu ya Chaya – Nyahua nilizungumzia umuhimu wa barabara hii. Barabara hii inaunganisha Mikoa ya Katavi, Mkoa wa Kigoma lakini pia ni njia rahisi kufika Bukoba, Kahama na Mwanza. Inapotengenezwa barabara hii maana yake tunawasaidia hata ndugu zetu wa mikoa ya jirani kuunganisha safari zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara hii kuna kipande ambacho naomba kifanyiwe kazi, kifanyiwe upembuzi kuanzia pale Chaya kuja Lutende kutokea Ndala kwenda kutokea Puge na Nzega. Barabara hii kama itatengenezwa itapunguza tena siyo chini ya kilometa 120 kutoka Dodoma – Tabora – Mwanza na maeneo mengine badala ya kupitia Singida na Nzega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niliomba barabara yangu ya Miswaki – Loya – Iyumbu kilometa 75 iweze kutengenezwa. Kwa nini niliomba barabara hii iweze kutengenezwa? Kuna kilimo kikubwa cha mpunga tunalima mpunga mwingi sana kule, barabara hazipitiki wakati wa mvua. Kupitia *TARURA* tuliomba fedha ili iweze kufunguliwa barabara hii. Kuna uchumi mkubwa wa Wilaya yetu ya Uyui,

Halmashauri inakusanya zaidi ya milioni 200 kutokana na kodi kwa sababu ya mpunga unaolimwa kule. Barabara hii ikitengenezwa itasaidia wananchi wetu kuweza kujikwamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la elimu. Nipongeze elimu bila ada. Wananchi wetu wanapata fursa kubwa ya kupata elimu, wale ambao walikuwa hawapati elimu lakini changamoto zilizojitokeza, kwanza vyumba vya madarasa vimepungua, nyumba za Walimu zimepungua, Walimu wamekuwa wachache na matundu ya vyoo pia yamekuwa machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosahuri ni kwamba Serikali sasa ije na mkakati maalum kama ilivyofanya kwenye madawati, tuwe na mkakati wa kuhakikisha kwamba tunajenga sasa nyumba za Walimu za kutosha, tuongeze Walimu, tujenge matundu ya vyoo lakini pia tuweze kupata nyumba za Walimu na madarasa pia yaongezeke ili kutatua changamoto hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani yake hapo wananchi wetu wamejenga majengo haya mengi ambayo maboma hayajakwisha kwa ahadi kwamba wakifikisha kwenye lenta Serikali itakuja kuwasaidia. Katika maeneo mengi majengo haya yapo, siyo katika Jimbo la Igalula tu, ni nchi nzima. Serikali sasa lazima ije na utaratibu wa kuhakikisha kwamba na haya maboma yote yanaisha ili nguvu za wananchi zisipotee bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie ofisi za Wabunge. Suala hili naomba lichukuliwe katika uzito mkubwa sana. Waheshimiwa Wabunge kuendelea kupewa ofisi kwenye ofisi za ma-*DC* siyo sawasawa. Waheshimiwa Wabunge kwenda kukodisha ofisi mitaani siyo sawasawa. Ninachoomba Bunge lije na mkakati maalum kusaidia upatikanaji wa ofisi za Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsate sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Boniphace na Meshimiwa Kakoso ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nianze kwa kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi na kwa Mkuu wake, jemedari wetu Mkuu Dokta John Pombe Magufuli, kwa kuongoza kazi nzuri anazozifanya, anatekeleza vizuri Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na hili niliseme tu, kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ninavyomuona namkumbukia sana Simba wa Nyika, Marehemu Mheshimiwa Mfaume Kawawa ambaye enzi hizo alikuwa akiagizwa kutekeleza jambo anatekeleza, Mungu amrehemu mahali alipo. Waziri Mkuu kila anapopewa nafasi ya kutekeleza mambo anatekeleza vizuri sana. Nimpongeze kwa kweli kwa mambo yote hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najiuliza mambo madogo tu kwenye hii bajeti na kwenye hii hotuba ninayotaka kuitoa hapa au kwa maelezo ninayotaka kutoa; kwamba, hivi mtu akipata nafasi ya kuchangia kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, hivi mwaka ujao yale aliyoyasema atayaona mawili, matatu yametendeka au ni kusema tu halafu yanaishia hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka kusema kwamba kwa nafasi hii nitakayokuwa nayasema hapa nataka kuyapima kwamba mwaka ujao nitakuja kuona nafasi nilichangia kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, yale niliyoyasema japo mawili matatu yametendeka? Kwa hiyo, nafikiri hili jambo litakuwa bora zaidi kwa Bunge kuchangia hii ofisi kwa sababu ndiyo eneo kubwa ambalo Waziri Mkuu analiongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijielekeze kwenye miradi ya Jimbo langu la Bunda. Tuna miradi ya maji, katika miradi ya maji ya Jimbo la Bunda iko miradi mingi sana. Nimpongeze Waziri wa Maji, amekuja pale mara nyingi sana, kuna Mradi mmoja unaitwa Nyang'alanga – Mgeta ambao

ulianza kwa bajeti ya milioni 495, sasa una milioni 910 mradi haujaisha na maji hayajatoka. Kila siku ripoti zinakwenda na hakuna ukaguzi unaofanyika wa kutoa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ahati nzuri Naibu Waziri wa Maji amesema wale wote wanaohujumu fedha za maji watakipata cha moto. Namwomba afike pale sasa aone namna ya kuwashughulikia mradi wa maji Nyang'alanga ili kuweza kumuondoa mtu ambaye amekaa pale kwa muda mrefu na hakuna kazi inayofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Mradi wa Malambo. Bunge lililopita nilizungumza hapa malambo 12 yaliyokuwa yanataka kutengenezwa ya zamani kuyafufua. Tunayafufua kwa sababu kutoka Ziwa Victoria kwenda kwenye Jimbo langu ni kilometa 25 lakini sisi maji hatuna tuna tabu sana ya maji katika Jimbo la Bunda. Tunataka kufufua malambo ya zamani yaliyochimbwa na Mtemi Makongoro na tumeleta bajeti kwenye Wizara ya Maji na Katibu Mkuu Wizara ya Maji alipokea huo mradi wetu na tunaomba aushughulikie, ninashauri haya mambo yafanyike mapema ili tuweze kupata maji kwenye Jimbo la Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza habari ya wanyama waharibifu kwenye Jimbo langu. Jimbo langu lina vijiji 11 ambavyo wanyama waharibifu wapo kila siku, kila mazao yanayolimwa yanaliwa, hata katani zinazopandwa zinaliwa, hata pamba inayolimwa sasa hivi inaharibika. Tunaomba Serikali sasa ichukue hatua za kutosha za kuzuia wale wanyama wasiwe wanakuja kuharibia wananchi mazao ili wananchi waweze kujineemesha kwa sababu yale mazao ndiyo kipato chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu fidia. Toka haya mazao yameanza kuliwa tunadai zaidi ya milioni 360, kulikuwa na milioni 400 wameshalipa karibu milioni 182, kwa hiyo bado milioni 360 zinadaiwa, tunaomba Serikali, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na nimwombe Waziri Mkuu ahimize hii fidia ya wakulima iweze kupatikana kwa Jimbo la Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze habari ya afya katika Jimbo langu. Tumejenga zahanati tano na mpaka zahanati zingine tumeshaezeka, tunaomba Serikali, kwa sababu Bunge lililopita Wabunge walisema hapa, maboma yote ya zahanati zote na maboma ya vituo vya afya wakasema na Bunge la Bajeti hapa tulizungumza na Bunge lililopita tulizungumza, kwamba maboma yote yashughulikiwe na yaletwe hapa Bungeni na tuweze kutengeneza mkakati maalum wa kuyamaliza, sasa sijui hatua imefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwa maboma matano ya vijiji vilivyotengeneza kwenye jimbo langu, Kijiji cha Kambubu, Chiling'ati, Komalio na Malambeka ili waweze kupewa fedha za kuweza kumalizia majengo haya. Nimuombe Waziri wa Afya aweze kutusaidia na Wizara ya TAMISEMI iweze kutusaidia katika jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza habari ya barabara, habari ya barabara ya lami kutoka Makutano kwenda Nyamswa hadi Sanzati, inaitwa makutano ya barabara ya lami kutoka Makutano – Sanzati. Ninavyozungumza hii barabara bila unafiki, Mheshimiwa Waziri Mkuu namshukuru sana alikuja Mkoa wa Mara na akapita kwenye ile barabara akaiona, ni vitu vya aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inayopita kwenye maeneo ya kaburi la Baba wa Taifa imekaa miaka zaidi ya sita haimaliziki na wale watu wanaotengeneza hiyo barabara wale wakandarasi hawaguswi, hivi ni akina nani hawa? Barabara ipo kila siku na vumbi zinakwenda kwenye kaburi la Mwalimu pale, hakuna mtu anamaliza hiyo barabara, *why?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii tupo tunavuta upepo, huu upepo tunaovuta ni wa Mwalimu. Jamani mambo gani hayo? Aibu hii. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameliona hilo, nadhani atalishughulikia haraka iwezekanavyo ili tuweze kuzungumza haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara ya Nyamswa – Bunda, tuliahidiwa kupewa mkandarasi lakini hajaenda. Tuna Barabara ya Sanzati – Nata, mkandarasi hajapatikana, na kuna barabara ya kutoka Bunda kwenda Buramba na Buramba – Kisoria, mkandarasi bado naye anasuasua hajawa kwenye uwezo mzuri. Tunaomba Serikali ione namna gani ya kumaliza zile ahadi zake na hasa ile miradi ya muda mrefu ambayo inahitaji kumalizika. Barabara ya Makutano – Nyamswa – Sanzati ni ya muhimu sana, imeleta kero kubwa sana kwa wananchi wa Butiama na wananchi wa Kata ya Nyamswa na maeneo mengine yaliyopakana na barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi; namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuja Mkoa wa Mara, amezungumza na ametusaidia mambo mengi, lakini migogoro ya Vijiji vitatu vya Silolisimba, Lemuroli na Mkomalilo bado vina matatizo ingawaje Mkuu wa Mkoa anajitahidi kumaliza tatizo hilo, lakini bado, tunamuomba na bahati nzuri siku moja Mheshimiwa Naibu Spika alitamka hapa Bungeni kwamba Serikali ishughulikie namna ya kumaliza tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuone namna gani ya kulimaliza ili wananchi waweze kukaa vizuri kwa sababu kila siku ni mapanga. Bahati nzuri miezi miwili iliyopita wananchi wawili walikufa kwa ajili ya mapigano ya hiyo mipaka, kwa hiyo tunaomba tuone namna ya kulimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze habari ya Watendaji; katika jambo ambalo Wabunge tunashauri kwa kila mara na kama tuko Kikatiba katika kushauri jambo hili, hili suala la Watendaji hawa ambao tumepanga kuwafukuza, nadhani katika jambo ambalo tunaweza kulihimiza Bunge lifanye ni namna gani ya kuwaacha wale Watendaji wamalize muda wao, kwa sababu wengi wamemaliza miaka miwili, mitatu, minne, mitano, kuna haja gani ya kuwatoa sasa hivi? Kwa hiyo, nafikiri kwamba ni vizuri tuone namna gani na tupate majibu mapema ili tujue namna ya kuwasaidia hao Watendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina miradi ya *REA* vijiji 21, Jimbo langu katika Mkoa wa Mara ndiyo Jimbo lenye vijiji vingi ambavyo havijafikiwa na umeme ingawaje Mheshimiwa Waziri amenisaidia vijiji vingine huko nyuma vilikuwa 32 sasa vimebaki 21. Tunamwomba yule mkandarasi wa *REA* kwenye Jimbo langu na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri alifungua mradi wa *REA* kwenye Jimbo langu, ajitahidi kumhimiza mkandarasi aweze kuimaliza ile miradi kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia habari ya Bandari ya Musoma, kuna miradi mikubwa pale ya Kimkoa, kuna mradi wa bandari na kuna mradi wa kiwanja cha ndege Musoma na mradi wa Hospitali ya Kwangwa. Kwa hiyo, Mkoa wa Mara kuna miradi mikubwa kimkoa, tunaomba Serikali iangalie namna ya kuimaliza ili wananchi wa pale waweze kupata huduma za kutosha katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo langu la Bunda na Bunda nzima na Jimbo la Bunda, ardhi yetu imechoka sasa, tunaomba kama kuna uwezekano wa kupata pembejeo kwa ajili ya wakulima sasa na sisi tuingizwe kwenye mradi huo wa kupewa pembejeo ili wakulima waweze kupata mazao mazuri kwa sababu ardhi yao imechoka kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie habari ya Walimu wa sayansi shule za msingi na sekondari. Katika maeneo mengi ya Jimbo la Bunda kuna sekondari zaidi ya tisa hakuna Mwalimu hata mmoja wa sayansi. Kwa hiyo, nafikiri kwamba ni vizuri sasa Waziri anayehusika aweze kuona namna gani ya kutusaidia Walimu wa sayansi kwenye sekondari tisa katika Jimbo la Bunda ambazo hazina Walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu vingine naviona hapa nikivisoma huwa vinanitia kichefuchefi kidogo. Kuna deni la watumishi wa Serikali, lakini ukiangalia deni la watumishi wa Serikali kuna vitu vingine vya kujitakia. Hivi inawezekanaje leo tuna watumishi wanaokaimu wengi

katika Wizara mbalimbali na kila mtumishi anayekaimu anapewa nusu ya mshahara wa mtu aliyekuwepo katika nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kama Mkurugenzi aliyetoka alikuwa anapokea mshahara wa milioni tano na yeye anaenda kukaimu anapokea milioni mbili na nusu na anakaa miaka kumi, mitano, saba, kumi na tano. Sasa hii kwa nini tunaitafutia Serikali madeni, kwa nini tusibadili sheria hizi za utumishi za kukaimu na sheria zile za kwenda kwa wakati wanakaimu kama ni mtu kwenda kukaimu tumwambie akaimu bure, sio akaimu kwa kulipa mshahara, tunatia madeni Serikali bure na tuangalie ile sheria namna ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kuangalia sheria ndogo hizi au sheria za Wanyamapori, Maliasili na Utalii na hasa zile sheria za fidia. Fidia imekuwa ndogo sana lakini mbaya zaidi kuna sheria zile za fidia ambazo hazijakaa sawa. Kwa mfano, kutoka mpaka wa wanyamapori kwenda kwa wananchi wanasema iwe ni mita 500, mita 500 ni nusu kilometa, lakini kutoka hiyo nusu kilometa *buffer zone* kwenda mpaka kilomita 1000 mkulima anatakiwa kulipwa kama amelima shamba heka 20 halafu tembo amekwenda amekula mazao yote, anatakiwa kulipwa heka tano tu, heka 15 nyingine ni sadaka, hii sheria ya wapi tena? Nafikiri kwamba ni vizuri wakaangalia hiyo sheria...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana anayoifanya ya kutekeleza miradi mikubwa katika Taifa letu. Nimshukuru sana

Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ya kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapainduzi. Niwapongeze kwa dhati Mawaziri wale ambao wamefanya kazi kwa nia njema ya kulisaidia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwa sababu tuna miradi ambayo imeanza kutekelezwa kwenye maeneo ya Mkoa wetu. Tuna miradi ya maji ambayo imetekelezwa kwa kiwango kikubwa, miradi ya afya, miradi ya elimu, miradi ya umeme vijijini, miradi ya barabara kwenye maeneo ya Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Tabora. Pale Serikali inapofanya vizuri tuna haki ya kuipongeza na pale ambapo pana changamoto tutaishauri Serikali ili iweze kutusaidia kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilayani kwangu nina miradi ya maji ambayo imeshaanza kutekelezwa, miradi mikubwa ya Kijiji cha Majarida, Kijiji cha Igagala, wananchi wanapata maji, Kijiji cha Ikola wana miradi mikubwa ya maji ambayo imetekelezwa. Nampongeza sana Waziri mwenye dhamana kwa jitihada ambazo anazifanya kuwatendea haki wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ipo miradi ya maji ambayo inatekelezwa Vijiji vya Mwese, Kamjela, Kabungu, hiyo yote ni miradi ambayo inatekelezwa na tuna visima 20 ambavyo vinachimbwa kwa ajili ya kuwapa huduma ya maji. Kwa hiyo tunaipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna miradi ya afya, tunavyo vituo vya afya cha Karema, Mwese, Mishamo, Serikali imetoa fedha kwenye vituo vya afya vya Mwese na Mishamo karibu zaidi ya shilingi milioni 800. Tuna matumaini makubwa sana kwamba Serikali itaendelea kusaidia kwenye sekta hii ili vituo hivi viweze kukamilika hasa kile kituo cha Mwese ambacho kinahitaji fedha kwa ajili ya kukamilisha ule mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi ya elimu ambayo inatekelezwa, kuna ujenzi wa shule za msingi, ujenzi

wa shule za sekondari, karibu kila sehemu shule zinajengwa kwa kutegemea nguvu za wananchi na Serikali yenyewe pale ambapo panahitajika kutoa huduma hiyo. Tunawapongeza na tunaiomba Serikali kwenye miradi hiyo iweze kuongeza nguvu kuwasaidia wananchi kwa sababu wengi wamejitokeza kujenga shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa ya kipekee kwenye miradi, hasa ya elimu, nimpongeze sana Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika kwa jitihada anazofanya za kusimamia utekelezaji. Pia nimpongeze Mkuu wa Mkoa kwa kulinda amani na usimamizi mkubwa wa miradi mingi inayotekelezwa Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto ambazo tunaiomba Serikali iweze kuzisimamia. Changamoto ya kwanza tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aingilie kati mgogoro wa Mradi wa Umeme Vijijini *(REA)* ambao unaunganisha Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma. Kwa nini tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, miradi ya *REA* imesimama kwenye Mikoa ya Kigoma na Katavi kwa sababu ya mgogoro ambao upo, watu walioomba tenda wamegombana na wakashtakiana wakapelekwa Mahakamani, kiasi kwamba sasa ule mradi umesimama, *REA* Awamu ya Tatu karibu sehemu nyingi nchini inatekelezwa, kwenye mikoa hii hakuna kilichotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliingilie hili jambo ili wananchi wa mikoa hii miwili waweze kuepukana na mgogoro ambao kwao wao hauna manufaa, tunaomba Serikali iingilie ili tupate huduma ya umeme vijijini kwa vijiji vya mikoa hiyo miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Serikali iongeze fedha za Mfuko wa Barabara. Fedha za Mfuko huu zikiongezwa zitasaidia sana kuimarisha ujenzi wa barabara za vijijini na mijini. Mfuko wa sasa ambao upo una fedha kidogo sana na karibu wananchi wengi wa nchi nzima wanategemea sana fedha hizi ziweze kuwasaidia kuimarisha miundombinu ya barabara. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali

iongeze fedha kwenye Mfuko wa Barabara ili barabara za vijijini, miradi ya barabara za mijini ziweze kuimarika na zifanye kazi vizuri kwa sababu huko ndiko kuna watu wengi wanaozalisha na wanahitaji huduma hii ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaomba Serikali iongeze fedha kwa ajili ya kupeleka kwenye miradi ya ujenzi hasa kwenye Wilaya ambazo ni mpya. Mkoa wa Katavi ni Mkoa mpya na una Wilaya mpya ya Tanganyika na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika kwenye maeneo hayo, anajua changamoto zilizopo. Tunahitaji fedha zipelekwe zikajenge Makao Makuu ya Wilaya, nyumba za watumishi, hospitali ya Wilaya na Hospitali ya Mkoa wa Katavi. Haya maeneo ni ya muhimu sana kwa ajili ya kuimarisha shughuli za kiutawala lakini vilevile kuimarisha shughuli za huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu katika jitihada za kufufua miradi ya kilimo, hasa kwenye mazao ya pamba na tumbaku. Ametoa msukumo mkubwa sana, tunampongeza, lakini yapo mambo ambayo yanahitajika kuyafanyia kazi ili kwenda sambamba na msukumo ambao kautoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunaomba Serikali inapokuwa inasukuma mazao haya ihakikishe inatengeneza mfumo mzuri wa kupeleka pembejeo. Pembejeo mwaka huu wakulima hawakuzipata kwa wakati, kuna baadhi ya maeneo wamepata hasara kwa sababu hawakupata pembejeo ambazo zilihitaji kuzalisha kwa wakati. Kwa hiyo, tunaomba usimamizi kwenye eneo hili uwe mkubwa sana ili tuweze kupata mazao ambayo yatawasaidia wananchi, hasa wakulima na vilevile kusaidia kipato cha Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta hii ya kilimo bado suala zima la masoko linahitaji ufuatiliaji wa hali ya juu. Wananchi wamelima pamba kwa wingi, tunaiomba sana Serikali wanapolima wahakikishe wanunuzi wa mazao haya wanakuwa wamejengewa mazingira ambayo

yatawafikia wakulima kwa wakati. Naomba kwenye jambo hili tulifanyie umuhimu sana kwa sababu jitihada ambazo amezionesha Waziri Mkuu za kuhimiza mazao ya pamba, tumbaku na korosho zinaweza zikafikia mahali ambapo hazitakuwa na tija pale ambapo wakulima watakosa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ni kuhakikisha wanapata pembejeo za madawa ambayo yanahitaji kuhudumia mazao haya ambayo wananchi wamepewa fursa na wamehimizwa wayalime. Bila masoko tutalima mazao mbalimbali lakini hayatakwenda mahali popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwenye zao la tumbaku, mfumo wa zao la tumbaku uko tofauti sana na mazao mengine. Tunaiomba sana Serikali ihakikishe inawashirikisha wadau kwa ujumla ili wajue changamoto ya lile zao lakini tuhakikishe tunawajengea mazingira ya masoko yenye uhakika. Bila kutafuta masoko na bila kusaidia Serikali kuingilia kati, zao la tumbaku linaweza likapotea na linaweza lisitoe tija kwa wananchi, tunaomba sana Serikali iyafanye hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya umwagiliaji. Kwenye eneo hili bado utekelezaji ni mdogo sana. Tunaiomba sana Serikali na tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aangalie au aunde Tume itakayosaidia kuangalia miradi mingi ya umwagiliaji ambayo kimsingi haijafanya kazi na haijaonekana kabisa. Serikali imetumia fedha nyingi kwa ajili ya miradi hii ambayo haijaonekana na ufanisi wake ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya hakuna mradi wa umwagiliaji ambao ulisimamiwa vizuri, hata Halmashauri zenyewe hawakushirikishwa, ni miradi ambayo ilikuwa inatoka huku juu inaenda moja kwa moja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, orodha yetu imekwisha na muda wetu ndiyo unakwisha.

Ninalo tangazo dogo tu kwamba Mheshimiwa Freeman Mbowe anaomba kuwatangazia kuwa wakati anaingia kwenye mlango eneo la *security* amepoteza simu yake ya *Samsung Duos,* anaomba yeyote aliyeiona ampatie.

**MBUNGE FULANI:** Imeonekana.

**MWENYEKITI:** Imeonekana?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Haya, simu imeonekana. Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru kwa michango mizuri, lakini nikushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, hizi pongezi unazopewa ni za dhati, mnafanya kazi nzuri sana Serikali pamoja na Mawaziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamis, Tarehe 5, Aprili, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*